# MSHIKAMANO WA KISARUFI KATIKA KISWAHILI

**VIFU SAIDI MAKOTI**

**SSC/D.PHIL/08/2004**

MACHAKOS UNIVERSITY LIBRARY

Signed........ Date........

**KAZI HII IMEWASILISHWA KWA AJILI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU YA CHUO KIKUU CHA MOI, ELDORET**

**AGOSTI 2013**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na wala haijawasilishwa na kutahiniwa katika chuo kingine.

12-09-2013

Makoti Vifu Saidi
SSC/D.Phil/08/2004

Tarehe

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu tukiwa wasimamizi waliochaguliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Moi.

14/9/13

P
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret, Kenya

Tarehe

7/10/13

itemi
a Nyingine za Kiafrika
ret, Kenya

Tarehe

**TABARUKU**

Kazi hii naitabarukia watoto wangu mapacha, Hassan na Hussein.

# ABSTRACT

This study investigated grammatical cohesion in Kiswahili texts. It elucidates the different devices which bring grammatical cohesion. These are reference, substitution, ellipsis and conjunction. Each device was explored to show how it is applied in bringing cohesion in the selected texts.To achieve this, texts from two Kiswahili prose works; *Watoto wa Maman'tilie* (Mbogo, E) and *Musaleo!* (Wamitila K.W) were analysed. The two authors of the texts are Kiswahili writers of repute in their respective countries, i.e Tanzania and Kenya respectively. In both countries, Kiswahili is extensively spoken, it is also official and a national language and is an important medium of communication. The choice of the two authors was done so as to give the study a wider scope of where Kiswahili is widely spoken.This study was guided by the Cohesion Theory of Halliday and Hassan. The study showed how reference, substitution, ellipsis and conjuction were used to connect Kiswahili sentences and presuppositions in selected texts to realize the cohesiveness and coherence in Kiswahili texts. Further, it investigated and explored some constraints found in the use of these devices in Kiswahili language. It also explored how these maintain or destroy the grammaticality of the texts. The study established that some devices are used more than others. For example reference, especially personal reference, is most used in the texts to bring cohesion. This was followed by conjuction, substitution and ellipsis in that order. It also established that the use of cohesive ties differed from one author to the other. Hence, it may be a style of an author in a prose work. The study also found some constraints in reference, substitution and conjunction. This was due to some rules governing these devices and grammar of the language. And in some instances, these rules have to be ignored to avoid ambiguity and nonsensical texts to achieve cohesion in Kiswahili texts.These findings will help writers, readers and students of Kiswahili at all levels of study to understand better how grammatical cohesion is realized in Kiswahili texts and the constraints involved. The findings will also contribute in the understanding of Kiswahili linguistics.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza mshikamano katika matini za Kiswahili. Pia ulichunguza na kufafanua vijenzi mbalimbali vinavyoleta mshikamano wa kisarufi. Vijenzi hivi ni urejeleaji, ubadilishaji, udondoshaji na uunganishaji. Kila kijenzi kilichanganuliwa na kuonyeshwa jinsi kinavyotumika kuleta mshikamano na ufungamano katika matini zilizochunguzwa. Ili kufikia malengo haya, matini mbili za nathari za Kiswahili zilitumika, nazo ni *Watoto wa Maman'tilie* (Mbogo, E) na *Musaleo!* (Wamitila, K.W). Wandishi wa matini hizi ni wandishi wanaofahamika katika nchi zao asili za Tanzania na Kenya mtawalia. Katika nchi hizi mbili, Kiswahili kinaongewa zaidi, ni lugha ya taifa, rasmi na lugha muhimu ya mawasiliano katika maisha ya kila siku ya jamii hizo. Uteuzi wa wandishi hawa ulifanywa ili kuupa utafiti huu mandhari pana ya maeneo ya Kiswahili kitumikako.Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Mshikamano ya Halliday na Hassan. Utafiti huu ulionyesha jinsi vijenzi vya mshikamano vilitumika katika kuunganisha sentensi na dhana ili kuleta mshikamano na ufungamano katika matini zilizoteuliwa. Aidha, ulichunguza ikiwa vijenzi hivi hukumbwa na vikwazo katika Kiswahili na kuharibu au kudhibiti sarufi katika matini. Ilidhihirika kuwa kuna vikwazo kati urejeleaji, ubadilishaji na uunganishaji. Vikwazo hivi hutokea kwa sababu ya mchakato na sheria za lugha yenyewe. Hivyo hubidi wakati mwingine, vikwazo hivi vipuuzwe ili kukwepa uharibifu wa mshikamano katika matini. Utafiti uligundua kuwa baadhi ya vijenzi vya mshikamano hutumika zaidi kuliko vingine. Kwa mfano urejeleaji, hususan wa nafsi, hutumika zaidi katika kuleta mshikamano kwenye matini. Ulifuatiliwa na uunganishaji, kisha ubadilishaji na udondoshaji ukamalizia. Vile vile, ilibainika kuwa utumiaji wa vishikanishi vya mshikamano, ulitofautiana kati ya waandishi. Hivyo kuwa ni mtindo wa kipekee wa kila mwandishi. Matokeo ya utafiti huu, nina imani kuwa yatasaidia wandishi,wasomaji na wanafunzi wa Kiswahili katika viwango mbalimbali vya elimu kuelewa mshikamano wa kisarufi na vikwazo vyake. Matokeo haya pia yatachangia katika kufahamu vipengele vingine katika isimu ya Kiswahili.

# YALIYOMO


IKIRARI .......... ii
TABARUKU .......... iii
ABSTRACT .......... iv
IKISIRI .......... v
YALIYOMO .......... vi
ORODHA YA MAJEDWALI .......... .ix
FAHARASA .......... x
SHUKURANI .......... xii

**SURA YA KWANZA** .......... 1
UTANGULIZI 1
1.0 Usuli wa Swala la Utafiti .......... 1
1.2 Swala la Utafiti .......... 4
1.3 Madhumuni ya Utafiti .......... 6
1.4 Nadharia-Tete .......... 6
1.5 Umuhimu wa Utafiti .......... 7
1.6 Upeo wa Utafiti .......... 8
1.7 Mbinu za Utafiti na Uchanganuzi wa Data .......... 10
1.7.I Utafiti katika Maktaba .......... 10
1.8 Ufafanuzi wa Dhana Kuu .......... 12
1.8.1 Mshikamano wa kisarufi .......... 13
1.8.2 Matini .......... 13
1.8.3 Vijenzi .......... 13
1.8.4 Dhana .......... 14
1.8.5 Dhana-dhaniwa .......... 14
1.8.6 Kirejelewa .......... 14
1.8.7Kirejelea .......... .14
1.8.8 Kibadala .......... 14
1.8.9 Kidondoshwa .......... 14

**SURA YA PILI** .......... **15**
DHANA YA MSHIKAMANO NA YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA 15
2.0 Utangulizi .......... 15
2.1 Dhana ya Mshikamano .......... 15
2.1.1 Urejeleaji .......... 17
2.1.2 Ubadilishaji .......... 32
2.1.3 Udondoshaji .......... 56
2.1.4 Uunganishaji .......... 66
2.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada .......... 71
2.2.1 Mshikamano kwa Jumla .......... 71
2.2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Urejeleaji .......... 78
2.2.3 Yaliyoandikwa kuhusu Ubadilishaji .......... 87
2.2.4 Yaliyoandikwa kuhusu Udondoshaji .......... 92
2.2.5 Yaliyoandikwa kuhusu Uunganishaji .......... 103

2.3 Hitimisho........ 113
**SURA YA TATU ........ 114**
UREJELEAJI........ 114
3.0 Utangulizi ........ 114
3.1 Urejeleaji Unavyotokea........ 115
3.1.1 Mrejeondani........ 120
3.1.1.1 Mrejeombele........ 125
3.1.1.2 Mrejeosabiki........ 126
3.1.2 Mrejeonje........ 128
3.2 Aina za Urejeleaji........ 129
3.2.1 Urejeleaji Nafsi........ 129
3.2.1.1 Urejeleaji wa Nafsi ya Kwanza........ 132
3.2.1.2 Urejeleaji wa Nafsi ya Pili........ 135
3.2.1.3 Urejeleaji wa Nafsi ya Tatu........ 137
3.2.2 Urejeleaji Onyeshi........ 139
3.2.3 Urejeleaji Linganishi........ 141
3.2.3.1 Urejeleaji Linganishi Jumla........ 141
3.2.3.2 Urejeleaji Linganishi Mahususi........ 143
3.3 Vikwazo........ 145
3.4 Hitimisho........ 147

**SURA YA NNE........ 150**
UBADILISHAJI........ 150
4.0 Utangulizi........ 150
4.1.Ubadilishaji Unavyotokea........ 150
4.1.1 Ubadilishaji wa Nomino na Kirai Nomino........ 152
4.1.1.1 Ubadilishaji wa Nomino........ 152
4.1.1.2 Ubadilishaji wa Kirai Nomino (K)........ 155
4.1.2 Ubadilishaji wa Kirai Kitenzi (KT)........ 156
4.1.3 Ubadilishaji wa Kirai Elezi/Chagizo (KE)........ 157
4.1.4 Ubadilishaji wa Kishazi na Sentensi........ 159
4.2 Hitimisho........ 166

**SURA YA TANO ........ 168**
UDONDOSHAJI........ 168
5.0 Utangulizi........ 168
5.1 Udondoshaji Unavyotokea........ 171
5.1.1 Udondoshaji wa Silabi ........ 170
5.1.2 Udondoshaji wa Nomino........ 176
5.1.2.1 Udondoshaji wa Nomino Kiima (NominoK)........ 177
5.1.2.2 Udondoshaji wa Nomino Yambwa (NominoY)........ 180
5.1.3 Udondoshaji wa Kitenzi ........ 183
5.1.4 Udondoshaji wa Kishazi na Sentensi ........ 189
5.1.5 Udondoshaji wa Kiashiria, Kimilikishi, Kiulizi, Kielezi na Kionyeshi...... 193
5.1.6 Udondoshaji wa kiunganishi *na* ........ 194
5.2 Vikwazo katika Udondoshaji........ 196

5.3 Hitimisho ... 197

**SURA YA SITA ... 199**

6.0 UUNGANISHAJI ... 199

6.0 Utangulizi ... 199

6.1 Uunganishaji na Aina zake Unavyotokea ... 204

6.1.1 Uunganishaji Nyongeza ... 204

6.1.1.1 Kiunganishi *Na* ... 205

6.1.1.1.1 Kuunganisha vipashio vya mawazo ... 206

6.1.1.1.2 Kuunganisha matendo au matukio ... 207

6.1.1.1.3 Kuunganisha habari ... 209

6.1.1.2 Kiunganishi *Au* ... 210

6.1.1.3 Kiunganishi *Pia/Tena* ... 213

6.1.1.4 Kiunganishi *Wala* ... 215

6.1.2 Uunganishaji Elezi ... 216

6.1.2.1 Kiunganishi *Lakini* ... 216

6.1.2.2 Viunganishi *Ingawa/Ingawaje/Japo/Japokuwa* ... 219

6.1.2.3 Viunganishi *Badala ya.../Bali* ... 221

6.1.2.4 Kiunganishi *Hata hivyo* ... 222

6.1.3 Uunganishaji Sababishi ... 223

6.1.3.1 Viunganishi *Kwa sababu/Kwa kuwa* ... 224

6.1.3.2 Kiunganishi *Kwa hivyo* ... 225

6.1.3.3 Kiunganishi *Hivyo* ... 226

6.1.3.4 Kiunganishi *Kutokana na* ... 228

6.1.4 Uunganishi Wakati ... 228

6.1.4.1 Kiunganishi *Kisha* ... 229

6.1.4.2 Kiunganishi *Baada ya* ... 231

6.1.4.3 Kiunganishi *Baadaye* ... 234

6.1.4.4 Kiunganishi *Hatimaye* ... 236

6.1.4.5 Kiunganishi *Kabla (ya)* ... 238

6.1.4.6 Kiunganishi *Mara* ... 239

6.2 Vikwazo ... 241

6.2.1 Kiunganishi *Na* ... 241

6.2.2 Kiunganishi *Tena* ... 242

6.2.3 Kiunganishi *Hivyo* ... 242

6.2.4 Kiunganishi *Baadaye* ... 243

6.2.5 Kiunganishi *Hatimaye* ... 243

6.3 Hitimisho ... 244

**SURA YA SABA ... 246**

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ... 246

7.1 Hitimisho ... 246

7.2 Mapendekezo ... 253

7.3 Mchango wa Utafiti ... 254

**MAREJELEO ... 255**

## ORODHA YA MAJEDWALI

1.1 Utokeaji wa vijenzi vya Mshikamano wa Kisarufi katika matini 12
1.2 Utokeaji wa vijenzi vya Mshikamano wa Kisarufi kwa jumla 13
2.1 Aina za Uunganishaji 108
3.1 Utokeaji wa Urejeleaji katika matini 114
3.2 Idadi ya utokeaji wa mrejeonje na mrejeondani 120
3.3 Idadi ya utokeaji wa mrejeombele na mrejeosabiki 123
3.4 Utokeaji wa Urejeleaji kwa asilimia (100%) 124
3.5 Utokeaji wa aina za Urejeleaji 129
4.1 Ubadilishaji katika daraja mbalimbali za sentensi 151
4.2 Jumla ya Ubadilishaji kwa asilimia (100%) 152
4.3 Muhtasari wa utokeaji wa vibadala 165
5.1 Udondoshaji katika matini 168
5.2 Aina za Udondoshaji zinavyotokea 169
6.1 Utokeaji wa aina za Uunganishaji 199
6.2 Muhtasari wa idadi ya utokeaji wa viunganishi 200
6.3 Utokeaji wa viunganishi mahususi katika matini 202

## FAHARASA

| | |
|---|---|
| Ala | Device |
| Dhania | Presuppose |
| Elementi kando | Marginal element |
| Elementi kiini | Nucleus element |
| Kiini | Head |
| Kionyeshi bainishi | Demonstrative article |
| Kionyeshi husika | Locative demonstrative |
| Kisabiki | Antecedent |
| Kishikanishi | Tie |
| Kisifa | Modifier/ qualifier |
| Kisifa-nusu | Submodifier |
| Kivumishanomino | Epithet |
| Maana rejelewa | Referential meaning |
| Mfungamano | Coherence |
| Mlinganuo | Contrast |
| Matini ya nje | Surface text |
| Mrejeombele | Cataphora |
| Mrejeondani | Endophora |
| Mrejeonje | Exophora |
| Mrejeosabiki | Anaphora |
| Mshikamano wa kinsitaksia | Syntactic cohesion |

| | |
|---|---|
| Mshikamano wa udondoshaji | Elliptical cohesion |
| Neno kisonde | Deictic word |
| Ubadilishaji kapa | Zero substitution |
| Udondoshaji wa kimuktadha | Contextual ellipsis |
| Uunganishaji | Conjuction/Coodination |
| Urejeleaji | Reference |
| Urejeleaji bainishi | Deictic reference |
| Urejeleaji linganishi | Comperative reference |
| Urejeleaji linganishi jumla | General comperative reference |
| Urejeleaji linganishi mahususi | Specific comperative reference |
| Urejeleaji nafsi | Personal reference |
| Urejeleaji onyeshi | Demonstrative reference |
| Vielezi onyeshi | Demonstrative adverbs |
| Vifuasi | Constituents |

## VIFUPISHO

N-----Nomino

KN---Kirai Nomino

T------Kitenzi

KT---Kirai Kitenzi

CH----Chagizo

KE---Kirai Elezi

V----Kivumishi

KV----Kirai Vumishi

KH---Kirai Husishi

**SHUKURANI**

Natoa shukurani zangu kwa wale wote walionisaidia, moja kwa moja ama kwa njia nyingine, kufanikisha kazi hii. Natoa shukurani kwa Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret kwa kunipa fursa ya kusoma na kukamilisha kazi hii. Aidha shukurani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Profesa Naomi Shitemi na Profesa Nathan Oyori Ogechi kwa kunisimamia na kunihamasisha kukamilisha kazi hii. Kweli hakuna safari isiyokuwa na mwisho, na leo safari nimeikamilisha. Ingawa walikuwa na shughuli nyingi za kiakademia na utawala, waliweza kutenga wasaa wa kupitia kazi hii na kunielekeza ipasavyo. Ahsanteni sana!

Shukurani zangu zingine za dhati zimwendee mke wangu Zainabu Mkambe na watoto wangu wote kwa kuvumilia kukosa ukaribu wangu na mtagusano nao wa mara kwa mara kwa sababu ya kazi hii. Nataka wafahamu ya kuwa mvumilivu hula mbivu.

Nawashukuru wahadhiri wenzangu walio na usuhuba nami kwa kunihimiza kila mara nikamilishe kazi hii. Hawa ni Dkt Issa Yusuf Mwamzandi (*Mtsedza*), Dkt Mohammed Mraja na Dkt. Balozi Chirongo. Msukumo wao ulinihamasisha na nikajizatiti kumaliza kazi hii. Dkt Mwamzandi namshukuru kwa kuchukua ari ya kibinafsi kuhakikisha kuwa nimekamilisha kazi yangu kwa kunikumbusha daima kuwa nisikate tamaa kwani masomo ni jitihada. Dkt Mraja naye namshukuru kwa kunisaidia kiufundi katika matumizi ya tarakilishi nilipokuwa nimekwama nikiandika tasnifu hii. Kwa kweli alijitolea nilipomuhitaji kwa maelekezo ya kiufundi na kitaaluma.

Tamati, naishukuru sana Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi, kwa kunilea, kunikuza kitaaluma na kunipa elimu hii ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Moi, kwangu mimi ni 'mama yangu' wa kitaaluma katika bahari pana ya kiakademia. Ikumbukwe kuwa titi la mama litamu ingawa la mbwa.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Swala la Utafiti

Mshikamano ni dhana ya kisemantiki, na hurejelea uhusiano wa maana iliyopo katika matini (Halliday na Hassan, 1976:4). Hii ni hali ya vipashio fulani (katika sentensi au matini) kukaa pamoja kwa uimara (*Kamusi ya Isimu na Lugha*, 1990). Aidha mshikamano ni dhana inayorejelea hususan jinsi sentensi, katika maongezi au maandishi, hushikamana pamoja kuunda matini inayoleta maana (Finch, 2000:210). Ili matini, yoyote, kuwa na maana na kueleweka na wasomaji, lazima iwe na mshikamano. Mshikamano hujitokeza katika sentensi ambazo hujenga matini zilizo na mshikamano. Matini hizi ni taarifa zilizo na zaidi ya sentensi moja. Riwaya zilizoteuliwa mahususi kwa minajili ya utafiti huu ni matini. Kuna mshikamano wa kisarufi na wa kileksia.

Mshikamano huelezwa kama seti za uwezekano, zile zilizomo katika lugha ili kufanya matini kushikamana: uwezo ambao mzungumzaji au mwandishi anao na kuweza kuutumia. Hii ni dhana ya kuhusisha, na mwongozo huja ikiwa tu elementi mojawapo katika matini hubeba mshikamano wa uhusiano ambapo moja kwa kawaida hufuata nyingine (Halliday, 1985:18-19). Hurejelea uhusiano uliopo katika matini na hutokea pale ambapo ufasiri wa elementi fulani katika usemi hutegemea ule wa elementi nyingine. Elementi moja hudhania ile nyingine iliyotangulia ili kupata maana (Halliday na Hassan, 1976:4). Katika elementi hizi mbili zinazobeba mshikamano wa uhusiano,

moja kwa kawaida, hufuata nyingine. Kwenye matini aghalabu elementi ya pili hutegemea ufafanuzi wake kutoka ile inayotokea mwanzoni (Halliday, 1985:18-19). Kwa hivyo mshikamano kama mwendelezo, hujumuisha sehemu moja kurejelea nyingine; ambapo sifa muhimu ya uhusiano wa mshikamano ni kwamba sehemu moja hutoa ufafanuzi wa sehemu nyingine. Uhusiano huu huweza kujumuisha elementi za mawanda yoyote, elementi ndogo na kubwa kuliko vishazi, na huweza kutokea katika mapengo ya mawanda yoyote, katika kishazi na zaidi ya vishazi.

Naye Barongo (1996:1) anaeleza kuwa neno 'ushikamano' linarejelea ile hali ya kutegemeana kati ya vipashio mbalimbali vya lugha kwa madhumuni ya kufasiriwa kama matini moja kamilifu. Kutegemeana ndilo jambo kuu katika mshikamano kwani kipashio kimoja katika matini lazima kitegemee kingine ili kuleta mshikamano na umoja unaoleta maana kamili na kueleweka.

Katika matini, vishazi huwekwa pamoja na hutokea kimoja baada ya kingine.Vishazi hivi hushikamana katika kawaida ya muundo wa kisarufi. Vishazi changamano ni muhimu katika kutoa maana. Ili kufanya hivyo ni lazima tuongeze elementi za mawanda yoyote, kubwa na ndogo kuliko vishazi, kutoka neno moja hadi makala ndefu kama matini, ambazo zinaweza kudhibiti mapengo ya aina yoyote. Elementi zote zikiwa katika kishazi na zaidi ya kishazi bila kujali kile kinachojitokeza kati. Hii haiwezi kupatikana kutoka kwa muundo wa kisarufi bali hutegemea asili za aina nyingine. Asili hizi ni zile za usemi zisizo na muundo na ndizo hujulikana kama mshikamano (Halliday, 1985:288).

Kwa hivyo mshikamano kama mchakato hujumuisha sehemu moja kurejelea nyengine; ambapo sifa muhimu ya uhusiano wa mshikamano ni kuwa sehemu moja hutoa asili ya ufafanuzi wa sehemu nyingine.Yaani elementi moja haiwezi kufafanuliwa bila kurejelea nyingine katika matini, ama imetangulia au itafuata baadaye. Ikiwa jambo hili litatokea, basi mshikamano utakuwepo katika matini.

Sentensi huungana ili kuunda matini. Uhusiano kati ya sentensi hizo ni kipengele cha mshikamano wa kisarufi (Coulthard, 1977:10). Mshikamano huelezwa kwa kupitia sarufi na pia kupitia leksia. Kwa hivyo, kuna mshikamano wa kisarufi na ule wa kileksia na hupatikana katika matini. Mshikamano huu wa kisarufi hujengwa na vipengele vifuatavyo; urejeleaji, ubadilishaji na udondoshaji, na uunganishaji. Hivi ndivyo kama gundi, ambayo hushikanisha sehemu tofauti za matini na kuifanya iwe na mfungamano (Salkie, 1995: X). Ufungamano huu huifanya matini kuwa na mtiririko na maana na hutokea wakati elementi za taarifa zaonekana zikiunganishwa, na au bila viunganishi vya kiisimu kati yao (Brown na Yule, 1983:224).

Vipengele vya mshikamano wa kileksia ni uteuzi kimantiki wa maneno, urudufishaji wa maneno, visawe, antonimu na maneno yanayohusiana (Halliday na Ruqaiya, 1976: 5-6, Salkie, 1985). Mshikamano ni sehemu ya mfumo wa lugha na lugha yenyewe ndiyo hutawala vijenzi hivyo vya mshikamano, na una umuhimu mkubwa katika kuifanya matini ieleweke na wasomaji. Vijenzi hivyo hutegemeana katika hali na sheria za kisarufi, na kwamba mshikamano hutegemea sarufi (Beaugrande na Wolfgang, 1981:3). Hivyo tulichunguza pia ikiwa vijenzi hivi, kwa mujibu wa sarufi ya Kiswahili vinaweza

kutokea popote katika sentensi na mshikamano ukabakia na maana isipotoke na sarufi sahihi kudumishwa.

Utafiti huu kwa hivyo ulichunguza mshikamano wa kisarufi katika matini teule za Kiswahili za riwaya. Ulichunguza vile mshikamano wa kisarufi kupitia vijenzi vyake unajitokeza na kuchangia ufungamano katika matini.

## 1.2 Swala la Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza mshikamano wa kisarufi katika matini za Kiswahili. Ulichunguza vile urejeleaji, udondoshaji, ubadilishaji na uunganishaji hutumika katika matini ili kuleta mshikamano. Matini teule za Kiswahili zilitumika katika utafiti huu, nazo ni *Watoto wa Maman'tilie* (Mbogo, 2002) na *Musaleo!* (Wamitila, 2004).Vile vile ulichunguza ni sehemu gani vijenzi hivi vya mshikamano hutokea na kutumika katika matini na kuifanya iwe na mfungamano na kukubalika katika sarufi ya Kiswahili. Kisha ulitalii na kuchunguza kama vijenzi hivi hutokea tu katika hali mahususi au la, na mshikamano bado udumishwe katika matini. Ili kufikia mshikamano huu, vijenzi vya urejeleaji, ubadilishaji, udondoshaji na uunganishaji hutumika pamoja na mshikamano wa kileksia (Kama hapo juu: 4).

Utafiti huu ulichunguza mshikamano unaoletwa na urejeleaji, ubadilishaji, udondoshaji na uunganishaji katika matini teule za Kiswahili. Mshikamano unaoletwa na vijenzi hivi ndio huitwa mshikamano wa kisarufi.

Matini lazima iandikwe kwa njia ambayo inakubalika kisarufi katika lugha husika na wakati huo huo iwe na mshikamano ili ieleweke na kuwa kazi nzuri ya kisanaa. Matini huwa matini ikiwa kuna uhusiano wa mshikamano katika sentensi na kati ya sentensi unaozalisha umoja wa jumla. Umoja huu ndio hupambanua matini na maandishi yasiyo matini. Umoja huu huletwa na mshikamano wa kuhusiana ambapo ufafanuzi wa elementi fulani hutegemea elementi nyingine.

Urejeleaji, udondoshaji, ubadilishaji na uunganishaji ambavyo ni vijenzi vya mshikamano wa kisarufi vilichunguzwa katika kiwango cha neno, kikundi, kishazi na sentensi kwenye matini. Katika mchakato huo mtafiti alimulika hali na sehemu ambazo vijenzi hivi vinaweza kutumika na pale ambapo haviwezi iwapo sheria za sarufi ya Kiswahili zitakiukwa na kusababisha kuharibika kwa mshikamano katika matini. Vijenzi hivi vinne vilichunguzwa jinsi vilivyotumika kufikia mshikamano katika matini za Kiswahili. Vilichunguzwa jinsi vinavyojitokeza katika neno, kikundi, kishazi na sentensi. Mathalan, urejeleaji hujitokeza vipi kwa kurejelea neno, kikundi, kishazi na sentensi. Utafiti ulifuata mkondo huo huo kwa vijenzi hivyo vingine. Ni kijenzi kipi hutokea zaidi katika matini hizi na kipi hutumika kwa uchache zaidi, ni mambo ambayo yalichunguzwa.

Vijenzi hivi vya mshikamano vilichunguzwa na kufafanuliwa kwa kuzingatia matini zilizoteuliwa pamoja na vikwazo vinavyoibuka katika matumizi yake ya kuleta mshikamano katika matini za Kiswahili.

Vijenzi hivi vina vikwazo katika matumizi yake iwapo vitaleta mshikamano katika matini. Utafiti uliangalia vikwazo hivi vinatokea vipi katika matini za Kiswahili zilizoteuliwa. Aidha ulionyesha athari za kuvipuuza katika kujenga mshikamano wa matini.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Azma kuu ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza mshikamano wa kisarufi katika Kiswahili. Utafiti ulitumia matini za riwaya mbili za Kiswahili katika uchunguzi wake. Utafiti huu una malengo yafuatayo;

1.3.1 Kuchunguza jinsi urejeleaji, ubadilishaji, udondoshaji na uunganishaji hujitokeza katika matini za Kiswahili na jinsi vijenzi hivi vinachangia mshikamano.

1.3.2 Kubainisha ikiwa vijenzi hivi vya mshikamano wa kisarufi hutokea tu katika sehemu mahususi katika matini.

1.3.3 Kuchunguza iwapo mshikamano na sarufi sahihi katika matini za Kiswahili hudumishwa wakati vijenzi hivyo vinatumiwa katika daraja zozote za sentensi.

1.3.4 Kuchunguza na kubainisha ikiwa kuna vikwazo katika matumizi ya vijenzi hivi vya mshikamano wa kisarufi.

## 1.4 Nadharia-Tete

Utafiti huu uliazimia kupima nadharia-tete zifuatazo:

1.4.1 Urejeleaji, ubadilishaji, udondoshaji na uunganishaji unaweza kutokea katika viwango mbalimbali katika sentensi kwenye matini kwa kuleta mshikamano wa kisarufi.

1.4.2 Vijenzi vya mshikamano wa kisarufi katika Kiswahili hutokea tu katika hali na sehemu mahususi katika matini.

1.4.3 Vijenzi vya mshikamano haviathiri usahihi wa kisarufi hata vikitumika popote katika muundo wa sentensi.

1.4.4 Kuna vikwazo kadha katika matumizi ya vijenzi vya mshikamano wa kisarufi katika matini ili mshikamano na ufungamano kupatikana katika matini.

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti wa lugha yoyote unaendelea kwani lugha hukua na Kiswahili ni mojawapo ya lugha ulimwenguni. Hivyo bado kuna vipengele vingi vya kiisimu vya lugha ya Kiswahili ambavyo havijafanyiwa utafiti. Ingawaje lugha hii ina umuhimu mkubwa katika Afrika Mashariki na Kati na ulimwenguni kwa jumla, bado utafiti wa kutosha wa isimu yake haujafanywa (Chimera, 2000, Munyua, 1992). Kama tujuavyo lugha hukua kila wakati na kuzaa mambo mapya ambayo yanahitaji kutafitiwa. Kwa hivyo utafiti huu ulichunguza kipengele cha mshikamano wa kisarufi katika matini za Kiswahili kwani hakijafanyiwa utafiti kama kipengele peke. Tafiti zilizopo ni za mshikamano kwa jumla, kwa mfano utafiti wa Barongo (1996).

Utafiti linganishi ulifanywa na Mohamed (1986) kuhusu kipengele cha udondoshaji katika Kiswahili na Kiingereza, na Contini (1985) aliandika makala inayozungumzia mshikamano wa masimulizi katika simulizi za Kiswahili. Alichunguza uteuzi wa viwakilishi vya wakati uliopita; LI, KA na KU katika masimulizi hayo. Kwa hivyo, ipo haja ya utafiti zaidi juu ya mshikamano katika Kiswahili.

Pia niliona haja ya kutafiti mshikamano katika matini za Kiswahili kama Munyua (1992:221) anavyodai na kupendekeza katika utafiti wake wa 'Uwakilishaji wa Nomino katika Kiswahili'. Anasema na anaamini kwamba mshikamano katika usemi, hususan usemi wa Kiswahili, hautegemei tu uwakilishaji lakini pia, kama ilivyoonyeshwa awali unategemea vipengee vingine kama vile uunganishaji, uwakilishaji, udondoshaji na kadhalika. Kwa mintarafu hiyo, utafiti huu ulichukua jukumu hilo la kutafitia vipengele hivyo ili kujua ni jinsi gani huleta mshikamano katika matini za Kiswahili..

Utafiti huu, kwa hivyo, ulidhamiria kutoa ufafanuzi na maelezo zaidi juu ya jinsi mshikamano wa kisarufi unavyojitokeza katika matini teule za Kiswahili na vikwazo vinavyopatikana ndani yake. Wengi wa wasomaji, wandishi na watafiti katika uwanja wa mshikamano watanufaika. Walimu na wanafunzi wa shule za upili watanufaika katika ufundishaji na uandishi wa insha bora.

Pia ulifafanua vikwazo vilivyopo vya matumizi ya vijenzi hivyo katika mshikamano wa matini za Kiswahili. Aidha ulisaidia kuchanganua dhana ya Halliday na Hassan (1976) ya mshikamano katika matini za Kiswahili. Ulionyesha vile dhana hii ina vikwazo katika Kiswahili katika matumizi yake kwani Halliday na Hassan waliitumia katika matini za Kiingereza na si Kiswahili.

## 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulijishughulisha tu na mshikamano wa kisarufi katika matini za Kiswahili zilizoteuliwa kimakusudi. Matini hizo ni riwaya za *Watoto wa Maman'tilie* (Mbogo) na *Musaleo!* (Wamitila). Riwaya hizi ziliteuliwa kwa sababu zilichapishwa katika karne hii

ya ishirini na moja. Isitoshe, ni za waandishi wa kutoka nchi mbili tofauti. Uteuzi wao ulitilia maanani kuwa lugha hukua kwa hivyo matumizi ya lugha katika riwaya hizi ni ya hivi punde. Pia ulijikita tu katika vijenzi vya mshikamano wa kisarufi katika matini hizo teule ambavyo ni urejeleaji, ubadilishaji, udondoshaji na uunganishaji. Utafiti ulichunguza jinsi vijenzi hivi vinatumika katika matini zilizoteuliwa kuleta mshikamano na mfungamano bila sarufi ya Kiswahili kupotoka. Uliangazia jinsi vipengele hivi hujitokeza katika daraja mbalimbali za sentensi zilizomo katika matini.

Ingawaje matini zilizoteuliwa ni kazi ya sanaa, hivyo lugha ni ya kisanii, utafiti huu haukujishughulisha na usanii huo bali mshikamano wa kisarufi katika matini hizo. Lugha yoyote ile, iwe ya kisanaa au ya kawaida lazima iwe na mshikamano kwa minajili ya kuleta maana na kueleweka kwa wasomaji au wasikilizaji. Aidha mshikamano wa kileksia haukushughulikiwa katika utafiti huu kwani uko nje ya mada yetu.

Pia vikwazo vilivyoibuka katika matumizi ya vipengele vya mshikamano wa kisarufi vilijadiliwa katika utafiti huu. Ufafanuzi ulifanywa juu ya vikwazo hivyo na sababu za kuwepo katika Kiswahili. Vile vile kwa kiwango kikubwa, utafiti huu ulijikita maktabani. Nje ya maktaba kulitumika tu ilipobidi katika mijadala kwa ufafanuzi zaidi juu ya sentensi za Kiswahili kwenye matini.

Sisi katika utafiti huu tunashikilia tu nadharia ya Halliday na Hassan inayodai kuwa ili mshikamano uweko lazima kuwe na habari inayodhaniwa au iliyotangulia ambayo inarejelewa. Kigezo cha habari au neno lililotangulia katika matini na jinsi

zinavyoshikanishwa na habari au maneno mengine, ndicho kitakuwa msingi wetu wa kujadili mshikamano.

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza vijenzi vya mshikamano wa kisarufi tu katika matini teule za Kiswahili. Uliangalia jinsi vijenzi hivi vinavyojitokeza kuunda mshikamano huo katika matini hizo. Pia, uliangazia vikwazo vilivyomo katika matini hizo wakati vijenzi hivyo vinatumika. Kwa hivyo, utafiti huu uko tofauti na tafiti tulizozitaja. Hata hivyo, utafiti huu ulirejelea tafiti tulizozitaja katika uchunguzi wake, na zilisaidia katika ufafanuzi na uchanganuzi wa mshikamano wa kisarufi na vikwazo vinavyopatikana katika matini za Kiswahili.

Hata hivyo utafiti huu ulikumbwa na matatizo kama utafiti wowote ule. Tatizo kubwa lilikuwa kupata maandishi ya kitaaluma ya Kiswahili juu ya mshikamano. Maandishi yalikuwa katika Kiingereza na mifano yote iliyotolewa ilitoka katika lugha ya Kiingereza. Mtafiti alilazimika kutafuta istilahi kwa lugha ya Kiswahili kusimamia istilahi za Kiingereza katika mshikamano. Maandishi juu ya mshikamano ama mshikamano katika Kiswahili yalikuwa haba sana. Na yale ya Kiingereza, machache sana yalizungumzia mshikamano kwa jumla, mfano maandishi ya Halliday na Hassan, na maandishi ya Salkie. Mengi yalizungumzia ama kipengele kimoja tu au viwili.

## 1.7 Mbinu za Utafiti na Uchanganuzi wa Data

### 1.7.I Utafiti Maktabani

Utafiti huu ulijikita makitabani na midahalo iliyotumika kufafanua sarufi ya Kiswahili ilipobidi. Mtafiti alipitia maandishi yaliyozungumzia mshikamano aliyoyapata katika

maktaba ya Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Chuo Kikuu cha Nairobi na Maktaba ya Umma, Mombasa. Matini mbili za riwaya zilitumika katika kukusanya data juu ya mshikamano wa kisarufi katika Kiswahili. Riwaya za Kiswahili zilizoteuliwa ndizo zilikuwa matini zilizotumika katika utafiti huu. Riwaya hizo ziliteuliwa kimakusudi kutoka waandishi wa Kenya na Tanzania, Kyalo Wamitia na Emmanuel Mbogo mtawalia. Tena waandishi hawa ni wazungumzaji wa Kiswahili na wameandika riwaya zaidi ya moja kila mmoja wao. Matini hizi ndizo zilizotumika kutoa data juu ya vijenzi vya mshikamano wa kisarufi. Maandishi ya watalaamu mbalimbali walioandika juu ya mshikamano kwa jumla, na baadhi walioandika juu ya kijenzi kimojawapo, sarufi yalipitiwa na kukusanya maoni yao katika daftari. Baadaye maoni haya yalichanganuliwa na kusaidia katika utafiti huu.

Mijadala mbalimbali ilifanywa na wanafunzi, wahadhiri na watalamu wa lugha ya Kiswahili katika Chuo cha Moi, Eldoret, Kenya na mjini Mombasa kuchunguza na kuthibitisha kama matumizi yaliyotumika katika matini yanakubalika kisarufi katika sentensi za Kiswahili.

Data ilikusanywa kwa kuzitalii matini na kuchanganua vijenzi vya mshikamano wa kisarufi kama vilivyotumika katika matini kwa kupitia kila ukurasa katika matini zote. Kwa hivyo kurasa tisini na tisa katika matini ya *Watoto wa Mama N'tilie* (98) na kurasa mia moja na mbili (102) katika matini ya *Musaleo!* zilipitiwa. Data ilirekodiwa katika daftari ikionyesha utokeaji wa kila kijenzi katika matini zote mbili na kuchanganuliwa kitakwimu..

### 1.7.2 Uchanganuzi wa Data

Data iliyopatikana katika utafiti huu ilipimwa kwa utokeaji, ulinganishaji, kukadiria au wastani na asili mia. Kila kijenzi kiliwekwa kwenye jedwali kuonyesha ni mara ngapi kimetumika katika matini zilizoteuliwa. Hii ilitusaidia kujua ni kijenzi au vijenzi vipi vya mshikamano vinatumika zaidi na vipi vinatumika kwa uchache katika matini hizi za Kiswahili. Vile vile ilidhihirisha tofauti ya matumizi ya vijenzi vya mshikamano wa kisarufi katika waandishi E. Mbogo na K. Wamitila. Hivyo kutuwezesha kutoa kauli na mapendekezo yetu. Pia tulifafanua utata wowote au vikwazo vilivyojitokeza katika matumizi ya vijenzi hivi. Hii ilitusaidia kutambua vijenzi vyenye utata katika matumizi kwenye matini teule. Data yetu kwa hivyo ilipima kitakwimu vijenzi vinavyojitokeza zaidi katika matini za Kiswahili na ikwazo vyake. Muhtasari wa vijenzi jinsi vilivyotokea unaonyeshwa katika Jedwali 1.1 na 1.2. Ufafanuzi na uchanganuzi zaidi umeshughulikiwa katika sura za tatu, nne, tano na sita za tasnifu hii.

| VIJENZI | UTOKEAJI % | |
|---|---|---|
| | *Watoto wa Mama N'tilie* | *Musaleo!* |
| Urejeleaji | 30.15 | 69.85 |
| Ubadilishaji | 40 | 60 |
| Udondoshaji | 57.1 | 42.9 |
| Uunganishaji | 33.8 | 66.2 |

JEDWALI 1.1 UTOKEAJI WA VIJENZI VYA MSHIKAMANO WA KISARUFI KATIKA *Watoto wa Mama N'tilie* NA *Musaleo!*

| VIJENZI | UTOKEAJI KWA JUMLA % |
|---|---|
| | *Watoto wa MamaN'tilie* na *Musaleo!* |
| Urejeleaji | 92.70 |
| Ubadilishaji | 0.11 |
| Udondoshaji | 0.84 |
| Uunganishaji | 6.35 |

JEDWALI 1.2 UTOKEAJI WA VIJENZI VYA MSHIKAMANO WA KISARUFI KATIKA MATINI KWA JUMLA

## 1.8 Ufafanuzi wa Dhana Kuu

### 1.8.1 Mshikamano wa kisarufi

Mshikamano wa kisarufi ni ile hali ya kushikana kwa sentensi katika matini kupitia vijenzi vya urejeleaji, udondoshaji, ubadilishaji na uunganishaji wa elementi mbalimbali katika matini ili kuleta muwala na maana.

### 1.8.2 Matini

Matini ni maandishi ambayo ni zaidi ya sentensi moja yanayojenga mfungamano. Ni riwaya zilizoteuliwa mahususi kwa minajili ya utafiti huu, nazo ni *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*

### 1.8.3 Vijenzi

Istilahi hii imetumika kwa zile ala mbalimbali zitumikazo katika kuleta mshikamano kwenye matini. Utafiti ulitumia istilahi ya vijenzi kwa kurejelea dhana za urejeleaji, udondoshaji, ubadilishaji na uunganishaji kwa kuwa ndizo hujenga mshikamano wa kisarufi.

### 1.8.4 Dhana

Ni wazo ambalo linajitokeza katika virai au vishazi au sentensi. Mawazo haya ndiyo hudhaniwa, hurejelewa, hudondoshwa, huunganishwa au huwekewa vibadala kwa madhumuni ya kuleta mshikamano wa kisarufi katika matini.

### 1.8.5 Dhana-dhaniwa

Ni wazo ambalo linarejelewa katika kishazi au sentensi fuatilizi katika matini.

### 1.8.6 Kirejelewa

Kirejelewa ni elementi katika sentensi au matini ambayo imerejelewa na kiwakilishi.

### 1.8.7 Kirejelea

Kirejelea ni elementi ambayo inarejelea kirejelewa katika sentensi au matini.

### 1.8.8 Kibadala

Ni neno linalosimama badala ya kitenzi au nomino au dhana katika matini.

### 1.8.9 Kidondoshwa

Ni nomino au kitenzi au kirai au kishazi au sentensi au msururu wa sentensi uliodondoshwa katika matini.

# SURA YA PILI

# DHANA YA MSHIKAMANO NA YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inajadili na kufafanua dhana ya mshikamano kwa jumla ambayo ndiyo dhana inayoongoza utafiti wetu. Dhana hii ni kwa mujibu wa Halliday na Hassan (1976) kama walivyoijadili na kuifafanua katika kitabu chao *Cohesion in English*. Imejadili mshikamano wa kisarufi katika matini na jinsi unavyojengwa na vijenzi vyake; urejeleaji, ubadilishaji, udondoshaji na uunganishaji. Vile vile inaonyesha mapito mbalimbali ya waandishi tofauti tofauti yaliyozungumzia mshikamano ama kwa jumla au baadhi ya vipengele vyake na vijenzi vinavyoleta mshikamano wa kisarufi. Haya yote yaliangaziwa na kudadisiwa katika sura hii.

## 2.1 Dhana ya Mshikamano

Utafiti huu uliongozwa na dhana ya Mshikamano ya Halliday na Hassan (1976). Hata hivyo mawazo ya wataalamu wengine walioelezea mshikamano yalitumika kujenga zaidi dhana hii. Halliday na Hassan (1976:4) wanadai kwamba dhana ya mshikamano ni ya kisemantiki na hurejelea uhusiano wa maana ndani ya matini fulani na kwamba mshikamano hutokea pale ambapo ufafanuzi wa elementi moja katika matini hutegemea ile nyengine. Dhana hii hujishughulisha na kipengele cha matini kinachobeba maana katika lugha. Matini huweza kuwa neno moja au sentensi moja au msururu wa sentensi, na sentensi hizi ziwe zimeunganishwa kimaana kwa utaalamu mkubwa ili kuwasilisha

wazo kamili. Katika utafiti huu matini ilichukuliwa kama mkururo wa sentensi zilizounganishwa kimaana na kujenga matini.

Muungano huu wa sentensi husababisha umoja na mshikamano katika maandishi au mazungumzo. Mshikamano ni dhana ya kisemantiki inayowakilisha uhusiano wa kimaana uliopo katika maandishi au mazungumzo. Uhusiano huu ni wa kisemantiki baina ya faridi moja na nyengine katika matini moja. Vijenzi vya mshikamano hutumika kuunganisha sentensi hizo katika matini kwa minajili ya kuepukana na urudufishaji ambao ukitumiwa sana, huharibu ule utamu wa lugha na sarufi wakati mwingine. Hivyo urejeleaji, udondoshaji, ubadilishaji na uunganishaji hutumika ili kukwepa urudufishaji huo na kuleta mshikamano wa kisarufi katika matini.

Halliday na Hassan (1976: 6) wanaeleza kwamba kuna mshikamano ndani ya sentensi ambapo vipengele mbalimbali vinavyoiunda sentensi vinashirikiana kwa ukubalifu ili kuunda sentensi inayokubalika kisarufi. Kuna mshikamano baina ya sentensi na sentensi, ambapo kiungo cha mshikamano huundwa na faridi mbili kila mojawapo ikiwa katika sentensi tofauti. Faridi hizi huunganisha sentensi kisemantiki. Pia kuna mshikamano baina ya kirai na kirai, kishazi na kishazi.

Barongo (1996:15) anadai mshikamano wa aina hii ni muhimu katika lugha ya Kiswahili ambayo uwiano wa kisarufi katika sentensi na baina ya sentensi ni kipengele kinachotawala lugha hii. Pia Halliday na Hassan (1976:9) wanashadidia hoja hii,

ingawaje walijadili Kiingereza, kwamba mshikamano katika mkururo wa sentensi hujitokeza wazi kwa sababu ndio asili pekee ya muwala.

### 2.1.1 Urejeleaji

Urejeleaji ni kijenzi kimojawapo cha mshikamano. Ni ile hali ya kuwa msomaji wa matini inambidi arejelee elementi nyingine katika matini ili kupata mshikamano wa sentensi au matini hiyo na kuleta maana na kueleweka. Barongo (1996: 20-21) anaeleza kwamba urejeleaji ni uhusiano wa kisemantii baina ya sehemu mbalimbali zinazoiunda matini. Hapa, maumbo fulani ya lugha hutumiwa kurejelea faridi fulani za kiismu ambazo ama hutokea mwanzoni mwa matini au baadaye. Maumbo haya hayawezi kutafsiriwa bila ya kurejelewa katika faridi hizi. Hii inamaanisha kuwa faridi hizo husimamiwa na virejelea vinavyowakilisha maumbo hayo.

Urejeleaji huwa na vitambulishi vyake. Vionyeshi vya urejeleaji huwa viwakilishi na pia huwa vionyeshi au viashiria. Urejeleaji katika Kiswahili unadhihirika kupitia kwa matumizi ya viwakilishi nafsi na vimilikishi, vivumishi vimilikishi, viashiria (vikitumika kama viwakilishi au vivumishi) na vielezi na vivumishi vya ulinganifu (Munyua, 1994:39). Pia virejeshi ni vitambulishi vya urejeleaji katika matini.

1. Kasimu hujigamba kila mara mbele ya wanafunzi wenzake.
   *Yeye* *a*na majivuno sana. Lazima *a*tambue kuwa majivuno
   ha*ya*ta*m*saidia maishani.

Katika matini hii, nomino zinazorejelewa ni mbili, Kasimu na majivuno. *Yeye*, *a-* na *–m-* ni virejelea. *Yeye* kinarejelea Kasimu na *a-* na *–m-* vinarejelea Kasimu, vile vile katika kimilikishi unganifu *a*na, na katika vitenzi *a*tambue na hayata*m*saidia. *Yeye* na *a-* ni

viwakilishi vya nafsi. *–ya-* ni kirejelea cha majivuno. Kwa hivyo hivi vyote ni virejelea vya nomino vinavyochangia mshikamano katika matini hii:

2. Mfanyi biashara hawezi kudhania kwamba kampuni *i*naweza kutatua matatizo *yake* ya uzalishaji. Ikiwa *yeye* hatafanya bidii, basi *i*tazorota. Itakuwaje *sisi tu*angalie tu kampuni *i*kizorota na kudidimiza uchumi wa nchi na kuleta ukosefu wa kazi?

Matini 2 ina virejelea *i-, yake, sisi* na *tu-*. *i-* ni kiwakilishi nafsi kikirejelea kampuni katika vitenzi *i*naweza na *i*kizorota. *yake* ni kimilikishi kirejelea cha Mfanyi biashara na *sisi* ni kiwakilishi nafsi kirejelea cha waashiriwa pamoja na mzungumzaji. Virejelea hivi vimeleta mshikamano wa matini hii.

Kuna aina mbili kuu za urejeleaji; urejeleaji nje na urejeleaji ndani. Urejeleaji nje ya matini huitwa mrejeonje na urejeleaji ndani ya matini huitwa mrejeondani. Mrejeondani hugawika mara mbili, mrejeosabiki na mrejeombele (Brown na Yule, 1983:192; Halliday na Hassan, 1976:4):

3. *Yeye* hakujua mambo siku hiyo yata*mw*endea kombo. Mwichande alikuwa mvuvi hodari. *Wote* walijua hivyo kijijini. Lakini bahari haina uhodari. Siku moja *a*lifika ufuoni kwa kazi yake. *A*kajitia ngalawani na ala zake. *A*sijue kuwa siku zote mambo si shwari.

Katika matini hii, kuna mrejeonje, mrejeondani, mrejeombele na mrejeosabiki. *Yeye* ni kirejelea cha nomino Mwichande. Hivyo ni mrejeombele. *Wote* ni kirejelea cha watu ambao hawapo katika matini, hivyo ni mrejeonje. *a-* katika kitenzi *a*lifika na *A-* katika vitenzi *A*kajitia na *A*sijue ni kirejelea cha Mwichande na ni mrejeosabiki.

Sentensi ni kipashio muhimu katika mshikamano kwa sababu ndicho kipashio kikubwa zaidi katika muundo wa kisarufi. Sentensi hubashiri vile mshikamano utafafanuliwa au utajitokeza. Kwa mfano ikiwa neno limerudiwa mara mbili katika sentensi moja, kuna sheria zinazotawala umbo hili. Hizi ni sheria za uwakilishaji wa nomino. Muundo wa sentensi ndio utakaobashiri kama neno hilo litatajwa tena au kiwakilishi kitatumika badala yake (kama hapo juu: 8):

4. a) *Mwalimu *mwalimu*lichukua kitabu *cha mwalimu mwalimu*kiweka kabatini.

Katika sentensi hii, muundo hauruhusu na haukubaliki. Mshikamano haupo na maana vilevile haipo. Kwa hivyo itabidi viwakilishi vitumike kurejelea nomino *mwalimu* ili ikubalike kisarufi. Hivyo kijenzi cha urejeleaji lazima kitumike, na sentensi yenye muundo sahihi na mshikamano itakuwa:

b) Mwalimu *a*lichukua kitabu *chake a*kakiweka kabatini.

Katika sentensi hii, nomino Mwalimu imewakilishwa na kirejelea *a-* na kitabu cha mwalimu kimewakilishwa na kimilikishi kirejelea *chake*.

Urejeleaji ama uwe mrejeondani au mrejeonje, huwa na mchakato fulani ambao huonyesha virejelea ni vya aina gani. Kwa kuzingatia hili, kuna aina mbalimbali za urejeleaji. Halliday na Hassan (1976:37) wanaainisha aina tatu za urejeleaji;

i) Urejeleaji nafsi

ii) Urejeleaji onyeshi

iii) Urejeleaji linganishi

Hatch (1992:223) pia anaainisha urejeleaji katika viwakilishi nafsi, vionyeshi na vilinganishi. Anasema hivi vyote hutumika katika urejeleaji wa kisarufi. Salkie (1995:66-68) naye hivyo hivyo anaainisha urejeleaji katika aina tatu kama Halliday na Hassan (1976). Halliday (1985) anaainisha urejeleaji kama alivyofanya Halliday na Hassan (1976). Hubbard (2000: 258-259) anadai kuwa elementi za urejeleaji ni:

i) Viwakilishi nafsi ( *mimi, sisi, wewe na yeye*)

ii) Viwakilishi milikishi ( *changu, chake, chako, vyao* n.k)

iii) Vibainishi ( *hiki, kile* n.k)

iv) Vionyeshi vielezi ( *hapa, pale, kule*)

Habbard, kama inavyojitokeza, hana vilinganishi katika maelezo yake. Katika Kiswahili viwakilishi milikishi na vionyeshi hubadilika maumbo kwa mujibu wa ngeli inayorejelewa (Kapinga, 1983, Mbaabu, 1985, Mohamed, 2001).

Tasnifu hii imezingatia uainishaji wa Halliday na Hassan (1976), Halliday (1985), Hatch (1992) na Salkie (1995) kuchunguza urejeleaji unavyojitokeza katika matini za Kiswahili na kuleta mshikamano.

Urejeleaji nafsi hutokea kwa njia ya uamilifu katika hali ya usemi, kupitia katagoria ya nafsi (Halliday na Hassan, 1976:37). Viwakilishi nafsi hutumika katika kurejelea nomino. Pia ni seti fungwa za faridi ambazo hutumika kukaa badala ya nomino au kirai nomino. Viwakilishi hivi huweza kutumika kwa kushikanishwa na baadhi ya nomino katika matini (Mohammed, 2001:108; Hatch, 1992: 224). Maneno yafahamikayo zaidi ya urejeleaji ni viwakilishi nafsi; *mimi*, *yeye*, *sisi*, *wao* na *ki-* (it) pamoja na hali yao ya

umilikishaji; *yako, yetu, yenu* n.k. (Halliday, 1985: 291; Salkie, 1995: 66). Katika Kiswahili, viwakilishi nafsi ni *mimi, yeye, sisi, wao, ki-* pamoja na hali zao za umilikishi (Mohammed, 2001: 108-114; Waihiga, 1999: 18-19, Kapinga, 1983: 108-109).

Pia kuna viambishi viwakilishi vya nomino katika usemi au matini za Kiswahili ambavyo ni virejelea na huchangia kuleta mshikamano katika matini. Mgullu, (1999:104-5) anaeleza,

> "Kiambishi ni istilahi ambayo hutumiwa hasa katika uwanja wa mofolojia kuelezea sehemu mbalimbali za maneno ambazo huongezwa (huambishwa) katika mizizi ya maneno... Viambishi ni mofu ambazo huongezwa kwenye mizizi ya maneno mbalimbali na viambishi hivyo huwakilisha maana fulani."

Kisha akaendelea kuanisha viambishi katika aina tatu;

i) viambishiawali

ii) viambishindani

iii) viambishitamati

Kapinga (1983:15) alieleza kwamba kiambishi ni mofimu inayoambatishwa kwenye mzizi au shina la neno ili kulitambulisha neno lenyewe. Viambishi vya ngeli vinaambatishwa kwenye viini au mashina ya maneno ya fungu moja yakiwa katika upatanisho wa kisarufi. Jina ndilo linaloambatishwa kiambishi chake kwenye maneno mengine.

Kwa hivyo viambishi (viwakilishi) vinavyowakilisha nomino katika usemi ni virejelea nafsi ambavyo huchangia kuleta mshikamano katika matini, na katika tasnifu hii

tumeviita virejelea nafsi. Munyua (1992: ix) anashadidia hoja hii anaposema kwamba imedaiwa uwakilishaji ni ukwasi mmojawapo wa kiisimu unaochangia ushikamano na muwala katika usemi. Hii ni kwa sababu matumizi ya KN (+ uwak.) yanazidi kudumisha KN iliyopatikana katika sentensi ya awali au za awali kwenye usemi unaopanuka hivi kwamba habari za awali zinahusishwa na habari mpya.

Huu ndio urejeleaji ambao huleta mshikamano katika matini. Tasnifu hii itajikita tu katika uwakilishaji ambao unarejelea kitu fulani katika usemi au matini. Kwa hivyo urejeleaji nafsi katika tasnifu hii utachukuliwa ni viwakilishi; ***mimi, yeye, sisi, wao*** na ***ki-*** pamoja na hali yao ya umilikishi na viambishi viwakilishi vya nafsi katika Kiswahili vinavyotegemea ngeli. Navyo ni;

| Ngeli | Viambishi wakilishi vya Kiima |
|---|---|
| M-WA (1) | a- |
| M- WA (2) | wa- |
| M-MI (3) | u- |
| M-MI (4) | i- |
| JI-MA (5) | li- |
| JI-MA (6) | ya- |
| KI-VI (7) | ki- |
| KI-VI (8) | vi- |
| N-N (9) | i- |
| N-N (10) | zi- |
| U-U (11-14) | u- |

| | |
|---|---|
| U-U (11-14) | zi- |
| U-U (11-14) | u- |
| KU (15) | ku- |
| PA (16) | pa- |
| KU (17) | ku- |
| MU (18) | mu- |

Ngeli za Kiswahili na viambishi viwakilishi vya Nomino (Mohammed, 2001:59). Hivi ndivyo virejelea vya nafsi katika tasnifu hii na vitachunguzwa hivyo.

Viwakilishi hivi vinapotumika katika matini, na ni lazima, vinafanya kazi ya urejeleaji. Hivyo vinakuwa faridi ya mshikamano. Na urejeleaji huo ni wa nafsi yaani nomino (KN) ambayo imeshatangulia kutajwa ama ambayo itatajwa mbele katika matini husika au pengine nje ya matini hiyo:

5. ...Nili*wa*karibisha *marafiki zangu* wa karibu watangaze kuwa nita*ya*tembelea *majumba* mbalimbali mtaa mzima siku moja. Kila sehemu ilikuwa, "Makoti anakuja!" "Makoti twamkaribisha." "Sasa hivi anafika!" Hii *i*likuwa *hatua* muhimu ya ku*u*weka *uongozi mzuri* kwa wananchi.

Katika matini hii kuna urejeleaji wa nafsi wa mbele na nyuma. Lakini tutadondoa urejeleaji mbele tu. Urejeleaji huu umetumia viambishi viwakilishi.

a) "*wa*" imerejelea "marafiki zangu".

b) "*ya*" imerejelea "majumba"

c) "*i*" imerejelea "hatua"

d) "*u*" imerejelea "uongozi mzuri"

Hivyo matini hii (5), ina mshikamano na unaleta maana, pia kukubalika kisarufi katika Kiswahili. Iwapo virejelea havingetumika, basi mshikamano na maana haitakuwapo, na kisarufi haikubaliki katika Kiswahili. Hebu tuchunguze matini ya 5 bila virejelea katika matini 6:

6. … Nili(marafiki zangu)karibisha marafiki zangu wa karibu (marafiki zangu)tangaze kuwa nita(majumba)tembelea majumba mbalimbali mtaa mzima siku moja…

Tukiichunguza matini hii (6) tunaipata na utata mwingi na haikubaliki katika Kiswahili. Haina mshikamano na hata kwa mzawa wa Kiswahili atashangaa lugha ilivyotumika. Kwa hivyo ni dhahiri virejelea vina dhima muhimu katika Kiswahili ili kuondoa urudufishaji unaozaa utata na kuleta maana, mshikamano na ukubalifu kisarufi.

Urejeleaji onyeshi ni urejeleaji kwa kutumia vionyeshi. Vionyeshi ni; *hiki, huyu, hii, hivi, hili, kile, wale, vile, lile.* Vionyeshi hivi ni virejelea vya mshikamano na huonyesha nomino au mawazo au dhana fulani. Vionyeshi *hiki, hili, huyu, hawa* n.k huashiria karibu, na *kile, vile, wale, lile* n.k. huashiria mbali. Katika uamilifu wao kwenye mshikamano huweza kutumika na nomino au bila nomino (Salkie, 1995:66-67). Aidha vinaweza kutokea bila nomino hiyo katika sentensi, na msomaji au msikilizaji hurejelea nomino inayoonyeshwa kidhahania.

7. a) Kitabu *hiki* ni kizuri.
   au
   b) *Hiki* ni kizuri.

Katika mfano 7(a) *hiki* imetumika na nomino 'Kitabu' na katika (b) *Hiki* imetumika bila nomino lakini inarejelea nomino au kitu nje ya sentensi hii. Nomino hiyo hurejelewa kidhahania ili kukamilisha maana. Katika Kiswahili vionyeshi hutegemea ngeli ya

nomino inayotumika na maumbo ya virejelea hubadilika kuwiana na nomino hiyo (Mbaabu, 1985; Kapinga, 1983: Mohammed, 2001):Virejelewa hivi hutawaliwa na ngeli ya nomino.

Halliday (1985:291-2) pia anaeleza kuwa vionyeshi ni; *hiki, kile, hivi* na *vile* na huweza kurejelea nje au nyuma. Vionyeshi *hiki* na *hivi* huashiria karibu na kile na vile huashiria mbali kwa mujibu wa mzungumzaji. Pia (*Kama hapo juu*: 294) anaeleza kuwa virejelea husika, *hapa*, na *kule* hutumika kama faridi za urejeleaji na huweza kurejelea mbele au nyuma huku zikitoa dhana ya karibu au mbali. Mzungumzaji hutambua kirejelewa kwa kuwa karibu au mbali nacho. Baadhi ya virejelea hivyo huonyesha dhana ya karibu au mbali (Halliday na Hassan, 1976:57):

| | Karibu | Mbali |
|---|---|---|
| (umoja) | *hiki* | *kile* |
| (wingi) | *hivi* | *vile* |
| (mahali) | *hapa* | *pale* |
| (muda) | *sasa* | *baadaye* |

Walieleza zaidi (*kama hapo juu*; 57-8) kuwa virejelea *hapa, pale, sasa* na *baadaye* ni vielezi ambavyo hufanya kazi ya chagizo (CH) katika kishazi wala si elementi katika KN. (kuanzia sasa tutatumia CH kwa chagizo). Pia hufanya kazi ya pili kama visifa ambavyo huja baada ya kiini. Katika Kiswahili jambo hili huweza kubadilika na kukubalika:

8. a) Yule mtu *pale*.
   b) Mtu yule *pale*.

Virejelea *hiki, hivi, kile* na *vile* huashiria mahali palipo mtu au kitu katika mchakato huo na hutokea kama elementi katika KN. Hivi huwa na uamilifu wa vionyeshi vibainishi:

9. a) *Kile* kiti ni kizuri.
   b) *Hivi* viti ni vizuri.

Hatch (1992:224) anasema kwamba vionyeshi pia ni vishikanishi vya mshikamano na vinaweza kurejelea mbele au nyuma:

10. a) Gari zuri ni lile ambalo halijaendeshwa sana na injini yake ni nzima. Ukitaka kununua gari lazima ujue *hili.*

*hili* ni kionyeshi kinachorejelea 'jambo' ambalo ni juu ya 'gari ambalo halijaendeshwa sana na injini yake ni nzima'. Huu ni mrejeosabiki, na unarejelea sentensi nzima. Kwa hivyo katika matini, ili pawe na mshikamano lazima sentensi iliyotangulia iambatane na sentensi ya pili. Bila hivyo hapana mshikamano. Hivyo hatuwezi kuchunguza mshikamano katika sentensi ya pili pekee bila ya kwanza. (Kuanzia sasa tutatumia virejelea kusimamia vionyeshi):

10. b) Watu wote lazima waamini *haya*$_1$; serikali haipendi ufisadi na uvunjaji sheria nchini. Na atakayethubutu kutenda *haya*$_2$ atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria za nchi.

*haya*$_1$ ni kirejelea kinachorejelea mbele- 'serikali haipendi ufisadi na uvunjaji sheria nchini. Na atakayethubutu kutenda haya atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria za nchi". Inarejelea mawazo yaliyo katika sentensi mbili zilizo mbele yake. Lakini *haya*$_2$ inarejelea nyuma.Virejelea hujitokeza katika wingi na uchache:

11. a) <u>Kiti</u> *hiki* ni kizuri. (umoja) <u>Viti</u> *hivi* ni vizuri. (wingi)
    b) <u>Mtoto</u> *huyu* ni mtundu. (umoja) <u>Watoto</u> *hawa* ni watundu. (wingi)

Virejelea katika mifano hii vimerejelea nyuma, tena nomino moja tu. Maumbo ya virejelea hivi yamebadilika katika hali ya wingi na vimetawaliwa na ngeli ya nomino. Virejelea pia huweza kurejelea kikundi au wazo linaloelezwa na sentensi moja au mkururo wa sentensi:

11. c) Watu wa kijiji hiki wameamua kulima kwa kutumia mbolea. *Hili* litawasaidia kupata mavuno mengi zaidi.

*Hili* inarejelea lile wazo la 'kulima kwa kutumia mbolea' lililoelezwa katika kishazi tegemezi. Pia katika Kiswahili kirejelea kikitumika na nomino, huja baada ya au kabla ya nomino hiyo:

12. a) Mtoto *huyu\yule* au *Huyu\yule* mtoto.
    b) Kiti *hiki\kile* au *Hiki\kile* kiti
    c) Majembe *haya\yale* au *Haya\yale* majembe

Katika mifano hii virejelea vimejitokeza baada na kabla ya nomino au kirejelewa. Virejelea lazima virejelee kirejelewa kilichodhaniwa ili kuleta mshikamano katika matini:

13. a) Omari: Mwizi ameuliwa na wananchi. Alikuwa mwizi sugu kweli. Sasa tutapata afueni hapa kijijini.
    Asha: *Huyu* aliniibia simu yangu ya mkononi wiki jana.

    b) Natoka Eldoret. *Huko* ndiko nilikozaliwa.

Katika 13a) *Huyu* imetumika kama faridi ya urejeleaji na kuleta mshikamano katika matini hii. Kisha imerejelea nyuma *'mwizi aliyeuliwa na sugu'*. Katika 14b) *Huko* inarejelea 'Eldoret'. Kwa hivyo vionyeshi hapa vimedhihirisha kwamba ni faridi za urejeleaji.

Kama tulivyotangulia kueleza, urejeleaji onyeshi hutumia vionyeshi; *hiki, kile, huyu, wale, hii, hivi lile, yale, vile* n.k. Vionyeshi hivi hubadilika umbo kulingana na ngeli husika iwe kwa umoja au wingi:

*ule* (umoja) – *ile* (wingi) Ngeli ya M-Mi

*kile* (umoja) – *vile* (wingi) Ngeli ya Ki-Vi

Hivyo virejelea katika Kiswahili hutawaliwa na ngeli ya nomino itumikayo katika sentensi na KN ndiyo kiini.

Urejeleaji linganishi hutokea wakati pana urejeleaji wa vitu viwili vinavyolinganishwa katika matini. Halliday na Hassan (1976: 37) wanadai kuwa ulinganishi ni urejeleaji usio kuwa wa moja kwa moja kwa njia ya utambuzi au ufanano. Toolan (1998: 26) anaeleza kwamba ulinganishi kama mbinu ya mshikamano inapotumika huleta maana tu iwapo pana mfananisho wa vitu viwili. Yaani kitu kimoja kinalinganishwa na kingine. Akaendelea kueleza kwamba ulinganisho huu hutumia faridi hizi; *sawa, fanana, kama, tofauti na, zaidi, chache kuliko, -ingine na nambari*. Faridi hizi ni vivumishi na vielezi. Hivi tutaviita virejelea linganishi.

Virejelea linganishi huleta uhusiano wa kulinganisha au kufananisha. Virejelea hivi ni; *kama, sawa, nyingine, tofauti na, kubwa kuliko\kama, ndogo kama,* na vielezi *sawa sawa, tofauti, kama hivyo*. Virejelea linganishi vinaweza kutumika katika mrejeombele, kurejelea KN (Halliday, 1985: 294).

14 . a) Juma alibeba *mkubwa zaidi* kuliko mzigo wa Asha.

Katika sentensi hii pana mrejeombele ambapo *mkubwa zaidi* unarejelea 'mzigo' na vile vile kufananisha mizigo miwili, wa Juma na wa Asha. Hata hivyo katika Kiswahili sentensi inayokubalika zaidi ingekuwa;

b) Juma alibeba mzigo mkubwa zaidi kuliko wa Juma.

Au

c) Juma alibeba mzigo mkubwa zaidi kuliko (mzigo) wa Juma.

Katika (b) KN mzigo imetangulia kirejelea linganishi na katika (b) mzigo umetokea mara mbili.Yaani urudufishaji wa neno 'mzigo' katika sentensi hii unakubalika katika Kiswahili. Inapotokea hivi katika (b) urejeleaji ni mrejeosabiki. Kwa hivyo katika Kiswahili urejeleaji linganishi huwa mrejeosabiki.

Salkie (1995:68) anasema kwamba ikiwa vitu viwili au zaidi vinalinganishwa katika matini, basi hii huchangia mshikamano. Toolan (1998: 26) anashadidia kuwa lazima pawe na mfananisho wa vitu ndiposa mshikamano utokee. Hivyo virejelea vyake ni vya kufananisha mfano faridi; *sawa, fanana, kama, tofauti, chache kuliko, kubwa kuliko, ndogo kama* n.k. Kwa hivyo ni wazi kwamba ulinganishi ni njia mojawapo ya kuleta mshikamano katika matini. Urejeleaji linganishi ni wa aina mbili; urejeleaji linganishi jumla na urejeleaji linganishi mahususi. Aina hizi zote zinapatikana katika Kiswahili:

15. Mimi hupenda *bora zaidi*; gari la mbio sana na linalotumia mafuta machache.

*bora zaidi*'inarejelea sifa hizo za gari zilizotolewa katika sehemu ya pili ya sentensi hii. Kama ilivyoelezwa katika 2.3 urejeleaji linganishi hutokea wakati pana urejeleaji wa vitu viwili vinapolinganishwa. Salkie (1995:68) anasema mfananisho huu katika matini mara nyingi huchangia mshikamano. Urejeleaji linganishi unaweza kuwa jumla au mahusuai.

Ulinganishi jumla hutokea wakati vitu viwili vinadhaniwa viko sawa au tofauti bila kuingilia ndani. Huu ni urejeleaji unaolinganisha bila kuangalia sifa fulani. Hulinganisha kwa jumla na huonyeshwa na vivumishi bainishi au vivumisha nomino au vielezi linganishi.Vivumishi hufanya kazi katika KN kama vibainishi au vivumisha nomino. Vielezi hufanya kazi katika kishazi kama chagizo (CH). Hivi huitwa vivumishi vya ulinganishi na vielezi vya ulinganishi ili kuvipambanua na vivumishi linganishi na vielezi linganishi. Urejeleaji linganishi jumla hutumia maneno kama; *sawa na, tofauti na,* n.k. Hapa huwa hakuna sifa mahususi inayokuwa kigezo. Mara nyingi hufafanuliwa na kundi fulani la vivumishi na vielezi. Vivumishi hivi hufanya kazi katika KN na vielezi hufanya kazi ya CH katika kishazi (Halliday na Hassan, 1976: 77).

Urejeleaji linganishi mahususi hutokea wakati vitu viwili vinalinganishwa kwa mujibu wa sifa mahususi. Kimoja kati ya viwili hivyo husemekana kuwa na sifa zaidi au chache kikilinganishwa na kingine (Salkie,1995:68). Urejeleaji huu hulinganisha vitu viwili kwa mujibu wa sifa fulani, inaweza kuwa ya idadi au umadhubuti au ubora. Ikiwa ulinganishi ni wa sifa ya idadi, basi huonyeshwa kwa elementi ya idadi katika KN kwa kutumia kilinganishi kivumishi (KV) kama *zaidi ya* au kielezi (KE) cha ulinganisho kama vile *kuliko, kadri* (Halliday na Hassan, 1976; Salkie, 1995). Ulinganishi huu hudhihirishwa na matumizi ya vivumishi au vielezi vya kawaida katika maumbo fulani ya ulinganishi. Mfano neno *zaidi* hutumika kama hivi; makosa *zaidi,* na kielezi cha ulinganishi *kadri* hutumika hivi: Alifanya *kadri* ya makosa mengi yasiyokubalika.

Ikiwa ulinganishi ni kwa ubora, huonyeshwa kwa njia mbili vile vile;

i) katika elementi ya sifa kwenye KN kwa kutumia kivumishi linganishi au kielezi cha ulinganishi kikivumisha nusu kivumishi. Mfano, a) Hii kazi ni *rahisi zaidi* kuliko ile. b) Alifanya kazi ngumu *kadri* ya uwezo wake.

ii) kama CH katika kishazi kwa kutumia kielezi linganishi au kielezi cha ulinganishi kikivumisha nusu kielezi. Mfano a) Hamisi aliendesha baiskeli kasi *zaidi* ya wengine. b) Fatuma aliimba kwa utamu *kama* Zainabu.

Halliday na Hassan (1976:77) wanasema kuwa ulinganishi mahususi humaanisha ulinganishi kwa kuegemea idadi au ubora. Ulinganishi huu hudhihirishwa kwa kutumia vivumishi au vielezi, si vya aina fulani lakini vivumishi na vielezi vya kawaida katika maumbo fulani ya ulinganishi. Vivumishi hufanya kazi katika KN, lakini si kama vibainishi, bali kama vivumishi vya idadi, mfano *zaidi*, au kama visifa mfano *nzuri/bora zaidi*. Vielezi navyo hufanya kazi kwa njia mbili; ama ni CH katika kishazi au nusu sifa vikijitokeza ndani ya visifa au katika idadi au ndani ya CH.

16. a) Wanafunzi wengine walifaulu *vyema zaidi*.(CH)

b) Baba alileta kadi nzuri *kama hizi*. (ndani ya sifa)

c) Alielezea kwa maneno *mengi mno*. (idadi)

d) Wanafunzi wengi walifanya vibaya *pia*. (ndani ya CH)

Ulinganishi mahususi pia huwa na urejeleaji; lazima pawe na kiwango wastani kubalifu cha kurejelewa ambapo kimoja huweza kuwa bora zaidi, sawa au duni kwa ubora au idadi (*kama hapo juu*:81). Kitu hakiwezi kuwa 'kama' lazima kiwe 'kama kitu fulani au chengine'. Kwa hivyo ulinganishi ni aina ya urejeleaji kama zile nyingine. Kirejelewa

cha urejeleaji huweza kuwa ndani au nje ya matini. Urejeleaji linganishi mahususi unaweza kuwa wa nyuma au mbele (ndani ya matini) au nje ya matini. Kisha wanadai kuwa kati ya faridi zote za urejeleaji, ulinganishi hurejelea zaidi nyuma kuliko nje ( Halliday na Hassan, 1976:78).

Hatch (1992: 224) anasema kwamba vilinganishi pia vinaweza kuwa kiunganishi kwa kirejelewa. Pia anashadidia hoja ya Halliday na Hassan (1976) anaposema kuwa mara nyingi vilinganishi hutumika kwa mrejeosabiki. Si mara nyingi kutumika kwa mrejeombele, lakini wakati mwingine hutumika.

### 2.1.2 Ubadilishaji

Ubadilishaji ni kijenzi mojawapo kinacholeta mshikamano katika matini. Ubadilishaji ni mchakato katika matini ambapo hutokea ubadilishaji wa kipashio kimoja na kuingiza kipashio kingine. Ni uhusiano wa vipashio vya kiisimu, mfano maneno au virai (Halliday na Hassan, 1976:88-89). Kipashio kinachosimamia kingine, tumekiita kibadala.

*Longman Dictionary of Contemporary English* (2001) inaeleza kibadala kama kitu kipya na tofauti, kilichotumiwa badala ya kile kilichotangulia kutumika husについて Kirai Nomino (KN). Hali hii ni kwamba kibadala husimama badala ya KN au Nomino. Hivyo ubadilishaji ni kutumia faridi nyingine mpya na tofauti na ile iliyotumika awali katika matini na isimamie ile faridi iliyotangulia awali.

Ubadilishaji unafanana na udondoshaji na ni njia mbili tofauti za kimuundo. Ubadilishaji ni ile hali ya kudondoa faridi moja katika muundo wa sentensi na pahali pake kuchukuliwa na kibadala. Lakini katika udondoshaji kunaachwa mapengo ya kimuundo ili yajazwe kutoka kwingineko. Kwa hivyo ubadilishaji ni pale ambapo pengo hujazwa na kibadala na udondoshaji huwa pengo la kimuundo hubaki wazi. Katika ubadilishaji vibadala hutumika kujaza mapengo hayo. Kwa mfano maneno *moja, sawa na, ndiyo, hicho, hivyo* n.k hutumika kujaza pengo kama kiwakilishi cha KN au KT kinachodhaniwa, na katika udondoshaji hakuna kinachoingizwa katika pengo hilo (Halliday na Hassan, 1976:143).

Ubadilishaji ni wakati ambapo kibadala hutumika kusimamia nomino au kitenzi au kishazi katika sentensi, na kwamba faridi hizi ni ziwe zimetokea awali katika matini (Salkie, 1995:35-36). Faridi zinazodondolewa na kubadilishwa na vibadala huwa zimeshatangulia kutajwa katika matini. Hivyo vibadala kutumika katika nafasi za faridi hizo badala ya kuzirudia. Inapofanyika hivi, urudufishaji wa faridi hizo huondolewa. Urudufishaji wa faridi katika matini huharibu sarufi na mshikamano wa lugha. Kwa hivyo utumiaji wa vibadala huleta muungano wa dhati kati ya sehemu na ile iliyotangulia awali na kuifanya matini kuwa na mshikamano.

Katika ubadilishaji kuna matumizi ya vibadala vya habari iliyotolewa. Aidha kuna ubadilishaji wa kipekee ambapo kiwakilishi cha nafsi huwekwa mwanzoni mwa sentensi. Kirai Nomino (KN) ambacho huwakilishwa huja mwishoni (Greenbaum na wenzake, 1972:632). Hii haitokei mara nyingi katika Kiswahili. Aghalabu KN huja mwanzoni na

MACHAKOS UNIVERSITY COLLEGE
LIBRARY
Signed.................. Date..............

kiwakilishi kikatokea baadaye. Baadhi ya watalamu mfano Quirk, Greenbaum, Svartrik n.k wanadai kuwa uwakilishi ni ubadilishaji vile vile. Lakini katika utafiti huu, uwakilishaji tumeuchukuliwa kama urejeleaji kwa kuwa unaafiki vyema kwa mujibu wa nadharia yetu inayotuongoza. Ubadilishaji ni wakati dhana hairudiwi tena iwapo imetajwa awali. Badala yake vibadala hutumika kusimama mahali pa dhana hiyo iliyodondoshwa:

17. a) Mpe Onyango kikombe cheupe na wewe chukua *hicho* cheusi.
 b) Mary alikuwa akiimba vizuri sana zamani lakini sidhani anaweza kufanya *hivyo* sasa.

Katika matini hii, kibadala ni *hicho* na *hivyo*. *hicho* kimesimama badala ya kikombe. Kwa hivyo badala ya kurudia nomino hiyo, kibadala hiki kimetumika kuiwakilisha. *hivyo* ni kibadala cha kitenzi na kielezi kuimba vizuri.

18. *Yeye* ni mkaidi sana, kaka yako.

Hapa kibadala ni *yeye* na kimekuja mwanzoni kabla ya kirai nomino, 'kaka yako'. Kwa mujibu wa utafiti wetu hiki si kibadala bali ni kirejelea. Na tulichunguza jambo hili katika urejeleaji.

Quirk na wenzake (1972: 677) wanaeleza ubadilishaji hivi;

> "Ubadilishaji ni mbinu ya ufupishaji na kuepuka urudufishaji. Ni matumizi ya leksia sawa ambazo hazileti urudufishaji fanani. Hata hivyo leksia hizi zisiwe visawe bali vibadala...Miongoni mwa sentensi ubadilishaji huwa ni hiari na pia kwa sababu za kimtindo. Lakini wakati mwingine ni lazima katika sentensi." (Tafsiri Yetu)

Kwa mujibu wa maelezo haya mfano ufuatao unafafanua hoja hii.

19. Sasa mwalimu alikasirika sana baada ya mwanafunzi kumtusi nakuendelea kukaidi amri yake. Mwalimu alikunja shati lake, akapasha msuli tayari kwa mapigao. Mwanafunzi naye kwa ujeuri wake akafanya *hivyo*. Wanafunzi wote walishituka!

Hapa kuna ubadilishaji. *hivyo* imesimama kama kibadala cha 'kukunja shati lake, akapasha misuli tayari kwa mapigano'. Ubadilishaji hapa umekuwa wa lazima kwa sababu hatuwezi kurudia kishazi hicho tena badala ya *hivyo*. Inapotokea hivyo, sarufi na mshikamano wa matini utazorota. Hebu natuchunguze matini inapoandikwa bila vibadala.

20. *Jungu kubwa la maua lilimwangukia Kassim kichwani na kumpasua kichwa vibaya. Alianguka chini akizirai. Mama yake alimwangalia na alipomuona (jungu kubwa la maualimemwangukia Kassim kichwani na kumpasua kichwa vibaya. Alianguka chini akizirai)$_1$ alipiga unyende. Unyende huu ulivuta majirani pale nyumbani. Nao walipofika hapo walifanya (walimwangalia na walipomuona jungu kubwa la maua limemwangukia Kassim kichwani na kumpasua kichwa vibaya, kuanguka chini na kuzirai*)*$_2$ walipiga unyende.

Matini hii (20) tunaona imejaa urudufishaji usiokubalika katika Kiswahili. Hii ni kwa sababu vibadala havikutumika. Hapa vibadala *hivyo* ni lazima katika mabano$_1$ na $_2$ ili kuleta maana inayokubalika na mshikamano.

Halliday (1985: 297) anaeleza kuwa kibadala hufanya kazi ya kijenzi cha kushika nafasi katika sentensi kikionyesha faridi fulani imeachwa nje, na vile vile kuonyesha uamilifu wa faridi hiyo kisarufi. Yaani kibadala husimama badala ya faridi fulani katika sentensi au matini na kuonyesha uamilifu wa kisarufi wa faridi hiyo iliyoachwa. Faridi hiyo kisarufi, inaweza kuwa kiima, kitenzi, kishazi au sentensi.

21. Ali: Asha unapenda nywele zako kukaa midimu midimu?
    Asha: Ndiyo, napenda *hivyo*.

Hapa *hivyo* ni kibadala cha 'nywele zako kukaa midimu midimu' ambacho ni kishazi tegemezi. Kinachodhihirika hapa ni kuwa *hivyo* ni kibadala cha hiari kwa sababu Asha anaweza kusema, "Ndiyo napenda (nywele zangu kukaa midimu midimu)."

22. Lazima walimwona mzeehuyo mjinga aliyeingia garini na kuvutia sigara zake mle. Aliamua kuwapungia vijana mkono waliokuwa humo garini. Alifanya *hivyo* mara mbili lakini hawakumwitikia.

Hapa *hivyo* ni kibadala cha 'kupungia vijana mkono'. Kwa matumizi ya kitenzi 'Alifanya' mwanzoni mwa sentensi, kibadala kimekuwa lazima. Hatuwezi kurudia kishazi kilichoachwa nje. Ikifanyika hivyo, sarufi katika matini hii itapotoka. Kwa hivyo kibadala kimefaa na kuleta mshikamano wa kisarufi.

Hatch (1992: 224) anaeleza kuwa ubadilishaji haurejelei kitu mahususi lakini hurejelea kundi moja au faridi zinazofanana. Anafafanua zaidi kuwa ubadilishaji hufanyika kwa nomino, virai kitenzi na vishazi. Yaani nomino, kirai kitenzi na kishazi vinaweza kubadilishwa kwa kutumia kibadala. Kwa mfano, mahali panapotokea nomino huchukuliwa na kibadala. Hili huweza kufanyika iwapo nomino hii ilitangulia kutokea katika sentensi tangulizi katika matini.

Hubbard katika Webb na Kembo (2000:295) anaeleza kuwa ubadilishaji katika mshikamano ni kuwa dhana na kinachodhaniwa, havirejelei kitu hicho kimoja, lakini vina maana moja:

23. Watu wengi wanafariki kwa sababu ya unywaji pombe.
    Nafurahia vile serikali yetu imeongeza bei ya bidhaa hii
    kwa sababu inataka watu waache au wanywe kidogo kuliko
    *wafanyavyo*.

Katika matini hii, kibadala *wafanyavyo*, inasimama badala ya 'kunywa zaidi', hivyo ubadilishaji umetokea. *Wafanyavyo* na 'kunywa zaidi' hazifanani kimuundo wala si visawe lakini zina dhana moja. Kibadala *wafanyavyo* kinasimamia 'kunywa zaidi'. Kwa hivyo ubadilishaji hutokea wakati kibadala kimetumika katika nafasi ya urudufishaji wa kipashio, kiwe nomino, kitenzi, kirai, kishazi au sentensi.

Greenbaum na wenzake (1972:678) wanadai kuwa vibadala ni vimilikishi na vionyeshi, na hutumika badala ya Kirai Nomino, Kitenzi, Kishazi na Sentensi. Hata hivyo katika tasnifu hii tumegundua kuwa vionyeshi hutumika pia kama virejelea. Lakini katika ubadilishaji tumeviangalia vionyeshi hivi kwa mujibu wa uamilifu wao katika matumizi. Hivyo vinakuwa vionyeshi vibadala.

Ubadilishaji unakurubiana sana na urejeleaji katika Kiswahili kwa sababu vijenzi vyote vinatumia vionyeshi. Tofauti hutokea kimuktadha. Kionyeshi kikitumika kusimamia kirai nomino au kirai kitenzi au kishazi au msururu wa sentensi, kinakuwa kibadala. Kwa hivyo ubadilishaji kama wanavyoeleza Halliday na Hassan (1976) hushughulikia maneno tu wala si maana, na urejeleaji hujumuisha maneno na maana pia. Ukaribu huu huleta utata lakini la msingi ni kuwa ubadilishaji hushughulikia maneno tu katika sentensi au matini, na urejeleaji hujumuisha maana pia. Yaani kirejelea kinaweza kurejelea maana inayojitokeza katika msururu wa sentensi katika matini.

Ili kutofautisha vijenzi hivi viwili, Halliday na Hassann (1976: 89-90) wanasema kuwa urejeleaji ni uhusiano wa kiwango cha semantiki na ubadilishaji ni uhusiano wa kiwango cha sarufi leksia (lexicogrammatical level), yaani kiwango cha sarufi ikizingatia leksia (msamiati). Ubadilishaji unapotokea, huwa kuna uhusiano wa kibadala na faridi iliyotangulia na huwa imedondoshwa. Uhusiano huo ni wa kisarufi (kama hapo juu: 90)

Hubbard (2000:259) amejaribu kutofautisha urejeleaji na ubadilishaji kwa kutoa mfano huu;

24. Rais alikuwa amevaa shati zuri lenye marembo ya Kiafrika.
    Nilitamani ningekuwa na *moja*. (Tafsiri yetu)

25. Rais alikuwa amevaa shati zuri lenye marembo ya Kiafrika.
    Nilitamani ningekuwa *nalo*.

Katika mfano 24, *moja* ni kibadala cha 'shati zuri lenye marembo ya Kiafrika'. Huu ni ubadilishaji, na iwapo neno 'nalo' lingetumika badala ya *moja*, basi ungekuwa urejeleaji. Katika Kiswahili neno 'nalo' limejengwa na mofimu mbili; na- + lo. "na-" ni mofimu inayoashiria "umilikishaji" na "–lo" ni mofimu au kiambishi rejeshi. Na katika mfano 25 Hubbard akadai *nalo* ni kionyeshi kinachorejelea 'shati zuri lenye marembo ya Kiafrika'. Kwa hivyo ni dhahiri tofauti kati ya ubadilishaji na urejeleaji upo. Lakini katika Kiswahili, kuna utata wa vionyeshi kuwa vibadala na kuwa virejelea.Tasnifu hii inakubaliana na Hubbard (2000) na Halliday na Hassan (1976) kuhusu dhana ya ubadilishaji. Ubadilishaji mara nyingi huwa ni wa nyuma, na hurejelea tu ndani ya matini.

Kwa hivyo ubadilishaji hutokea pale ambapo nomino au kirai nomino, kitenzi au kirai kitenzi au sentensi imesimamiwa na kibadala na si kipashio hicho kurudiwa tena katika matini:

26. Watu wanasema huu ni ugonjwa hatari mwingine!
Bado haujapatiwa dawa na haujulikani vizuri maambukizi yake.
Inasemekana hata wataalam wa maradhi hawajautambua vizuri *huu*.

Hapa kionyeshi *huu* kimesimama badala ya ugonjwa hatari ( kirai nomino). Kwa hivyo *huu* ni kibadala katika muktadha wa matumizi katika 26.

27. ...Mwalimu Mkuu, mwalimu Chikoya aliwatangazia wanafunzi,
"Wote ambao hamjalipa ada na hamna sare, hakuna shule! Nisizione sura zenu bila ada na sare. Waambieni wazazi wenu *hivyo*."
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 1)

Hapa 27 neno *hivyo* ni kibadala cha sentensi zilizopigwa msitari. Badala ya mwandishi kurudufisha sentensi hizo ametumia kibadala *hivyo*. Ubadilishaji hapa ni wa lazima ili kudhibiti sarufi na kuleta mshikamano wa matini. Ubadilishaji katika mifano hii yote ni wa nyuma na umerejelea ndani.

Hii inaonyesha kuwa badala ya kurudia kipashio au vipashio, neno jingine linasimamia badala yake. Haya ndiyo maelezo yaliyotumiwa katika tasnifu hii kwa dhana ya ubadilishaji na ufafanuzi wake. Kwa hivyo faridi zifuatazo ni mifano ya vibadala kwa mujibu wa matumizi katika matini; *hivyo, huu, hiyo, -moja* n.k.

Ubadilishaji unaweza kuainishwa kwa mujibu wa kinachobadilishwa katika sentensi. Ubadilishaji unaotokea katika matini ni ule wa kubadili nomino, nomino na vifuasi vyake (Kirai Nomino), kitenzi, kitenzi na vifuasi vyake (Kirai Kitenzi) na ule wa kishazi na

sentensi (Halliday na Hassan, 1976; Halliday, 1985; Hatch, 1992; Salkie, 1997). Hata hivyo Quirk na wnzk (1972) wanaendeleza aina nyingine zaidi, ya ubadilishaji wa kirai elezi (KE). Wakatoa mfano wa Kiingereza.

28. a) We saw John at eight on Monday evening. We told him *then* that we would be coming to the party.
(Quirk na wenzake, 1972: 296)

Katika mfano huu, walidai kuwa *then* inasimamia "at eight on Monday evening", ambacho ni kielezi cha wakati. Tunapoitafsiri matini hii Kwa Kiswahili inaleta utata na kwa maoni yetu haikubaliki.

b) *Tulimuona John saa mbili za usiku siku ya Jumatatu. Tukamwambia *hapo* kwamba tungeenda kwenye sherehe. ( Tafsiri yetu)

Tunapotalii matini hii tunaona kwamba kibadala *hapo* hakiafiki na badala yake "wakati huo" ingetumika. Hii inashadidia maoni yaliyopo kuwa kila lugha ina mfumo wake.

Ubadilishaji mwingine ni wa Kirai. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inaeleza kirai kama kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini hakina muundo wa kiimakiarifu. Kwa hivyo ni kikundi cha maneno ambacho hakina muundo wa sentensi. Sentensi huundwa na virai viwili, kirai nomino + kirai kitenzi, au sehemu mbili, kiima na kiarifu. Kiima huwa nomino na vifuasi vyake, na kiarifu huwa kirai kitenzi.

Burton- Roberts (1986:14) anaeleza kuwa kirai ni mfululizo wa maneno ambayo yanafanya kazi ya uambajengo katika muundo wa sentensi. Hii inamaanisha maneno yanayojenga neno kuu katika sentensi ni kirai na hujumuisha hilo neno kuu. Hivyo kirai hujengwa na neno kuu na vifuasi vyake.

Horrocks (1987:30-31) naye anafafanua kirai kama sehemu ndogo ndogo za maneno zinapowekwa pamoja, na huunda virai vya aina nyingi. Virai hivi vinapowekwa pamoja huunda sentensi. Kwa hivyo kirai ni sehemu ya sentensi mfano kirai nomino, kirai kitenzi, kirai vumishi, kirai elezi, kirai husishi. Kimsingi, sentensi huundwa na kirai nomino na kirai kitenzi. Kwa hivyo kirai kinaweza kuwa nomino na vifuasi vyake au kitenzi na vifuasi vyake. Lakini katika Kiswahili, kirai kitenzi (KT) huweza kuwa kishazi au sentensi sahili, kwa mfano *Alipika chakula kitamu.* Kirai hiki ni sentensi sahili ambayo ni KT kilichojengwa na kitenzi *Alipika* na nomino *chakula,* na kivumishi *kitamu.* Hivyo kina muundo huu; KT---- T+N+V.

Naye Raddford (1981:35-36) anaeleza kuwa maneno hupangwa pamoja na kuunda kipashio chenye muundo na huitwa kirai. Hii ina maana kuwa kirai ni kipashio chenye muundo lakini si sentensi. Virai vinapowekwa pamoja, mfano kirai nomino na kirai kitenzi, ndipo huunda sentensi. Mathews (1981:161) anajeleza kirai kuwa ni kipashio kinachodhihirisha muundo ulio na neno kiini au neno kuu. Neno kuu hili huwa na vifuasi vyake, na kuunda kirai.

Kwa hivyo kulingana na vijelezi hapo juu, kirai ni kipashio cha kimuundo katika sentensi kilicho na neno zaidi ya moja, na mojawapo ya maneno hayo, liwe ni neno kiini au neno kuu, lakini kipashio hicho si sentensi. Hata hivyo kuna upekee katika lugha ya Kiswahili ya kwamba KT huweza kuwa sentensi.

Sasa tuchunguze kirai nomino kinavyowakilishwa na kibadala katika matini za Kiswahili. Kwanza tuchunguze vifuasi mbalimbali vya kirai nomino (KN).

Mohammed (2001:221) anaeleza kuwa kikundi na kirai huashiria kipashio kimoja. Kirai ni istilahi inayomaanisha kipashio katika mizani ya daraja kati ya kishazi na neno. Aliendelea kufafanua uambajengo wa kirai nomino (KN) kama ifuatavyo.

a) Nomino moja au mbili zilizounganishwa na kiunganishi.

b) Nomino ikifuatwa na kivumishi.

c) Nomino ikitanguliwa na kiashiria.

d) Kiwakilishi.

e) Kiwakilishi na kivumishi.

f) Nomino ikifuatwa na kitenzi-nomino.

g) Nomino ikitanguliwa na kitenzi-nomino.

Mohammed ameonyesha maumbo saba ya KN ingawaje kuna mengine zaidi. Hata hivyo ufafanuzi wake ulizingatiwa katika tasnifu hii ila tu kiwakilishi na nomino moja au mbili zilizounganishwa zimechukuliwa kama nomino wala si kirai.

Huddleston (1988: 85) naye anafafanua uambajengo wa kirai nomino kwa kusema kuwa hujumuisha nomino kama kiini, ikiwa pekee au ikiwa pamoja na kifuasi kimoja au zaidi. Baadhi ya vifuasi hivi hutangulia nomino hiyo na vingine huja baada ya nomino hiyo. Tunavyoona katika maelezo ya Huddleston, ni kuwa yeye anachukulia kuwa hata nomino moja pekee ni kirai nomino. Katika tasnifu hii, iwapo nomino pekee imejitokeza katika

matini na kusimamiwa na kibadala katika sentensi fuatilizi, tumeuita ubadilishaji huu, ubadilishaji wa nomino. Na umejadiliwa hapo juu.

Naye O'Grady na wenzake (1996: 189) wanaeleza kuwa kirai nomino hujumuisha kibainishi, kiini nomino, na kirai husishi (KH) kama kisifa. Hawa katika kijelezi chao wameongeza kijalizo cha nomino ambacho huwa ni kivumishi katika umbo la kirai husishi. Katika Kiswahili kirai husishi kikifuata nomino hujitokeza hivi; Mtoto [wa Omari] amelazwa hospitalini. [wa Omari] ni kirai husishi kikisifu nomino 'Mtoto' na hivyo kuwa na uamilifu wa kivumishi (V).

Ubadilishaji pia unaweza kuwa wa nomino au kirai nomino. Pahali pa nomino ama kirai nomino huchukuliwa na kibadala ili kukwepa urudufishaji wa kipashio au elementi fulani katika matini. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inaeleza nomino ni aina ya neno linalotaja mtu, kitu, mahali, hata tendo ambalo linaweza kukaa mahali pa kiima au yambwa.

Kwa mujibu wa Kapinga (1983:36), jina (nomino) ni neno linalotaja kitu fulani. Vitu vyenye uhai kwa mfano watu, wanyama, ndege, samaki, wadudu, miti. Hata vitu visivyo na uhai kama kisu, jiwe, njia, udongo, mahali ni nomino.

Nao Habwe na Karanja (2004: 131) wakinukuu Sarufi Mapokeo, wanasema nomino ni neno la kutaja vitu, yaani ni majina ya vitu. Kwa hivyo nomino hutaja majina ya watu,

vitu, hali, mahali, vyeo na dhana. Wakatoa mifano ya Kamau, Nairobi, kuimba, ubaharia, joto, kiti, blanketi, kitabu, mtu na kisu.

Aidha Kihore na wenzake (2008: 86) wanaeleza kuwa nomino ni jina linalotaja kitu, kiumbe, hali, dhana, au tendo lolote liwalo. Wakaendelea kueleza kwamba katika uamilifu wake nomino hufanya kazi ya kupambanua au kukibainisha kitwaja kwa madhumuni ya kukitofautisha na vitajwa vingine. Kwa hivyo nomino si mtajo tu, pia ni mtajo bainishi.

Waihiga (1999: 4) anafafanua nomino kwamba ni neno linalotaja mtu, kitu, hali au mahali. Anaendelea kueleza kuwa nomino ni muhimu sana katika lugha kwa sababu kila sentensi ni lazima iwe na nomino au kiwakilishi chake. Anadai kuwa mara nyingi tunapoongea tunatumia sentensi, na ni wazi kwamba hatuwezi kuwasiliana bila kuwa na nomino.

Dai hili la Waihiga lina tashwishi kwa sababu si kila mara lazima nomino iweko. Kurejelea nomino kila mara katika sentensi huweza kuleta urudufishaji, hivyo kuharibu mshikamano wa matini. Ili kukwepa urudufishaji katika matini, wakati mwingine inabidi nomino idondoshwe na mahali pake pawe na neno ambalo ni kibadala cha nomino hiyo. Neno hili tutaliita *kibadala* na ndilo neno litatumika katika tasnifu hii kuanzia sasa na kuendelea.

Naye Huddleston (1988:84-85) anadai nomino ni maneno ambayo hurejelea mtu au vitu halisi na hufanya kazi ya kiima au yambwa katika muundo wa kishazi.Thompson (2004: 187) anasema kibadala huweza kuwakilisha kishazi au nomino. Hivyo nomino inapojitokeza tena katika msururu wa sentensi, hubadilishwa na pahali pake kibadala hutumika ili kuleta mshikamano unaofaa. Ubadilishaji wa nomino hutumia vibadala; *hiyo, hizi, hiki, hivi* na *-moja*.

Baker (1978:326) anaeleza kuwa vibadala vya nomino, *hiyo/hizo* n.k hutokea katika matini ikiwa huko mwanzoni nomino imeshatajwa. Kwa hivyo vibadala hivi hutokea katika matini vikisimama mahali pa nomino tangulizi ili kuondoa urudufishaji.

Culicover (1976: 185) anasema sheria hii ya kuweka vibadala *hiyo/hizo* ni kuwa kibadala *hiki*, huweko ikiwa kuna nomino fanani katika sehemu yote ya sentensi au matini. Katika Kiswahili, kibadala husimama pahali pa nomino kwa kulingana na ngeli ya nomino ili kuleta upatanisho wa kisarufi. Tunapotumia kibadala kisichoowana na ngeli ya nomino husika, sentensi hiyo haitakuwa sahihi na haikubaliki kisarufi:

29. a) Natamani kikombe cha kahawa. Basi nitajitilia
*kimoja.*

Katika matini hii, kibadala *kimoja* kinasimamia 'kikombe cha chai'. Hivyo nomino kikombe na vifuasi vyake inasimamiwa na kibadala *kimoja.* Iwapo 'kikombe cha kahawa' kingerudiwa, matini ingekuwa na hitilafu ya urudufishaji, hivyo kukosa mshikamano wa kisarufi. Hebu natuchunguze matini hii.

b) *Natamani kikombe cha kahawa. Basi nitajitilia
kiombe cha kahawa.

Hapa kibadala ni bora kikitumika, tena ni lazima, ili kuleta mshikamano unaositahili.

c) *Natamani kikombe cha kahawa. Basi nitajitilia *mmoja*.

Matini hii si sahihi kisarufi kwa sababu kibadala *mmoja* hakioani na ngeli ya nomino kikombe. Mifano hii 29 a-c, inaonyesha umuhimu wa ubadilishaji na uzingatifu wa ngeli ya nomino ili kuleta mshikamano wa kisarufi katika matini. Huu ni mfumo wa Kiswahili.

Kitenzi pekee au Kirai Kitenzi huweza kutotumika kwa mara ya pili katika matini na husimamiwa na kibadala ili kuleta mshikamano wa kisarufi. Vibadala husimama pahali pa kitenzi au kirai kitenzi katika matini. Hili hufanyika ili kuondoa urudufishaji unaoharibu mshikamano wa matini na sarufi ya lugha.

Kitenzi ni sehemu muhimu katika sentensi ya Kiswahili. Katika sentensi, kitenzi kikikosekana basi sentensi hiyo huwa si kamili. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inaeleza kuwa kitenzi ni aina ya neno ambalo huarifu aina ya tendo linalofanyika.

Kapinga (1983:111) anaeleza vitenzi ni aina ya maneno ambayo hayasimami peke yake, bali huambatana na viambishi mbali mbali ili kuunda vitenzi halisi. Katika Kiswahili, kitenzi kikiambishwa, huweza kuwa sentensi kamili hata bila ya kiima, mfano; *Alikimbia*. Kitenzi ni *–kimbia* na kimeambishwa kiambishi kiima *A-* na kiambishi cha njeo *–li-* na kuwa sentensi kamili.

Naye Mbaabu (1985: 40) anasema kitendo (au kitenzi) ni neno lolote lenye kuonyesha jambo linalofanywa au linalotendwa na mtu, mnyama au kitu chochote. Kwa mfano,

*andika*, *tembea*, *lia*, na *vunja* ni vitendo. Kwa hivyo kitenzi ni vitendo mbalimbali vinavyofanywa na viumbe au kitu chochote kisichokuwa kiumbe, mfano mpira, jiwe, jua, mvua n.k. Vitu hivi visivyokuwa kiumbe pia hutenda, k.m *Jua limetua*.

Waihiga (1999: 21) anasema vitenzi ni maneno yanayoarifu jambo linalofanywa au kufanyiwa nomino au kiwakilishi chake. Kwa hivyo, kwa mujibu wa maelezo haya, kitenzi ni jambo linalofanywa na nomino kiutendaji. Na ikiwa linafanyiwa nomino pia huwa kuna nomino inayotenda kitendo (kitenzi) hicho. Mfano, *Mtoto alichapwa na baba*. Katika mfano huu, kitenzi ni *alichapwa* na pana nomino kiima na nomino yambwa. Kiima ni *baba* na yambwa ni *Mtoto*. Nomino *Mtoto* inatendwa na nomino *baba* inatenda.

Mgullu (1999: 182) anaeleza vitenzi ni aina ya maneno ambayo hutumika kama sehemu muhimu sana ya kiarifu cha sentensi na ambayo huarifu au hueleza jambo fulani linalohusu kiima cha sentensi. Kwa maelezo haya ni kwamba vitenzi hueleza juu ya kiima na ni sehemu ya kiarifu katika sentensi.

Habwe na Karanja (2004:173) wanaeleza kuwa kitenzi ni sehemu kuu ya kiarifu. Kitenzi ndicho neno kuu la kifungu tenzi. Hawa hawakujeleza kitenzi bali wametuambia tu nafasi ya kitenzi katika kiarifu. Kihore na wenzake (2008:114) wanasema kitenzi ni aina ya neno linalotoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalotendwa na kiumbe au kitu. Maelezo haya ni faafu kwa kujeleza kitenzi ni nini.

Vijelezi hivi vyote ni mwafaka na vinafanana. Kwa hivyo maelezo haya juu ya kitenzi ndiyo yalitumika katika tasnifu hii kubainisha vitenzi na husimamiwa na vibadala:

30. Rudisha *alikimbia* na akashinda mbio za mita mia nane. Naye Jelimo akafanya *hivyo* na kushinda mbio hizo kwa wanawake.

Katika mfano huu 30, kibadala ni *hivyo* na kimesimama badala ya kitenzi *kimbia* ambacho kimetangulia katika sentensi tangulizi. Hii imeondoa urudufishaji iwapo kitenzi *kimbia* kingerudiwa katika sentensi fuatilizi. Ubadilishaji hapa ni wa kitenzi.

*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inafafanua Kirai Kitenzi (KT) kuwa ni sehemu ya kiarifu ya sentensi. Sehemu hii ndiyo huarifu linalofanyika katika sentensi. Huelezea kiima kinafanya kitendo gani.

Burton-Roberts (1986:71) anaeleza kirai kitenzi kuwa ni ile sehemu katika sentensi iliyo na kitenzi kamili na huweza kutanguliwa na kitenzi saidizi. Kwa hivyo KT kinaweza kuwa kimejengwa na kitenzi au kimejengwa na kitenzi saidizi + kitenzi kamili. Kwa mfano *Alikuwa anacheza*. Hapa *Alikuwa* ni kitenzi kisaidizi (Ts) na *anacheza* ni kitenzi kamili/kikuu.

Huddleston (1988:52) anasema kirai kitenzi hujumuisha kitenzi kama kiini na huweza kufuatiliwa na kifuasi kimoja au zaidi.Vifuasi hivi ni vya aina mbili; vijalizo au chagizo. Vijalizo ni vile vipashio vinavyokamilisha vipashio vingine katika tungo, na chagizo ni kipashio kinachotumika kuelezea zaidi juu ya kitenzi.

Mohammed (2001:223) aneleza kuwa muundo wa kimsingi katika kirai kitenzi katika Kiswahili huwa;

a) Kitezi kamili.
b) Kitenzi kamili kikifuatwa na kitenzi kimoja au zaidi.
c) Kitenzi ungio/shirikishi kinachofanya kazi ya kitenzi kamili.

Verma na Krishnaswamy (1989:111) wanaeleza kirai kitenzi hujumuisha kitenzi pekee, au kitenzi saidizi pamoja na kitenzi, au kitenzi na kirai nomino, au kitenzi na kirai husishi. Maelezo haya, yamepanua uambajengo wa kirai kitenzi. Pia Burton-Roberts (1986:41, 155) anaeleza kuwa kirai husishi (KH) ni kifuasi cha kirai kitenzi.

Tunapotalii vijelezi hivi, tumechukulia kirai kitenzi kuwa ni ile sehemu katika sentensi inayoarifu juu ya kirai nomino na yenye uambajengo unaojumuisha kitenzi, kitenzi saidizi au ungio na vifuasi vyake. Vifuasi vilivyomo kama vijalizo au chagizo vilifafanuliwa kama virai mahususi kwa sababu katika ubadilishaji wao kwenye matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* vimejitokeza kama vipashio vinavyojitenga na kujitegemea kama virai. Katika mshikamano wa matini kirai kitenzi huweza kusimamiwa na kibadala badala ya kurudiwa rudiwa. Kibadala kinapotumika, huwa ni ubadilishaji na huleta mshikamano katika matini:

31. Asubuhi Juma *alikuwa analalamika mchezoni*. Baadaye mchana
 Mariga naye ikawa *hivyo*.

Katika matini 31, KT ni *alikuwa analalamika mchezoni* na kibadala chake katika sentensi fuatilizi ni *hivyo*. Kwa hiyo kibadala kimesimama pahali pa KT. Iwapo KT kingerudiwa

katika nafasi ya kibadala katika sentensi fuatilizi, mshikamano ungeharibika kwa sababu ya urudujishaji wake. Hivyo ubadilishaji huu ni wa KT.

*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inaeleza kuwa kirai nomino ni kirai ambacho hufanya kazi ya nomino. Huweza kukaa mahali pa kiima au kijalizo. Kijalizo hiki ni kile kinachoelezea zaidi juu ya nomino.

Burton- Roberts (1986:54-55) anajeleza kirai nomino kuwa ni kirai kinachojumuisha nomino. Pia hujumuisha maneno mengine ya katagoria tofauti. Aidha hujumuisha nomino zaidi ya moja. Kinachojitokeza hapa ni nomino na vifuasi vyake na ndivyo viambajengo vya KN.

Kutokana na vijelezi hivi, kirai nomino ni kipashio katika sentensi kinachojumuisha nomino na vifuasi vyake na hufanya kazi ya kiima, yambwa na kijalizo au kijalizo katika kirai husishi. Hivyo katika tasnifu hii kirai nomino kimechukuliwa kama nomino na vifuasi vyake, kikiwa kama kiima au yambwa au kijalizo. Hivi ndivyo ubadilishaji wa kirai nomino ulichunguzwa na nomino pekee ilichunguzwa kama ubadilishaji wa nomino. Ubadilishaji kama kijenzi cha mshikamano, hutumika katika matini wakati ambapo kirai nomino kinadondoshwa na badala yake kuwekwa kibadala. O'Grady na wenzake (1996:193) katika uchanganuzi wa muundo wa sentensi wanaeleza kuwa kirai nomino kinaweza kuwakilishwa na kibadala. Mfano, wa vibadala ni *wao*, *-cho* na *hivyo* katika Kiswahili.

Hubbard (2000: 259) anasema kuwa kirai nomino huweza kubadilishwa na kibadala kimoja katika matini. Hivi ni kwamba neno moja (kibadala) linaweza kutumika mahali pa kirai nomino badala ya kurudia kirai hicho. Hili linapotokea, ubadilishaji huwa umesibu.

Kulingana na fafanuzi hizi, ubadilishaji wa kirai nomino hutokea katika matini ili kukwepa urudufishaji na kuleta mshikamano. Urudufishaji ni kule kurudia rudia elementi fulani katika sentensi au matini. Urudufishaji huu huharibu mshikamano wa matini na huleta hitilafu katika sarufi. Elementi inaweza kurudiwa tu ikiwa hakuna budi ili kutoleta utata wa maana katika matini. Ubadilishaji unapotokea, vibadala mbalimbali husimama mahali pa kirai nomino. Vibadala hivi hutumika kwa mujibu wa ngeli ya nomino iliyopo katika kirai nomino:

32. a) Natamani *kikombe cha kahawa*. Wacha nijitilie *kimoja*.

Katika matini hii, kibadala *kimoja* kinasimamia *kikombe cha kahawa* ambacho ni kirai nomino (KN). Hivyo nomino kikombe na vifuasi vyake imesimamiwa na kibadala kimoja. Iwapo KN kingerudiwa katika matini hii (32a), matini ingekuwa na urudufishaji ambao ungeharibu mshikamano:

b) *Natamani *kikombe cha chai*. Wacha nijitilie *kikombe cha chai*.

Katika matini hii (33b), urudufishaji wa KN umeharibu mshikamano wa matini. Hili ni dhihirisho kuwa katika matini, ubadilishaji ni muhimu. Ubadilishaji katika matini hii ni lazima ile kuwe na mshikamano wa kisarufi.

c) *Natamani *kikombe cha kahawa*. Wacha nijitilie *limoja*.

Katika matini hii (32c), kibadala *limoja* hakioani na ngeli ya nomino *kikombe* ambayo ni *ki-vi*. Kwa hivyo matini hii ina dosari ya kisarufi. Kibadala sahihi kingekuwa *kimoja* ili

kioane na ngeli ya kikombe (*ki-vi*). Matini 32a-c, zinadhihirisha umuhimu wa ubadilishaji katika matini na uzingatifu wa ngeli ya nomino ili kuleta mshikamano wa kisarufi katika matini.

Ubadilishaji mwinge ambao hutokea katika matini ni wa kirai elezi au chagizo. Chagizo ni sehemu mojawapo ya sentensi. Mara nyingi sehemu hii huwa ni ya hiari. Kabla ya kuchunguza ubadilishaji wa chagizo, tudahili maana ya chagizo. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inaeleza chagizo ni kipashio ambacho hutumika kama nyongeza ya maana, na ambacho kinaweza kuondolewa na bado sentensi ikabakia na maana ya msingi; neno litumikalo kuelezea zaidi juu ya kitenzi. Burton-Roberts (1986) anashadidia kuwa chagizo ni sehemu ya hiari katika sentensi. Kwa hivyo chagizo kina muundo wake. Na Mohammed (2001:230) alitoa sifa za chagizo kama ifuatavyo;

a) Chagizo hujumuisha kielezi au kirai elezi rejeshi.
b) Ni kipashio cha hiari katika sentensi.
c) Na huwa lazima tu ikiwa kuna matumizi ya kitenzi-ungio katika sentensi.
d) Huweza kutokea zaidi ya mara moja katika mfululizo wa kishazi.
e) Mara nyingi ni kirai elezi katika muundo wa kishazi.

Nao Quirk na Greenbaum (2002:207) wanaeleza kuwa chagizo (Kirai Elezi) ni kipashio kilicho na uamilifu wa kielezi. Aidha wakasema pindi kirai husishi kina uamilifu wa kielezi basi hicho ni chagizo.

Kulingana na maelezo haya ni kuwa chagizo ni kile kipashio katika sentensi kinachoelezea zaidi juu ya kitenzi kiuamilifu. Hivyo kirai husihi (KH) kinapofanya kazi ya kuelezea zaidi juu ya kitenzi ni chagizo. Na katika tasnifu hii kimechukuliwa kama chagizo.

Chagizo kinaporudiwa rudiwa hupotosha mshikamano katika matini. Ili kurekebisha jambo hili, ubadilishaji hutumika ili kudhibiti mshikamano wa kisarufi katika matini. Vibadala mbali mbali hutumiwa kusimama pahali pa chagizo hicho.

Ubadilishaji hutokea vile vile katika kiwango cha kishazi na kwenye msururu wa sentensi. Vibadala hutumika katika nafasi zao kwenye matini, na hivyo kuachwa nje. Hii hutokea ikiwa kishazi au sentensi zimeshatangulia kwenye matini na mbele hazirudiwi tena bali vibadala hutumika katika nafasi zao. Ili kufafanua ubadilishaji huu, ni vyema tujadili dhana za kishazi na sentensi kwanza.

*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990:12) inajeleza kishazi kama tungo ambayo ni ndogo yenye uanifu (uainifu) ndani mwake, na inaweza kusimama peke yake au kuwa sehemu ya sentensi. Dhana inayojitokeza hapa ni kuwa kishazi kinaweza kuwa sentensi kamili.

Naye Mohammed (2001:227) anaeleza kwamba kishazi ni dhana iliyotumiwa na baadhi ya vielelezo vya sarufi kuashiria kipashio cha kisarufi kidogo kuliko sentensi lakini

kikubwa kuliko vikundi, maneno au mofimu. Aidha anadai (kama hapo juu: 244) kuwa sentensi sahili ni kishazi kimoja.

Vile vile Burton-Richards (1986:155,165-166) anaeleza kuwa kishazi ni lile umbo la muundo linalofanana na sentensi. Ni yale maumbo ambayo hufanya kazi ya uambajengo katika muundo wa sentensi. Kuna kishazi kikuu na kishazi tegemezi. Kishazi kikuu huwa kinajisimamia kimaana na kishazi tegemezi hakijisimamii kimaana.

Mdee (1986:9) anaeleza sifa za vishazi. Anasema kwamba vishazi huru vinaleta maana iliyo kamili. Vinajitegemea vyenyewe kwa sababu havihitaji kutegemea vishazi vingine ili kuweza kukamilisha maana iliyokusudiwa... ni sentensi sahili.

Kwa hivyo kishazi kinaweza kuwa sentensi sahili au sehemu ya sentensi ikiwa sentensi ina muundo changamano wenye kishazi kikuu na kishazi tegemezi. Kishazi kikuu hujitegemea kimaana ilhali kishazi tegemezi hutegemea kishazi kikuu ili kupata maana inayokusudiwa.

Sentensi ni kipashio cha juu zaidi katika lugha. Sentensi zikiwekwa pamoja, huunda matini. Dhana ya sentensi imefafanuliwa na wataalamu anuwai. Natuchunguze fafanuzi hizo.

*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inaeleza sentensi kama tungo yenye kiima na kiarifu, na yenye maana kamili. Linalodhiri hapa ni kuwa ili kuitwa sentensi, tungo lazima iwe na maana kamili na imejengwa na kiima na kiarifu.

Kwa mujibu wa sarufi mapokeo, sentensi ni kipashio chenye maelezo kamili ya wazo (Crystal, 1997:94). Mohammed (2001:244) anasema sentensi ni kipashio cha juu zaidi ambamo taarifa za kisarufi hutolewa. Mathews (1981:26) anaeleza kuwa sentensi ni mfululizo wa maneno katika usemi au maandishi ulio na mshikamano, unaounda maelezo kamili ya dhana moja kisarufi. Hivyo sentensi lazima iwe na maelezo ya dhana moja, iliyo na maana kamili na inakubalika kisarufi.

Mkude (1983) anaeleza sentensi ni kile kipande cha usemi-lugha chenye kujitosheleza kimaana. Nao Massamba na wenzake (2001:12) wanajeleza sentensi kuwa ni kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo chenye maana kamili.

Kutokana na maelezo haya, tunachukulia kuwa sentensi ni tungo yenye maana kamili na huweza kuwa na kiima na kiarifu na kukubalika kisarufi. Kiima hicho huwa kinaelezwa zaidi na kiarifu katika sentensi. Katika Kiswahili, kiima huwakilishwa pia katika kitenzi na kiambishi kiwakilishi hata kama kiima nomino kipo, na kuwa sentensi kamili. Na iwapo kiima hicho hakipo, bado kitawakilishwa na kiambishi nafsi kwa mujibu wa ngeli ya kiima.

Mfano: Alicheza vizuri.
Katika sentensi hii kiima dhahiri hakipo lakini kipo kwani kimewakilishwa na kiambishi nafsi *A*- katika kitenzi.

Katika ubadilishaji kwenye matini, kishazi au sentensi au sentensi zaidi ya moja huweza kuondolewa na kusimamiwa na kibadala. Hii hufanyika ili kukwepa urudufishaji ambao huharibu mshikamano wa matini:

> 33. Umati mkubwa ulimshambulia mwizi sokoni kwa mateke, ngumi, fimbo na hata mawe. Watu waliokuwa na ghadhabu walimrukia kwa mateke na ngumi na fimbo. Kila aliyefika hapo alifanya *hivyo.*

Katika matini 33, kibadala *hivyo*, kinasimamia msururu wa sentensi zenye maelezo ya yale yaliyotendewa mwizi hapo sokoni. Kibadala hiki kimeondoa urudufishaji wa maelezo yaliyotangulia mwanzoni mwa matini. Ubadilishaji hapa umeleta mshikamano katika matini.

### 2.1.3 Udondoshaji

Kijenzi kingine ni udondoshaji. Udondoshaji ni kijenzi kimojawapo cha mshikamano kinacholeta umoja wa matini. Udondoshaji hutokea tu wakati matini inapoandikwa, na hutokea ukatizwaji wa maumbo ya nje ya sentensi katika matini hiyo (Beaugrande na Dressler, 1981:49). Maelezo hayo ni sahihi lakini yana upungufu kwa sababu hata katika usemi simulizi udondoshaji hutokea. Si katika maandishi pekee.

*Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inaeleza kuwa udondoshaji ni hali itokeayo katika usemaji ambapo baadhi ya maneno ambayo ni muhimu kisarufi huachwa bila ya kuathiri maana. Maneno haya hudondoshwa kwenye muundo wa sentensi na kuacha mapengo ya kimuundo. Wakati wa kufasirfi maana, msomaji hurudia maneno haya kutoka sentensi zilizotangulia na kupata maana kamili.

Hubbard katika Sure na Webb (2000:260) anaeleza kwamba kuna mshikamano wa udondoshaji. Maelezo haya yanaleta dhana kuwa udondoshaji huleta mshikamano katika matini. Naye Thompson (1979:64) anaeleza kwamba ili kuwe na mshikamano katika matini tunapodondosha, ni muhimu elementi moja ibakie katika matini kati ya mbili hizo kama sharti. Udondoshaji huchangia mshikamano wa kisintaksia, na hutokea iwapo kipashio au elementi moja hutegemea nyingine kufafanua maana katika matini. Kwa hivyo, udondoshaji ni kijenzi cha mshikamano na hutokea wakati elementi moja imedondoshwa na kuacha pengo ambalo hujazwa kwa kutumia dhana ya elementi iliyobakia katika matini.

Halliday na Hassan (1976:142) wanaeleza kuwa udondoshaji ni 'kuacha kitu nje'. Kitu hiki kinachoachwa nje ni kipashio au elementi fulani ya kisarufi katika sentensi. Jambo hili hutokea ili kuondoa urudufishaji wa vipashio au elementi fanani. Vipashio au elementi hizi hubidi zidondoshwe ili kuleta mshikamano wa kisarufi. Tuchunguze mifano hii:

34. Kamau alimwangalia mamake machoni. Uso wa mama ulikuwa umekwiva kwa ghadhabu. ( 1 ) Ulifinyaa, ( 2 ) ukakunjiana na kutoa nditi kipajini. Kamau alitetemeka, ( 3 ) akitamani ardhi immeze.

Katika mfano huu 34, nomino 'uso'limeachwa nje katika sentensi inayofuatia (mapengo 1 na 2 hapo juu). Nomino hii imedondoshwa kwa sababu imetangulia katika sentensi ya awali. Hivyo kisarufi, si lazima nomino 'uso' iwepo tena. Katika pengo 3, nomino Kamau imedondoshwa na imelazimu kwa sababu ingeleta urudufishaji utakaoharibu mshikamano na sarufi. Huu ni udondoshaji ulioleta mshikamano.

35. Majambazi waliotuvamia nyumbani mwetu walikuwa sita.

> Baadhi walikuwa na mapanga na mashoka, lakini mmoja alikuwa ameshika bunduki. Yeye alituamuru tulale chini. Hatukukaidi. Tulijibwaga sakafuni. Mara mlipuko ulisikika nje. Majambazi hawa walitetemeka, na bunduki ikamdondoka. Kuangalia hivi, (      ) hakuwa nayo. Nilimrukia!

Katika matini hii nomino 'bunduki' limedondoshwa na kuacha pengo katika sentensi kama ilivyoonyeshwa kwenye mabano. Hata hivyo matini inaeleweka kwa sababu lazima turudi nyuma katika matini na kupata nomino hiyo na kuirejesha kidhana katika pengo kukamilisha maana. Katika matini hii nomino 'bunduki' limetokea mwanzoni mwa matini na baadaye kudondoshwa.

Watajwa hapo juu (1976:142) aidha wanadai kuwa kinachoachwa nje si kuwa hakieleweki, bali kinaeleweka. Kinaeleweka kwa sababu huwa tunakidhania kutoka sentensi iliyotangulia katika matini. Kipashio kilichodondoshwa huacha pengo mahususi la kimuundo ambalo hujazwa kwa kurejelea kipashio hicho kidhana tu na hapawekwi kipashio hicho tena. Hivyo hubaki wazi. Halliday na Hassan (1976: 143) wanauita udondoshaji, "ubadilishaji kapa".

Hatch (1992:225) anakubaliana na maelezo haya kwa kusema udondoshaji unaweza kudhaniwa kama 'kishikanishi sarufi', kwa sababu kishikanishi hicho hakitajwi. Hakitajwi katika sentensi iliyofuata lakini mwanzoni mwa matini huwa kimetajwa. Kwa hivyo kinapotajwa mwanzoni, huko mbele ya matini hakitajwi.

Naye Halliday (1985:288) anasema kuwa kishazi au sehemu ya kishazi au sehemu ya kitenzi (ikijumuisha elementi ya kimsamiati) au kikundi nomino, kinaweza kudhaniwa katika sehemu ya mbele katika matini kwa njia ya kukiwacha au kukidondosha. Ama

muundo huo (wa sentensi) unawachwa bila kujazwa. Huu ndio huitwa udondoshaji. Aidha udondoshaji ni njia mojawapo ambayo huchangia kuleta maana na mshikamano wa usemi.

Katika udondoshaji hakuna vibadala au visimamizi kuonyesha urudufu wa maana. Urudufu huu hueleweka tu kutoka kwa muktadha kama anavyodai Hubbard katika Webb na Kembo Sure (2000:260). Kwa hivyo ile sehemu ilivyodondoshwa hurejelewa tu ili kupata maana. Hurejelewa kutoka nyuma ilikotangulia kwa kuidhania katika pengo liliopo. Inapofanyika hivyo, maana kamili inapatikana katika matini na kuleta mshikamano wa matini hiyo.

Beaugrande na Dressler (1981:49) wanaeleza kuwa udondoshaji ni kurudia umbo fulani na viungo lakini kuwacha nje baadhi ya vielelezo vyake. Hii inamaanisha kuwa neno linaweza kurudiwa katika sentensi fuatilizi lakini visifa au vifuasi vya neno hili havitajwi kwa mara ya pili bali vitarejelewa kidhana tu. Hii huondoa urudufu na kuchangia mshikamano wa matini. Udondoshaji hufanya kazi kwa kushirikisha miundo ya viambajengo miongoni mwa vishazi vya matini ya nje. Hata udondoshaji ukitokea, muundo kamili wa sentensi lazima uweze kurejeshwa (kidhana) katika matini. Udondoshaji kwa kawaida hutokea katika sentensi mpya fuatilizi. Kwa hivyo, ifahamike kuwa udondoshaji hutokea katika sentensi inayofuata nyingine huku ikiacha kipashio au vipashio fulani vilivyotangulia kutajwa katika sentensi tangulizi. Vitenzi na hata kiima vinaweza kudondoshwa katika vishazi:

36. Katika barabara ile ya matope, gari letu lilikuwa na shida kwenda. Ilibidi tushuke mara kwa mara na kulisukuma. Dereva alikuwa ndani

> aking'ang'ana lisipoteze njia. Ghafla liliteleza, dreva akashika breki, ( 1 ) likaserereka na kutoka nje ya barabara. Bahati mbaya mbuzi mmoja alikuwa karibu akakwaruzwa mguuni. ( 2 ) Alilia kwa uchungu na kuruka mbali kutetea uhai wake.

Katika matini hii tunaona udondoshaji (1) ambapo neno 'Gari' limedondoshwa katika kishazi kinachofuata. Na katika (2) neno 'mbuzi' limedondoshwa. Kama ilivyoelezwa hapo juu kuwa udondoshaji hutokea katika sentensi fuatilizi, maneno 'Gari' na 'mbuzi' yamedhihirisha maelezo hayo. Hata hivyo imetokea kuwa udondoshaji (1) umefanyika katika sentensi hiyo hiyo moja. Hii ni kwa sababu sentensi hiyo ni ambatano yenye vishazi vitatu ambapo viwili vya kwanza vimeunganishwa kwa matumizi ya koma na cha tatu kimeunganishwa kwa kutumia kiunganishi *na.* Vishazi hivi tukivichunguza zaidi, tunapata kuwa ni sentensi sahili. Na katika udondoshaji (2), udondoshaji umetokea katika sentensi fuatilizi. Hapa maneno 'Gari' na 'mbuzi' ni kiima
katika sentensi mahususi. Tutalii mfano huu pia:

> *37.* Marehemu baba yangu alinisimulia mambo mengi kuhusu utamaduni wetu wa ndoa. Wakati binti yangu ameolewa na wazazi wa mumewe walipokuja kujadili mahari, nilikaa na kuwaza nitakavyo. Katika harakati hii niliyakumbuka ( ) yote niliyoambiwa na baba.

Matini hii inaonyesha udondoshaji wa neno 'mambo' katika sentensi ya mwisho. Neno hili limetajwa awali katika matini. Hivyo tunalirejelea kutoka nyuma lilikotangulia kutajwa ndipo tupate maana kamili na mshikamano wa matini kudhihiri.

Crystal (1997:119) anaeleza kuwa udondoshaji ni wakati kisehemu cha muundo kimedondoshwa (au kuwachwa) na kinaweza kupatikana tena kutoka kwa usemi uliotangulia. Matthews (1981:38) anasema udondoshaji ni pale ambapo maneno au elementi fulani zimedondoshwa katika matini na huweza zikarejelewa, na kwamba

udondoshaji huenda sambamba na muktadha. Yeye alifafanua udondoshaji katika matini ya sentensi mbili tu. La muhimu ni kuwa alitaka kuonyesha ile dhana ya uwezekano wa kurejelea nyuma ili kupata kile kilichodondoshwa.

Burton-Roberts (1986) alielezea udondoshaji kama kuacha nje elementi zinazohitajika katika sentensi zilizo na uwezekano wa kueleweka katika muktadha wa matumizi yao. Akadai udondoshaji unakubalika katika Kiingereza lakini huzalisha sentensi zisizo kamili kisarufi. Dai hili ni kweli tukifuata kigezo cha muundo lakini sentensi huwa kamili kimaana na huleta mshikamano katika matini. Maana inakamilika kwa sababu msomaji hurejelea nyuma kupata elementi zilizoachwa nje na kukamilisha sentensi iliyo na pengo lililotokana na udondoshaji. Maneno yanayorejelewa kwa kudhani ndiyo hujaza mapengo yaliyopo.

Brown na Yule (1983) wanasema kuwa mwandishi anaweza kuchagua kipashio kama kiini katika mfululizo wa matukio katika sentensi, halafu asikitaje tena kipashio hicho katika sentensi zifuatazo kwa kutumia udondoshaji. Hii inamaanisha kuwa kiini hicho hakitajwi tena, na kupata maana itabidi kipashio hicho kurejelewa kidhana tu kuziba pengo hili wala si kwa kuandikwa.

Quirk na wenzake (1972:536) wanashadidia hoja hii wanaposema kuwa udondoshaji hasa ni pale ambapo maneno yamedondoshwa lakini yanaweza kurejelewa katika sentensi. Mara nyingi maneno haya hudondoshwa katika sentensi zinazofuata na hurejelewa kidhana ili kupata maana ya matini. Wanadai kuwa udondoshaji ni kijenzi

kinachopunguza urudufishaji na kazi yake muhimu ni kukwepa urudufishaji katika matini. Hivyo ni wazi kuwa udondoshaji katika matini ni kuondoa urudufishaji wa kipashio au vipashio ambavyo huharibu mshikamano wa matini pindi vitaandikwa katika kila sentensi fuatilizi.

Verma na Krishnaswamy (1989:245) wanasema mtu hawezi kudondosha elementi kiholela. Baadhi ya elementi haziwezi kudondoshwa, na kuna zile ambazo zinaweza kudondoshwa. Kwa hivyo hii inaonyesha kuwa katika lugha, kuna ukubalifu wa kimuundo unaoruhusu udondoshaji. Mwandishi hawezi kudondosha atakavyo kwani anapofanya hivyo atapoteza maana na mshikamano wa matini. Katika Kiswahili viwakilishi nafsi vinaweza kudondoshwa katika sentensi mfano *wewe*, pia visifa vya Nomino Kiima (NominoK) katika vishazi, elementi zinazofanana katika tungo linganishi, na elementi zinazofanana katika sentensi ambatano au linganishi huweza kudondoshwa:

38. a) ( *Wewe*) Nenda nyumbani haraka.

b) Mtu huyo (tuliyemuona) ni mwizi.

c) Zahra ni mrefu kama mimi (ni mrefu pia).

d) i) Hamisi alienda kuogelea lakini Njuguna hakuenda (kuogelea).

ii) Otieno anasoma Kifaransa na Asha (anasoma Kifaransa) pia.

Maneno yaliyo katika mabano katika 38 (a – d) yanaweza kudondoshwa na sentensi bado zikaeleweka. Kudondoshwa kwao ni kwa sababu elementi hizi zimetangulia kutajwa kimuktadha katika matini.

Radford (1981:66-68) anasema kuwa katika hali fulani za usemi/matini baadhi ya vipashio vinavyofanana katika sentensi vinaweza kudondoshwa ikiwa kimoja kinatokezea kwingineko katika sentensi moja au katika usemi. Hapa, ifahamike kuwa sentensi moja aliyotaja Radford ni sentensi ambatano.

Salkie (1995) anafafanua udondoshaji na kueleza kuwa katika baadhi ya miktadha kuna uwezekano wa kuacha nje neno au kirai kuliko kurudufisha neno au kirai hicho. Aidha anatahadharisha kuwa si kila tunapoacha maneno nje, kuna udondoshaji. Lazima kuwe kuna sentensi tangulizi iliyotaja neno au maneno au jambo lililotokeza awali katika matini. Hata hivyo sentensi tangulizi hii ni sehemu ya sentensi ambatano.

Udondoshaji hutokea katika daraja ya sentensi. Hapa sentensi kamili hudondoshwa na kuachwa pengo la kimuundo katika matini. Udondoshaji huu huondoa urudufishaji na kuchangia mshikamano katika matini.

Thompson (2004:184) anashadidia kuacha pengo katika muundo wa sentensi, anapodai kuwa udondoshaji ni wakati kuna pengo lililowachwa na kujazwa na elementi zinazorejelewa kutoka kwa habari tangulizi. Anaendelea kudai kuwa udondoshaji hujitokeza zaidi katika usemi halisi kuliko maandishi, palipo na majibu "Ndiyo" au "La". Majibu haya hudhania maneno kutoka kwa taarifa tangulizi. Tutalii mifano hii.

39. Kaka aliniita chumbani mwake. Akanitumbulia macho na kuniuliza.
    "Ni nani alichukua mkoba wa wangu mle kabatini? Nilishangaa kwani nilikuwa sijaingia kwa siku tatu hivi.
    "Ni jibu haraka!" Alifoka.
    Kwa woga Juma akajibu, "La kaka ( )."

Katika matini hii sentensi " sijachukuwa mkoba wako." imedondoshwa katika usemi wa Juma. Kilichodondoshwa ni sentensi. Huu ni udondoshaji wa sentensi.

Katika udondoshaji vitenzi hudondoshwa pia katika matini badala ya kuvirudia rudia. Allerton (1975:212) anasema vipashio vya kiisimu vinavyorudufiwa mara nyingi hupunguzwa ukubwa na kubadilishwa na vibadala au kudondoshwa kabisa. (Katika sura hii hatuhusiki na vibadala bali udondoshaji). Anadai kuna udondoshaji wa lazima na udondoshaji wa hiari. Udondoshaji wa hiari ni ule wa kudondoa yambwa au kitenzi kinachofanya kazi ya kielezi katika kirai linganishi, na kazi yake ni kuondoa urudufishaji. Udondoshaji wa lazima hutokea wakati ambapo kipashio kinakatazwa (na sarufi) kutokea katika muundo.

40. "( 1 ) Nini?"
"Mfyatuko mkubwa"
"( 2 ) Wa tairi?"
"Hapana, ( 3 ) risasi; nyuma karibu na mgunga!"
"Mugogo unaota wewe?"
"Nimeamka Bwa 'Mbu!"
"Hatujasikia sie. Labda wengine (4)..."
(*Musaleo!* u.k. 6)

Katika usemi huu halisi, vitenzi 'Kusikia' (1) na 'walisikia', nomino 'Mfyatuko' (2) na kihusishi 'wa' (3) vimedondolewa. Vitenzi hivi, badala ya kurudiwa ni wazungumzaji vimedondolewa na kuacha mapengo ya kimuundo.

41. "Nendeni mkabadilishe nguo za shule, mje mnisaidie
kazi mie."
"Hee! Mama?" Zita alianza. "Hizi si nguo za shule mama."
Mamantilie alipandisha hasira, "Najua!( )"
(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 6)

Hapa yambwa 'nguo' imedondoshwa pamoja na kitenzi ungio 'si' na kivumishi 'za shule'. Huu ni udondoshaji wa hiari kwa sababu kishazi 'si nguo za shule' kinaweza kurudiwa kutajwa na sentensi ikakubalika kisarufi na ikawa na mshikamano vile vile.

Kutokana na maelezo yote haya ni kuwa udondoshaji wa kuleta mshikamano huwepo tu ikiwa neno, maneno au kishazi kimedondoshwa katika sentensi na kinapatikana tunaporejelea nyuma katika matini. Tunaporejelea elementi dondoshwa iliyo nyuma, ndipo dhana kamili inapatikana.

Udondoshaji ni wakati kisehemu cha muundo kimedondoshwa na kinaweza kupatikana kutoka kwa usemi uliotangulia (Crystal, 1997:119). Halliday (1976:288) anaeleza udondoshaji ni wakati ambapo kishazi au sehemu ya kishazi au sehemu ya kitenzi (ikijumuisha elementi ya kileksia) au kirai nomino, kinaweza kudondoshwa katika sehemu ya mbele katika matini kwa ala ya 'kuwachwa' katika muundo na pengo hilo linabaki wazi bila kujazwa. Burton-Roberts (1986: 100-103) anaeleza kuwa kuondoa elementi zinazohitajika katika sentensi ili kueleweka katika miktadha ya matumizi yake huitwa udondoshaji:

42. "Oh! Yule! Ni mwizi mkubwa. Pia ni mkorofi sana wakati mwingine." Halifani alisema.
 Siti na Halifani walinyamaza kimya. "Unakaa wapi?"
 "( ) Kisauni", Siti alijibu. "Na wewe ( )?

Katika matini hii, udondoshaji umetokea. Halifani alipomuuliza Siti anakokaa, Siti alijibu lakini alidondosha kitenzi "Ninakaa...". Na Siti alipomuuliza Halifani anakokaa, alidondosha kishazi "...unakaa wapi?". Kwa hivyo udondoshaji umetokea hapa.

Udondoshaji hutokea katika viwango mbalimbali vya sentensi. Leech na Svartivik (1975:165,168) wanadai kuwa udondoshaji unaweza kuwa wa sentensi yote au sehemu ya sentensi. Pia wanadai hutokea katika vishazi visoelekezi na vishazi viso vitenzi. Hatch (1992:225) naye anaeleza kwamba udondoshaji hutokea katika nomino, vitenzi na vishazi. Toolan (1998:27) anashadidia haya kwa kusema kuwa udondoshaji unaweza kuwa wa nomino, kitenzi na kishazi. Hii ni kumaanisha kuwa kinachoweza kudondoshwa katika matini ni nomino, kitenzi na kishazi.

Thomas (1979:43) anadai kuwa kuna udondoshaji wa lazima ili kudondosha nomino. Nao Allerton (1995) na Thomas (1979) pia wanasema kuwa kuna udondoshaji wa hiari na wa lazima. Udondoshaji wa hiari ni kwamba mwandishi anaweza akadondosha kipashio fulani au la na mshikamano haupotoki. Na udondoshaji wa lazima ni ule ambao ni lazima kipashio fulani kidondoshwe kwani bila hivyo mshikamano hupotoka na sarufi vile vile.

Halliday na Hassan (1976) wameeleza juu ya udondoshaji wa nomino, kitenzi na kishazi unavyotokezea katika matini. Halliday (1985) akashadidia maelezo haya kwa kuelezea vile vile udondoshaji wa kishazi, kirai kitenzi na kirai nomino. Vipashio hivi hudondoshwa katika sentensi ili kuleta mshikamano katika matini. Kwa hivyo kuna udondoshaji wa viwakilishi, vimilikishi, nomino, kitenzi, kirai nomino, kirai kitenzi, kishazi na sentensi.

### 2.1.4 Uunganishaji

Uunganishaji ni kule kuunganisha vipashio viwili au zaidi na wakati mwingine kipashio kimoja huwa tegemezi. Halliday na Hassan (1976) wanaeleza kuwa uunganishaji

hushirikisha na kuhusisha elementi za kiisimu zinazotokea zikifuatana mfululizo na hazina uhusiano wa kimuundo. Elementi hizi ni sentensi au vishazi au virai. Kwa hivyo uhusiano kati ya elementi hizi huletwa tu na uunganishaji. Uunganishaji huu huwa ni uhusiano wa kisemantiki wenye uamilifu wa mshikamano. Uunganishaji kama kipengele cha mshikamano ni kuangalia zile elementi za kiisimu zinazotokea mfululizo na zinavyohusiana katika matini wala si uhusiano wa kimuundo. Elementi hizi kwa kawaida huwa zina mshikamano wa kimaana (kisemantiki).

Viunganishi hutumika kuunganisha uhusiano wa kisemantiki kati ya sentensi iliyotangulia na ile inayofuta katika matini. Uunganishaji pia hutokea katika sentensi moja ikiwa kiunganishi kinaunganisha dhana inayotokea katika kishazi tangulizi na kile kinachofuata katika sentensi hiyo moja. Mfuatilizo wa wakati katika sentensi moja au mbili huwa kipengele cha mshikamano kwa sababu ya uhusiano wa kisementiki unaounganisha dhana mbili. Mfuatilizo huu huweza kuonyeshwa na kielezi. Hivyo kielezi kinakuwa kiunganishi.

Kuna viunganishi vya kategoria za kisintaksia (leksia) na kisemantiki. Viunganishi vya katagoria za kisintaksia ni vile ambavyo huunganisha sentensi katika daraja moja na kuunganisha sentensi katika daraja tofauti (Quirk na Greenbaum, 2000). Uunganishaji huu hujikita katika muundo wa sentensi. Viunganishi vinapounganisha sentensi kimuundo, huzaa sentensi ambatano. Mfano wa viunganishi vya kisintaksia ni *lakini, kwa sababu, au, wala, ingawaje* n.k. Hata hivyo viunganishi hivi hutumika pia

kuunganisha dhana, na vinapotumika hivi huwa na uamilifu wa kisemantiki unaoleta mshikamano katika matini.

Uunganishaji wa kisemantiki huenda zaidi ya viunganishi vya kategoria ya kisintaksia. Viunganishi vya kisemantiki, huunganisha dhana mbili au zaidi katika matini ambazo lazima ziwe na uhusiano kimuktadha. Aidha dhana moja hudhania dhana tangulizi. Uunganishi unapotokea katika hali hii, ndipo huleta mshikamano katika matini. Mfano wa viunganishi hivi ni, *hata hivyo, baada ya, kabla ya, baadaye, kisha, kwa minajili ya, kutokana na, hivyo, tena, pia, au, hatimaye, zaidi ya, kando ya*, n.k.

43. Mamantilie alichukua ndoo ya maji baridi na kuingia msalani. Alijimwagia akijisemea, "Maji dawa ya homa." *Baada ya* muda alitoka hadi chumbani.

(*Watoto wa Maman'tilie*, 2002:4)

*Baada ya* ni kielezi katika katagoria ya leksia lakini hapa kimetumika kama kiunganishi cha vitendo vinavyotendwa na Mamantilie; kuingia msalani + alitoka hadi chumbani. Hapa mwandishi ameunganisha vitendo viwili kwa kuelezea kilichotokea baada ya kitendo kimoja. na kuonyesha mfululizo wa vitendo vya Mamantilie. Kwa hivyo tunaona kitendo kimoja kilitokea na kingine kikifuata. Kufanya hivi, kiunganishi baada ya kimeshikanisha vitendo hivyo viwili kuonyesha mfululizo wa kutokea na kuleta mshikamano katika matini.

Uunganishaji wa kisemantiki ni pale ambapo msomaji hutafuta na kupata uhusiano wa kisemantiki kati ya sentensi zinazofuatana (Halliday na Hassan, 1976: 226-230; Quirk na Greenbaum, 2000: 262- 264). Hutokea sentensi mfululizo zikielezea habari fulani na hakuna viunganishi vilivyotumika. Lakini dhana zinazopatikana katika sentensi hizo

zinatiririka na kuungana kutoa maana. Inapotokea hivi, huo ni uunganishi wa kisemantiki:

44. a) Walikuwa kisiwani humo kwa muda mrefu. Hali ya upweke *na* mawasiliano waliyokuwa nayo yalikuwa ya kati yao hao wenyewe.

b) Siku zilienda. Maisha yakawa magumu jangwani humo. Jambo hili liliwahuzunisha mno. Walizidi kujipa moyo. Siku moja asubuhi waliona chombo kwa mbali kikiwajia. Matumaini yaliwajaa nyoyoni, wakajua usaidizi hatimaye umefika.

Katika mifano hii miwili; 44 a) tumeonyesha mshikamano kwa kutumia kiunganishi *na* , na b) kuna uunganishi usiotumia kiunganishi chochote katika matini na umeleta mshikamano. Uunganishi uliopo ni ule wa dhana na huitwa mshikamano wa kisemantiki.

Mshikamano wa kisemantiki hutokea pale ambapo sentensi zinahusiana kimaana. Mkururo wa sentensi unaweza kuhusiana kimaana kuleta umbo halisi katika matini. Sentensi hizi huelezea jambo lile lile katika aya moja au zaidi. dhana iliyotangulia huungana na ile inayofuata.

Jambo muhimu ni kwamba elementi moja inafasiriwa kwa kurejelea elementi nyingine katika matini. Wakati ufasiri wa maana unalazimika kutokea kwa kurejelea elementi nyingine katika matini, basi hapo mshikamano hujitokeza (kama hapo juu; 11). Kwa hivyo dhana ya mshikamano ni uhusiano kati ya sentensi, aya moja na nyingine au uhusiano kati ya maelezo.

Elementi za uunganishaji (viunganishi) zinasababisha mshikamano usio wa moja kwa moja bali wa maana mahususi na huelezea maana inayodhaniwa kuwepo katika viambajengo vingine katika matini au usemi. Yaani huunganisha maana au dhana inayokuja na ile ambayo imekwisha kutangulia.

> 45. Lakini ada? (1) Sare? Wapi! Jambo hili lilimsumbua akili Peter.
> Kuna siku halali. (2) Kuna siku hushinda njaa.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 14)

Tunapochunguza mfano huu 45, tunaona kuwa senentesi au dhana zilizopo zimeunganishwa na viughanishi visivyo dhahiri. Katika (1) kiunganishi *lakini* hakipo. Tukichunguza zaidi, katika pengo hili, kiunganishi *na* kinaweza kutumika. Kwa hivyo kati ya hivyo viwili chochote kinafaa. Na katika (2), kiunganishi hakipo lakini kidhahania kipo, nacho ni *Na*. Hakuna udondoshaji katika matini hii ila wakati mwingine viunganishi si dhahiri katika matini. Tuchunguze mfano mwingine:

> 46. Peter naye aliruka, akamzaba Doto makofi mawili mfululizo, lakini Doto alikuwa kazoea mapigano ya aina hii. Yeye na dada yake wamezaliwa vichochoroni. Walikuwa chokora namba moja. Kupigana,(1) kulala na njaa, (2) kukamatwa na polisi, (3) kupigwa na baridi, (4) kuugua *na* kuponea chupuchupu, haya yote yalikuwa sehemu ya maisha yao katika jiji hili.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k.22)

Katika 46 kiunganishi *na* kimedondoshwa katika vishazi tangulizi (1,2,3,4) isipokuwa kile kinachofuata kitenzi nomino cha mwisho, *kuponea chupuchupu*. Viunganishi hivi vilikuwa vinaunganisha vishazi katika matini.

Uunganishaji unaweza kuwa wa Kundi Nomino (KN) na Kundi Elezi (KE) au Kundi Komino na Kundi Vumishi (KV) (Burton-Roberts, 1986:62). Uunganishaji huu ni wa

ndani ya sentensi. Kuna uunganishaji kwa kutumia viunganishi mfano *na, tena, kisha, au* n.k kati ya sentensi, na uko uunganishaji wa kisemantiki ambapo viunganishi havitumiki. Utafiti huu uliongozwa na dhana hii kuchunguza mshikamano wa kisarufi katika Kiswahili.

## 2.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

### 2.2.1 Mshikamano kwa Jumla

Swala la mshikamano lilishughulikiwa na wataalamu mbalimbali. Baadhi ya wataalamu hawa walichunguza mshikamano kwa jumla na wengine walichunguza baadhi ya vipengele fulani vinavyochangia mshikamano katika sentensi au matini. Wengi wao walichunguza mshikamano katika Kiingereza na wachache walishughulikia mshikamano katika Kiswahili mfano Barongo (1996), Mohamed (1986) na Contini- Morava (1985).

Barongo (1996) alitafitia swala la mshikamano kwa jumla katika insha za Kiswahili za wanafunzi wa kidato cha nne, Wilayani Kisii, nchini Kenya. Alichunguza vijenzi vyote vya mshikamano jinsi vilivyotumika katika insha za wanafunzi hao. Pia alichunguza kama vilitumika kwa usahihi ili kujenga mshikamano unaotakikana katika insha. Na alipata kwamba wengi wa wanafunzi hawakutumia vijenzi hivyo kwa usahihi katika insha zao, hivi kukosa mshikamano na kutuzwa alama za chini. Utafiti wa Barongo ulisaidia utafiti huu kufafanua mshikamano na jinsi vijenzi vya mshikamano wa kisarufi hujitokeza katika Kiswahili.

Contini- Morava (1985) naye alizungumzia mshikamano wa matukio katika usimulizi wa Kiswahili. Alichunguza matumizi ya viwakilishi vya wakati uliopita; LI, KA na KU katika usimulizi wa Kiswahili. Alifafanua dhana ya viwakilishi hivi, sababu zilizomfanya mwandishi au mzungumzaji kuteua kimojawapo na athari mbalimbali za viwakilishi hivi katika maana zao juu ya kinachowasilishwa. Yeye basi alishughulikia nyakati hizo tatu zinavyochangia mshikamano katika usimulizi wa Kiswahili. Hakuchunguza jinsi vijenzi vya mshikamano wa kisarufi katika Kiswahili vinatumika kwenye matini. Utafiti huu ulisaidia katika kuonyesha mshikamano wa dhana bila matumizi ya viunganishi. Huu ni mshikamano wa kisemantiki.

Halliday (1985: 287-297) alielezea dhana ya mshikamano katika sura moja katika kitabu chake *Functional Grammar*, akijikita katika Kishazi, Kundi Tenzi na Kundi Nomino katika lugha ya Kiingereza. Akafafanua njia nne ambazo huleta mshikamano katika matini. Akaziorodhesha kama ifuatavyo (kama hapo juu:288).

i) urejeleaji

ii) udondoshaji na ubadilishaji

iii) uunganishaji

iv) mpangilio wa msamiati

Alifafanua vijenzi hivi akitoa mifano ya Kiingereza. Pia naye hakushughulikia Kiswahili. Alizungumzia mshikamano kwa jumla katika Kiingereza tofauti na utafiti huu. Maelezo yake yalifaidi utafiti wetu kufafanua vijenzi vya mshikamano wa kisarufi.

Omondi (1993) vile vile alichunguza umilisi wa mshikamano unavyohitajika katika uandishi wa insha za Kiingereza. Alichunguza kazi za insha za Kiingereza za wanafunzi wa kidato cha nne wa shule za upili Wilayani Migori, Kenya. Aliangalia matumizi ya vijenzi vya mshikamano katika usemi andishi. Alichunguza mshikamano wa kisarufi na kileksia kwa pamoja. Alichunguza matumizi ya urejeleaji, ubadilishaji, udondoshaji, uunganishaji na leksia katika insha hizo. Katika uchunguzi huu alitumia maswali ya uteuzi, kujaza vijenzi vya mshikamano katika mapengo ambamo vjijenzi viliachwa kwa maksudi na katika insha zilizoandikwa na wanafunzi wenyewe. Hata hivyo utafiti wake ulisaidia utafiti wetu katika ufafanuzi wa mshikamano kwa jumla.

Mchunguzi mwingine alikuwa Olateju (2006). Alichunguza jinsi vijenzi vya mshikamano vilitumika katika insha za Kiingereza za wanafunzi huko Shule ya Upili ya Wasichana ya Ooni, Jimbo la Osun, nchini Nigeria ambao Kiingereza ni lugha yao ya pili. Alichunguza vijenzi hivyo katika mshikamano wa kisarufi na mshikamano wa kileksia. Data aliyoipata ilidhihirisha kuwa wanafunzi hawakuwa na umilisi wa kutumia vijenzi hivi. Hivyo insha zao zilikosa mshikamano ingawaje walikuwa wamejifunza Kiingereza kwa muda wa miaka sita sekondari. Matokeo ya utafiti wake aliyaandika kwenye makala tu. Kwa hivyo huyu alichunguza mshikamano kwa jumla katika matini za Kiingereza kama inavyodhihirika katika makala yake. Utafiti wake ulisaidia utafiti wetu kuangalia ni vijenzi vipi vya mshikamano wa kisarufi hutokea zaidi katika matini za Kiswahili.

Mwingine aliyezungumzia mshikamano ni Hubbard. Hubbard (2000:245-262) alizungumzia mambo kadhaa katika makala yake "Usemi: Lugha katika Muktadha".

Yeye alizungumzia kwa jumla muwala katika usemi. Akasema (kama hapo juu:257) kuwa usemi unakuwa na mshikamano, kwa maneno mengine, mshikamano hujenga makala kwa jumla, iliyoungana na yenye maana. Hapo akaelezea aina tano za mshikamano; urejeleaji, ubadilishaji, udondoshaji, uunganishaji na mshikamano wa kileksia. Alidokezea vile kila aina inavyojenga mshikamano katika sentensi na vishazi, usemi au matini. Alielezea aina hizi kwa muhtasari na kuzifafanua akitumia mifano ya sentensi katika Kiingereza. Katika utafiti huu aina hizi hatukuziita aina bali vijenzi vya mshikamano kwani ndivyo hutumika katika matini kuleta huo mshikamano. Akatoa mifano yake kutoka kwa barua kwa mhariri katika gezeti moja mashuhuri ambalo hakulitaja. Barua hiyo iliandikwa kwa Kiingereza. Utafiti wake ulisaidia utafiti wetu katika ufafanuzi wa vijenzi vya mshikamano wa kisarufi.

Crystal (1997: 116-119) alielezea vile uchanganuzi wa sentensi umepiga hatua kinyume na vile wanamapokeo walivyokuwa wakichunguza. Akazungumzia uchunguzi wa sentensi za Kiingereza:

> Uchanganuzi wa sentensi wa kimapokeao ni wa utungaji sentensi. lakini miaka ya hivi karibuni kumeongezeka msukumo wa kuchanganua vile sentensi katika mfuatiliano huleta muwala na mshikamano wa lugha. Sentensi zikishikana hivi huunda matini na uchunguzi wa matini huchunguza muundo wa lugha iliyoandikwa. (kama hapo juu:116) (Tafsiri yetu)

Katika kufafanua haya, Crystal alielezea mshikamano ni nini na alitoa mifano ya vijenzi vya mshikamano vikiwemo udondoshaji katika sentensi za Kiingereza. Naye vile vile hakushughulikia Kiswahili. Utafiti wake ulisaidia utafiti huu kufafanua mshikamano na vijenzi vyake.

Toolan (1998: 23-45) alipokuwa anatalii lugha katika fasihi alifafanua mshikamano katika matini. Alichunguza vile sentensi zinavyosukwa katika matini ili kuleta mshikamano. Katika uchunguzi huu aligusia vijenzi mbalimbali vya mshikamano vikiwemo urejeleaji, udondoshaji, uunganishaji na mshikamano wa kileksia. Vijenzi hivi alivijadili kwa muhtasari jinsi vinavyotumika katika matini za Kiingereza. Akatoa mifano kutoka kwa majibizano aliyoyatunga mwenyewe na shairi moja la Kiingereza. Alieleza mshikamano kama njia ya kiisimu ambayo hutumika kuunganisha sentensi pamoja kujenga matini. Akaeleza kuwa matini hujengwa na sentensi na huhitaji kuunganishwa kwa njia mbalimbali ili zishikane pamoja. Hivyo mshikamano hurejelea njia zote za kiisimu ambapo maneno katika matini, kupitia sentensi hurejeleana na kuungana. Utafiti wake ulisaidia utafiti wetu kupambambanua vijenzi vya mshikamano vya Kiswahili na jinsi vinavyotumika katika matini.

Yule (1997:140-142) alielezea juu ya mshikamano na muwala katika lugha. Akasema kwamba matini inahitaji muundo fulani tofauti na ule wa sentensi moja. Akaita vishikanishi vinavyojitokeza katika matini kuwa ndio mshikamano. Akatoa mfano wa matini ndogo ya Kiingereza kufafanua hoja yake. Akaeleza kuwa vishikanishi hivi huweza kuwa viwakilishi vya nafsi na viunganishi vya leksia. Akaendelea kueleza kuwa vishikanishi katika matini hutoa mwangaza jinsi wandishi hutumia muundo fulani kuelezea au kusimulia katika matini zao. Katika matumizi haya ya vishikanishi ni lazima vitumike kwa hali ya kuleta muwala. Hivyo yeye alielezea viwakilishi nafsi na viunganishi vya kileksia, hakushughulikia vijenzi vyote vya mshikamano, wala si katika Kiswahili. Utafiti wetu hautashughulikia mambo ya leksia. Hata hivyo utafiti wake

ulitusaidia kuchanganua viwakilishi nafsi kama urejeleaji na jinsi vinavyochangia mshikamano wa matini.

Salkie (1995) katika uchanganuzi wa matini na usemi, alieleza aina za mshikamano na vijenzi vyao. Alibainisha mshikamano wa kileksia na mshikamano wa kisarufi na kuonyesha jinsi vijenzi vya aina hizi za mshikamano vinatumika katika matini za Kiingereza. Alionyesha urejeleaji, udondoshaji, ubadilishaji, uunganishaji na mshikamano wa kileksia. Katika mifano yake alitumia dondoo kutoka matini za Kiingereza za magazeti ya Uingereza mfano '*The Gurdian*', '*Economic Times*' na hotuba mbalimbali. Mshikamano wa kileksia akaeleza kwamba ni ule huletwa na urudufishaji wa maneno, matumizi ya visawe, maneno jumuishi mfano hiponimu, antonimu na maneno husishi. Pia akaeleza mshikamano wa kisemantiki unavyojitokeza katika matini za Kiingereza ambao hautegemei vijenzi vya mshikamano. Huyu pia hakushughulikia Kiswahili lakini utafiti wake ulisaidia utafiti huu katika kuchunguza na kuchanganua mshikamano wa kisarufi katika Kiswahili ambao hujumuisha dhana zinavyoshikanishwa.

Carrell (1982) alijadili swala la mshikamano katika makala yake, "Mshikamano si Muwala". Alipinga nadharia ya Halliday na Hassan ya mshikamano (1976) akijiegemeza katika nadharia ya *Schema*. Katika madai yake ni kwamba mshikamano katika matini hauleti muwala bali ni habari ya awali aliyonayo msomaji au mwandishi ndiyo hutumika kupata mshikamano na muwala katika matini wala si vijenzi vya mshikamano kama wadaivyo Halliday na Hassan. Kwa hivyo, anavyodai Carrell si kweli kwa sababu habari-tangulia aliyonayo msomaji au mwandishi huwa anairejelea kutoka nje, na hiyo ni njia

mojawapo ya kuleta mshikamano katika matini. Yeye alikosoa tu nadharia ya hawa wawili kuhusu mshikamano katika Kiingereza. Hali kadhalika hakushughulikia Kiswahili. Mjadala wake ulitupa ufahamu wa mshikamano katika matini bila viunganishi. Coulthard (1977: 9-10) aligusia tu mshikamano alipokuwa anazungumzia 'Uchanganuzi wa Usemi' na kwamba sentensi huungana kujenga matini, na uhusiano kati ya sentensi ni vipengele vya mshikamano wa kisarufi. Na hakueleza uhusiano huu huja vipi. Akatoa mifano miwili ya Kiingereza kuonyesha tofauti kati ya mshikamano na muwala katika usemi. Katika mifano hiyo miwili akasema kuwa wa kwanza ndio una mshikamano kwa sababu udondoshaji umetokea. Alieleza kwamba matamshi huungana kuunda usemi na uhusiano wao ni kipengele cha muwala. Haya aliyazungumza katika aya mbili tu. Hakuzungumzia vijenzi vyote vya mshikamano isipokuwa mfano huo wa udondoshaji. Aidha hakuzungumzia Kiswahili. Hata hivyo alitupa mwanga katika suala la mshikamano katika matini.

Halliday na Hassan (1976) walielezea mshikamano katika Kingereza na walipambanua aina mbili za mshikamano;

i) Mshikamano wa kisarufi

ii) Mshikamano wa kileksia.

Wakazidi kuelezea jinsi vijenzi vinavyojenga kila aina mojawapo. Wakajadili mshikamano wa kisarufi unavyotokea katika Kiingereza na kutoa mifano mbalimbali ya Kiingereza ya mshikamano wa kisarufi. Vile vile wakaelezea uteuzi mantiki, urudufishaji wa maneno, visawe, antonimu na maneno fanani zinavyounda mshikamano wa kileksia

(kama hapo juu:5-6). Hawakuzungumzia Kiswahili lakini maelezo na ufafanuzi wao ndio ulikuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu.

### 2.2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Urejeleaji

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inaeleza kuwa urejeo (urejeleaji) ni hali ya kipashio kimoja cha kiisimu kudokeza juu ya kipashio kingine kilichotangulia. Halliday na Hassan (1976) walielezea urejeleaji wa Kiingereza kama kijenzi kimojawapo cha mshikamano.Wakafafanua aina mbili kuu za urejeleaji; mrejeondani na mrejeonje. Wakafafanua mrejeondani na mrejeonje unavyotokea kwa kutoa mifano ya Kiingereza:

47. Three blind mice, three blind mice.
See how they run! See how they run!
(Halliday na Hassan, 1976:31; 2.1a)

Katika mfano huu, wakaeleza kuwa *they* inarejelea *Three blind mice*. Huu ni mrejeondani. Kirejelea *they* kinarejelea kirejelewa kilicho ndani ya matini nacho ni *Three blind mice*. Mrejeondani wakaeleza ni wa aina mbili; mrejeonyuma na mrejeombele. Mrejeonyuma ni wakati kirejelea kinarejelea kirejelewa kilicho nyuma, kama katika 9. ambapo *they* inarejelea hao *three blind mice* waliotajwa mwanzo. Katika mrejeombele, hawakutoa mfano. Hata hivyo mfano wa mrejeombele ni:

48. *A*licheza vizuri sana leo. Kila mmoja alifurahia hasa pale *Omari* alipochenga mabeki wawili wa Gor Mahia na kupiga mkwaju mpaka ndani na vile vile kuchangia kupatikana kwa bao la ushindi.

Hapa *A*- ni kirejelea cha *Omari* (kirejelewa) aliyetajwa mbele katika matini na kirejelea *A*- kutangulia. Hivyo *A*- kinarejelea mbele (*Omari*).

Mrejeonje walieleza ni wakati kirejelea kinarejelea nje ya matini. Wakatoa mfano:

49. That must have cost a lot of money.

(Halliday na Hassan, 1976:33; 2.3)

Katika mfano huu, wanadai *That* ni kirejelea kinachorejelea nje. Hata hivyo wanadai pana utata wa kufahamu iwapo ni mrejeleonje au mrejeleondani. Hii ni kwa sababu, kimuktadha lazima mzungumzaji huyu anarejelea kirejelewa ambacho wanakizungumzia na mwenzake.

Aidha waliendelea kuelezea aina mbalimbali za urejeleaji. Aina hizi ni urejeleaji nafsi, onyeshi na urejeleaji linganishi. Wakaeleza kuwa vitambulisho vya urejeleaji nafsi ni viwakilishi nafsi: *I, we, she, he, they, it* (kama hapo juu:44). Urejeleaji nafsi hudhihirishwa na *the, this, that, these, those, here, there, now, then* (kama hapo juu:57). Urejeleaji linganishi wakasema hudhihirishwa na *same, equal, identical, identically, such similar, so similarly likewise, more, fewer, less, further, additional, differently, otherwise, better, more, less* (kama hapo juu:77). Mifano hii ni ya Kiingereza lakini katika utafiti wetu tulitumia mifano ya Kiswahili kueleza na kufafanua urejeleaji katika matini za Kiswahili. Maelezo ya Halliday na Hassan yalisaidia sana katika utafiti wetu.

Munyua naye (1992:39) anadai kuwa "urejeshi" (urejeleaji) unadhihirika kupitia kwa matumizi ya viwakilishi nafsi na vimilikishi, vivumishi milikishi, viashiria vikitumika kama viwakilishi au vivumishi, na vielezi na vivumishi vya ulingano. Akatoa mifano:

50. a) Ali alituhadithia *hadithi* ya fisi. *Ile* ya sungura hakuifahamu.

b) Rabeka alikuwa anateswa sana na bwanake. *A*likuwa amekonda sana aliporudi kwa wazazi *wake.*

c) *Viazi vitamu* vilipikwa vizuri. Baba yangu ali*vi*furahia.

(Munyua, 1992, 22a-c)

Katika 50 (a) kiashiria *Ile* kinarejelea neno *hadithi*. (b) kiwakilishi nafsi "*A-*" kinarejelea '*Rabeka*' na kimilikishi *wake* kinarejelea 'wazazi wa Rabeka'. Katika (c) kiambishi *–vi-* katika kitenzi alivifurahia kinarejelea *viazi vitamu*.

Kwa hivyo viwakilishi nafsi ni muhimu sana katika kuleta mshikamano katika Kiswahili na ni lazima katika urejeleaji kwa mujibu wa muundo wa lugha hii (Mohammed, 2001:58).

Urejeleaji katika Kiswahili hujitokeza kwa njia mbalimbali. Hujitokeza kama uwakilishi wa nafsi, viashiria, viulizi, vimilikishi, virejeshi, jirejee (Munyua, 1992). Mara nyingi urejeleaji huchukuliwa kuwa katika tungo rejeshi ambapo sentensi au kishazi hushushwa daraja na kuwa sentensi au kishazi tegemezi (Mekacha, 1987). Lakini urejeleaji hasa wa mshikamano katika matini huenda zaidi ya hivyo. Hujumuisha uwakilishi wa nomino.

Munyua (1992: viii) anaeleza kwamba kiwakilishi baada ya KN kinachotambulikana kutokana na mazungumzo ya awali yanadumisha KN hiyo kama kitu kimojawapo kati ya vinavyozingatiwa katika usemi. Kwa hivyo uwakilishaji ni urejeleaji na tuliuchukulia hivyo katika tasnifu hii. Hata hivyo Munyua (1992: viii) anadai kuwa uwakilishaji katika Kiswahili umeonekana kutokea katika upande wa mbele pekee. Uwezekano wa kutokea uwakilishaji wa nyuma umekataliwa.

Yeye hatuambii umekataliwa na nani. Inaonekana ameathiriwa na Delisle (1973: 18) anayedai kwamba katika usemi sahihi au kubalifu, hakuna kabisa kitu kama uwakilishaji

nyuma. Mtaalamu huyu alikuwa anashughulikia uwakilishaji katika usemi katika lugha ya Kiingereza. Sisi tunapinga maoni haya kwani uwakilishaji wa nyuma unaweza kutokea katika Kiswahili:

51. a) "Aaa! Nasikia afueni kidogo. *Huu mwarubaini* umenifaa mwanangu. Kesho, nadhani nitarudi kazini kwangu. Nimezikosa *pesa* leo Zenabu."

(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k.5)

b) "Mamantilie ali*m*tupia jicho *bintiye, Zita* akasema..."

(*Kama hapo juu*,u.k. 6)

Katika 51 (a) na (b) uwakilishaji wa nyuma wa KN, mwarubaini, umetokea. Katika (a) *huu* inawakilisha *mwarubaini* na (b) *m-* inawakilisha *bintiye, Zita.*

Pia Mohammed (2001:114-115) anapinga wazo la Munyua (1992) na Delisle (1973) anapoelezea kwamba wanasarufi zalishi wameonyesha kuwa uwakilishaji unaweza kutokea nyuma au mbele na akatoa mifano katika Kiswahili 24.a) na (b)

52. a) *A*lipoingia chumbani tu, *John* akaanza kula chakula.

b) *Salima* kauza gari mpya *a*li*yoi*nunua hivi karibuni.

c) Mimi napenda msichana aliye *hivi*; mrembo, mrefu, mwenye kiuno cha nyigu na heshima nyingi.

(Mohammed, 2001: 114-115)

Katika sentensi (a) *A-* inawakilisha *John*, (b) *a-* inawakilisha *Salma* na *–yo-, -i-* zinawakilisha gari, na (c) *hivi* (ni kibainishi) inawakilisha sifa zilizotolewa za msichana, hivyo kuonyesha uwakilishi nyuma. Hata hivyo katika (a) Delisle (1973) amepinga kuwa pana uwakilishaji. Anadai kuwa sentensi moja hii haiwezi kuchanganuliwa kisarufi

katika uwakilishaji ila usemi ndio unaoweza kuchunguzwa kudhihirisha uwakilishaji. Tasnifu hii haitaingia katika mabishano hayo.

Lazima ifahamike kwamba kuna tofauti kati ya urejeleaji na uwakilishaji. Urejeleaji nyuma ni uwakilishi mbele na urejeleaji mbele ni uwakilishaji nyuma. Tasnifu hii itatumia urejeleaji tu. Kwa hivyo uwakilishaji utaitwa urejeleaji na kuonyeshwa katika dhana ya urejeleaji nyuma na mbele na nje.

Viwakilishi nafsi katika sintaksia ya Kiingereza ni kama *Mimi, Sisi, Wewe, Yeye* (mke au mume), *Wao* na *ki*-(it). Hivi husemekana vinasimama kama vibadala vya nomino zilizotangulia kutajwa. Wakati mwingine husimama badala ya kundi nomino zima si nomino tu (Postal, 1976:201). Viwakilishi hivi pia hupatikana katika Kiswahili na hatutaviita vibadala bali virejelea.

Viwakilishi nafsi vijulikanavyo zaidi katika urejeleaji ni; *mimi, yeye, sisi, wao* na *ki*- pamoja na hali zao za umilikaji (Salkie, 1995; Halliday, 1985; Halliday na Hassan, 1976). Katika Kiswahili urejeleaji nafsi huenda zaidi ya hivyo na kutumia viambishi vya nomino pia (Mohammed, 2001; Mgullu, 1999; Munyua, 1992; Mekacha, 1987; Mbaabu, 1985; Kapinga, 1983; Ashton, 1944). Kwa hivyo uambishaji wa nomino unapotokea katika matini ni urejeleaji. Urejeleaji huu ni ule unaoleta mshikamano.

Barongo (1996: 20-21) aidha, alifafanua urejeleaji. Akaeleza kwamba urejeleaji ni uhusiano wa kisemantiki baina ya sehemu mbalimbali zinazoiunda matini. Hapa,

maumbo fulani ya lugha hutumiwa kurejelea faridi fulani za kiisimu ambazo ama hutokea mwanzoni mwa matini au baadaye. Maumbo haya hayawezi kufasiriwa bila ya kurejelewa katika faridi hizi. Hii ina maana kuwa faridi hizo husimamiwa na virejelea vinavyowakilisha maumbo hayo. Na kufasiri maana katika matini, lazima virejelea hivyo vihusishwe na virejelewa. Hivyo kuleta mshikamano wa kisarufi katika matini.

Vile vile Hatch (1992:223-233) alichunguza vijenzi vya mshikamano, jinsi vinavyounganisha vipande au sentensi katika matini kwa njia mahususi. Aligusia urejeleaji na vionyeshi vyake kama vile viwakilishi, vionyeshi, vilinganishi kama vijenzi vya mshikamano. Pia alionyesha viwakilishi nafsi, vionyeshi na vilinganishi kama vijenzi vya mshikamano. Haya yote aliyachunguza katika Kiingereza wala si katika Kiswahili. Ufafanuzi wake ulisaidia utafiti wetu katika kuchanganua urejeleaji kama kijenzi kimojawapo cha mshikamano wa kisarufi.

Olateju (2006:319) katika kuchunguza insha za wanafunzi wa Shule ya wasichana ya Ooni, Jimbo la Osun, Nigeria alizungumzia urejeleaji na vionyeshi vyake. Vionyeshi alivyovitaja ni viwakilishi nafsi; *he, she, it*. Pia akaonyesha vionyeshi *the, this* na *that* akidai kuwa matumizi yake huchangia mshikamano katika matini. Aliendelea kuelezea mrejeondani na mrejeonje kisha akatoa mifano:

53. I shall give you this report now; Bola missed the plane at last.

(Olateju; No.6)

Mfano huu alisema ni wa mrejeombele. *this* inarejelea *Bola missed the plane at last*. Kwa hivyo *this* inarejelea mbele. Huu ndio mrejeombele.

54. Tinu can never agree, she has decided to go.

(Olateju; No.7)

Akaeleza kwamba mfano huu ni wa mrejeonyuma. *she* inarejelea *Tinu* na ametajwa awali katika matini. Kwa hivyo *she* inarejelea nyuma. Huu ndio mrejeonyuma. Katika uchanganuzi wake akaonyesha matumizi mabaya ya urejeleaji katika isha za wanafunzi hao na isha zao kukosa mshikamano. Utafiti wake, ingawa ulikuwa wa Kiingereza, ulitusaidia kuchanganua urejeleaji katika matini za Kiswahili.

Toolan (1998:25-26) aligusia urejeleaji katika kitabu chake *Language in Literature*. Alieleza urejeleaji kama aina mojawapo ya mshikamano na unatokea wakati kuna matumizi ya neno la kisarufi katika sentensi moja iliyotangulia likihusishwa na neno au kirai katika sentensi tofauti. Pia akaelezea aina za urejeleaji; urejeleaji nafsi na urejeleaji linganishi huku akionyesha vionyeshi vyake. *it, its* ni vionyeshi vya urejeleaji nafsi. *this, that, these, those, here, there, then* kama vionyeshi milikishi katika urejeleaji nafsi. *same, similar, such, different, other, more, less, first, secondly, as* na vilinganishi vya vivumishi na vielezi. Maelezo haya tunatofautiana nayo katika uanishaji wake wa urejeleaji. Sisi tumeainisha aina tatu; urejeleaji nafsi, urejeleaji onyeshi na urejeleaji linganishi. Hata hivyo maelezo ya Toolan yalitusaidia katika uchunguzi wetu wa urejeleaji katika Kiswahili.

Hubbard katika Webb na Kembo Sure (2000:258-259) alizungumzia urejeleaji kama kijenzi cha mshikamano. Alieleza elementi za urejeleaji katika Kiingereza kama viwakilishi nafsi (*I, me, we, us, you, he,she, it* na *they*), viwakilishi milikishi (*my, our,*

*your, his, hers, its na their*), faridi mahususi na vibainishi (*the, this, these, that, na those*) na vionyeshi elezi (*here, there,* na *then*). Akaeleza kuwa si nyakati zote elementi hizi hutumika kimshikamano na akatoa mfano wa neno *the* kwamba wakati mwingine halidhanii neno lililotangulia awali:

> 55. Many people are dying as a result of cigarettes and alcohol.
> I appreciate that the government has raised the price on these items because it wants people to quit or consume less than they usually do.
> (Hubbard, 2000:258)

Hapa *the* inayofuata neno *government* si elementi ya mshikamano kwa sababu haidhanii elementi yoyote nyingine katika matini hii. Vile vile anaeleza kwamba viwakilishi vya nafsi, vimilikishi, vionyeshi na vielezi onyeshi ni elementi za mshikamano. Kwa hivyo urejeleaji ni ile hali katika matini ambapo faridi moja hurejelea nyingine ndani au nje ya matini hiyo ili kuweza kufasirika na kuleta maana. Bila kurejelea faridi iliyotangulia, faridi ya mbele haileti maana wala mshikamano. Katika kuleta mshikamano na maana, faridi inayorejelea nyingine huwa vikiwakilishi nafsi, vimilikishi, viashiria au vielezi. Haya ndiyo maelezo yaliyozingatiwa katika utafiti huu kuhusu urejeleaji.

Quirk na Greenbaum (2000: 302) walielezea urejeleaji wa usemi. Wakasema kuwa urejeleaji ni pale ambapo kinachozungumzwa na kilichozungumzwa vina uhusiano. Vitu hivi huletwa pamoja na urejeleaji. Urejeleaji huu huweza kuwa wa nyuma (mrejeosabiki) au wa mbele (mrejeombele) katika usemi. Wakatoa mifano ya Kiingereza katika kufafanua aina hizi za urejeleaji. Wakafafanua na kuonyesha kwa mifano ya Kiingereza urejeleaji wa Kirai Nomino na urejeleaji linganishi. Maelezo haya yalisaidia utafiti wetu katika kuzifahamu na kuzichanganua dhana hizi katika Kiswahili, na mifano yetu ikawa ya Kiswahili kutoka matini zetu teule.

Pia Thompson (2004:180-184) alizungumzia urejeleaji na kutoa mifano yake kutoka Kiingereza. Alieleza urejeleaji kuwa ni seti ya rasilimali ya kisarufi inayoruhusu msemaji kutambua iwapo kitu kinarudiwa kutoka kwingineko katika matini ambacho kimeshatangulia au kama hakijatajwa bado katika matini hiyo. Aidha alielezea aina za urejeleaji; mrejeonje na mrejeondani. Aina hizi alizifafanua akitumia sentensi mbili za Kiingereza. Akaendelea kusema kuwa mrejeonje huunganisha lugha katika muktadha ulio nje ya matini, na mrejeondani huonyesha jinsi ujumbe hujikita katika muktadha hususan ulio ndani ya matini.

Kisha akaeleza kuwa urejeleaji unaweza kuwa mrejeonyuma au mrejeombele, na mara chache tu, kuna mrejeonje. Naye kama wale niliotangulia kuwataja, alielezea aina tatu za urejeleaji; urejeleaji wa kutumia viwakilishi nafsi, urejeleaji onyeshi na urejeleaji linganishi. Alionyesha elementi za urejeleaji wa nafsi ya tatu kuwa ni *he* na *it* tu. Ule onyeshi akatoa elementi *this, that, these, those, here, there, the, now* na *then*. Kati ya hizi, akafafanua matumizi ya *this* na kusema kuwa hurejelea msururu wa sentensi katika matini. *The* akaeleza kuwa husimamia dhana ya "unajua kile kinachoelezewa, ama kwa kuwa kimeshatajwa au kwa sababu kinataka kuelezewa au kinafahamika kwa msikilizaji kutokana na ufahamu au tajriba yake". Kisha akasema kuwa urejeleaji linganishi hutokea wakati vitu viwili vinalinganishwa. Urejeleaji linganishi huleta mshikamano kwani huwa kitu kimoja kati ya viwili hivyo huwa kimeshatajwa. Akatoa mfano:

56. Do you want some *more* wrapping paper?

(Thompson, 2004:183)

Katika mfano huu, anadai kuwa lazima neno *paper* lilikuwa limeshazunguziwa awali na wote, msemaji na msikilizaji wanafahamu hili. Akataja elememti linganishi; *more, another, different, the same* na *similarly*, na zote zinaleta mshikamano katika matini. Maelezo haya yote, ingawaje yalitolewa kwa Kiingereza na mifano kutoka Kiingereza vile vile, yalisaidia sana katika kutupa mwelekeo wa kuchunguza na kuchanganua urejeleaji katika Kiswahili.

### 2.2.3 Yaliyoandikwa kuhusu Ubadilishaji

Halliday na Hassan (1976:88-89) walifafanua dhana ubadilishaji. Walielezea kuwa ubadilishaji hutokea katika matini na ni kuweka faridi moja badala ya nyingine. Faridi moja hutumika kama kibadala cha faridi nyingine badala ya kuirudia. Katika ubadilishaji, kuna uhusiano wa faridi za kiisimu kama vile maneno na virai. Uhusiano huu huwa katika kiwango cha sarufileksia. Walitoa mifano ya Kiingereza kufafanua dhana hii:

57. a) My *axe* is too blunt. I must get a sharper *one*.
b) You think Joan already *knows*?- I think everybody *does*.
(Halliday na Hassan, 1976:89)

Katika mifano hii walieleza kuwa *one* katika (a) na *does* katika (b) ni vibadala. *one* ni kibadala cha nomino *axe* na *does* ni kibadala cha kitenzi *knows*. Wakaeleza, kama sheria ya jumla, kibadala kina uamilifu wa kimuundo sawa na faridi iliyobadilishwa. Hivyo *one* na *axe* ni viini katika kirai nomino, na *does* na *knows* ni viini katika kirai kitenzi. Wanadai kuwa mara nyingi ubadilishaji huwa sabiki, na mara chache sana ubadilishaji huwa nje. Vile vile waliainisha ubadilishaji katika aina tatu;

a) Ubadilishaji wa nomino

b) Ubadilishaji wa kitenzi

c) Ubadilishaji wa kishazi

Aina hizi walizifafanua na kutoa mifano ya Kiingereza na kuelezea masharti ya udondoshaji wa nomino, kitenzi na kishazi. Ufafanuzi huu ulitupa mwongozo wa kuchanganua ubadilishaji katika Kiswahili.

Thompson (2004) alielezea ubadilishaji katika Kiingereza. Aliainisha ubadilishaji kutegemea vibadala vinasimamia nini. Akasema kuwa katika miktadha fulani *so, neither* na *nor* husimama badala ya vitenzi na hata vishazi. Mifano mbalimbali aliitoa kuonyesha ubadilishaji huo:

58. a) 'Are you there, Luce?'
'I've just said so [=that I'm there].'

b) 'Do you think it is possible?'
'I hope not [=that it is (not) possible].'
(Thompson, 2004:187)

Mifano hii yote inaonyesha ubadilishaji wa kirai; katika (a) *so* ni kibadala cha kirai 'that I'm there' na (b) *not* ni kibadala cha kirai 'that is not possible'. Huu ndio ubadilishaji. Hata hivyo vibadala katika Kiingerza ni tofauti na vile vya Kiswahili kwa sababu ya utofauti wa miundo. Katika mifano 58 (a) na (b) *so* katika Kiswahili ni *hivyo* na *not* ni *si-*. Suala hili lilijitokeza katika Sura ya Tatu ambapo swala la ubadilishaji katika matini za Kiswahili lilichanganuliwa. Maelezo haya yalisaidia utafiti wetu kuchunguza ni vipashio gani vya kimuundo hubadilishwa katika Kiswahili.

Brown na Jim Miller (1991: 24, 55, 101,) walizungumzia ubadilishaji katika sentensi na matini na jinsi unavyoleta mshikamano. Lakini ubadilishaji walioushughulikia wao, zaidi

ni ule wa vipashio kubadilishana nafasi katika Kiingereza. Kazi yao ingawaje haikushughulikia Kiswahili, ilifaidisha utafiti huu pale ambapo walionyesha jinsi kibadala husimamia kishazi. Utafiti wetu haukushughulika na ubadilishaji kama walivyoonyesha wao. Hata hivyo kazi yao ilisaidia kufafanua dhana ya ubadilishaji katika kiwango cha kishazi.

Baker (1978: 237-238) alianglia ubadilishaji katika daraja ya sentensi. Alionyesha jinsi kibadala *one* (*-moja*) kinavyoweza kuwakilisha nomino katika sentensi iwapo nomino hiyo itatokea awali katika sentensi. Vile vile akaonyesha jinsi kibadala kinavyoweza kuwa cha hiari. Haya yote aliyaeleza akijikita katika Kiingereza na si Kiswahili. Maelezo yake yalikuwa ya manufaa katika kuchunguza ubadilishaji katika matini za Kiswahili hususan ule uhiari na ulazima.

Quirk na Greenbaum (2000:294-300) walishughulikia kipengele cha ubadilishaji. Walijeleza ubadilishaji kama kijenzi cha kufupisha na kuondoa urudufishaji katika matini. Walifafanua ubadilishaji wa nomino, vitenzi, vishazi na sentensi. Katika ubadilishaji wa nomino au kirai nomino walitumia viwakilishi nafsi, *he, his, them, theirs, we* kama vibadala. Hapa tunatofautiana nao kwa kuzingatia dhana ya Mshikamano kwa mujibu wa Halliday na Hassan (1976). Katika tasnifu hii, hivi ni virejelea. Hivyo hivyo walielezea juu ya ubadilishaji wa vielezi na wakasema vibadala vyake ni *then, that, here, there*, na *that* na *it* ikiwa ni kiima na kitenzi kisoelekezi. Vibadala vingine ni *in that, that way* na *like that*. Vile vile *do* na *so*. Katika maelezo haya kuna baadhi tunayotofautiana nayo katika tasnifu yetu. Hii ni kwa sababu Kiingereza na Kiswahili ni lugha tofauti na

zenye miundo tofauti. Walitoa mifano kufafanua dhana hii. Baadhi ya maelezo yao wameonyesha viwakilishi vya nomino na vimilikilishi kuwa ni vibadala pia:

59. John and Mary stole a toy from my son. *Their* mother told *them* to return the toy, but *they* said it was *theirs*.
(Quirk na Greenbaum, 2000:294)

Katika mfano huu wanadai kuwa *Their, them, they* na *theirs* ni vibadala. Waliendelea kueleza kuwa kibadala one huweza kutumika kama kibadala cha nomino kiini na kirai nomino. Nacho kibadala do hutumika kama kibadala cha kiarifu au kitenzi na so hutumika kama kibadala cha kitenzi. Aidha walionyesha (kama hapo juu:300) vikwazo vya utumiaji wa vibadala katika Kiingereza, kwa mfano vibadala haviwezi kusimama pekee katika vishazi visoelekezi (non-finite clauses) ila vitumike kwa ukubalifu wa kisarufi na vitenzi mahususi:

60. a) *Yes, I have watched him *do*.
b) Yes, I have watched him *do that*.
(Quirk na Greenbaum, 2000:30)

Sentensi 60 (a) wakasema haikubaliki katika Kiingereza lakini sentensi (b) inakubalika baada ya kuongezwa kionyeshi *that*. Hapa *that* ni kibadala cha kitenzi ambacho hakijaonyeshwa katika matini hii lakini lazima kilitokea awali na hivyo kuleta mshikamano wa kisarufi.

Maelezo yao yalisaidia utafiti wetu kuchuunguza na kuchanganua ubadilishaji katika Kiswahili, na vile vile kutudhihirishia tofauti zilizopo katika ubadilishaji wa Kiingereza na Kiswahili.

Hubbard katika Webb na Kembo Sure (2000:259) alizungumzia ubadilishaji kama kijenzi cha mshikamano vile vile. Akatoa mifano ya Kiingereza kufafanua ubadilishaji. Akaeleza kuwa kitenzi *do* huweza kuwa kibadala cha kitenzi na kirai kitenzi ilhali kivumishi *one* ni elementi inayoweza kusimama badala ya nomino na kirai nomino.

Hatch (1992) alizungumzia ubadilishaji katika Kiingereza alipokuwa anaeleza dhana ya mshikamano. Alisema kuwa ubadilishaji ni kijenzi cha mshikamano. Aidha alieleza kuwa ubadilishaji huwa wa nomino, virai vitenzi na vishazi. Akatoa mifano ya ubadilishaji huu. Maelezo yake yalichangia katika ufafanuzi na uchanganuzi wa ubadilishaji katika Kiswahili ingawaje mifano yake ilikuwa ya Kiingereza.

Culicover (1976) alielezea ubadilishaji wa *–moja* unavyotokea kuwakilisha nomino ikiwa kuna mfanano wa kisarufi na nomino nyingine katika sentensi. Ubadilishaji huu ameuchunguza katika daraja ya sentensi na kishazi rejeshi katika Kiingereza. Aidha akaonyesha vikwazo vyake katika sentensi ya Kiingereza. Pia (kama hapo juu:258) alijadili udondoshaji wa '*that*' (*-le*) katika sentensi za Kiingereza na vikwazo vyake. Akatoa mifano ya sentensi za Kiingereza zenye '*that*' na zile ambazo '*that*' imedondoshwa. Kwa hivyo hakuangalia ubadilishaji wala udondoshaji katika kiwango cha matini na si katika Kiswahili. Pia naye maelezo yake yalisaidia kufafanua kipengele cha ubadilishaji katika utafiti wetu.

Leech na Svartvik (1975) waliligusia swala hili la mshikamano walipokuwa wanafafanua sarufi ya Kiingereza. Walieleza kwamba mshikamano ni kipengele cha sarufi. Pia

wakaeleza jinsi mshikamano unavyochangia katika kuleta usahihi wa sarufi na maana katika Kiingereza. Walidondoa na kuvifafanua vijenzi vya ubadilishaji na udondoshaji katika kuleta mshikamano huku wakitoa mifano ya Kiingereza. Waliangalia ubadilishaji na udondoshaji katika kuunganisha maana katika sentensi zilizounganishwa. Vipengele hivi hutumika ili kuondoa urudufishaji katika sentensi na kuondoa utata. Ubadilishaji na udondoshaji huweza kutumia viwakilishi au kudondosha elementi fanani katika sentensi. Wanaendelea kueleza kwamba hata uwakilishaji wa nomino (au unominishaji) ni ubadilishaji. Hata hivyo katika tasnifu yetu tunachukulia unominoshaji kama kipengele cha urejeleaji na si ubadilishaji na tumeujadili katika sura ya pili kama kijenzi cha mshikamano wa kisarufi. Hivyo waliangalia ubadilishaji na udondoshaji katika sentensi ambatano za Kiingereza.

### 2.2.4 Yaliyoandikwa kuhusu Udondoshaji

Mohamed (1986) alifanya utafiti linganishi kuhusu kipengele cha udondoshaji kati ya Kiingereza na Kiswahili. Alichunguza vile udondoshaji unajitokeza katika Kiswahili na Kiingereza. Utafiti wa Mohamed ulisaidia utafiti wetu katika ufafanuzi wa udondoshaji katika Kiswahili na athari yake katika mshikamano.

Allerton (1975:212) alielezea udondoshaji wa lazima na ule wa hiari katika Kiingereza. Akasema kuwa udondoshaji hupunguza urudufishaji na huzalisha sentensi mpya. Udondoshaji wa hiari hutokea tunapodondosha yambwa na kitenzi elekezi katika kirai linganishi. Hutokea pale ambapo elementi kadhaa zinaweza kudondoshwa au la na sentensi kubakia na usahihi wa wake wa kisarufi. Nao udondoshaji wa lazima hutokea

wakati ambapo elementi fulani lazima idondoshwe katika muundo ili kupata usahihi wa kisarufi. Hii ina maana kuwa elementi fulani isipodondoshwa, sentensi husika si sahihi:

61. A: *Ulikuwa unaimba wimbo?
B: Ndiyo (nilikuwa naimba wimbo).

Katika mfano huu, yambwa 'wimbo' haifai kurudiwa kwa sababu kitenzi 'imba' hakihitaji yambwa. Msikilizaji ataelewa tu kwani kawaida watu huimba 'wimbo'.

Allerton (kama hapo juu) anaeleza kuwa kuna aina mbili za udondoshaji zinazoleta uitikisadi wa kiisimu.

a) Udondoshaji wa kimuktadha

b) Udondoshaji uso-elekezi

Udondoshaji wa kimuktadha hudondosha kipashio ambacho kinaweza kurejeshwa katika muktadha, ama kiisimu au kihali. Udondoshaji huu huwa ni wa nyuma. Hapa yambwa haitajwi lakini hupatikana katika muktadha wa kihali. Udondoshaji uso-elekezi hutokea wakati yambwa haiwezi kurejelewa. Hii ni kwa sababu kitenzi kilichotumika ni kiso-elekezi, mfano *kucha, lala, kufa, imba, soma n.k.* Aina mbili hizi za udondoshaji ni za hiari. Pia (kama hapo juu:222) alieleza kuwa udondoshaji huweza kuwa wa kiima, vibainishi au vihusishi au sehemu ya neno. Sehemu ya neno ina maana ya silabi, yaani silabi fulani inaweza kudondoshwa katika neno.

Udondoshaji unaweza kuwa wa kimuktadha au fiche. Udondoshaji wa kimuktadha ni ule ambao kipashio kilichodondoshwa kinaweza kujengwa upya kutoka muktadha huo, ama kiisimu au kihali. Allerton akatoa mfano:

62. I went to see the cricket. George was watching (      ) already.

63. A: I can't find my book.
B: Well, look for it.
A: I have already looked (        ).
(Allerton, 1975:214)

Katika 62, yambwa '*cricket*' imedondoshwa, na katika 63, kihusishi na yambwa '*for it*' vimedondoshwa. Huu ni udondoshaji wa kimuktadha kwa sababu tunarejelea vidondoshwa hivi kiisimu au kihali.

Udondoshaji fiche ni ule ambao yambwa haiwezi kurejelewa kwa sababu hata msikilizaji haijali bali anafahamu mara moja tu. Hutokea kwa vitenzi visoelekezi. Allerton akatoa mfano huu:

64. A: What's John doing?
B: He's reading.
(Allerton, 1975:214)

Katika mfano huu, msikilizaji hana haja ya kuuliza zaidi, anajua anachofanya John. Hii ni kwa sababu kitenzi '*reading*' ni kisoelekezi. Allerton (kama hapo juu:215) anadai kuwa katika Kiingereza udondoshaji fiche hutokea kwa vitenzi visoelekezi kwa sababu hakuna haja ya kurudia yambwa kwa sababu kitenzi chenyewe kinaeleweka moja kwa moja bila yambwa. Udondoshaji hapa ni wa lazima vile vile.

Thomas (1979) alizungumzia udondoshaji kati ya uhusiano wa muundo wa sentensi na muktadha katika Kiingereza. Akajeleza udondoshaji kuwa ni kutokuwepo kwa vipashio vya kiisimu katika muundo wa sentensi. Vipashio hivi hupatikanan tu kwa kuchunguza muktadha ambamo sentensi ilitumika. Vipashio hivi huwa na habari fulani ambayo hurejelewa ili kukamilisha ujumbe. Hivyo baada ya udondoshaji sentensi huwa na pengo. Vile vile alionyesha udondoshaji wa yambwa katika vitenzi elekezi katika Kiingereza na

Kijapan, na udondoshaji wa kirai kitenzi katika Kiingereza. Pia alielezea udondoshaji wa hiari na wa lazima. Akasisitiza (kama hapo juu:64) kuwa ni muhimu katika udondoshaji kuwepo kwa elementi moja kama sharti la kuwepo kwa elementi nyingine. Hii ina maana kuwa tunapodondosha, elementi lazima ziwe mbili na moja kudondoshwa. Pengo linaloachwa huzibwa na ile elementi iliyobakia ili kukamilisha maana:

65. A: Juma, unapenda maembe?
B: Ndiyo napenda (maembe).

Katika mfano huu, elementi '*maembe*' ndiyo imedondoshwa katika B lakini tunaweza kuirejelea kutoka A. Kwa hivyo elementi '*maembe*' katika A ni lazima iwepo kwa kuirejelea katika B. Maelezo ya Allerton na Thomas yalitusaidia kuchunguza na kufafanua udondoshaji kwa jumla na ule wa hiari na lazima kama unavyojitokeza katika Kiswahili.

Barker (1978) katika kitabu chake *Intoduction to Generative-Transformational Syntax*, alionyesha udondoshaji katika Kiingereza. Alionyesha jinsi Kirai Kitenzi (KT) kinavyoweza kudondoshwa. Alitoa mifano kadhaa (kama hapo juu:89). Hata hivyo mifano yake na maelezo, kwa mujibu wa mtazamo wa tasnifu hii, si udondoshaji bali ni ubadilishaji kwa sababu baada ya kudondosha KT anaweka "*too*" badala yake. Katika udondoshaji, huwa pengo hilo linaachwa vivyo hivyo. Kwa hivyo maelezo yake yanaafiki yetu tulipojadili ubadilishaji katika Kiswahili tukijiegemeza katika mada yetu.

Radford (1981: 257-282)) katika kitabu chake *Transformational Syntax* amezungumzia udondoshaji katika Kiingereza. Udondoshaji aliueleza tu katika vishazi rejeshi vyenye viwakilishi ulizi na kuchunguza vikwazo vilivyopo na hatimaye akaibuka na sheria yake.

Akasema kuwa ni elementi zile tu hazina maana ya kimuktadha zinaweza kudondoshwa. Aidha akasema kuwa udondoshaji wa vishazi rejeshi vyenye viwakilishi ulizi vinakuwa hiari katika vishazi vyenye nyakati na ni lazima katika vishazi viso nyakati. Hivyo maelezo ya Baker (1978) na Radford (1981) yalisaidia kuchanganua udondoshaji katika utafiti wetu.

Gunter (1963) alichunguza udondoshaji katika sentensi za Kiingereza cha Marekani. Akadai (kama hapo juu:37) kuwa sentensi iliyo na udondoshaji ni ile ambayo inaweza kupanuliwa kuwa ndefu kimuundo na akatoa mfano:

66. Who can see the boy?
The man.
(Gunter, 1963:37)

Akaeleza kuwa katika sentensi '*The man.*' ndipo udondoshaji umetokea na inaweza kupanuliwa na kuwa '*The man can see the boy.*'. Kwa hivyo KT '*can see the boy*' ndicho kimedondoshwa. Akadai kuwa sentensi nyingi katika mazungumzo huwa dondoshi. Vile vile akaeleza kuwa kuna udondoshaji wa aina mbili;

i) Udondoshaji wa arafa ii) udondoshaji wa muktadha.

Ule (i) ni udondoshaji ambao hauhitaji muktadha bali ufahamu wa muundo wa lugha inayotumika. Hivyo msikilizaji hujaza tu lile pengo kutokana na ufahamu wake wa lugha, na (ii) ni udondoshaji ambao ili kulijaza pengo katika sentensi dondoshi, hutegemea sentensi tangulizi. Maelezo yake yalitusaidia kufaanua udondoshaji katika mada yetu.

Quirk na Greenbaum (2000) walijadili udondoshaji walipozungumzia uunganishaji na mrejeosawa. Wakaeleza kuwa udondoshaji hutumika zaidi katika kukwepa urudufishaji.

Wakauonyesha udondoshaji wa kirai elezi na vikwazo vyake. Aidha wakaonyesha udondoshaji wa virai visoelekezi, virai vumishi (baada ya kiima), na virai tegemezi. Wakatoa mifano kufafanua haya. Pia wakaonyesha udondoshaji usiotegemea muktadha wa kiisimu. Kutokana na mifano yao, inadhihirika kuwa vidondoshwa huweza kurejelewa tu, kutokana na ufahamu wa lugha tumika:

67. a) Beg your pardon.
    b) (I've) Got to go now.

Katika mifano hii 67 (a) na (b) inadhihirika madai haya. Katika (a) kiwakilishi nafsi '*I*' kimedondoshwa na katika (b) kiwakilishi nafsi '*I*' na kitenzi saidizi '*have*' vimedondoshwa. Ili kuvirejelea, lazima kuwe na ufahamu wa lugha ya Kiingereza kwa sababu hakuna sentensi tangulizi ya kurejelea elementi hizo. Pia (kama hapo juu:256) walitoa kikwazo katika Kiingereza kuwa udondoshaji wa kiima katika kishazi, hutokea tu iwapo kiima kipo pia katika kishazi fuatilizi:

68. I may see you tomorrow or (*I*) may phone later in the day.
69. They didn't like it, yet (*they*) said nothing.
(Quirk na Greenbaum, 2000:256)

Katika mifano hii 68 na 69, kiima '*I*' na '*they*' katika vishazi fuatilizi, vimedondoshwa. Jambo hili si kikwazo katika Kiswahili kwa sababu kiwakilishi cha kiima daima lazima kiwepo katika kitenzi. Kisha walionyesha udondoshaji unavyotumia muktadha wa kiisimu na nje ya miktadha ya kiisimu katika sentensi za Kiingereza. Vile vile (kama hapo juu:305-306) walielezea kuwa udondoshaji katika majibizano, hutokea katika hali tatu;

a) urudiaji

b) upanuaji

c) ubadilishaji

Urudiaji hutokea wakati msemaji wa pili hurudia yanayozungumzwa na yule msemaji wa kwanza. Upanuaji ni wakati msemaji wa pili huongezea yale yaliyozungumziwa na msemaji wa kwanza. Ubadilishaji huwa msemaji wa pili hubadilisha yale yaliyozungumzwa na msemaji wa kwanza. Haya yote hutokea katika mazungumzo ya maswali. Walifafanua kwa mifano ifuatayo:

70. A: Have you spoken to the doctor?
    B: (Yes,) *I have* (spoken to the doctor.)

71. A: Will they lose the game?
    B: *Probably* (they will lose the game.)

72. A: Who told your father?
    B: *Mary* (told my father.)
    (Quirk na Greenbaum, 2000:206)

Katika mfano wa 70, mzungumzaji B amerudia kitenzi saidizi *have*, mfano 21 amepanua sentensi kwa kuongezea neno *Probably* na katika 71 amebadilisha kiulizi na neno *Mary*. Sehemu nyingine za sentensi zilizo katika mabano ndizo hudondoshwa, na kimuundo ni virai na katika 70 (Yes) ni kielezi. Tena walielezea na kufafanua udondoshaji wa kiima, kitenzi saidizi, kirai kitenzi, yambwa, kielezi na kisifa. Haya yote waliyafafanua kwa kutoa mifano ya kiingereza.

Thompson (2004:182) anajeleza udondoshaji kwa kusema kuwa ni seti ya raslimali ambayo hufanya urudiaji wa kishazi au elementi fulani kukwepwa, na kudokezwa kwa wasomaji kuwa warejee kwa kishazi tangulizi ili kukamilisha maana. Akaeleza kuwa kuna aina mbili za kimsingi katika udondoshaji; i) udondoshaji asili na ii) udondoshaji

ambapo pengo hujazwa na elementi badala. Udondoshaji asili ni ule ambao pengo hujazwa elementi kutoka habari tangulizi.

Udondoshaji, kama anavyoeleza (kama hapo juu: 184) hutokea katika vishazi viwili fuatilizi. Vile vile akadai kama Gunter (1963) kuwa udondoshaji hutokea zaidi katika mazungumzo kuliko maandish na hutokea zaidi katika majibu. Akatoa mifano ya sentensi za Kiingereza kufafanua dhana hii:

73. 'You've got a black eye.'
Yes (I've got a black eye.)'
(Thompson, 2004:185)

Katika mfano huu kishazi '*I've got a black eye.*' kimedondoshwa na kupata maana kamili katika jibu, lazima msomaji arudi kwa sentensi ya kwanza kukamilisha jibu lake la '*Yes*'. Hivyo msomaji atadhania sehemu hiyo ya kirai. Aidha akeleza kuwa sehemu inayodondoshwa inaweza kusimamiwa na elementi nyingine:

74. 'You're suffering from shock.'
'Yes, *that's it*, ...'
(Thompson, 2004:185)

Hapa pametumika kibadala '*that's it*' kusimamia '*suffering from shock*'. Akaita jambo hili ubadilishaji chini ya udondoshaji. Katika maelezo yake, udondoshaji na ubadilishaji ni mamoja. Hapa tunatofautiana naye kwa sababu katika tasnifu yetu, udondoshaji ni tofauti na ubadilishaji na vyote ni vijenzi vya mshikamano. Udondoshaji na ubadilishaji vimejadiliwa peke yake kila kimoja.

Hatch (1992:225) alijeleza udondoshaji kuwa ni kutotumia kishikanishi katika kuunganisha mawazo. Akatoa mifano ya Kiingereza kufafanua udondoshaji:

75. 'Would you like to hear another verse? I know twelve (verses).'

Katika mfano huu, '*verses*' ni nomino iliyodondoshwa. Pia akaonyesha udondoshaji wa kitenzi na kishazi katika sentensi za Kiingereza. Maelezo haya yalisaidia kuonyesha udondoshaji wa vipengele alivyovionyesha.

Toolan (1998:27) alieleza kuwa udondoshaji ni aina ya pili kuu katika aina nne za mshikamano. Katika tasnifu yetu tumechukulia udondoshaji kama kijenzi cha mshikamano wala si aina. Akajeleza kuwa udondoshaji ni kuacha (kudondoa) nje ya matini faridi fulani kwani urudiaji wake si muhimu katika sentensi fuatilizi. Hakuna haja ya kutaja faridi hiyo kwa mara ya pili kwa sababu hudhaniwa katika muktadha uliopo. Faridi dondoshwa huweza kuchotwa kutoka kwa sentensi tangulizi na kujazwa katika pengo lililoachwa na udondoshaji katika muundo wa sentensi. Akazidi kueleza kuwa kinachoweza kudondoshwa ni nomino, kitenzi au kishazi. Udondoshaji wa kishazi kamili hudhihirishwa na majibu '*Ndiyo*' na '*La*'. Naye vile vile akadai kuwa udondoshaji hutokea zaidi katika majibizano. Akafafanua aina mbili za udondoshaji: i) Udondoshaji nusu ( au ubadilishaji) ii) Udondoshaji kamili. Tooolan kama Thomson (hapo juu) ubadilishaji ameuchukulia kama udondoshaji tofauti na sisi katika tasnifu hii. Udondoshaji nusu, kama alivyouita, sisi tumeuita ubadilishaji kwa kuegemea dhana ya mshikamano inayoongoza tasnifu hii. Toolan katika kufafanua maelezo yake akatoa mifano ya sentensi za Kiingereza kuonyesha udondoshaji nusu na udondoshaji kamili:

76. Kimberley: *Can I look at your watch?*
Martin: *Sorry, I'm not wearing one.*

Kimberley: *You mean you don't usually wear a watch?*
Martin: *I usually do, but today I left it in at the shop to be repaired.*

(Toolan, 1998:27)

Katika mfano huu *one* na *do* zinasimamia '*watch*' na '*wear a watch*' mtawalia. Huu ameuita udondoshaji nusu.

77. Martin: *I heard that everyone in the hockey squad had to do extra training this week.*
Kimberley: *Yes.*
(Toolan, 1998:27)

Katika mfano huu, aliita udondoshaji kamili. Sisi katika tasnifu yetu tunakubaliana naye kuwa huu ni udondoshaji na tumeuchanganua hivyo.

Halliday na Hassan (1976) nao walieleza udondoshaji katika kitabu chao *Cohesion in English*. Walifafanua udondoshaji kama 'kutosema kitu'. "Kutosema kitu' huku huwa kunaeleweka, yaani kilichoachwa nje kinaeleweka kwa kudhania kwa mujibu wa muundo wa sentensi iliyopo. Maana yake ni kuwa katika sentensi faridi fulani huachwa. Sentensi hiyo huwa fuatilizi na katika sentensi tangulizi huwa imetajwa. Hivyo hakuna haja ya kutaja faridi hiyo tena. Kwa hivyo kukamilisha maana huwa tunadhania faridi hiyo iliyoachwa kutoka sentensi tangulizi kwa mujibu wa muundo wa sentensi. Kufafanua haya zaidi wakatoa mfano wa sentensi hii:

78. Joan brought some carnations, and Catherine ( ) some sweet peas.
(Halliday na Hassan, 1976:143)

Katika mfano huu, kitenzi '*brought*' kimedondoshwa katika kishazi cha pili na kupata maana tunadhania kitenzi hicho kutoka kishazi tangulizi. Huu ni udondoshaji kwani pengo limetokea na tunalijaza kutoka sehemu tangulizi. Vile vile walielezea udondoshaji wa nomino na kirai nomino, kitenzi na kitenzi nomino, na kishazi huku wakitoa mifano

ya sentensi za Kiingereza. Wakaelezea udondoshaji katika kirai nomino (KN), kirai kitenzi (KT) na katika kishazi. Vile vile wakaelezea vikwazo vilivyopo katika udondoshaji katika Kiingereza. Wakaelezeza zaidi (kama hapo juu:148) kuwa udondoshaji nomino hujumuisha kukweza daraja neno lililo na uamilifu wa uonyeshi, hesabati, kivumishi au kiainishi kutoka kisifa hadi kiini. Kwa hivyo KN chenye kionyeshi, hesabati, kivumishi na kiainishi kama kiini, wakati wote kinaweza kudondoshwa. Na ikiwa kina kihusishi kama kisifa, hakiwezi kudondoshwa isipokuwa tu, kisifa husishi kinadondoshwa. Hiki ni kikwazo walichokieleza katika udondoshaji wa KN katika Kiingereza. Pia walielezea udondoshaji KT. Wakasema (kama hapo juu:167) kuwa KT chote kinaweza kudondoshwa na kikadhaniwa kama neno moja au zaidi ya moja kutoka kwa KT kilichotangulia.

Walidai (kama hapo juu:173-4) kuwa kuna aina mbili za udondoshaji katika KT; a) udondoshaji wa kileksia ambapo kitenzi halisi hudondoshwa, na b) udondoshaji wa visifa ambapo visifa vyote kabla ya kitenzi halisi hudondoshwa:

79. a) Have you been swimming? – Yes, I have.
    b) What have you been doing? –Swimming.
    (Halliday na Hassan, 1976:167)

Mfano 79(a) ni udondoshaji wa kileksia ambapo leksia zimeachwa nje, na 79(b) ni udondoshaji wa visifa, yaani visifa vyote kabla ya kitenzi halisi 'swimming' vimedondoshwa.

Katika Kiswahili, aina hizi zote hazitokei kwa sababu ya muundo wa Kiswahili:

80. a) Umekuwa ukiogelea?- *Ndiyo, nimekuwa.

Udondoshaji huu haukubaliki. Unaokubalika ni 'Ndiyo.' au kusidondoshwe faridi yoyote ila kuongezea,'Ndiyo, nimekuwa nikiogelea.' Vinginevyo havikubaliki.

b) Umekuwa ukifanya nini?- *Ogelea.

Udondoshaji huu haukubaliki kwa sababu katika Kiswahili lazima kitenzi kiambishwe kiambishi wakilishi kwa mujibu wa ngeli. Hivyo itakuwa 'Nikiogelea.'. Hii ni sentensi kamili ya KT kwani ina kiima 'Ni-', kiambishi cha wakati (timilifu) na kitenzi 'ogelea'. Maelezo ya Halliday na Hassan ndiyo dhana iliyotumika kuongoza tasnifu hii. Kwa hivyo ndiyo msingi na yale ya wengine yalichangia na yalipohitilafiana, mawazo ya Halliday na Hassan ndiyo yalizingatiwa.

Salkie (1995) anadai kuwa katika udondoshaji tunadondoa nomino, kitenzi na kishazi. Kisha akafafanua zaidi kuwa kiima na kitenzi elekezi pia huweza kudondoshwa. Katika Kiswahili udondoshaji wa vipashio hivi hutokea na kwenda zaidi na kudondoa hata silabi katika neno.

### 2.2.5 Yaliyoandikwa kuhusu Uunganishaji

Hatch (1992:225) anasema uunganishaji ni kijenzi kimojawapo cha mshikamano. Kiunganishi husaidia kufasiri uhusiano wa vishazi. Vishazi hivi vinapounganishwa huzaa uhusiano ambao huleta mshikamano wa mawazo yanayokusudiwa na kuendeleza maana iliyopo katika matini. Uunganishaji husaidia wasomaji kufasili uhusiano kati ya vishazi. Hivyo dhana katika kishazi tangulizi inashikanishwa na dhana katika kishazi fuatilizi. Jambo hili linapotokea, mshikamano hujitokeza pia.

Toolan (1998:28-29) anaeleza mshikamano unganishi hurejelea matumizi ya baadhi ya maneno au virai, kawaida maneno haya huwa mwanzoni mwa sentensi, kwa madhumuni ya kufafanua uhusiano wa kisemantiki au kimantiki kati ya habari ifuatayo na ile tangulizi. Uunganishi huu unaweza kuwa fiche (usio wazi) kati ya elementi iliyotangulia na inayofuata. Hata hivyo matumizi ya kiunganishi hufanya uunganishaji kuwa wazi zaidi. Hivyo viunganishi vya mshikamano vina uamilifu wa kisemantiki.

Hubbard (2000:260) akiwanukuu Halliday na Hassan, anasema kuwa uunganishaji ndiyo aina pekee ya mshikamano ambayo daima huunganisha maana ya vishazi na sentensi kama kazi jumla, ambayo hueleza kile kinachofuata kwa mfumo fulani na kile kilichotangulia. Hivyo ni kwamba kuna maana mbili zinazounganishwa ili kuleta mantiki. Kama adaivyo Dijk (1977:47) ni kuwa sharti la kwanza katika uunganishaji ni uhusiano kati ya maana au fahiwati ya maneno katika sentensi. Vishazi au sentensi ziwe zimeungana au kuunganishwa na kuwa ukweli unaodhihirishwa na dhana zao, ambazo uhusiana. Dhana hizi ziwe zinaungana kwa mujibu wa mada na ukweli wa dhana hizo.

Thompson (2004:19) anadai uunganishaji hurejelea uchanganyaji wa elementi zozote za kimuundo mbili katika kipashio changamano cha kisemantiki katika mshikamano. Elementi hizi huweza kuwa na miuundo mbalimbali na si lazima iwe miundo yao inafanana. Kwa mfano kishazi tegemezi kuunganishwa na kishazi kikuu au sentensi sahili, kirai kitenzi kuunganishwa na sentensi sahili, nomino kuunganishwa na kirai husishi. Uunganishaji huu unapotokea huleta mshikamano katika matini husika.

Quirk na Greenbaum (2000:253) wanaeleza kuwa uunganishaji hutokea ama kwa kutumia viunganishi au kwa kutokuwepo viunganishi lakini viunganishi hivyo vinaweza kurejelewa katika muktadha wa dhana. Hivyo ni kusema kwamba inalazimu mrejeonje ili kupata maana. Tunapochanganua matini kama hiyo tunapata uunganishaji umetokea lakini bila viunganishi dhahiri lakini tunaweza kuvipata nje ya matini kwa mujibu wa muktadha. Uunganishaji hujumuisha uunganishi wa vipashio vya kisintaksia na pia maana. Uunganishaji tuliourejelea katika tasnifu yetu ni ule wa kisemantiki, yaani unaounganisha maana au dhana mbalimbali. Quirk na Greenbaum (2000:257, 288-293) wameueleza uunganishaji huu kwa kutumia viunganishi *and, or, but, so, furthermore, finally, as a result of, however, besides, still of course* n.k. Wakaeleza aina mbalimbali za uunganishaji kama vile elezi, nyongeza, matokeo (sababishi), kubalifu, na wakatoa mifano mbalimbali ya Kiingereza.

Naye O'grady na wenzake (1996:223) wanasema viunganishi hutumika kuunganisha elementi au katagoria za kisintaksia mbili au zaidi. Wanazidi kuelezea kuwa viunganishi vya nomino vinaweza kudondoshwa isipokuwa kile kinachotokea mara tu kabla ya nomino ya mwisho. Hii inamaanisha kwamba ikiwa kuna viunganishi vinavyounganisha nomino kadhaa zinazofuatana, viunganishi vinavyotokea awali vinaweza kudondoshwa na kile cha mwisho tu kikabakia. Hata viunganishi hivi vinapodondoshwa, mshikamano bado upo katika matini. Si katika nomino peke yake jambo hili hutokea, hata katika mfululizo wa vitenzi au vitendo, viunganishi vinaweza kudondoshwa isipokuwa kile cha kabla ya kitenzi cha mwisho. Viunganishi hudondoshwa ili kukwepa urudufishaji.

Schiffrin (1987) alielezea viunganishi '*and*' (*na)*, '*but*' (*lakini*) na '*or*' (*au*) katika Kiingereza. Alionyesha jinsi na inavyojenga matini katika Kiingereza. Alitumia matina za mazungumzo baina ya wazungumzaji. Akaonyesha viwango mbalimbali vya sentensi kiunganishi hiki hutumika, uunganishi wa nomino, vitenzi na sentensi. Alijadili matumizi ya na na arthari zake mfano kuonyesha maendelezo ya kitendo, kuunganisha matukio na mawazo mbalimbali. Vile vile alizungumzia matumizi ya 'so' (*hivyo*) na 'because' (*kwa sababu*). Alionyesha jinsi viunganishi hivi hutumika kuunganisha nomino, vitendo na dhana katika sentensi.

Van Dijk (1977) alielezea uunganishaji na viunganishi katika semi za Kiingereza. Alionyesha matumizi ya viunganishi vielezi mfano "*but yet*' (*lakini bado*), '*but nevertheless* (*lakini hata hivyo*), '*because although*' (*lakini hata hivyo*) na vikwazo na athari zake katika usemi. Alionyesha matumizi yasiyokubalika katika Kiingereza mfano '*but although*' (*lakini hata hivyo*). Maelezo ya Van Dijk yalisaidia sana utafiti wetu kufafanua matumizi ya viunganishi hivi katika Kiswahili na athari zake. Pia yalitusaidia kushadidia kuwa kila lugha ina muundo wake.

Halliday na Hassan (1976) walielezea uunganishaji. Walisema (kama hapo juu:226) elementi za uunganishaji zina mshikamano usio wa moja kwa moja. Huelezea maana ambazo hudhania elementi nyingine katika usemi au matini. Viunganishi huunganisha dhana kisemantiki ambapo dhana tangulizi huunganishwa na dhana fuatilizi katika matini. Walitoa (kama hapo juu:231) mifano ya viunganishi katika Kiingereza kama vile *but, so, then,next, subsequently, actually, therefore* n.k. Vile vile walizungumzia

uunganishaji nyongeza, elezi, sababishi na wakati. Wakatoa mifano mbalimbali (kama hapo juu:241-244) ya aina hizi za uunganishaji kwa kutumia viunganishi vya Kiingereza. Uanishaji huu na mifano yake ndio ulitupa mwelekeo wa kujadili, kuchanganua na kudondoa mifano kutoka matini za Kiswahili zilizotumika.

Halliday na Hassan (1976:267), Hatch (1992:225), Salkie (1995:76), Toolan (1998:29) na Hubbard (2000:262) waliainisha uunganishaji katika aina mbalimbali kama tulivyoziweka katika Jedwali 2.1. Walianisha hivi kwa mujibu wa uamilifu wa viunganishi hivi katika matini.

Halliday na Hassan, Hatch na Hubbard waliainisha aina nne. Salkie aliweka aina nne vile vile lakini ana aina pinzani badala ya elezi. Toolan aliweka aina tano akiwa na aina endelezi ambayo wenzake hawana. Tofauti na wengine ni Dijk (1977:53) ambaye aliainisha viunganishi kwa mujibu wa katagoria za kisintaksia na uamilifu wao katika kuleta mshikamano katika matini, na akapata aina tano: i) Viunganishi vya kuunganisha na utegemezi ii) Vielezi vivumishi iii) Vihusishi vyenye sifa ya uunganishaji iv) Viingizi/vihisishi na faridi peke v) Katagoria za kisintaksia kama vile nomino, vitenzi, vivumishi, virai kamili na vishazi.

Katika tasnifu hii, uunganishaji uliochunguzwa ni ule unaoleta mshikamano katika matini. Wataalamu anuwai wameainisha uunganishaji kama unavyojitokeza katika matini. Uainishaji huu unakurubiana sana miongoni mwa wataalamu mbalimbali. Halliday na Hassan (1976:267) waliugawanya uunganishaji katika aina nne; i)

Uunganishi nyongeza ii) Uunganishi elezi iii) Uunganishi sababishi na iv) Uunganishi wakati. Vile vile Salkie (1995) aliainisha aina nne; i) Uunganishi nyongeza ii) Uunganishi pinzani iii) Uunganishi sababishi na iv) Uunganishi wakati. Naye Hatch (1992) alipata aina nne vile vile; i) Uunganishi nyongeza ii) Uunganishi elezi iii) Uunganishi sababishi na iv) Uunganishi wakati. Pia Hubbard (2000) alipata aina nne; i) Uunganishi nyongeza ii) Uunganishi elezi iii) Uunganishi sababishi iv) Uunganishi wakati. Toolan (1998) alitofautiana na wengine na alipata aina tano ambazo ni; i) Uunganishi nyongeza ii) Unganishi elezi iii) Uunganishi sababishi iv) Uunganishi wakati na v) Uunganishi endelezi. Wataalamu hawa wote ni Toolan tu aliye na aina tano, na ile iliyo tofauti na wengine ni uunganishi endelezi (Jedwali 2.1). Halliday na Hassan (1976: 267-271) wamezungumzia viunganishi hivi na kusema kwamba vinaleta mshikamano katika matini. Wakaviita viendelezi, navyo ni *sasa, bila shaka, barabara, vyovyote vile, kweli, hata hivyo*.(Tafsiri yetu)

| WAAINISHAJI | AINA ZA UUNGANISHAJI |
|---|---|
| Halliday na Hassan (1976) | Nyongeza, Elezi, Sababishi, Wakati |
| Hatch (1992) | Nyongeza, Elezi, Sababishi, Wakati |
| Salkie (1995) | Nyongeza, Pinzani, Sababishi, Wakati |
| Toolan (1998) | Nyongeza, Elezi, Sababishi, Wakati, Endelezi |
| Hubbard (2000) | Nyongeza, Elezi, Sababishi, Wakati |

2.1 AINA ZA UUNGANISHAJI

Uunganishaji nyongeza huwa unaongezea habari juu ya ile iliyotangulia. Dhana ya kwanza inafafanuliwa zaidi na dhana ya pili. Dhana hizi huunganishwa kwa kutumia viunganishi. Viunganishi hivi huitwa viunganishi nyongeza. Halliday na Hassan (1976) wametaja viunganishi hivi kama *na, au, pia, wala, zaidi ya hayo, fauka ya hayo, kwa maneno mengine, kwa kuongezea, kwa mfano, kwa upande mwingine.*

Salkie (1995) pia alielezea viunganishi nyongeza. Anaeleza kuwa viunganishi nyongeza huongeza habari mpya au ishara kwa dhana iliyotangulia katika matini. Aidha hudokezea kuwa yanayokuja yanatokana na yaliyotangulia. Alitaja viunganishi hivi kama *na, pia, kwa maneno mengine, hususan, kwa mfano*. Toolan (1998:29) alitoa mifano ya *na, au, wala, zaidi ya hayo, kwa maneno mengine, mfanano wa* kama viunganishi nyongeza. Naye Hubbard (2000:262) alitaja *na, zaidi ya hayo, kwa mfano, mfanano wa* kama viunganishi nyongeza. Alieleza kuwa huunganisha dhana kwa kuongeza habari kwa ile iliyotangulia.

Quirk na Greenbaum (2000:289) wanaeleza kuwa uunganishi nyongeza huonyesha kuwa yanayosemwa katika sehemu moja ya sentensi ni nyongeza ya yale yaliyotangulia kutajwa. Hivyo dhana hizo mbili zimeunganishwa na kuleta mantiki ya yale yanayozungumziwa katika matini. Inapotokea hivi, basi kuna mshikamano katika matini. Kutokana na maelezo haya ni kwamba viunganishi nyongeza huongezea habari zaidi juu ya ile iliyotangulia. Na wakati huo huo huunganisha vishazi au sentensi. Baadhi ya viunganishi vilivyotajwa vimetumika katika matini zilizochunguzwa.

Uunganishi elezi huleta mshikamano katika matini. Hujitokeza panapotumika viunganishi *lakini, ingawaje, ingawa, bado, hata hivyo, badala yake, vinginevyo, kwa vyovyote, kwa minajili ya* (Halliday na Hassan, 1976:255). Kinachounganishwa tunapotumia viunganishi elezi ni maana, na sehemu ya mbele ya sentensi, mara nyingi huwa sentensi tegemezi. Sentensi hii hudhania na kuunganisha maana hiyo. Dhana au jambo moja lililotangulia huunganishwa na lile jipya. Uunganishaji huu unatokana na matumizi ya viunganishi vinavyoelezea zaidi dhana au jambo.

Pia uunganishaji elezi huelezea kinyume cha mambo. Huwa sehemu moja ya sentensi inapinga ile nyingine na kuleta utofauti wa dhana. Dhana tangulizi inaonyeshwa kinyume chake na ile dhana fuatilizi. Hivyo Salkie (1995:77) anauita uunganishi pinzani na huonyesha kuwa kinachofuata katika matini kinapinga kile kilichotangulia. Akataja viunganishi pinzani kuwa ni *lakini, angalau, ingawaje, ilhali*. Naye Hubbard (2000:261) anaeleza kuwa uunganishi elezi ni uunganishi wa uhusiano wa kinyume cha matarajio. Hapa ni kwamba kulikuwa na matarajio fulani lakini kinachotokea ni kinyume na matarajio hayo.

Uunganishi sababishi ni uunganishi unaoonyesha sababu ya jambo kutokea. Aidha huonyesha matokeo baada ya kitendo fulani kutendeka. Uunganishi huu hudhihirishwa na viunganishi mbalimbali katika matini. Dhana zilizounganishwa katika sentensi mbalimbali huleta mshikamano. Pia huonyesha uhusiano wa kimshikamano kati ya sentensi. Halliday na Hassan (1976:256) wanaeleza kuwa usababishi hudhihirishwa na

viunganishi *hivyo, kwa hivyo, kwa sababu, kutokana na*. Aidha viunganishi hivi huweza kutumika pamoja na *na*. *na* hutangulia, kwa mfano, *na kwa hivyo*.

Katika usababishi kuna jambo linalotokea na lilisababishwa na lingine. Hii ni kwamba jambo au dhana tangulizi katika sentensi tangulizi husababishwa na jambo au dhana fuatilizi inayopatikana katika sentensi fuatilizi. Dhana hizi huunganishwa na kiunganishi sababishi. Zinapounganishwa huleta maana inayokubalika na kuleta mshikamano katika matini. Kiunganishi sababishi huonyesha kuwa sentensi inaelezea matokeo ya kilichozungumzwa mwanzoni (Quirk na Greenbaum, 2000:290).

Viunganishi sababishi huonyesha kuwa sehemu mbili za matini zina uhusiano wa sababu na matokeo. Viunganishi sababishi vinavyotumika zaidi, adaivyo Salkie (1997:77) ni *kwa sababu*, na *kwa hivyo*. Dai hili halikudhihirika katika matini za Kiswahili za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*. Salkie pengine alitoa uamuzi huu baada ya kushughulikia matini za Kiingereza. Viunganishi sababishi vingine ni *kutokana na haya*, *hivyo, kwa sababu hiyo, kwa mtazamo huu*.

Hubbard (2000:261) anaorodhesha viunganishi sababishi kama walivyofanya Halliday na Hassan (1976) hapo juu. Dijk (1977:76) anaeleza kwamba katika viunganishi sababishi, kuna kiunganishi sharti, nacho ni *ikiwa...basi*. Ifahamike kuwa mifano iliyotolewa na wataalamu hawa ni kutoka lugha ya Kiingereza. Hata hivyo viunganishi sababishi pia hupatikana katika Kiswahili. Natuchunguze viunganishi hivi jinsi vinavyotumika katika matini za Kiswahili.

Junganishi wakati ni uunganishaji unaoonyesha jambo au kitendo kutokea katika wakati ulani na kufuatwa na jambo au kitendo kingine. Mambo haya huonyeshwa katika sentensi zinazofuatana mfululizo (Halliday na Hassan, 1976:261). Mambo haya huwa na ıhusiano katika sentensi hizo na uhusiano huu huonyeshwa na viunganishi wakati. Viunganishi wakati kwa mujibu wa Halliday na Hassan (1976) hujumuisha *kisha, wakati nwingine, baada ya, baadaye, hatimaye/mwishowe, kabla, kabla ya, awali, mara, wakati ıuo.*

Viunganishi hivi huonyesha wakati katika mrejeombele kwenye sentensi tangulizi kitarajia wakati kwenye sentensi fuatilizi iliyo na mrejeosabiki. Wanadai kuwa (kama ıapo juu:264) baadhi ya viunganishi wakati, wakati mwingine si vijenzi vya mshikamano kwa sababu havidhanii chochote. Lakini ikiwa vinadhania, huleta mshikamano. Viunganishi hivi ni *sasa, mpaka sasa, wakati ujao.* Kwa madai haya, utafiti huu ımejishughulisha tu na viunganishi wakati vinavyoleta mshikamano katika matini. Kwa iivyo pale ambapo vilijitokeza kimshikamano vilichunguzwa.

Salkie (1997:78) anasema viunganishi wakati huonyesha mfuatilizo wa wakati katika natini. Pia huweza kuonyesha matukio mawili yanayotokea kwa wakati mmoja vakifuatana. Viunganishi alivyovitaja ni *kisha, mwanzo, hatimaye/mwishowe* na *kabla.*

Naye Hubbard (2000:261) anatoa mifano ya viunganishi wakati kuwa ni *kisha, baadaye, baada ya, kabla, awali* na *hatimaye*. Aidha Toolan (1998:29) anavitaja kuwa ni *kisha, fuatilizi, hatimaye, kwa kumalizia, wakati huo*. Schriffn (1987:246) ametaja viunganishi

wakati viwili tu, navyo ni *sasa* na *kisha.* Quirk na Greenbaum (2000:286) wametoa orodha ya viunganishi wakati kama *mwanzoni, baadaye, fuatilizi, kabla, kisha, kufikia sasa, baadaye, baada ya, mara.* Kwa hivyo wote hawa wamekubaliana kuhusu viunganishi wakati. Viunganishi hivi huunganisha vitendo vilivyotokea kwa mujibu wa muda, kimoja kikifuatwa na kingine. Viunganishi wakati vimetumika katika matini za Kiswahili za *Watoto wa* Maman'ilie na *Musaleo!* kuunganisha mambo/vitendo au dhana kiwakati. Vimeonyesha dhana au kitendo kimoja kikitokea baada ya kingine.

Katika utafiti huu, tumezingatia uainishaji wa Halliday na Hassan (1976:267-271) kwa sababu nadharia yao ya mshikamano ndiyo iliuongoza utafiti huu. Kwa hivyo kuna aina nne mahususi za viunganishi tulizozichunguza katika matini teule.

## 2.3 Hitimisho

Maandishi mengi yapo kuhusu vijenzi vya mshikamano. Baadhi ya maandishi haya, yanajadili kuhusu kijenzi kimoja au vyote kwa kuvifafanua na kutoa mifano ya Kiingereza. Maelezo na mifano imesaidia sana katika utafiti huu ingawaje ni wa matini za Kiswahili. Hata hivyo kila lugha lazima iwe na mshikamano ili kuleta maana. Mifano hii ilitoa mwanga wa kujadili na kutoa mifano ya Kiswahili.

Kwa hivyo yaliyoandikwa kuhusu mada hii, yamechangia pakubwa katika kufanikishi kazi hii.

# SURA YA TATU

# UREJELEAJI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumechunguza urejeleaji kama unavyojitokeza katika Kiswahili. Tumeutalii, kuuchunguza na kuonyesha jinsi unavyotumika tukirejelea matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*. Ilipobidi, tulifafanua urejeleaji kwa kutoa mifano yetu ya Kiswahili. Katika kuchanganua urejeleaji, tumedondoa mifano mbalimbali kutoka matini teuzi ili kufafanua utokeaji wake . Aidha tumechunguza aina mbalimbali za urejeleaji na vijenzi vyake. Aina hizi tumeziangazia vile zitumikavyo katika matini teuzi ili kuleta maana na mshikamano. Vile vile tumeangazia vikwazo vya urejeleaji katika Kiswahili kwa kurejelea matini zilizotumika. Kwa hivyo, sura hii imechunguza urejeleaji na kufafanua ala zilizotumika kujenga urejeleaji huo na jinsi unavyoleta mshikamano wa kisarufi. Jedwali limetoa muhtasari wa urejeleaji unavyojitokeza katika matini zilizotumika.

| MATINI | IDADI | ASILIMIA (%) |
|---|---|---|
| *Watoto wa Maman'tilie* | 6338 | 30.15 |
| *Musaleo!* | 14686 | 69.85 |
| **JUMLA** | **21024** | **100%** |

3.1 UTOKEAJI WA UREJELEAJI KATIKA MATINI

Katika jedwali 3.1 tunaona kuwa urejeleaji umejitokeza mara elfu sita, mia tatu na thalathini na nane (6,338) katika *Watoto wa Maman'tilie* ambayo ni asilimia thalathini

nukta moja tano (30.15%). Katika *Musaleo!* ni mara elfu kumi na nne mia sita na thamanini na sita (14,686) ambayo ni aslimia sitini na tisa nukta nane tano (67.85%). Hii ni kwa mujibu wa idadi yote kwa pamoja katika matini hizi mbili. Katika udadisi wetu wa tofauti hizi ni kuwa matini ya *Watoto wa Maman'tilie* ilitumia hati kubwa kubwa katika uandishi wake na ina idadi ya kurasa tisini na nane (98), na matini ya *Musaleo!* ilitumia hati ndogo ndogo sana na hivyo kuwa na maneno mengi zaidi na kurasa mia moja na mbili (102).

### 3.1 Urejeleaji Unavyotokeza

Urejeleaji ni kijenzi kimojawapo cha mshikamano (Salkie, 1995; Halliday, 1985; Halliday na Hassan, 1976). Kijenzi hiki hutumika ili kuondoa urudufishaji wa maneno katika matini. Nomino (kiima au yambwa) haiwezi kurudiwa rudiwa katika matini kila mara bali kiwakilishi nomino, mfano *mimi, yeye*, hutumika kuwakilisha nomino hiyo pindi inapojitokeza mara ya pili (Halliday, 1985:291). Viwakilishi hivi husimama mahali pa nomino, au vionyeshi hutumika kusimama mahali pa nomino au kirai. Katika Kiswahili kiambishi cha nafsi pia hutumika kukaa mahali pa nomino ili kukwepa urudufishaji (Kapinga, 1983). Hii inamaanisha kuwa kuna vipashio viwili vya kiisimu katika matini, na kimojawapo kinarejelea kingine kilichotokea mwanzoni. Urejeleaji ni hali ya kuwa faridi moja haiwezi kufasiriwa peke yake kisemantiki mpaka irejelee faridi nyingine ndipo iweze kufasiriwa.

Kwa hivyo katika matini, faridi moja hurejelea nyingine ili iweze kufafanuliwa na kuleta maana kwani haiwezi kutumika kila mara katika muundo wa sentensi. Bila urejeleaji huo, hakuna maana inayoweza kupatikana. Katika Kiswahili tuligundua urejeleaji hutawalwa

zaidi na viambishi nafsi kuliko viwakilishi vya nomino. Urejeleaji ulijitokeza kama ifuatavyo katika matini zilizotumika:

> 81. ...Mbwa huyu *a*likuwa mweusi, mwenye mkia mweupe. *A*lionekana *a*kitembea mwendo wa polepole. Ulimi wake mrefu *u*lionekana *u*kidondoka mate ya utelezi. *A*likwenda *a*kakatiza barabara kuu...
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k.1)

Hapa Nomino Kiima ni mbili; 'Mbwa' na 'Ulimi'. Nomino 'Mbwa' inarejelewa na faridi *a-* katika kitenzi saidizi ($T_s$) alikuwa na vitenzi kamili ($T_k$) Alionekana, akitembea, Alikwenda na akakatiza. Nomino Ulimi inarejelewa na faridi *u-* katika vitenzi kamili Ulionekana na ukidondoka. Hapa tunaona kuwa urejeleaji umewakilishwa na kiambishi nafsi *a-*. Faridi (virejelea) hizi zikitolewa, matini hii itakosa mshikamano na kupotosha sarufi. Hata hivyo kwa mujibu wa Halliday na Hassan (1976) walivyofafanua urejeleaji wakijikita katika Kiingereza, faridi *u-* inayorejelea Ulimi si faridi ya mshikamano, hiyo ni kiwakilishi cha nafsi tu. Faridi virejelea hutokea katika sentensi fuatilizi kurejelea nomino iliyotangulia katika sentensi iliyotangulia. (Swala hili tutalijadili katika 3.2).

Faridi hizi katika matini zinaelekeza kuwa habari fulani ni itolewe kutoka kwengineko. Habari hii ni habari au maana rejelewa inayotambua kitu au kundi la vitu ambalo linarejelewa; na mshikamano hapa hutegemea mfuatilizo wa urejeleo, ambako kitu hicho hicho hupatikana katika usemi au matini kwa mara ya pili. Kurejelewa kwake huonyeshwa na kiwakilishi au kionyeshi (*Kama hapo juu*: 31). Katika tasnifu hii tutaviita virejelea.

> 82. . ..Kulikuwako na mgunga mkubwa uliokuwa ukiyaangusha majani yaliyopukutwa na upepo huo. Chini palikuwa na

> kigenge cha watoto. *Hawa* wahuni *wa*nawafunza wanetu kuvuta bangi, niliyakumbuka maneno ya jirani yetu aliyekuwa akifanya kazi serikalini.
>
> (*Musaleo!*, u.k 1)

Katika 82 kuna virejelea viwili; *Hawa* na *wa-*. *Hawa* ni kionyeshi kirejelea cha *watoto* na *wa-* ni kiwakilishi cha ngeli ya *watoto*. Virejelea hivi vimetumika kuondoa urudufishaji wa nomino *watoto* na kuleta maana na mshikamano unaokubalika katika Kiswahili.

Salkie (1995; 64-66) aliita kiwakilishi na kionyeshi, maneno rejeshi. Akasema kwamba haya ni maneno ambayo hayana maana kamili yakiwa pekee. Ili kujua yana maana gani, lazima kurejelea kitu au sehemu nyingine katika matini. Maneno haya rejeshi yanayofahamika ni viwakilishi nafsi, *mimi*, *wewe*, *wao*, n.k. na viwakilishi milikishi; *changu, chako, vyenu* n.k. Kwa hivyo, urejeleaji ni uhusiano kati ya maana ya neno na mazingira yake, ambapo mazingira haya huweza kuwa matini au ulimwengu halisi.

Katika urejeleaji, kiwakilishi au kionyeshi hutumika. Halliday (1996: 20-21) anashadidia wazo hili anaposema kwamba mshiriki au elementi fulani ambayo imetajwa katika sehemu mojawapo katika matini inaweza kuchukuliwa kama pointi ya urejeleaji kwa kitu kile kinachofuata. Hii ina maana kuwa kiwakilishi au kionyeshi kinatumika kurejelea nomino iliyotangulia. Hata hivyo, mifano ya faridi hizi aliyotoa Salkie na Halliday ilitoka katika Kiingereza. Lakini katika Kiswahili viwakilishi nafsi hujumuisha viambishi pia vinavyopachikwa katika vitenzi, vivumishi, viashiria na vimilikishi (Kapinga,1983; Mbaabu,1985; Mgullu,1999). Mifano bora ya maneno haya ni viwakilishi nafsi na vivumishi vya ulingano:

83. . a) Mamantilie alimvuta ndani na Lomolomo akakaa kizingitini...

> Lomolomo alitema mate, yakatua kwenye mguu wa mkewe.
> "Alaa! Mkewe alisema kwa hasira. "*Wewe*! Hivi *wewe u*na akili.
> *U*nanitemea mate yako ya ulevi *mimi*! Ee?"
> (*Watoto wa Maman"tilie*, u.k 11)

> b) Wachapishaji wake waliendelea ku*mwa*mbia, "Mzee, samahani
> lakini ndivyo hivyo bwana; watu nchi hii hawasomi siku hizi!
> Vitabu hatuuzi tena! Karibu tutafunga *sisi*!" Kimya.
> (*Musaleo!*, u.k 2)

Hapa 83 a), virejelea ni *wewe, u-* na *mimi*. *Wewe* kinarejelea Lomolomo, *u-* kinarejelea Lomolomo na *mimi* kinarejelea Mamantilie. Virejeleo hivi ni viwakilishi vya nafsi na vimetumika ili kuondoa urudufishaji. Visingetumika katika nafasi hizo na badala yake kutumia nomino Lomolomo na Mamantilie, mshikamano katika matini hii ungeharibika. Na katika 83 b) virejeleo ni *mwa-* na *sisi*. *mwa-* kinarajelea nomino Mzee na *sisi* kinarejelea Wachapishaji. Hii inatokea ili kuondoa urudufishaji unaoharibu mshikamano. Kwa hivyo viwakilishi nafsi *wewe, u-, mimi*, *mwa-* na *sisi* vimetumika kurejelea nomino zilizo kwenye matini kuondoa urudufishaji na kuleta mshikamano. Viwakilishi *u-,* na *mwa-* ni viambishi nafsi katika Kiswahili.

Urejeleaji una sifa ya kisemantiki ya umahususi. Umahususi huu hupatikana kwa kurejelea muktadha wa hali fulani. Kwa hivyo uhusiano wa urejeleaji ni wa kisemantiki:

> 84. . Mara hii Kingunge alikatizwa uandishi wake na makelele
> yaliyotoka *huko*$_1$ nje. *A*liinuka kitini na kuelekea chumbani
> alikokuwa Zamda. *A*likuwa *a*mejilaza *huko*$_2$ labda kutokana na
> uchovu wa safari ya kutoka kwao…
> (*Musaleo!* u.k 15)

Matini 84, nomino ni 'Kingunge' na 'Zamda'. Pia pana kielezi cha mahali, 'chumbani'. Vitu hivi viwili vimerejelewa kwa kutumia virejeleo *A-*, na *huko*. *A-* katika sentensi ya pili kwenye kitenzi '*A*liinuka' inarejelea 'Kingunge' na kirejelea *huko*$_2$ kinarejelea

'chumbani'. Hivyo vimeondoa urudufishaji na kuleta mshikamano. Ifahamike virejelea vingine hapa ni *a-* katika kitenzi alikatizwa na *huko*$_1$ katika sentensi ya kwanza. Hivi pia vimechangia mshikamano wa kisarufi katika matini. *Huko*$_2$ ni kirejelea kwa sababu kimuktadha, neno 'nje' limeshatajwa mwanzoni katika matini. Kwa hivyo *huko*$_2$ inarejelea 'nje' iliyotokea mbeleni, na 'nje' tunayoiona katika mfano huu imetumika kusisitiza tu hapo mahali. *Huko*$_2$ pia ni kibainishi cha mahali mahususi katika dondoo hili.

> 85. . "...Pole, pole Zita, ee!" walianza tena kusema kwa mzaha
> baada ya kugundua kuwa kalikuwa kajeraha kadogo tu.
> Sara, rafiki yake, hakucheka. *A*li*mwo*nea huruma. *A*li*m*karibia
> na ku*m*futa vumbi. "Pole rafiki yangu."
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 4)

Na matini 85, kuna urejeleaji wenye sifa ya kisementi. *A-*, *mwo-* na *–m-* ni virejelea vya nomino Sara na Zita. Virejea hivi vinauhusiano wa kisemantiki na nomino hizo. Msomaji atavihusisha kisemantiki na nomino hizo ili kupata maana. Hivyo kuleta mshikamano katika matini na kuondoa urudufishaji wa nomino hizo.

Urejeleaji huweza kutokea katika njia mbili;

i) Urejeleaji nje

ii) Urejeleaji ndani

Njia hizi za urejeleaji pia huitwa urejeleaji wa hali na urejeleaji matini. Urejeleaji wa hali ni wakati tunaporejelea kitu katika muktadha wa hali, na urejeleaji matini ni pale tunaporejelea kitu kama kinavyoonyeshwa katika matini. Tukichunguza ni kuwa urejeleaji wa hali ndio mrejeonje na urejeleaji matini ni ule mrejeodani. Katika tasnifu hii

tumetumia mrejeonje na mrejeondani, sawa na urejeleaji nje na urejeaji ndani. Aina hizi zimejitokeza katika matini za Kiswahili teuzi.

| MATINI | MREJEONDANI | MREJEONJE | JUMLA (IDADI) |
|---|---|---|---|
| *Watoto wa Maman'tilie* | 6335 | 3 | **6338** |
| *Musaleo!* | 14572 | 114 | **14686** |

3.2 IDADI YA UTOKEAJI WA MREJEONJE NA MREJEONDANI

### 3.1.1 Mrejeondani

Urejeleaji ndani hutokea wakati virejelea vinarejelea nomino zilizo ndani ya matini. Urejeleaji ndani ni pale ambapo itambidi msomaji arejelee ndani ya matini ili kuelewa yale yanayozungumzwa. Yaani faridi moja hurejelea faridi ya nyuma au iliyotangulia kutajwa katika matini. Kwa hivyo msomaji anapoiona faridi hii ya mbele, hupata maana tu anaporejelea ile ya nyuma (kitajwa).

Urejeleaji ndani huweza kugawanywa mara mbili; urejeleaji nyuma na urelejeaji mbele. Uhusiano wa urejeleaji nyuma ni kujenga mshikamano kati ya kirejelewa kilicho nyuma na kirejelea kitokeacho mbele katika matini. Ikiwa virejelea vitatumika, msomaji hana budi kuangalia kwingineko ili apate maana ya kirejelea hicho; na ikiwa basi itambidi msomaji aangalie kile kilichozungumzwa awali katika matini na kupata maana, hii huleta ufungamano kwa kuunganisha aya mbili (au sentensi mbili) na kuunda matini moja (Halliday, 1985:291; Halliday na Hassan, 1976:33). Mrejeondani umetokea mara elfu sita, mia tatu na thalathini na sita (6335) katika *Watoto wa Maman'tilie* na mara elfu

kumi na nne, mia tano na sabini na mbili (14,572) katika *Musaleo!*. Tuangalie jinsi mreombele ulivyo katika matini teule:

> 86. a) Peter alinyamaza kidogo akawa anampima mwenzake kwa
> Macho makali. *A*liziona nywele za kipilipili za Musa, ngumu kama
> katani, haz*i*jaonja maji wala sabuni.
> "*Wewe* mama yako anasemaje?" Musa aliuliza.
> "Hasemi kitu," Peter alijibu. "Ila *mimi* lazima *ni*rudi shule."
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 17)

Katika matini hii 86a), kuna mrejeondani. Vile vyote vinavyorejelewa, vimo ndani ya matini. Kirejelewa ni nomino 'Peter' na virejelea vyake ni kiambishi *A-*, *ni-* na viwakilishi nafsi *Wewe* na *mimi*. *Wewe* kiko katika nafsi ya pili na kilitamkwa na Musa akimrejelea 'Peter'. *Mimi* ni kirejelea katika nafsi ya kwanza. Kilitamkwa na Peter akijirejelea 'mwenyewe'. Kwa hivyo hapa kuna mrejeondani.

> b) *Ni*lisikia vicheko vikinijia. *Ni*lipogeuka macho yangu yalitua
> juu ya jamaa wawili. Nilisoma nao zamani...*Ni*liwakaribisha...
> *Wa*lichofanya nikuhamia *ni*lipokuwa...
> *Tu*likunywa kwa kipindi kirefu. Baadaye *tu*lianza kupiga
> makelele ya ulevi.
> (*Musaleo!* u.k 6)

Katika 86b) virejelewa ni 'jamaa wawili' na 'msimulizi' mwenyewe. Virejelea ni *Ni-* kikirejela 'msimulizi' na *Tu-* kikirejelea 'jamaa wawili + msimulizi'. Virejelea hivi vimeondoa urudufishaji wa kundi nomino (KN) ambao ungeharibu mshikamano. Kwa hivyo, urejeleo wao umeleta mshikamano.

Viwakilishi nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu aghalabu hutumika katika urejeleaji katika Kiswahili. Nafsi zote tatu zinaweza kutumika katika mrejeonje na mrejeondani.. Virejelea (viwakilishi) katika nafsi ya tatu hujumuisha nafsi ya kundi nomino (KN). Kutoka sasa tutatumia KN. KN ndiyo huteuwa kirejelea katika ulimwengu wa usemi

(Haegeman, 1994: 226). Pia vionyeshi *hiki, kile, hivi, vile* hutumika katika mrejeondani (Salkie, 1995:66-67). Katika Kiswahili virejelea hivi hutawaliwa na ngeli ya KN. Kwa hivyo KN ndiyo huongoza ni kirejelea gani kitatumika katika maneno ya mbele yajayo au hata yale ya nyuma yake:

> 87. Sikuwa na nia ya kwenda Mkwiro Inn siku hiyo kabisa. Ilitokea *hivi*. *Ni*lipofika nyumbani *ni*liamua kujipumzisha kitandani kwa sababu ya machovu ambayo yalinilaza. Usingizi wangu ulikatizwa na mlio wa simu ya nyumbani. *A*likuwa rafiki yangu mkubwa wakati nasoma sekondari...
> *A*litaka tukutane huko Mkwiro Inn.
> (*Musaleo!* u.k 8)

Katika 87, *hivi* ni kirejelea cha 'sababu' iliyotolewa na msimulizi kutotoka nyumbani kwake. Kirejelea hiki kinarejelea dhana iliyo ndani ya matini. Dhana hiyo ni jinsi msimulizi alivyofanya alipofika kwake nyumbani na yaliyotokea huko. Kwa hivyo ametumimia kirejelea *hivi* kumdokezea msomaji yale atakayosimulia hapo mbele yake. *A-* ni kirejelea cha 'rafiki wa msimulizi' na ni nafsi ya tatu. Virejelea vyote hivi vinatudhihirishia mrejeondani. Hata hivyo *A-* vile vile inaweza kuwa inarejelea nje kwani 'rafiki' huyo hajatajwa awali. Kirejelea *Ni-* katika kitenzi 'Nilipofika', kinarejelea 'msimulizi' katika matini hii katika nafsi ya kwanza.

> 88. Mama alisema, "*M*siwe *m*nachezea na kuchokoza mbwa, ala!"
> "Hata mama!" Peter alisema. "*Sisi tu*likuwa *tu*napita tu, *a*kaanza ku*tu*fukuza."
> "Nende*ni*$_1$, *m*badilishe nguo za shule, *m*je m*ni*$_2$saidie kazi mie."
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 6)

Katika 88, *M-*, *m-* na *–ni*$_2$, ni virejelea vya 'Peter, Zita na wenzao' na ni nafsi ya pili. Virejelea Sisi na tu- vinarejelea 'Peter na wenzao' na ni nafsi ya kwanza, pia *ni*$_2$ ni nafsi ya kwanza ikirejelea 'Mama'. *a-* ni nafsi ya tatu ikirejelea 'mbwa'. Virejelea hivi vyote vimechangia mshikamano kwa kuondoa urudufishaji wa nomino.

Kuna ishara nyingi zinazoonyesha utambuzi kati ya kile kinachotajwa au kuzungumzwa na kilichotangulia katika usemi au matini. Hivi vyote vina urejeleaji bainishi, na hurejelea nyuma au mbele. Vionyeshi hivi ni *hapa, ki-, hiki, huyu, kile* (Quirk na Greenbaum, 2000: 302). Safir (2004:29) anadai kuwa vionyeshi bainishi vyote vya nomino huwa ni mrejeosabiki. Hii ni kwa sababu nomino inayobainishwa huwa imeshatajwa awali katika matini. Hivyo inarejelewa na kuwekwa mahususi. Virejelea vyote tulivyovitaja hapo juu, iwe ni katika mrejeonje au mrejeondani, huweza kuwa vya mrejeombele au mrejeosabiki. Mrejeombele na mrejeosabiki umetokea katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*. Jedwali 3.3 linatoa muhtasari wa utokeaji huu.

| MATINI | MREJEOMBELE | MREJEOSABIKI | JUMLA (IDADI) |
|---|---|---|---|
| *Watoto wa Maman'tile* | 811 | 5524 | **6335** |
| *Musaleo!* | 1160 | 13412 | **14572** |

3.3 IDADI YA UTOKEAJI WA MREJEOMBELE NA MREJEOSABIKI

Katika Jedwali hili 3.3 tunaona kwa jumla utokeaji wa mrejeombele na mrejeosabiki katika matini zote mbili. Mrejeombele umejitokeza mara mia nane na kumi na moja (811) katika *Watoto wa Maman'tilie* na mara elfu moja, mia moja na sitini (1,160) katika *Musaleo!*. Nao mrejesabiki umetokea mara elfu tano, mia tano na ishirini na nne (5,524) katika *Watoto wa Maman'tilie*, na mara elfu kumi na tatu, mia nne na kumi na mbili (13,412) katika *Musaleo!* Hivyo kutudhihirishia kuwa mrejeosabiki umetumika zaidi kwa sababu ya mchakato na muundo wa Kiswahili kuwa ni lugha ya uambishaji.

Baada ya maelezo haya tuchunguze jinsi mrejeombele na mrejeosabiki ulivyotokea katika matini tulizozitumia.

| | MREJEO NDANI | | |
|---|---|---|---|
| MATINI | MBELE | SABIKI | NJE |
| *Watoto wa Maman'tilie* | 12.79 | 87.16 | 0.05 |
| *Musaleo!* | 7.89 | 91.33 | 0.78 |

3.4 UTOKEAJI WA UREJELEAJI KWA ASILIMIA (%)

Tunavyoona katika jedwali 3.4 ni kwamba mrejeosabiki ndio umejitokeza zaidi katika matini zote mbili; *Watoto wa Maman'tilie* asilimia thamanini na saba nukta moja sita (87.16%) na katika *Musaleo!*, asilimia tisini na moja nukta tatu tatu (91.33%). Uliofuata ni mrejeombele ambapo katika *Watoto wa Maman'tilie* umetoza kwa asilimia kumina mbili nukta saba tisa (12.79%) na katika *Musaleo!* ni asilimia saba nukta nane tisa (7.89%). Urejeleaji uliotumika kwa uchache zaidi ni mrejeonje ambapo katika *Watoto wa Maman'tilie* ni asilimia sufuri nukta sufuri tano (0.05%) na katika *Musaleo!* ni asilimia sufuri nukta saba nane (0.78%). Jambo hili linaonyesha kuwa lugha ya Kiswahili ina mrejeosabiki zaidi. Hii ni kwa sababu kiima au nomino hutangulia katika sentensi na ndio muundo wa Kiswahili, na viambishi ndivyo virejelea na huja baada ya kiima au nomino.

### 3.1.1.1 Mrejeombele

Mrejeombele ni wakati kirejelea kionyeshi au kiwakilishi nafsi kinarejelea faridi itakayokuja katika sentensi fuatilizi. Kirejelea hiki huja mwanzo katika matini kisha nomino inayorejelewa kuja baadaye (Halliday na Hassan, 1976:233). Na ili kukifasiri kirejelea hiki lazima uangalie mbele ya matini ili upate kile kinachorejelewa na kuunga

maana kamili. Virejelea vya namna hii huleta mshikamano katika matini. Hivi ndivyo mrejeombele ulivyojitokeza katika matini teule:

> 89. *Ukolongwe aliendelea na tabia yake. Hakujali. Ahhh! Lazima nikutajie hili. Sifa moja inayohusishwa na Ukolongwe ni kubadilisha mambo ya kimsingi aliyoyakuta siku hizo.*
> (*Musaleo!* u.k.30)

(Maandishi ni ya mlazo katika matini yenyewe.)

*Hili* ni faridi (kionyeshi) inayorejelea mbele, 'sifa ya Ukolongwe ya kubadilisha mambo'. Kwa hivyo *hili* imeshikanisha maelezo ya tabia ya Ukolongwe na kufafanuliwa zaidi na sifa iliyotolewa ya kubadilisha mambo aliyoyaona na kuyafanya kivyake. Hivyo maelezo ya tabia, ili kuwa na muwala ilibidi mwandishi au msimulizi ayashikanishe na maelezo anayoyaendeleza ya Ukolongwe ambayo ni sifa yake kuu, 'kubadilisha mambo'. Kwa kuyashikanisha masimulizi tangulizi na fuatilizi, ametumia kirejelea *hili*. Kwa hivyo kirejelea hiki kimeshikanisha tabia ya Ukolongwe kwa jumla na ile sifa ya kubadilisha mambo. Urejeleaji huu umeunganisha dhana hizi mbili na kuleta mshikamano wa matini, hivyo kuupa maana na kueleweka na kujenga mtiririko wa maelezo au mawazo.

> 90. "Unasemaje Kurwa?" Dan aliuliza.
> "Mnakosea . Ni *hivi*," Kurwa alieleza... "Mkirudi *hivi*$_2$- kwangu, itakuwa hatari kubwa . Mimi naona mkishachukua mali- mnatoka, mnatoka, mnazunguuka huku nyuma, mnatokea uchochoro huu kushoto, mnapotea kufuata barabara ya Relwe".
> (*Watoto wa Maman'tilie,* u.k. 42)

Katika matini hii, virejelea ni *hivi*$_1$ na *hivi*$_2$. *hivi*$_1$ ndiyo inayorejelea mbele. Kirejelea hiki kinarejelea maelezo ya Kurwa na kuyashikanisha na maelezo ya awali ya Dan jinsi watakavyotimiza nia yao ya kuiba duka la mhindi. Hivyo kuunganisha mawazo haya na kuleta mshikamano. Urejeleaji hapa ni wa msururu wa sentensi na mawazo. *hivi*$_2$ si kirejelea cha mbele ila cha nyuma, hivyo mrejeosabika.

### 3.1.1.2 Mrejeosabiki

Huu ni urejeleaji ambapo kirejelea kionyeshi au kiwakilishi nafsi kinarejelea faridi iliyokwisha kutangulia katika matini. Kirejelewa hutokea mwanzo katika matini na kirejelea huja baadaye kwenye matini hiyo hiyo (*Kama hapo juu*). Safir (2004:4) anasema kuwa matumizi ya lugha kwa minajili ya kuwasiliana, hubidi urejeleaji wa kipashio kimoja au zaidi katika matini. Urejeleaji wa kipashio unaotokea baadaye katika matini/usemi ndio huwa mrejeosabiki. Kwa hivyo kirejelea huwa kiko mbele na kirejelewa kiko nyuma. Huu ndio huitwa mrejeosabiki. Tuchunguze matini 91a na 91b..

91. .a) ...Nyumba haikuwa na mtu ila Peter. *A*likuwa kakaa nje kiambazani *a*kiwaza, *a*kiota jua, "Leo *ni*takwenda *ni*jaribu." Tatizo *a*liloliona Peter ni moja tu. *Nalo* ni mama yake.
(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 14)

Hapa 91a) virejeleo *A-, ni-, a, Nalo* vimetumika kushikanisha virejelewa nomino 'Peter' na 'Tatizo'. Badala ya nomino hizi kutumika katika kila kishazi, viwakilishi virejeleo vimetumika ili kuipa matini hii sarufi inayokubalika katika Kiswahili. *A-, a-* na *ni-* ni virejeleo vya' Peter' na *Nalo* ni kirejelea cha 'Tatizo'. Iwapo nomino rejelewa zingetumika badala ya virejelea (viwakilishi) kungetokea urudufishaji ambao ungeharibu mshikamano wa matini. Matini hii kama ilivyo ina mshikamano kwa sababu ya matumizi ya virejelea hivyo. Tunapochunguza zaidi, kiwakilishi *a-* katika kitenzi '*a*liloliona' ni kwamba kinaweza kurejelea nyuma (Peter aliyetangulia kutajwa) au kurejelea Peter mbele. Hapa kimetumika kama mfano wa mrejeosabiki.

b) "Huku kila mtu anajua alivyo Mzee; ana watoto wengi kila

mahali. Zipo mimba chungu nzima *zi*nazotunzwa. Zo..oote ni zake!" Nilishindwa kuelewa. "Je una maana ya Mzee nim-juaye kweli? *Huyo* hana mke asilani!"
(*Musaleo!* u.k. 40)

Katika 91b) *Huyo* ni kirejelea cha nomino kirejelewa 'Mzee'. Kimewekwa hapo kuwakilisha 'Mzee' kikirejelea nyuma na kushikanisha maana katika matini kikileta mshikamano. Huu ni mrejeosabiki.

Kwa hivyo mrejeombele na mrejeosabiki unatokea katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* kuleta mshikamano. Urejeleaji unaweza kuwa mrejeondani au mrejeonje. Mrejeondani huwa ama mrejeombele au mrejeosabiki. Pia kuna vionyeshi mbalimbali vya urejeleaji vinavyodhihirisha kijenzi hiki katika matini. Aidha kiwakilishi au kionyeshi kinaweza kurejelea neno au kirai au sentensi kadha, na kirai kinaweza kurejelea kirai kingine katika matini. Katika urejeleaji wa sentensi au msururu wa sentensi, kinachorejelewa huwa ni ile dhana katika sentensi hizo.

### 3.1.2 Mrejeonje

Mrejeonje hutokea wakati inambidi msomaji arejelee nje ya matini ili kupata maana au kuelewa kinachozungumzwa (Brown na Yule, 1983:192; Halliday na Hassan, 1976:4). Mrejeonje ni wakati ambapo faridi, inabidi msomaji arejelee nje ya matini anayoisoma ili kuifasiri. Akifanya hivi ndipo hupata maana na kuleta mshikamano. Katika Jedwali 3.2 matini ya *Watoto wa Mamn'tilie* mrejeonje umetokea mara tatu (3) tu, na katika *Musaleo!* umetokea mara mia moja na kumi na nne (114). Katika matini tulizozichunguza mrejeombele ulijitokeza kama ifuatavyo:

> 92. "Wazee hawa ni wakongwe walioifanyia nchi hii kazi kubwa! Ni wapiganaji wa uhuru; unaweza kuwaita **War veterans**. Wali-ahidiwa mengi kama mashamba, nishani pamoja na kujengewa minara katika Uwanja wa Uhuru...lakini bado wanasubiri. Nili-pitisha kipindi kirefu nikiwaza. Mwanzo nilitaka kuwalaumu *hao*

> waliotangulia kwa kutotambua nafasi ya wazee muhimu kama hawa...".
>
> (*Musaleo!* u.k. 15)

Katika matini 92, *hao* inarejelea nje kwa sababu *hao* ni watu ambao hawajatajwa popote katika matini. Tunawadhania tu kuwa ni 'wale watu ambao waliwaahidi **War veterans**' kama inavyoelezwa kwamba kuna watu ambao waliwaahidi hawa **War veterans**. Hawakutajwa ni akina nani. Kirejelewa kawaida hakitajwi moja kwa moja. Tunaweza kukirejelea kwa kutumia vidokezo katika matini husika ama katika mazowea yetu ya mchakato wa lugha tunayoifahamu. Hivyo huwa kuna ile dhana ambayo ni kipashio muhimu katika mshikamano. Kwa hivyo hapa pana mrejeonje kwa sababu kirejelea *hao* hakifungamani moja kwa moja na kirejelewa dhahiri bali tunadhania tu, na katika kudhania huko ni hao **War veterans**.

> 93. Kurwa aliita, "Zitaaaaa! Zitaaaweee!"
> Lakini Zita dada yake hakumsikiliza. Jiji halikumsikiliza. Polisi hawakumsikiliza. Tangu amezaliwa hakuna *a*liyewahi kumsikiliza wala kumjali.
> Nani *a*najali?
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 98)

Katika matini hii kuna mrejeonje. Kirejelea *a-* katika 'aliyewahi' na 'anajali' kinarejelea 'watu' ambao hawajatajwa katika matini bali wako nje ya matini hii na wanarejelewa kisemantiki. Huu ni mrejeonje.Tunaposoma matini hii kutoka mwanzo au nyuma, hakuna mahali msimulizi aliongea juu ya warejewa. Virejea hivi vimejitokeza tu katika usemi huu. Wanaorejelewa tunawadhania tu kwamba ni watu kwa mujibu wa mchakato wa Kiswahili na muktadha uliopo katika matini hii. Kwa hivyo watu wanaowarejelea wako nje ya matini yote ya *Watoto wa Maman'tilie.* Kwa hivyo matini 89 na 90 inaonyesha mrejeonje unavyojitokeza na umezaa mshikamano wa dhana unaoyafanya masimulizi kueleweka.

### 3.2 Aina za Urejeleaji

Kama tulivyoeleza hapo awali kuna aina tatu za urejeleaji zinazojumuisha mrejeombele au mrejeosabiki. Aina hizi ni;

i) Urejeleaji nafsi

ii) Urejeleaji onyeshi

iii) Urejeleaji linganishi.

Kwa muhtasari, utokeaji wa aina hizi katika matini unadhihirishwa na Jedwali 3.5

| MATINI | AINA ZA UREJELEAJI | | |
|---|---|---|---|
| | NAFSI | ONYESHI | LINGANISHI |
| *Watoto wa Mamantilie* | 5767 (27.6%) | 563 (2.7%) | 5 (0.02%) |
| *Musaleo!* | 13446 (64.3%) | 1117 (5.34%) | 9 (0.04%) |
| JUMLA | **19,213 (91.9%)** | **1,680 (8.04)** | **14 (0.06)** |

3.5 UTOKEAJI WA AINA ZA UREJELEAJI KATIKA MATINI

Katika utafiti huu ilibainika kuwa urejeleaji linganishi hutumika kwa mara chache sana katika matini za Kiswahili. Mfano katika *Watoto wa Maman'tilie* (Mbogo) umejitokeza mara tano (5) tu katika riwaya ya kurasa tisini na nane (98), na katika riwaya ya *Musaleo!* (Wamitila) yenye kurasa mia moja na mbili (102) umejitokeza mara tisa (9). Urejeleaji nafsi umetokea katika matini zote mbili kwa wingi zaidi kuliko aina hizo nyingine; katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* umetokea mara elfu tano, mia saba na sitini na saba, na katika *Musaleo!* mara elfu kumi na tatu, mia nne na arobaini na sita (13,446).

### 3.2.1 Urejeleaji Nafsi

Urejeleaji nafsi ni wakati nomino inarejelewa baada ya kutajwa awali katika usemi au matini. Badala ya hiyo nomino kutajwa tena katika maelezo fuatilizi kwenye matini, kirejelewa hutumika ili kuondoa urdufishaji unaoharibu mshikamano. Virejeleaji vya nafsi ni viwakilishi nafsi; *mimi, yeye, sisi, wao, ki-* pamoja na hali zao za umilikishi (Mohamed, 2001:108; Hatch, 1992:224; Wihiga, 1999:18-19; Kapinga, 1983:108-109). Katika utafiti huu tumecukulia viambishi nafsi kama virejeleaji nafsi. Virejeleaji nafsi huambatishwa kwenye vitenzi, vionyeshi na vimilikishi vikioana na ngeli ya nomino inayorejelewa.

Viwakilishi vyote ni faridi za urejeleaji. Hurejelea kitu kwa kufafanua kazi au dhima katika usemi. Umuhimu wa viwakilishi nafsi ni kuwa ni njia ya kurejelea watu au vitu. Katika katagoria ya kimapokeo viwakilishi hujulikana kama nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu zikijumuisha umoja na wingi wao. Viwakilishi vya nafsi ya kwanza ni *mimi, sisi*; nafsi ya pili ni *wewe, nyinyi*; na nafsi ya tatu ni *yeye, hao, ki-* (Halliday na Hassan, 1976: 39, 44-45). Nafsi ya kwanza na ya pili aghalabu hurejelea nje na ile ya tatu mara nyingi hurejelea ndani kisha nyuma ama mbele. Hata hivyo nafsi ya kwanza na ya pili huweza kurejelea ndani ikiwa zinatumika katika usemi halisi na katika maandishi ya masimulizi ya bunilizi. Nafsi za kwanza na pili aghalabu hutumika katika mrejeonje na nafsi ya tatu hutumika katika mrejeonje au mrejeondani.

Faridi za urejeleaji nafsi mara nyingi hurejelea nyuma. Hurejelea yule au yale yaliyotangulia katika matini. Kiwakilishi cha nafsi kinapotumika humbidi msikilizaji au

msomaji arejelee kwengineko katika matini, hususan nyuma ili kupata ufasiri wa maana. Akifanya hivyo huweza kupata ulingano wa matini na kuleta ufungamano (Halliday, 1985: 291).

Virejeleaji nafsi hutumika ili kukwepa kutumia nomino hiyo hiyo katika kila sentensi au ndani ya sentensi hiyo moja. Hivyo huweza kupunguza urudufishaji ambao wakati mwingine huweza kupotosha maana au mshikamano:

> 94. a) *Peter Peterlinyamaza kidogo Peterkawa Peternampima
> Mwenzake kwa macho makali. *Peter*ziona nywele za kipili-
> pili za Musa...
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 17)

Matini hii 94 a) virejelea nafsi havikutumika. Nomino (Kiima) imerudiwa katika kila sentensi na zile sehemu za uwakilishaji kwa mujibu wa muundo wa lugha ya Kiswahili. Kilichotokea ni kuwa matini hii haileti maana na imepotoka kisarufi. Tuchunguze matini hii ikitumia viwakilishi virejelea.

> b) Peter *a*linyamaza kidogo *a*kawa *a*nampima mwenzake kwa macho
> makali. *A*liziona nywele za kipilipili za Musa...

Matini hii 94b) inaleta maana na mshikamano kwa kutumia viwakilishi nafsi kurejelea nomino kiima, Peter tofauti na ile 94 a).

Viwakilishi milikishi kama virejelea vinatofautiana na viwakilishi nafsi katika urejeleaji wake wa nyuma. Viwakilishi nafsi huhitaji tu kirejelewa kimoja ili kufasirika, viwakilishi milikishi huhitaji virejelewa viwili, mwenye kumiliki na kimilikiwa (Halliday na Hassan, 1976: 55). Jambo hili linadhihirika katika Kiswahili:

> 95. ...*Peter* alitafuta nyuzi za katani, akatengeneza brashi nzuri na
> kuinamia kibao. Chovya, andika chovyo, andika... taratibu.

> Hadi kazi ikawa tayari... Alirudi hatua tatu nyuma, *a*kawa *a*name-
> zea mate ufundi *wake* mwenyewe...
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 66)

Hapa kimilikishi ni *wake* kinarejelea 'ufundi wa Peter'. Kwa hivyo kinarejelea virejelewa viwili, Peter (Mmiliki) na *ufundi* (kimilikiwa) na kuleta mshikamano unaohitaji katika matini hii. Kwa hivyo viwakilishi nafsi ni muhimu sana katika kuleta mshikamano katika Kiswahili na ni lazima katika urejeleaji kwa mujibu wa muundo wa lugha hii (Mohammed, 2001:58).

Kuna urejeleaji wa nafsi mbalimbali katika Kiswahili kwa kutumia virejelea tulivyotangulia kuvitaja. Virejelea hivi hutokea katika nafsi mbalimbali na kutawaliwa na nafsi husika katika muundo na mchakato Kiswahili. Tuangalie jinsi viwakilishi hivi vimetumika kama virejelea katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*

### 3.2.1.1 Urejeleaji wa Nafsi ya Kwanza

Katika Kiswahili kirejelea nafsi ya kwanza kinaweza pia kuwa kiambishi kiwakilishi cha nomino katika kitenzi:

> 96. "Mbwa mama!" Peter alidakia huku akicheka, "Mbwa mweusi
> alikuwa ana*tu*fukukuza. Zita alianguka chini. Hee! Mama! Karibu
> yule mbwa amng'ate."
> Zita akasema, "Ame*ni*kwaruza kidogo na makucha yake." Aligeuza
> mguu wake ili kumwonyesha mama yake.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 6)

Katika matini 96, kuna viwakilishi nafsi viwili, *-tu-* na *-ni-*. Kiwakilishi nafsi *–tu-* ni hali ya wingi na *-ni-* ni cha hali ya umoja. –tu- kinawakilisha nomino Peter na Zita. Badala ya kurudia nomino hizi imebidi kirejelea hiki kitumike kuondoa urudufishaji na kuleta mshikamano katika sentensi na matini. *-ni-* vilevile kimetumika kurejelea na kuwakilisha

nomino Zita badala ya kuirudia katika kitenzi *–kwaruza*. Hali hii imeleta maana na mshikamano kama inavyohitajika katika Kiswahili.

> 97. *Ni*likimbia ndani kwenda kuvaa shati (sikuvaa shati nikiwa chumbani majira haya)... Ili*ni*chukua muda kulipata shati la kuvaa... Sikuwa na muda wa kuvaa viatu bali *ni*li*vi*chopea tu huku *ni*ki*vi*buruta...
>
> (*Musaleo!* u.k. 1)

Hapa pana kirejelea *Ni-* ambacho ni kiwakilishi nafsi umoja. Kiwakilishi hiki kinawakilisha nomino msimulizi wa habari hii. Hakuweza kutaja jina lake katika masimulizi haya, ni lazima atumie kiwakilishi kirejelea. Muundo na mchakato wa Kiswahili unalazimisha hivyo. Tunapochunguza matini hii, –ni- kimetumika kurejelea mwandishi katika sentensi zote fuatilizi baada ya kwanza. Kirejelea hiki kimeshikanisha mawazo, kikaondoa urudufishaji na kuleta maana katika matini hii. *–vi-* aidha kimetumika kuwakilisha nomino *viatu* katika sentensi kadhaa katika matini. Kimechangia kuleta mshikamano wa matini.

Kama tulivyotangulia kueleza kuna viwakilishi nafsi ya kwanza, *mimi* na *sisi*. Viwakilishi hivi huingia katika muundo wa sentensi kama mshiriki au mmilikaji. Katika mshiriki huwa na uamilifu wa kiini katika KN:

> 98. "Mama yako anasemaje?"
> "Aa! Mama ana hamsini zake. Na *mimi ni*na sitini zangu," Musa alijibu.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 17)

*Mimi* ndicho kiini na kiima katika matini hii. Pia ni kiwakilishi nafsi. *Mimi* ni kiwakilishi nafsi na kinarejelea 'Musa'. *ni-* katika 'nina' ni faridi ya mshikamano kwa sababu inarejelea faridi iliyotangulia, na ni kirejeleo cha '*Mimi*'. Musa hangeweza kujitaja jina lake, lazima atumie kiwakilishi mimi kujirejelea. Iwapo atatumia jina lake, matini hii

itakuwa na urudufishaji ambao ungeharibu mshikamano wa kisarufi na haukubaliki katika Kiswahili. Kwa hivyo katika matini hii kuna urejeleaji wa nafsi uliotumia kiwakilishi nafsi *mimi* na kiambishi nafsi *ni-*. Virejeleo hivi ni nafsi ya kwanza.

Ili kiwakilishi nafsi kidhihirishe mshikamano katika matini lazima kiwe kinarejelea nafsi (Kiima au Yambwa) ama iwe nyuma au mbele. Katika matini 98, *mimi* inarejelea kiima Musa na kusimama kama kiima. Katika Kiswahili hii hudhihirisha mshikamano katika sentensi moja au msururu wa sentensi au iwe katika usemi.

> 99. "...Uandishi! Uandishi! Uandishi wa nini?" lakini mara hii alipomweleza mkewe uandishi wenyewe bali alilazimika kusikiliza kwa makini. "Mara hii ni tofauti. Inajisimulia *mimi* naandika tu..."
> (*Musaleo!* u.k 12)

Katika matini hii, *mim*i ni kiwakilishi kirejelea cha nafsi ya kwanza. Kirejelea hiki kinarejelea 'msimulizi au msemaji'. Kwa hivyo kama wadaivyo Halliday na Hassan (hapo juu) katika bunilizi, kirejelea *mimi* cha nafsi ya kwanza kimemrejelea 'msimulizi' ndani ya matini.

> 100. Mama alisema, "Msiwe mnachezea na kuchokoza mbwa, ala!" "Hata mama!" Peter alisema. "*Sisi* tulikuwa tunapita tu, akaanza kutufukuza."
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 6)

Katika matini 100, kiwakilishi nafsi 'Sisi' ndicho kirejelea cha Peter na Zita watoto wake waliofukuzwa na mbwa walipotoka shuleni. Nafasi ya Sisi katika muundo huu hairuhusu nomino Peter na Zita kuchukua nafasi yake, mfano, *"Peter na Zita tulikuwa tunapita...". Hapa pana urudufishaji wa nomino ambao haukubaliki na unaharibu mshikamano na usahihi wa sentensi hii. Kwa hivyo katika masimulizi na usemi halisi, msimulizi au msemaji lazima ajirejelee kwa kutumia kiwakilishi nafsi. Salkie (1995:66) anashadidia

hoja hii kwa kueleza kuwa katika simulizi ya bunilizi nafsi ya kwanza *mimi* hutumika kurejelea *msimulizi* au *mwandishi mwenyewe*.

**3.2.1.2 Urejeleaji wa Nafsi ya Pili**

Virejelea vya nafsi ya pili huwa viwakilishi nafsi *wewe* na *nyinyi*. Viwakilishi hivi ni katika umoja na wingi mtawalia. Viwakilishi hivi hutumika katika usemi halisi ambapo wanaojibizana hurejeleana kwa viwakilishi badala ya majina yao pale ambapo yanatokea. Hii huondoa urudufishaji wa nomino hizo na kuleta lugha inayokubalika na kuwa na mshikamano unaofaa.

> 101. "Nini *wewe*?"
> Mtu alikuwa amemgusa begani naye aligeuka.
> "Aa! Musa."
> "Habari zako, Peter."
> "Nzuri Musa," Peter alijibu. Alimwona Musa kashika paketi
> ya sigara, anauza. "Za nani?"
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 17)

Katika 101, *wewe* ni kiwakilishi kirejelea katika nafsi ya pili kikimrejelea 'Musa'. Kirejelea hiki kimewakilisha nomino *Musa.* Kutokea kwa kirejelea hiki, kumekwepa kurudia nomino hii. Iwapo ingerudiwa rudiwa, mshikamano utaharibika na usahihi wa Kiswahili kutokubalika. Lakini matumizi ya *wewe* yameleta mshikamano wa kisarufi.

Aidha viambishi viwakilishi *u-* na *m-* huwa virejelea katika nafsi ya pili umoja na wingi mtawalia. Hivi pia hutawaliwa na ngeli ya nomino rejelewa. Vitumikapo huondoa urudufishaji wa nomino na kuleta usahihi wa Kiswahili na mshikamano wa kisarufi. Silabi *–ni* pia huchukua nafsi ya pili wingi na kuwa kirejelea ikiambishwa mwisho wa kitenzi:

102. "*U*naelekea kujiingiza katika mambo yasiyokuhusu...
Sio ujasiri kumwendea bafe macho wazi, *u*nasikia!
(Niliitikia). Tunakuangalia tu; hata tumejua *u*mekuwa wapi leo

na nani! Tunajua kila kitu! Hatuna tusilolijua. Hivi *u*najua
kilichompata Ngwena?"

(*Musaleo!*, u.k. 11)

Katika matini 102, kiwakilishi nafsi u- ndicho kirejelea katika nafsi ya pili umoja. Kinarejelea *Kingunge,* na anayeongea ni rafiki yake, Kitungule. Anayeambiwa maneno haya ni *Kingunge*. Anaambiwa na Kitungule ambaye hawezi kurudia jina la *Kingunge* pale kirejelewa hiki kingestahili kuwa. Kufanya hivyo ni kuharibu mshikamano wa kisarufi kwa kuleta urudufishaji usiokubalika katika Kiswahili. Kwa ajili hii, kirejelea kiwakilishi nafsi *u-* kimeafiki katika nafasi hizo zote ambazo nomino *Kingunge* ingekaa kwa mujibu wa muundo wa Kiswahili. Hii imeleta mshikamano wa kisarufi unaofaa na kukubalika:

103. "Nende*ni*, *m*badilishe nguo za shule, *m*je *m*nisaidie kazi mie."
"Hee! Mama? Zita alianza. "Hizi si nguo za shule mama."
(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 6)

Katika 103, kiambishi tamati-*ni* kimetumika kama kirejelea na kiwakilishi cha nomino Peter na Zita katika kitenzi 'nende*ni'*. Ni kiambishi cha wingi. Nafasi yake haiwezi kuchukuliwa na nomino hizo kimuundo. Hivyo mnenaji, Mamantilie ametumia *–ni* kurejelea Peter na Zita ili kukamilisha usahihi wa mazungumzo haya. Kufanya hivyo, kumeleta mshikamano wa kisarufi unaostahiki. Kiambishi kiwakilishi *m-* ni kirejelea katika nafsi ya pili wingi, vile vile kikiwarejelea Peter na Zita. Haikubaliki katika Kiswahili nafasi yake kuchukuliwa na nomino hizo. Hivyo ni lazima kirejelea hiki kitumike ili kuleta mshikamano wa kisarufi katika matini hii. Pindi kirejelea hiki

kikitolewa na badala yake kuweka nomino hizo basi matini itakuwa haina mshikamano na haitaleta maana.

### 3.2.1.3 Urejeleaji wa Nafsi ya Tatu

Nafsi ya tatu kawaida huoyesha kuwepo kwa kirejelewa mahali fulani katika matini na ikiwa kirejelewa hakipo, basi matini huonyesha kutokamilika. Virejelea vya nafsi ya tatu ni *yeye, wao, hao* na viambishi *a-* na *wa-*. *yeye* na *a-* ni hali ya umoja na *wao, hao* na *wa-* ni hali ya wingi. Nafsi ya tatu pia huweza kurejelea nje, ikirejelea mtu au kitu ambacho kimo katika muktadha wa hali au mazungumzo (Halliday na Hassan, 1976:49). Katika matini za Kiswahili jambo hili hutokea:

> 104. ...*Alisisitiza kuwa lazima watoto waliokuwa wakizaliwa wakati huo wafundishwe nyimbo mpya. Aliiteka nyara lugha na kubadilisha maana za maneno. Wanasema kadri alivyoendelea kukua ndivyo alivyozigeuza maana. Kuna wengine waliosema kuwa alikuwa na tatizo la masikio...*
> (*Musaleo!* u.k 26)

Katika matini hii, viwakilishi virejelea *A-, a-* ni vya nafsi ya tatu umoja na vinarejelea ndani ya matini. Vinarejelea mtu ambaye katika hadithi anaitwa *Ukolongwe*. Ametajwa mwanzoni kabla ya sehemu hii ya matini. Hivyo hapa amerejelewa na virejelea hivyo. Itaharibu mshikamano iwapo nomino Ukolongwe itarudiwa katika nafasi zilizochukuliwa na kirejelea *a-*. *Wa-* na *-o-* ni viwakilishi virejelea katika nafsi ya tatu wingi na vinarejelea 'watu' ambao hawajatajwa katika matini. Hivyo vinarejelea nje ya matini katika muktadha wa masimulizi haya. Vinarejelea watu ambayo wanadhaniwa na mwandishi au msimulizi wanaokuwa na mawazo juu ya mtu Ukolongwe. Viwakilishi virejelea hivi vimetumika kuondoa urudufishaji ambao ungetokea pindi nomino rejelewa

ingetumika katika nafasi hizo. Matumizi ya viwakilishi virejelea hivi vimeleta mshikamano katika matini 104.

> 105. ...Watoto *wa*liingia ndani. Magharibi jua *li*lionyesha rangi
> ya dhahabu nyekundu na Mamantilie *a*lihisi baridi mwilini. Baridi
> ya huzuni *i*limwingia moyoni, *a*kifikiri juu ya elimu ya watoto *wa*ke.
> (*Watoto wa Maman'tilie,* u.k 7)

*wa-* , *li-*, *a-* , *i-* ni virejelea katika nafsi ya tatu na vinarejelea nyuma. *wa-* kinarejelea 'Watoto', *li-* kinarejelea 'jua', a- kinarejelea 'Mamantilie' na *i-* kinarejelea 'Baridi'. Virejelewa vyote hapa vimetangulia kutajwa na katika masimulizi ya mbele, vinapotokea, havitajwi tena bali virejelewa kwa kutumia virejelea nafsi. Kwa hivyo vinarejelea nyuma na kuondoa urudufishaji na kuleta mshikamano katika matini.

Nafsi ya tatu ina sifa ya kuchangia pakubwa katika mrejeosabiki. Panapotokea nomino (kiima) moja katika matini na kuendelea kutokea ndani ya matini viwakilishi hutumika. Na tukio hili huzaa mshikamano katika matini kwani huzua mtandao wa urejeleaji ambapo kila kiwakilishi huunganishwa na vile vyote vilivyotangulia mpaka kwa kirejelewa cha awali (*Kama hapo juu*:52). Katika matini tulizozichunguza jambo hili limetokea na kuchangia mshikamano wa kisarufi katika matini.

> 106. ..."Gunia nita*li*pata wapi?" Peter *a*liuliza *a*kapiga chafya.
> "Tafuta tu kwenye majalala huko" Peter *a*lizunguuka *a*kaleta
> gunia. "*Wewe* nusu na*mi* nusu"
> "Hapana," Peter *a*likataa. "Nipe kidogo tu. *Wewe* *u*mefanya
> kazi kubwa zaidi yangu"
> Kurwa *a*licheka kidogo na kuendelea kugawa ule mchele. Peter
> Hakuelewa kile kicheko kilikuwa na maana gani. Kurwa *a*lisema,
> "Leo *mimi*, kesho *wewe*."
> (*Watoto wa Maman'tilie*,u.k. 27-28)

Matini hii ni mazungumzo kati ya Peter na Kurwa na yalianzia mbali. Hili ni dondoo tu

Tunapoichunguza matini hii tunaona mrejeosabiki unaotumia viambishi viwakilishi na virejelea nafsi.

a) "*li*" inarejelea "gunia"

b) "*a*" Inarejelea "Peter"

c) "*Wewe*" inarejelea "Kurwa"

d) "*-mi*" inarejelea "Peter"

Virejelea hivi vinarejelea nyuma mfano *a-* inarejelea $KN_1$ ya nyuma ambayo ni Peter na *Wewe* inarejelea $KN_2$, Kurwa. Kufanya hivyo kumeondoa urudufishaji, na kutokubalika kisarufi. Hivyo kuleta mshikamano wa kisarufi. Katika matini hii, ili ikubalike katika Kiswahili, ni lazima urejeleaji utumike. Hii inadhihirisha kuwa urejeleaji ni kijenzi muhimu cha mshikamano katika Kiswahili. Tusipoutumia urejeleaji, tungepata matini hii;

107. ..."Gunia nita(gunia)pata wapi?"Peter, (Peter)liliza, (Peter)piga chafya.
"Tafuta tu kwenye majalala huko." Peter (Peter)lizunguuka (Peter)kaleta gunia. "(Kurwa) nusu na (Peter) nusu."
"Hapana," Peter (Peter)likataa. "(Peter)pe kidogo tu. Kurwa (Kurwa)mefanya kazi kubwa zaidi yangu."
(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k.27 )

Tunaposoma matini hii, tunaona urudufishaji wa KN katika kila sentensi. KN hizi, Peter na Kurwa, zinaharibu kabisa mshikamano katika matini na kupotosha maana na kusinya. Hivyo umuhimu wa urejeleaji unajidhihirisha wazi katika mshikamano wa kisarufi.

### 3.2.2 Urejeleaji Onyeshi

Baada ya kutalii urejeleaji onyeshi na ufafanuzi wake katika **2.2**, sasa natuangalie jinsi unavyojitokeza katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*:

108. .....Zita Lomolomo, darasa la sita, na Peter Lomolomo, darasa la tano, walikumbwa na tangazo la mwalimu Chikoya.

> Baba yao, mzee Lomolomo, alikuwa hajawalipia ada
> wala kuwanunulia sare. Lakini *hayo* hayakuwasumbua watoto
> wakati *huu*.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k.1)

Katika 108 *hayo* inarejelea hali hiyo ya Zita na Peter kufukuzwa, haiwajalishi! Na kionyeshi *huu* kinarejelea nomino wakati. Virejelea hivi vimeondoa urudufishaji wa maelezo mengi ambayo yangerudiwa yangeharibu mtiririko na mshikamano wa mawazo hayo na matini hii.

> 109. . ... Katika uchochoro, karibu na kituo cha Msufini, alitokeza
> mbwa. Mbwa *huyu* alikuwa mweusi, mwenye mkia mweupe...
> Na ghafla *yule* mbwa mweusi alisimama, akaunguruma...
>
> (*Watoto wa Maman'tilie,* u.k.1-2)

Katika 109 virejelea *huyu* na *yule* vinarejelea mbwa mweusi. Kisementiki huyu inarejelea mbwa alipokuwa karibu na *yule* ina maana alikuwa mbali kidogo katika masimulizi haya. Hata hivyo *huyu* ina dhana ya msisitizo.

> 110.. ... *Lile* neno kongwe ndilo lililolifufua jina lililokuwa
> limejizika akilini: Ukolongwe. Ilinibidi nimwite *yule* Profesa ambaye
> alipaswa kuchunguza uhusiano uliokuwako kati ya jina *hilo* na langu...
>
> (*Musaleo!* u.k.15)

Mfano 110 kirejelea *Lile* kinarejelea neno, *yule* kinarejelea Profesa na *hilo* kinarejelea jina. Virejelea *huu, yule, huyu* na *hilo* ni elementi za KN ambavyo vinarejelea nomino hizi katika matini hii. Vile vile, *yule* ina msisitizo wa Profesa mahususi na *hilo* kinasisitiza jina. (Maandishi ya mlazo yamo katika matini asili.)

> 111. *Mimi nilikuwa kisasili; kuwako kwangu kulikuwa kisasili kilichofumbata*
> *uhalisi; nilishaanza kuwa sehemu ya fasihi simulizi kama alivyosema*
> *profesa siku siku moja.*
> *Nilipoelezwa hili niliagiza ikaletwe ngoma ya ajabu. Siku iliyofuatia*
> *nilitokeza hadharani. "Mzee, ametueleza kitu kingine jamani, ngoma!"*
> *Huo ukawa mwanzo wa ngoma kuchezwa nchi nzima...*
>
> (*Musaleo!*, u.k.5)

Katika 111, kirejelea *hili* kinarejelea maelezo kuwa "mzungumzaji ni kisasili kilicho na uhalisia', na *Huo* kinarejelea "kutokeza hadharani kwa msimulizi na ngoma". Hapa virejelea hivi vimeondoa urudufishaji ambao ungeharibu mshikamano wa matini.

Pia katika mifano hii pana mrejeosabiki na mrejeombele. Katika 108 na 109 pana mrejeosabiki na mrejeombele. *hayo*, *huu* na *huyu* ni virijelea vinavyodhihirisha mrejeosabiki, na *yule* kidhihirisha mrejeombele. Katika 110, *Lile* na *yule* vinadhihirisha mrejeombele ilhali *hilo* inadhihirisha mrejeosabiki.. Urejeleaji huu ni onyeshi na una sifa ya kisemantiki ya msisitizo na mahususi katika matini hizi. Pia virejelea hivi vimebadilika kiumbo kwa mujibu wa ngeli za Nomino:

| | | |
|---|---|---|
| Wakati *huu* (umoja) | Nyakati *hizi* (wingi) | Ngeli ya N |
| Neno *lile* (umoja) | Maneno *yale* (wingi) | Ngeli ya Ji-Ma |
| Jina *hilo* (umoja) | Majina *hayo* (wingi) | Ngeli ya Ji-Ma |

### 3.2.3 Urejeleaji Linganishi

Urejeleaji linganishi hutokea wakati vitu viwili vinalinganishwa kwa kutumia urejeleaji. Hii ni mbinu mojawapo ya kuleta mshikamano katika matini. Kuna aina mbili za urejeleaji huu; urejeleaji linganishi jumla na urejeleaji linganishi mahususi. Tuchunguze jinsi aina hizi zinavyojitokeza katika matini za Kiswahili.

#### 3.2.3.1 Urejeleaji Linganishi Jumla

Ulinganishi huu ni ule unaolinganisha vitu viwili bila kutumia sifa fulani au mahususi kati ya hivyo viwili. Sifa hizo huwa za jumla. Ulinganishi jumla unaweza kuwa wa mbele au nyuma katika matini au hata wa nje ya matini:

> 112. Tulikuwa tumeenda nusu njia niliposikia sauti za kwanza. *Lakini yafungue masikio yako kabisa yatanasa sauti muhimu.* Nilikumbuka maneno ya profesa. Lazima haya ndiyo aliyokusudia. Nilitega masikio tu. *Haki za mtoto*. Nilisikia sauti *zilizofanana na* za watoto.
>
> (*Musaleo!* u.k. 97)

"*zilizofanana na*" inalinganisha sauti mbili, zilizosikika na zile za watoto bila kutumia sifa yoyote. Huu ni urejeleaji linganishi jumla. Msimulizi analinganisha sauti alizosikia na za watoto yaani zilifanana.

> 113. ...Kazi yangu ilikuwa kuzunguuka huku na huku nikisomba waliokwenda kinyume na matarajio ya Dogmzee. *Intelligence Network* ilikuwa nzuri. Tulikuwa na mfumo ulioundwa *kama bao kuu la kugawia umeme*.
>
> (*Musaleo*! u.k. 86)

Katika 113 " *kama bao kuu la kugawia umeme*" ni kielezi kinachofanya kazi katika kishazi. Hapa ulinganishi ni wa mfumo wa *Network* uliowekwa na ukubwa wa bao. Bao hili huwa kuu na hugawa kwa wingi na mapana. Kwa hivyo mfumo wa *Network* utasambaa kote nchini na kunasa watu wapinzani. Hivyo kuwa kama *bao kuu.*

> 114. ... Ulikuwa mchana ingawa jua halikujitokeza wazi. Joto kubwa lilienea kila mahali. Sehemu tulikokuwa ilikuwa na mteremko. Huko chini kulikuwa na *kitu kama bonde hivi* lakini sikuweza kuona chochote kutokana na kuwako na kitu kilichofanana na ukungu.
>
> (*Musaleo!* u.k.81)

Kwenye matini hii, "<u>kitu kama bonde hivi</u>" ni kivumishi (KV) kinachovumisha KN "kitu". Hivyo kitu hicho kilikuwa kinafanana na bonde. Ndiyo msimulizi analinganisha kitu hicho na bonde. Kwa hivyo kuna ulinganishi wa 'kitu' na 'bonde' ambao ni wa jumla.

> 115. ...Upande wa juu parakacha parakacha. Baada ya muda nilisikia king'ora kama cha meli. "Ni Kasuku. Alihamia huku na king'ora cha meli!" Kimya.

Nilisikia kitu *kilichofanana na* radi za mvua.
(*Musaleo!* u.k. 96)

Mfano huu unaonyesha urejeleaji jumla. "*kilichofanana na*" inarejelea "radi za mvua". Hivyo hapa sifa mahususi iliyotolewa bali ni ule mlio wa radi wakati wa mvua. Kitu fulani kilitoa sauti iliyolinganishwa na radi. Hii ni kwamba msimulizi anarejelea mngurumo wa radi kufananisha na sauti aliyosikia.

### 3.2.3.2 Urejeleaji Linganishi Mahususi

Ulinganishi mahususi hutumia vilinganishi; *zaidi ya, chache/nyingi kuliko' nyingi zaidi, kubwa kuliko* n.k. Hutumia dhana ya idadi. Ulinganishi mahususi hufafanuliwa na vivumishi na vielezi katika muundo wa ulinganishi. Vivumishi hivi hutumika katika KN kuonyesha idadi au vivumisha-nomino. Vielezi navyo hutumika kwa njia mbili;

i) kama CH katika kishazi

ii) visifa-nusu ambapo hutokea ndani ya kisifa

Na ikiwa ulinganishi ni wa umadhubuti, huonyeshwa kwa njia mbili;

i) kwenye kivumisha-nomino katika KN kwa kutumia kivumishi linganishi au kielezi cha ulinganishi kikivumisha kivumishi.

ii) Kama CH katika kishazi kwa kutumia kielezi linganishi au kielezi cha ulinganishi kikivumisha kivumishi.

Tuchunguze mambo haya yanavyojitokeza katika matini za Kiswahili zinazorejelewa:

116. "Gunia nitalipata wapi?" Peter, aliuliza akapiga chafya.
"Tafuta tu kwenye majalala huko" Peter alizunguuka akaleta gunia. "Wewe nusu na mimi nusu."
"Hapana," Peter alikataa. "Nipe kidogo tu. Wewe umefanya kazi *kubwa zaidi* yangu."
Kurwa alicheka kidogo na kuendelea kugawa ule mchele..
(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k.27)

Mfano huu, ni wa urejeleaji linganishi mahususi wa idadi au kiwango. "*kubwa zaidi*" inarejelea kiwango cha kazi aliyofanya Kurwa ikilinganishwa na Peter, ndiyo maana imetumia maneno "zaidi yangu". Na hii "kubwa zaidi" ni KV katika KN.

Tuchunguze mifano mingine:

> 117. a) Tangu wakati waliponicheka zamani, nilishindwa kuwaamini binadamu. Lakini sikutaka wajue. Kila mmoja aliamini kuwa ndiye aliyekuwa rafiki yangu *mwaminifu kuliko* wenzake.
> (*Musaleo!* u.k.7)
>
> b) Bado macho yake yamekoza wekundu, yamelegea kwa usingizi. Aliegemea kizingiti, akamtazama mtu aliyekuwa mlangoni pake. Peter alikuwa kasawajika, *mchafu zaidi kuliko* asubuhi alipompa chai kwa muhogo wa kuchemsha.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k.29)

Katika 117(a) *kuliko* imetumika kama KE kikivumisha KV "mwaminifu" katika kishazi. Na 117(b) kuna KE viwili, *zaidi* na *kuliko*, vikielezea juu ya KV "mchafu". *zaidi* (KE) inafafanua KV "mchafu" na "kuliko" (KE) inafafanua KE "zaidi".

Kwa mujibu wa Gichohi (1999:24) kielezi ni kundi lenye maneno yanayofafanua vitenzi, vivumishi au vielezi vingine. Kwa hivyo KE katika 117(a) ni kielezi cha ulinganishi kikivumisha kivumishi, na 117(b) ni vielezi vya ulinganishi vikivumisha i) kivumishi na ii) kielezi. Hivi ni vilinganishi vya umadhubuti au ubora.

### 3.3 Vikwazo

Vikwazo hutokea katika lugha yoyote ile kinyume na kaida zake au tunapozingatia sarufi bia. Kama wataalamu mbalimbali wasemavyo, mfano Crystal (1997), Chomsky (1962) kuwa kila lugha ina sarufi yake, hivyo Kiswahili kina sarufi yake. Ingawaje lugha

ulimwenguni zina ubia, baadhi ya ubia huu haukubaliki katika kaida fulani. Katika Kiswahili, kaida hii inapatikana katika urejeleaji. Katika matini ya Kiswahili hufikia wakati kwamba kirejelea hakitoshelezi maana na huleta utata. Kawaida kirejelea hutumika kuondoa urudufishaji lakini nyakati zingine inabidi urudufishaji utokee hususan KN ili kuondoa utata:

> 118. ...Muda si mrefu Mamantilie alisikia sauti za watoto. Alitazama upande wa pili wa mtaa, akawaona wanawe, Zita na Peter na mtoto wa jirani, Sara, wakikimbizana na kupiga vidali. Lakini mchezo huu ulikatika mara tu Zita alipomuona (*mama yake*) pale nje.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 6)

Katika matini hii KN "mama yake" kinapodondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na –*mwo-* katika KT, alipo*mwo*na, basi kuna utata mkubwa. Haitajulikana kirejelea hicho kinarejelea nani, Peter au Sara au mtu mwingine nje ya matini hii. Ili kuondoa utata huu, KN lazima kirudufishwe kwa kuleta mshikamano na maana inayokusudiwa.

> 119. ...Niligeuka kwa nia ya kuanza safari ya kurudi lakini mjarabu wa kufanyo hivyo tu nilisikia radi kubwa iliyofuatiwa na umweso uliojaza kila sehemu mwanga mkali. Nilitoka Njiani na kusimama kando. Ile (*radi*) ilirudia tena na tena.
> (*Musaleo!* u.k. 62)

Neno "***radi***" hapa limerudiwa, lakini kuna virejeleo vyake viwili; *Ile* (kirejeleo kionyeshi) na ***-i-*** katika "*i*lirudia" kama kirejelea nafsi. Kwa sababu ya kikwazo cha kuleta mshikamano katika matini lazima neno "*gari*" lirudufiwe.

> 120. ...Alikuwa yule kijana...Kitungule aliyakodoa macho yake. Aliwatambua wawili. Sasa alielewa kwa nini mjomba wake alikazana waje huku kwa mara ya kwanza. Kingunge alitoa kitu fulani na kukitia kwenye kiganja cha mkono wake mdogo. Alishukuru na kukimbilia upande wa chini. Kitungule na Kingunge walishika njia kuelekea alipokuwa ameegesha gari *yake*.
> (*Musaleo!* u.k.80)

Katika matini hii, utata unakuja na kirejelea kimilikishi "*yake*". Je, kimilikishi hiki kinarejelea nani katika matini? Kitungule au Kingunge? Hivyo kirejelea hiki kina utata sana. Isitoshe, kutoka mwanzo wa sehemu hii, u.k 79 hakuna mahali pametajwa nani akaja kwa hilo gari. Hivyo kunahitajika KN iwekwe katikati ya *alipokuwa* na *ameegesha*, ili kuondoa utata huo na iwe hivi:

> 121. ... Kitungule na Kingunge walishika njia kuelekea
> alipokuwa *(Kitungule / Kingunge)* ameegesha gari yake.
> (*Musaleo!* u.k 80)

Tumetumia majina yote mawili katika matini 121, *Kitungule* na *Kingunge* kwa sababu hatujui ni nani kati yao alikuwa na hilo gari. Majina haya kwa muktadha wa matini hii, haijulikani gari ni ya nani kati ya Kitungule na Kingunge. Majina tuliyoyaweka katika mabano ni ufafanuzi wetu. Katika matini halisi hayapo na kutokuwepo kwa jina mojawapo, kumeleta utata katika matini hii (Tazama Kiambatisho II). Kwa hivyo hapa ni lazima palihitajika jina moja la mmiliki wa gari hiyo. Hiki ni kikwazo, pengine Wamitila hakukiona.

Mohammed (2001: 115) anaeleza kikwazo hiki cha urudufishaji kwa kusema;

> Ingawaje unominishaji wakati mwingine ni muhimu ili kukwepa urudufishaji wa maneno mahususi, kuna vikwazo vikiuzingira. Mojawapo ya vikwazo hivi ni kuwa panaweza kuhitajika kurudufisha kirai nomino (KN) kuondoa utata wa maana, hasa ikiwa pana hatua kubwa kati ya kirejelea na kirejelewa, KN. (Tafsiri Yetu)

Jambo hili limejitokeza katika matini zilizorejelewa. Palitokea hatua kubwa kati ya kirejelea na kirejelewa , na ilibidi KN kutajwa:

> 122. Walipokuwa wakipita karibu na kigari cha mwuza ice cream,
> Kingunge alivutwa shati. Alikuwa yule kijana..."Walikuwa wale
> pamoja na polisi!" Kitungule aliyakodoa macho yake.
> Aliwatambua wawili. Sasa alielewa kwa nini mjomba wake

> alikazania waje huku kwa mara ya kwanza. Kingunge alitoa
> kitu fulani na kukitia kwenye kiganja cha mkono wake mdogo.
> (*Musaleo!* u.k 80)

Katika matini hii, nomino kiima ni Kitungule na Kingunge. Majina haya yametokea mbali katika matini ya *Musaleo!*. Hapa uwakilishi wa urejeleaji umeshindwa na imebidi jina Kingunge litumike. Pengine angetumia kiambishi wakilishi *A-* kurejelea nafsi ngeli, kungekuwa na utata. Isingejulikana kirejelea hicho kinamrejelea nani kati ya hawa; kijana, Kitungule au Kingunge. Ili kuondoa utata huu, ilibidi nomino kirejelewa, Kingunge, iwekwe kwenye matini katika nafasi ile.

### 3.4 Hitimisho

Tumeona ya kwamba kuna urejeleaji aina tatu; i) uerjeleaji nafsi ii) urejeleaji onyeshi iii) urejeleaji linganishi. Aina zote hizi zinaleta mshikamano katika matini. Mshikamano huo hujitokeza katika usemi na hata katika sentensi moja katika Kiswahili. Inabidi msomaji asome mfululizo wa sentensi kadha ndio usemi ushikamane na kuwa na maana. Na katika sentensi moja ya Kiswahili viwakilishi nafsi virejelea huchangia mshikamano katika sentensi. Bila hivyo kutumika, sentensi inakuwa na urudufishaji uliokithiri na kutokubalika kisarufi. Kwa hivyo vinachangia mshikamano wa kisarufi hata katika sentensi moja, na ni vya lazima kwa mujibu wa muundo wa lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu umegundua kwamba urejeleaji nafsi ndio unaotamalaki matini kwa kujitokeza zaidi na hutokea zaidi kama mrejeosabiki (Tazama Jedwali 3.5). Umetokea takribani katika kila sentensi kwenye matini zilizorejelewa. Huu ulijitokeza kuwa ndiyo nguzo ya kuleta usahihi wa sentensi za Kiswahili. Aidha unachangia mshikamano wa matini.

Urejeleaji huu umejikita katika uambishaji na hutokea kuwa wa nyuma na wa mbele. Urejeleaji nje katika matini zilizotafitiwa ni mchache sana kwani katika matini za fasihi, waandishi huelezea kisa na hutaja kila mhusika, jambo au tukio. Urejeleaji onyeshi kwa utokezi katika matini unafuata ule wa nafsi kwa idadi. Nao vile vile ni wa nyuma au wa mbele.

Urejeleaji linganishi upo wa aina mbili; i) ule wa jumla na ii) ule mahususi. Urejeleaji linganishi jumla, hulinganisha vitu viwili kwa kutotumia sifa fulani na ule mahususi hutumia sifa fulani ikipimwa kati ya vitu hivyo viwili. Sifa inaweza kuwa ile ya idadi au kiwango na ile ya umadhubuti au ubora.

Ulinganishi mahususi pia huwa na urejeleaji; lazima pawe na kiwango wastani kubalifu cha kurejelewa ambapo kimoja huweza kuwa bora zaidi, sawa au duni kwa ubora au idadi (*Kama hapo juu*: 81). Kitu hakiwezi kuwa 'kama' lazima kiwe 'kama kitu fulani au kingine'. Kwa hivyo ulinganishi ni aina ya urejeleaji kama zile nyingine. Kirejelewa cha urejeleaji huweza kuwa ndani au nje ya matini. Halliday na Hassan (1976:78) wanasema kuwa urejeleaji linganishi unaweza kuwa wa nyuma au mbele (ndani ya matini) au nje ya matini. Kisha wanadai kuwa kati ya faridi zote za urejeleaji, ulinganishi hurejelea zaidi nyuma kuliko nje (*Kama hapo juu*: 83).

Hatch (1992: 224) anasema kwamba vilinganishi pia vinaweza kuwa kiunganishi kwa kirejelewa. Pia anashadidia hoja ya Halliday na Hassan anaposema kuwa mara nyingi vilinganishi hutumika kwa urejeleaji nyuma. Si mara nyingi kutumika kurejelea mbele,

lakini wakati mwingine hutumika. Hizi ndizo tofauti au vikwazo vya lugha kwamba hali fulani hulazimisha mchakato fulani kutumika.

Aidha urejeleaji wote katika Kiswahili hudhihirika waziwazi kwamba unaleta mshikamano wa kisarufi katika kiwango cha usemi. Hata hivyo haukukosa vikwazo hususan urejeleaji nafsi au milikishi ambapo inabidi wakati mwingine nomino au kiima kirudufishwe ili matini iwe na mshikamano na kuondoa utata.

Jambo tuliloligundua ni kwamba katika Kiswahili uambishaji wote unachangia mshikamano katika matini. Unachangia katika sentensi na hata matini yote. Kiswahili ni lugha ya uambishaji, na popote kiambishi kinapotumika kuwakilisha nomino, huo ni urejeleaji na unaleta mshikamano katika sentensi hiyo moja. Bila uwakilishi, sentensi ya Kiswahili haikubaliki kisarufi kwani inaharibu sarufi na mshikamano.

# SURA YA NNE

# UBADILISHAJI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia ubadilishaji katika matini za Kiswahili zilizochaguliwa. Imedhihirisha ubadilishaji ulivyotokea katika matini teule. Majedwali yametumika kuonyesha utokeaji wa ubadilishaji katika matini hizo na vibadala mbalimbali vilivyotumika. Aidha sura hii imeonyesha jinsi ubadilishaji unavyotokea katika daraja mbalimbali za sentensi katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* Imeangazia ubadilishaji wa nomino na kirai nomino, kitenzi na kirai kitenzi, kishazi na sentensi. Vile vile imeonyesha ubadilishaji wa msururu wa sentensi. Utokeaji wa ubadilishaji katika daraja mbalimbali za sentensi katika matini teule umeonyeshwa katika majedwali 4.1, 4.2 na 4.3, na mifano mbalimbali ya ubadilishaji imedondolewa kutoka matini hizo. Ubadilishaji umedhihirishwa kuwa ni muhimu katika kujenga mshikamano katika matini. Huondoa urudufidhaji katika matini.

## 4.1 Ubadilishaji Unavyotokeza

Ubadilishaji ni kijenzi kimojawapo kinacholeta mshikamano katika matini kama tulivyotangulia kueleza. Ni mchakato katika matini ambapo hutokea ubadilishaji wa kipashio kimoja na kuingiza kingine. Mchakato huu husaidia kuhifadhi sarufi ya lugha na kuleta mshikamano katika matini. Mshikano ni muhimu kwani huleta uelewekaji wa matini na wakati huo huo kuhifadhi usarufi wa matini unaokubalika kwa mujibu wa lugha tumizi. Ubadilishaji uliopatikana katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na

*Musaleo!* ni wa Nomino, Kirai Nomino, Kirai Kitenzi, Kirai Elezi (Chagizo), kishazi na sentensi.

| DARAJA ZA SENTENSI | *Watoto wa Maman'tilie* (Idadi) | *Musaleo!* (Idadi) | JUMLA YA IDADI |
|---|---|---|---|
| NOMINO | 1 (3.85%) | 3 (11.54%) | 4 (15.39%) |
| KIRAI NOMINO | 0 | 2 (7.69%) | 2 (7.69%) |
| KIRAI KITENZI | 1 (3.85%) | 2 (7.69%) | 3 (11.54%) |
| KIRAI ELEZI | 1 (3.85%) | 1 (3.85%) | 2 (7.69%) |
| SENTENSI/KISHAZI | 7 (26.92%) | 8 (30.75) | 15 (57.69%) |
| **JUMLA** | **10 (38.46%)** | **16 (61.54%)** | **26 (100%)** |

4.1 UBADILISHAJI KATIKA DARAJA MBALI MBALIMBALI ZA SENTENSI NA UTOKEAJI WAKE KATIKA MATINI

Kutokana na jedwali hili 4.1, tunaona kwa jumla ubadilishaji umetokea mara ishirini na sita (26) katika matini zote mbili za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*. Ubadilishaji katika daraja ya nomino umetokea mara nne (4) kwa jumla; katika *Musaleo!* kuna mara tatu (3) na katika *Watoto wa Maman'tilie* mara moja (1). Ubadilishaji katika daraja ya kirai, kwa jumla umetokea mara kumi (10); ubadilishaji wa kirai nomino haukutokea kabisa katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie,* ubadilishaji wa kirai kitenzi umetokea mara moja (1) na wa kirai elezi umetokea mara moja (1) vile vile. Katika matini ya *Musaleo!* kirai nomino mara mbili (2), kirai kitenzi mara mbili (2) kirai elezi mara moja (1). Ubadilishaji katika daraja ya sentensi katika matini zote mbili, umetokea mara kumi na tano (15): katika *Maman'tilie* mara saba (7) na katika *Musaleo!* mara nane.

Kwa hivyo katika Kiswahili, kwa mujibu wa matini mbili zilizochunguzwa, ubadilishaji hutokea zaidi katika daraja ya kishazi/sentensi. Aidha ubadilishaji wa kirai ni wa idadi ndogo sana pamoja na ule wa nomino.

| *Watoto wa Maman'tilie* | *Musaleo!* | JUMLA |
|---|---|---|
| 10 | 16 | **26** |
| 38.46% | 61.54% | **100%** |

4.2 JUMLA YAUBADILISHAJI KWA ASILIMIA %

Katika Jedwali 4.2 tunaona matini ya *Musaleo!* imetumia vibadala mara kumi na sita (16) na matini ya *Watoto wa Maman'tilie* imetumia vibadala mara kumi (10). Vile vile tunaona kuwa ubadilishaji kwa jumla umetokea zaidi katika matini ya *Musaleo*, asilimia sitini (61.54 %) , na katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* umetokea kwa asilimia arobaini (38.46 %).

### 4.1.1 Ubadilishaji wa Nomino na Kirai Nomino

Katika ubadilishaji wa Nomino na Kirai Nomino tulichunguza ule wa Nomino pekee (N) na ule wa Kirai Nomino (KN), yaani nomino na vifuasi vyake. Ubadilishaji wa Nomino ulitokea mara moja (1) tu katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* na mara tatu (3) katika matini ya *Musaleo!* (Jedwali 3.1)

#### 4.1.1.1 Ubadilishaji wa Nomino

Nomino ni katagoria ya kileksia inayosimamia neno au kitu. Nomino husimamiwa na kibadala badala ya nimino hiyo hiyo kurudiwa tena katika sentensi za mbele katika matini ikiwa imetangulia kutajwa. Vibadala hivi huondoa urudufishaji ili kuleta

mshikamano na maana katika sentensi. Ubadilishaji wa nomino ulitokea katika matini teule; matini ya *Watoto wa Maman'tilie* mara moja (1) na *Musaleo!* mara tatu (3). Tuangalie jinsi ubadilishaji huu ulivyotokea:

> 123. "...Wote waliomo wanagoma na kulalamika baada ya kulisikia jina hilo!" alisema hatimaye.
> "Kumbe wanamjua hata huku?"
> "Nani asiyemjua Kinyonga?"
> "Kinyonga?"
> "Huyo umwitaye Mzee ana uzee gani wa kuitwa *hivyo*?"
> (*Musaleo!* u.k 47)

Hapa kibadala *hivyo* kimesimama mahali pa nomino Kinyonga, jina la dhihaka analopewa mhusika Mzee. Kibadala hiki kimetumika kuchukuwa pahali pa nomino Kinyonga. Nomino Kinyonga hapa imetajwa mara mbili katika mazungumzo haya. Kwa hivyo katika sentensi ya mwisho, hakuna haja ya kurudia nomino hiyo. Ndiyo mwandishi akatumia kibadala *hivyo*. Msomaji anaposoma matini hii na kufikia kibadala hicho, moja kwa moja atajuwa kinasimamia jina *Kinyonga*. Kurejelea kipashio kilichotangulia katika matini na kukamilisha maana, ndiko kujenga mshikamano wa matini. Mshikamano unaotekea hapa ni ule wa kisarufi.

> 124. "...Alizaliwa kisha baadaye akakimbia nyumbani. Aliporudi alijiita *Musee* watu hawakulisikia jina lake vizuri kwa kuwa ana ulimi mzito wakadhani anajiita *Mzee*. Walimwita *hivyo* kuanzia siku hiyo."
> (*Musaleo!* u.k 47)

> 125. Tulimfikia. Wakati wote huo aliendeea kuongea kwa sauti ya juu. Niliweza kuyasikia vizuri maneno aliyoyasema. "Nilisema! Nilisema! Nilisema! Ung'amuzi haufi! Giza halitandi milele!" Nilimsogelea Mamanchi na kumwuliza "Je alikufa lini *huyu*?" "Nilisema kwa sauti ya chini lakini aliyasikia. "...Mimi sijafa, bado naishi milele! Mimi *Veritas* sio mtu wa kufa. Nifeje? Aliyekufa ni wewe!"
> (*Musaleo!* u.k 53)

Katika matini hizi 124 na 125 kuna ubadilishaji wa nomino vile vile. Vibadala *hivyo* na *huyu* vinasimamia nomino *Musee/Mzee* na *Veritas* mtawalia. Kibadala *hivyo*, kinasimamia jina *Musee/Mzee* lililotangulia kutajwa katika matini. Kwa hivyo msomaji atalirejelea nyuma kukamilisha maana inayojitokeza kuwa *hivyo* ni jina *Musee/Mzee*. Kibadala *huyu,* kimuktadha ni kibadala cha *Veritas*. Badala ya nomino kutangulia kibadala, hapa kibadala kimetangulia na nomino kuja baadaye. Msomaji inambidi aende mbele katika matini kupata nomino inayosimamiwa na kibadala hivyo. Jambo hili la kurejelea kwingineko katika matini kupata kipashio kinachosimamiwa na kipashio kingine ndio mshikamano. Hata hivyo kuna utata ya kwamba kibadala hiki kinaweza kufasiliwa kama kirejelea. Lakini kwa kuzingatia dhana ya ubadilishaji na masharti yake, *huyu* imejitokeza kama kibadala katika matini ya 125.

> 126. *Ratiba* ya baba yao, mzee Lomolomo, ilikuwa *ileile*. Kama ibada, asubuhi anatafuta kiporo, anakula. Saa nne au saa tano, anaondoka kwenda kutia mtindi. Saa tatu usiku hurudi nyumbani akiyumba, wimbo mdomoni na harufu ya pombe mwili mzima.
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 48)

Aidha katika matini hii, kuna ubadilishaji wa nomino. Kibadala *ileile* kinasimamia nomino *'Ratiba'* ambayo ni taratibu fulani zinazofanywa na Mzee Lomolomo siku nenda siku rudi. Katika muundo wa matini hii, nomino *Ratiba* haiwezi ikarudiwa tena katika nafasi ya *ileile* na inaporudiwa hupotosha mshikamano wa kisarufi. Kwa hivyo hapa kuna lazima ya kuweka kibadala ili kuwe na mshikamano na sarufi inayokubalika katika Kiswahili. Hivyo kibadala *ileile* kimesimama mahali pa msururu wa sentensi tatu zinazoeleza ratiba ya Mzee Lomolomo, ambazo zinazotokea mbele ya kibadala hiki katika matini hii. Kwa hivyo, kufasili maana lazima kurejelee nomino *Ratiba* iliyotangulia kutajwa kisha tuende mbele kupata ufafanuzi wa *Ratiba* hiyo. Vile vile pana

utata katika kufasiri kibadala *ileile* kwa sababu kinaweza kuwa kionyeshi kirejelea cha '*Ratiba*' kutegemea hali ya ufasiri.

**4.1.1.2 Ubadilishaji wa Kirai Nomino**

Kirai nomino ni sehemu mojawapo ya sentensi. Quirk na Greenbaum (2002: 59) wanaeleza kuwa kirai nomino hufanya kazi ya kiima, yambwa, kijalizo cha sentensi, na kama kisifa katika kirai husishi. Mara nyingi katika sentensi KN huwa kiima, na pia huweza kuwa yambwa. Katika matini ya *Watoto wa Maman'tile* ubadilishaji wa KN haukutokea kabisa na katika *Musaleo!* umetokea mara mbili tu kama tulivyoonyeshwa katika Jedwali 3.2. Tuchunguze mifano ifuatayo tuone jinsi kilivyowakilishwa na vibadala katika matini:

> 127. Niliona jabali kubwa lililoonekana na macheo ya jua. Juu ya jabali hilo palikuwa na kiumbe aliyejitandaza kama mjusi kafiri. Alikuwa akicheka kwa sauti ya juu... Tulimfikia. Wakati wote huu aliendelea kuongea kwa sauti ya juu... Nilimsogelea Mamanchi na kumwuliza, "Je, alikufa lini *huyu*? Nilisema kwa sauti ya chini lakini alisikia.
> (*Musaleo!* u.k 52-53)

Katika matini hii, kibadala *huyu* kinasimama mahali pa kiumbe aliyejitandaza kama mjusi kafiri ambacho ni KN kilichojengwa na Nomino + Kishazi rejeshi. "kiumbe" ndiyo nomino na kishazi rejeshi ni "aliyejitandaza kama mjusi kafiri". Kwa hivyo *huyu* imesimama badala ya KN. Iwapo KN kingerudiwa pahali pa kibadala *huyu*, mshikamano kwenye matini ungepotoka. Matumizi ya kibadala katika sehemu hii ya matini, yameafiki na kuleta mshikamano unaostahili. Kwa hiyo ubadilishaji uliotokea hapa ni wa KN.

> 128. Mzee, wanasema *huu*$_1$ ni upepo mwingine! Bado sijajua na sijui kama hata wataalam wa hewa wanautambua *huu*$_2$...
> (*Musaleo!* u.k 66)

Vile vile hapa kibadala *huu* kimesimama mahali pa 'upepo mwingine'. Kipashio hiki ni KN kilichojengwa na Nomino (upepo) + Kivumishi (mwingine). *Huu*$_1$ katika sentensi ya mwanzo kimetumika kama kionyeshi na katika sentensi ya pili *huu*$_2$ ni kibadala kwa sababu kimesimama mahali pa *'upepo mwingine'* kutoka sentensi ya kwanza. Kukifasiri kwake inabidi turudi nyuma ya matini kupata kipashio kinachosimamiwa na kibadala hiki. Ubadilishaji wa KN katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* umetokea kwa uchache mno (Jedwali 4.1).

**4.1.2 Ubadilishaji wa Kirai Kitenzi**

Ubadilishaji unaoangaziwa katika sehemu hii ni ule wa Kirai Kitenzi yaani jinsi KT kilivyobadilishwa katika matini. KT kimechukuliwa kama kitenzi na vifuasi vyake. Hakuna ubadilishaji T uliotokea katika matini zote mbili teule ila ule wa KT. Ubadilishaji wa KT umetokea mara moja tu (1) katika *Watoto wa Maman'tilie* na mara mbili tu (2) katika *Musaleo!* Katika matini teule ubadilishaji wa aina hii ulitokea kama ifuatavyo:

> 129. ...Wakati wote nilikuwa nimetulia hadi nilipochochewa na maelezo yake kumwuliza jina la hadithi yake.
> " Inajiita Mzee!"
> "Inajiita?"
> "Ehh, inajiita hii!"
> "Yenyewe tuseme?" "*Hivyo* hasa!"
> (*Musaleo!* u.k10-11)

Katika matini hii kibadala *hivyo* kinasimamia 'Inajiita Mzee' ambacho ni kirai kitenzi kilicho na uambajengo wa Kitenzi + Nomino. KT kimedondolewa na badala yake kibadala '*Hivyo*' kimetumika. Kibadala hiki kimetumika kuondoa urudufishaji wa KT hicho. Inapofanyika hivi, mshikamano wa kisarufi unakamilika. Iwapo kibadala hakingetumika, KT 'Inajiita Mzee' kingetumika na kuleta urudufishaji. Kibadala kimeondoa urudufishaji huo, na kukifasiri inabidi msomaji arudi nyuma ya matini kupata

kipashio kinachosimamiwa na kibadala hiki ili kukamilisha maana. Hali hii ndiyo imeleta mshikamano katika matini hii.

> 130. ...Ilibidi ile nyama ishughulikiwe mapema, la *sivyo* ingeharibika kabisa.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 63)

Matini 130 inaonekana kama sentensi moja katika umbo la nje lakini katika umbo la ndani ni sentensi mbili zilizounganishwa na kiunganishi ghaibu (au kilichodondoshwa). Neno *sivyo* ni ufupisho wa maneno *si hivyo*. Kwa hivyo hiki ni kibadala kanushi. Ni kibadala cha 'ishughulikiwe mapema' na ni kirai kitenzi (KT) chenye vifuasi kitenzi + kielezi. Ubadilishaji uliotokea hapa ni wa KT 'ishughulikiwe mapema' na pahala pake katika kishazi cha pili pamechukuliwa na kibadala '*sivyo*'. Hii imeondoa urudufishaji unaoharibu mshikamano wa kisarufi katika matini. Kurudia KT hiki tena katika matini kungeharibu mshikamano wa matini. Hivyo ilibidi mwandishi atumie kibadala sivyo kusimamia KT hicho. Hii huongozwa na mchakato na muundo wa Kiswahili na vinginevyo ni kuharibu sarufi na mshikamano wa matini.

### 4.1.3 Ubadilishaji wa Kirai Elezi /Chagizo

Maelezo yametueleza kuwa katika kirai kitenzi, kuna chagizo ndani mwake. Katika ubadilishaji tuligundua kuwa chagizo kinaweza kusimamiwa na kibadala na bado kitenzi kikabaki kama kilivyo katika sentensi au matini. Kwa hivyo ubadilishaji wa namna hii ni ubadilishaji wa chagizo, na tumeuchunguza katika ubadilishaji wa chagizo ingawa ni sehemu ya KT.

Kirai elezi ni ile sehemu katika sentensi inayoelezea juu ya kitenzi kilivyofanyika. KE hiki huwa na vifuasi vyake. KE katika matini huweza kusimamiwa na kibadala kuondoa urudufishaji unaoharibu mshikamano wa matini hiyo. Katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* ubadilishaji wa chagizo ulijitokeza mara moja tu (1) katika kila matini na kwa jumla umetokea mara mbili (2) pekee. Hivi ndivyo ulivyojitokeza:

> 131. Paukwa...Pakawa. Njaa kubwa ndiyo iliyonihamisha kwetu. Sijui ilivyotokea. Usiniulize, nina utesi mkubwa wa jana. Mama alikufa wakati *huo*.
>
> (*Musaleo!* u.k 2)

Hapo kibadala *huo* kinasimamia 'wakati wa njaa kubwa'. Hiki ni KE au chagizo katika sentensi hiyo iliyoandikwa kizalishi na kisanii lakini kawaida ingekuwa "Mama alikufa wakati wa njaa kubwa huko kwetu". Kibadala kimetumika ili kukwepa urudufishaji katika matini. Urudufishaji, mara nyingi huharibu sarufi na mshikamano. Iwapo chagizo hicho kingetumika tena hapo mahala pa kibadala *huo* basi urudufishaji ungeharibu mshikamano wa kisarufi katika matini na masimulizi haya yangekuwa si sahihi kisarufi.

> 132. ...Kurwa alitabasamu kwa huzuni, huku machozi mengi ya moto yakiyasafisha mashavu yake. Alikuwa hajala tangu asubuhi. Peter naye hakuweza kujizuia, alilia kwa sauti ya chini chini, mikono yake imemkumbatia Kurwa. "Oh! Kurwa!" Peter aliendelea kulia na Kurwa alisema, "Oh! Peter nini sasa? Nyamaza, wewe ni mwanaume... Lazima unisaidie badala ya kulia..." Ghafla, Peter alinyamaza...Eee! Kweli! Yeye alikuwa mwanamume. Na, vipi alilia *vile*, kirahisi *vile*, kama mtoto mdogo?..."
>
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 51-52)

Ubadilishaji uliotokea katika matini hii ni ule wa Kirai Elezi (KE). KE hiki ni kirai husishi kinachofanya kazi ya kielezi cha kitenzi *lia*. Kirai husishi ni *kwa sauti ya chini chini* na mahala pake pamechukuliwa na kibadala *vile* kilichotokea mara mbili katika matini ili kukwepa urudufishaji ambao ungeharibu mshikamano. Matumizi ya kibadala

*vile* kimeleta mshikamano unostahili katika matini hii. Iwapo hakingekuwepo, mshikamano wa matini ungekuwa na mushikeli unaoletwa na urudufishaji wa KE katika pahali pa *vile*. Kwa hiyo matini hii ina mshikamano kwa sababu ya kibadala kutumika badala ya KE 'kwa sauti ya chini chini'.

### 4.1.4 Ubadilishaji wa Kishazi na Sentensi

Baada ya kutalii vijelezi vya kishazi na vya sentensi na uchanganuzi wangu katika tasnifu hii, tumechukulia kuwa kishazi ni sentensi sahili. Kwa hivyo sentensi sahili ikiwekewa kibadala imechukuliwa kuwa ni ubadilishaji wa kishazi. Pale ambapo pametokea ubadilishaji wa sentensi changamano au msururu wa sentensi imechukuliwa ni ubadilishaji wa sentensi vile vile. Kwa hivyo ukirejelea Jedwali 4.1 tuna sentensi/kishazi na ubadilishaji umetokea mara saba (7) katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* na mara nane katika *Musaleo!* Katika matini teule ubadilishaji wa vishazi na sentensi ulitokea:

> 133. Kama mtumwa anayeelekezwa kwenye hatua zake zote, alitii. Alielekea kwenye chumba chake cha kuandikia. Mashine yake ya kuandikia ilikuwa pale pale tangu alipoandika riwaya ya mwisho. Yenyewe imetafsiriwa katika lugha sita. Wachapishaji wake walienda kumwambia, "Mzee, samahani lakini ndio *hivyo* bwana; watu nchi hii hawasomi siku hizi! Vitabu hatuuzi tena!..."
> (*Musaleo!* u.k 2)

Katika matini hii ubadilishaji wa sentensi mbili umetokea. Kibadala kilichotumika ni *hivyo* kusimama mahali pa 'watu nchi hii hawasomi siku hizi! Vitabu hatuuzi tena!' Kibadala hapa kimetumika kisanii kwa kubadili mbele, na kuleta mshikamano wa kisarufi. Sentensi hizo mbili zingefaa ziwe zimetangulia kibadala katika matini ili zibadilishwe na kibadala. Kwa vile zimewekwa mbele, haya ni matumizi ya lugha kisanii na sarufi yake inakubalika katika Kiswahili. La muhimu ni kuwa mshikamano umetokea.

> 134. Ilitoka kama sadfa. Tulipokuwa tukitoka nje ya baa tulikumbana na mjomba wake, yule mwandishi. Alikuwa jamaa aliyetimkwa na nywele na aliyevalia suruali ya kaki na fulana ilioishia (sic) shingoni. Viatu vilikuwa vya makubadhi. Hii ilikuwa mara ya kwanza kukutana naye uso kwa macho na kusema kweli sikumtarajia awe *hivi*...
>
> (*Musaleo!* u.k 10)

Hapa kibadala *hivi* kimetumika kuondoa urudufishaji. Kinasimamia maelezo ya hali ya mjomba wa rafiki wa msimulizi; ile 'hali ya nywele kutimka na mavazi duni ya suruali ya kaki na fulana, na viatu vya makubadhi'. Hivyo kibadala *hivi* kimesimamia sentensi tatu zinazofululiza kuelezea hali ya mjomba wa rafikiye msimulizi. Kutumika kwake kumeleta mshikamano wa kisarufi kwa sababu mwandishi angerudia maelezo hayo ya hali ya mjomba wake msimulizi tena mahala pa *hivi*, matini ingekuwa na urudufishaji na kuharibu mshikamano wa kisarufi.

> 135. "Ndilo jina lake hilo hasa! Tena linasibu tu!"
> "Umejuwaje wewe?"
> "Nimejuaje?"
> "Ehh...!"
> "Ni ndugu yangu: tulizaliwa mapacha!"
> "Hata hilo *nalo* hatulijui!"
>
> (*Musaleo!* u.k 47)

Katika matini hii neno *nalo* ni kibadala cha 'Ni ndugu yangu; tulizaliwa mapacha!'. Badala ya kurudia sentensi hizi mbili tena katika maelezo fuatilizi, mwandishi alitumia kibadala *nalo* kuondoa urudufishaji, hivyo kupata mshikamano wa kisarufi. Kibadala hapa kimesimama pahali pa sentensi kwa mujibu wa muundo wa Kiswahili na itakuwa kuharibu mshikamano na sarufi iwapo sentensi 'Ni ndugu yangu; tulizaliwa mapacha!' ingerudiwa badala ya kibadala *hilo*.

> 136. ...*Kuna kisa kinachosimuliwa kuuhusu ulimwengu. Inasemwa zamani ulikuwa pande moja tu, bara moja lililotanda huku na*

> *huku kisha kukazuka tetemeko na kugawa mapande mengi... Hali iliendelea hivyo, yaani tetemeko, kizalizali, tetemeko, kizalizali mpaka hatimaye yakawa mapande matano. Manne makubwa lakini la tano dogo.*
> (*Musaleo!* u.k 67)

Katika matini hii, *hivyo* ni kibadala cha nyuma yaani kinasimama badala ya yale yaliyotangulia katika matini. Ubadilishaji nyuma ni kuwa kibadala hiki kinasimama mahali pa 'kukazuka tetemeko na kugawa mapande mengi'. Hivyo ubadilishaji wa kishazi umetokea. Na iwapo tutachukulia neno *hivyo* kuwasilisha yaliyo mbele ya neno hili, basi halitakuwa kibadala bali kirejelea cha 'tetemeko, kizalizali, tetemeko, kizalizali'. Hii ni kwa sababu ya muundo wa matini ilivyojengwa na kusababisha urejeleaji. Mfano huu (136) umetumika hapa kuonyesha ubadilishaji.

> 137. ...Ilikuwa lazima watu wajiandae kufikwa na lolote. Unajua Mzee ni kama mkuu wa familia. Kitu kama Baba au hata chifu. Tuliamini *hivyo*...
> (*Musaleo!* u.k 88)

*Hivyo* katika matini hii ni kibadala cha kishazi 'Unajua Mzee ni kama mkuu wa familia'. na kimeondoa urudufishaji na kuleta mshikamano wa kisarufi. Matumizi haya yamesaidia kutunza sarufi ya Kiswahili na kuleta huo mshikamano unaohitajika katika masimulizi ya hadithi au dhana yoyote ile. Mwandishi hawezi kutumia urudufishaji wakati kibadala kinafaa kusimamia dhana au wazo fulani katika matini. Kwa hivyo matini hii imebidi kutumia kibadala kwa kuleta mshikamano na habari inayokusudiwa kueleweka kwa wasomaji.

> 138. Tulishinda kupiga mijusi na bundi mawe kwa manati. "Inama uunawe uso wako!" alisema profesa. Nilifanya alivyosema bila kuuliza swali lolote. Naye alifanya *hivyo hivyo*. (*Musaleo!* u.k 94)

Kibadala *hivyo hivyo* kinasimama mahali pa kishazi 'Inama uunawe uso wako!' na kuondoa urudufishaji. Huu ni ubadilishaji wa kishazi na umeleta mshikamano katika matini. Matumizi ya kibadala *hivyo hivyo* yameleta mshikamano wa Kiswahili hapa na kuondoa urudufishaji unaosinya na kuharibu mshikamano wa matini.

> 139. ...Mwalimu Mkuu, mwalimu Chikoya aliwatangazia wanafunzi, "Wote ambao hamjalipa ada na hamna sare, hakuna shule! Nisizione sura zenu bila ada na sare. Waambieni wazazi wenu *hivyo*."
>
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 1)

Kibadala *hivyo* katika matini hii, ni kibadala cha sentensi mbili; 1) Wote ambao hamjalipa ada na hamna sare, hakuna shule! 2) Nisizione sura zenu bila ada na sare. Kibadala hiki kimetumika kuepuka urudufishaji ili kuleta mshikamano wa kisarufi katika matini hii. Iwapo mahali pa kibadala *hivyo*, mwandishi angerudia sentensi hizi mbili, sarufi na mshikamano wa matini ungeharibika. Aidha kimetumika kusisitiza maneno hayo ya Mwalimu Mkuu.

> 140. ...Alikuwa kapata wazo juu ya hoteli yao pale Msufini. Haikuwa na jina, bali genge tu, kama magenge mengine. Hapana, yeye Peter hakutaka *hivyo*. Alitaka atafute jina...
>
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 65)

Vile vile katika matini hii kibadala ni *hivyo*, na kinasimamia 'hoteli kutokuwa na jina, bali genge tu, kama magenge mengine'. Kwa hiyo ni kibadala cha sentensi. Kimeepusha urudufishaji na kuleta mshikamano wa kisarufi. Mahali pa *hivyo,* katika 140, tungerudia sentensi iliyodondoshwa, mshikamano haungetokea na kutokubalika tukizingatia sarufi ya Kiswahili.

> 141. ..."Sasa unasemaje Peter...? *Nikukonekti* kwenye *mesheni* zetu za unga na coca?" Peter aliuliza, "Kwani itakuwaje hasa?"
> "Aa! Rahisi tu. Sisi tutakwenda bandarini. Tutawakuta watu

> wetu... Tunakutana na wale Waitaliano melini. Tunameza
> vidonge."
> Vidonge! Peter aliruka akashangaa...
> "Mambo rahisi. Pale kwa bosi unakunywa dawa ya kuharisha,
> kwisha. Bosi, anakuhesabia majani kibao. We unadhani bila
> *hivyo*, vitu vyote hivi ningevipata wapi?"
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 78-79)

*hivyo* hapa imesimama kama kibadala cha 'ile taratibu yote ya kuuza madawa ya kulevya hadi kulipwa ujira wa utaratibu huo'. Kwa hiyo ni kibadala cha wazo lote la biashara ya mihadarati inayosimuliwa kwa kutumia sentensi kumi. Kibadala hiki kimeepusha urudufishaji na kuleta mshikamano wa matini. Haiwezikani kurudia sentensi zote kumi mahala pa kibadala *hivyo*, na inapofanyika, haikubaliki kwa mujibu wa mshikamano katika Kiswahili. Kwa hivyo ubadilishaji huu ni wa lazima.

> 142. ..., alisema, "Tena, nasikia we Peter umeanza wazimu wa
> kwenda jaa la Tabata! Si mjinga wewe!" Musa alimkazia
> mwenzake macho...
> Musa aliendelea kumtesa rafiki yake kwa namna ya msuto,
> "Siyo *hivyo* tu, na yule msichana Kurwa."...
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 79)

Kibadala *hivyo* kimesimamia "...we Peter umeanza wazimu wa kwenda jaa la Tabata". Hii imeondoa urudufishaji wa sentensi hiyo katika sentensi ya mwisho na kuleta mshikamano wa matini. *hivyo* kimekuwa kibadala cha sentensi tuliyoitaja hapo juu. Sentensi hii ingerudiwa ingepotosha mshikamano wa matini. Uradidi wa maneno hayo hayo au sentensi haufai katika lugha ndipo vibadala kutumika kudhibiti sarufi na mshikamano ili lugha ikubalike kisarufi.

> 143. ... Sasa Zita alizoa mchanga akijimwagia kichwani. Alifanya
> *hivyo* mara tatu...
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 81)

Katika matini hii, *hivyo* ni kibadala cha sentensi, 'Sasa Zita alizoa mchanga akajimwagia kichwani.' Matumizi yake yameondoa urudufishaji wa sentensi tuliyoitaja na kuleta mshikamano wa kisarufi katika matini. Sentensi hii ingerudiwa katika nafasi iliyo hicho kibadala haingekubalika kisarufi na mshikamano ungepotea.

> 144. ...Mamantilie kaegemea mti, midomo imekauka, kashika tama, moyo umefadhaika. Jirani na rafiki yake Mama Sara naye *hivyo hivyo*.
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 81)

*hivyo hivyo* ni kibadala cha sentensi, halikadhalika kusisitiza yale yanayoelezwa. Kibadala hiki kinasimamia sentensi, 'Mamantilie kaegemea mti, midomo imekauka, kashika tama, moyo umefadhaika.' Hapa ubadilishaji wa sentensi umetokea. Badala ya kuelezea hali ya Mama Sara pia kama ile ya Mamantilie, ametumia hicho kibadala *hivyo hivyo* kusimamia hiyo hali. Mwandishi angerudia sentensi hiyo tena, pangetokea urudufishaji na kuharibu mshikamano wa kisarufi katika matinin hii (144).

> 145. ... "Aisee! Sijui kama nitazoea," Peter alisema.
> "Nasikia tumbo langu limechafuka. Nataka kutapika."
> Musa alisema, "Aa utazoea tu..." Musa alisimama, akachukua ndimu toka kabatini. Alikata nusu, akasema, "Lamba, itasaidia kupoteza kichefuchefu na machafuko. Na zaidi ya hayo, *blaza* Peter, heri *hilo* kuliko noma ya jaa la jiji au vipi?
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 95)

*hilo* katika matini hii ni kibadala na kinasimamia hali ya Peter iliyosimuliwa kwa kutumia sentensi mbili; 1) Nasikia tumbo langu limechafuka. 2) Nataka kutapika.

Kibadala hiki kimeondoa urudufishaji iwapo sentensi hizo zingerudiwa katika mahala pa kibadala *hilo*. Kufanya hivyo kumechangia mshikamano wa matini.

| KIBADALA | IDADI | | JUMLA |
|---|---|---|---|
| | *Watoto wa Maman'tilie* | *Musaleo!* | |
| hivyo | 7 (26.92%) | 8 (30.72%) | 15 (57.69%) |
| huo | _ | 1 (3.85%) | 1 (3.85%) |
| hivi | _ | 1 (3.85%) | 1 (3.85%) |
| hicho | _ | 1 (3.85%) | 1 (3.85%0 |
| nalo | _ | 1 (3.85%) | 1 (3.85%) |
| huyu | _ | 2 (7.69%) | 1 (3.85%) |
| huu | _ | 1 (3.85%) | 1 (3.85%) |
| hivyo hivyo | _ | 1 (3.85%) | 1 (3.85%) |
| vile | 1 (3.85%) | - | 1 (3.85%) |
| ile ile | 1 (3.85%) | - | 1 (3.85%) |
| hilo | 1 (3.85%) | - | 1 (3.85%) |
| **Jumla** | **10 (38.46%)** | **16 (61.54%)** | **26 (100%)** |

## 4.3 MUHTASARI WA MATOKEO YA VIBADALA KATIKA MATINI ZA *Watoto wa Maman'tilie* NA *Musaleo!*

Tunapochunguza Jedwali 4.3 ni dhahiri kuwa kibadala kilichotumika zaidi katika matini zote mbili ni *hivyo,* na kimetumika mara kumi na tano (15); katika matini ya *Musaleo!* kimetumika mara nane (8) na katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* kimetumika mara saba (7). Vibadala *huo, hivi, hicho, nalo, huyu, huu, hivyo hivyo* katika *Musaleo!* vimetumika mara moja moja (1), na katika *Watoto wa Maman'tilie* havikutumika kabisa.

Katika matini ya *Musaleo!* vibadala *vile, ile ile* na *hilo* havikutumika kabisa, na katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie*, vimetumika mara moja moja (1).

## 4.2 Hitimisho

Ubadilishaji katika matini hizi za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* umetokea kwa kiwango kidogo (Tazama Jedwali 4.1) lakini ni muhimu sana katika kuleta mshikamano wa lugha. Ubadilishaji hutokea katika daraja ya nomino, kitenzi, kirai, kishazi na sentensi. Kuna wakati ni lazima ubadilishaji utumike katika matini ili kuleta mshikamano na kuna wakati ni hiari, yaani hata usipotumika matini bado ina mshikamano. Ubadilishaji huondoa urudufishaji katika Kiswahili, na kuleta mshikamano unaofaa. Hata hivyo tahadhari ichukuliwe katika kubainisha vionyeshi vibadala na vionyeshi virejelea katika Kiswahili. Mukhtadha na nafasi katika sentensi ambamo vibadala vinatokea ni muhimu kutofautisha faridi hizi.

Jambo lingine linalodhihirika ni kuwa vibadala huenda kulingana na ngeli ya Nomino, kwa mfano; katika *Watoto wa Maman'tilie* kibadala *ile ile* (u.k 48) kinatawaliwa na ngeli ya nomino Ratiba, kibadala *hilo* (u.k 95) kinatawaliwa na ngeli ya nomino Jambo.
Katika *Musaleo* kibadala *nalo* (u.k 47) kinatawaliwa na ngeli ya nomino Jambo, kibadala *huyu* (u.k 53) kinatawaliwa na ngeli ya nomino mtu Veritas, kibadala *huo* (u.k 2) kinatawaliwa na ngeli ya nomino, wakati.

Vibadala *hivyo* na *hivyo hivyo* havitawaliwi na ngeli bali vinasimamia hali au tendo. Mfano kibadala hivyo katika *Musaleo* (u.k 11) kinasimamia 'anajiita Mzee'. Katika

*Watoto wa Maman'tilie* kibadala *hivyo* (u.k 65) kinasimamia 'hali ya hoteli ya Mamantilie kutokuwa na jina'.

Kulingana na Jedwali 4.1 ubadilishaji umetumika zaidi katika daraja ya sentensi katika matini zote mbili, *Watoto wa Maman'tilie* 28% na *Musaleo* 32% ukilinganisha na daraja nyingine. Hizi mbili idadi asilimia zimechukuwa 60% . Pia tumeona kuwa matini ya *Musaleo!* kwa jumla imetumia ubadilishaji zaidi (60%) kuliko matini ya *Watoto wa Maman'tilie* (40%)

Kwa hivyo, ubadilishaji ni muhimu katika matini za Kiswahili kwa kuondoa urudufishaji na kudhibiti mshikamano wa matini. Hata hivyo katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*, umetumika kwa uchache ukilinganishwa na vijenzi vingine vya mshikamano (Jedwali 1.1). Ubadilishaji uliojitokeza zaidi katika daraja mbalimbali ni ule wa sentensi/vishazi (60%) na uliotumika kwa kiwango cha chini zaidi ni ubadilishaji wa Kirai Nomino (4%) ambapo katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* haukutokea kabisa (0) na katika *Musaleo!* umetokea mara moja (1) tu.

# SURA YA TANO

# UDONDOSHAJI

## 5.0 Utangulizi

Sura hii imechanganua udondoshaji kama unavyojitokeza katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo*! Udondoshaji hapa uliochanganuliwa ni wa vipashio katika daraja mbalimbali za sentensi. Kuna udondoshaji wa silabi, nomino kama kiima na kama yambwa, kirai nomino, kitenzi na kirai kitenzi na udondoshaji wa kishazi na sentensi. Katika tasnifu hii, udondoshaji wa vipashio katika daraja za sentensi tumeuchukulia kama aina mbalimbali za udondoshaji. Pia udondoshaji katika katagoria za kileksia kama vile kielezi, kimilikishi, kiulizi, kiashiria/kionyeshi na kiunganishi umedhihirishwa.

Aidha vikwazo vya udondoshaji katika mshikamano wa matini umefafanuliwa hususan vilipojitokeza katika matini teule za Kiswahili. Kwa muhtasari, udondoshaji katika matini zote mbili umejitokeza kama inavyoonyeshwa katika majedwali haya:

| MATINI | UTOKEAJI KWA JUMLA | ASILI MIA |
|---|---|---|
| *Watoto waMaman'tilie* | 126 | **61.17%** |
| *Musaleo!* | 80 | **38.83%** |

5.1 UDONDOSHAJI KATIKA MATINI

| AINA | MATINI | | UTOKEZI KWA JUMLA |
|---|---|---|---|
| | *Watoto wa Maman'tilie* | *Musaleo!* | |
| Silabi | 53 | 11 | **64** |
| NominoK | 16 | 17 | **33** |
| NominoY | 11 | 14 | **25** |
| Kitenzi | 16 | 23 | **39** |
| Kishazi/Sentensi | 25 | 12 | **37** |
| Kiashiria/Kionyeshi | 2 | 1 | **2** |
| Kimilikishi | 1 | 0 | **1** |
| Kiulizi | 0 | 1 | **1** |
| Kielezi | 0 | 1 | **1** |
| Kiunganishi | 2 | 0 | **2** |
| **JUMLA** | **126** | **80** | **206** |

5.2 AINA ZA UDONDOSHAJI ZINAVYOJITOKEZA

Kutokana na Jedwali 5.2, udondoshaji umetokea zaidi katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie*, mara mia moja na ishirini na sita (126) ikiwa asilimia sitini nukta saba nane (60.78%), na katika *Musaleo!* umetokea mara thamanini (80) ikiwa asilimia thalathi na nane nukta nane tatu (38.83%). Katika jedwali 5.2 Udodoshaji wa silabi umetokea zaidi katika *Watoto wa Maman'tile*, mara hamsini na tatu (53) na katika *Musaleo!* mara kumi na moja (11). Udondoshaji wa Nomino tumeugawa mara mbili, ule wa Kiima (K) na ule wa Yambwa (Y). Katika *Watoto wa Maman'tilie* udondoshaji wa K umetokea mara kumi na sita (16) na katika *Musaleo!* umetokea mara kumi na saba (17); ule wa Y katika

*Watoto wa Maman'tilie* umetokea mara kumi na moja (11) na katika *Musaleo!* umetokea mara kumi na nne (14). Udondoshaji wa kitenzi umetokea mara kumi na sita (16) katika *Watoto wa Maman'tilie* na katika *Musaleo!* umetokea zaidi, mara ishirini na tatu (23). Udondoshaji wa kishazi/sentensi umetokea mara ishirini na tano (25) katika *Watoto wa Maman'tilie* na mara kumi na mbili (12) katika *Musaleo!*. Udondoshaji wa kiashiria/kionyeshi umetokeza mara mbili (2) katika matini ya *Watoto wa Maman/tilie* na mara moja (1) katika *Musaleo!*. Ule wa kimilikishi umetokea mara moja tu (1) katika *Watoto wa Maman'tilie* na haupo kabisa katika *Musaleo!* (0). Udondoshaji wa kiulizi na kielezi umetokea mara moja moja (1) katika *Musaleo!* na haupo kabisa katika *Watoto wa Maman'tiliie.* Udondoshaji wa kiunganishi umetokea mara mbili (2) katika *Watoto wa Maman'tilie* na haukutokea katika *Musaleo!* (0).

Udondoshaji katika matini husika zinazorejelewa katika utafiti wetu, *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo*! Aina kuu za udondoshaji zilizojitokeza ni zile za silabi katika neno, nomino, kitenzi, kishazi na sentensi. Aidha kuna udondoshaji wa kimilikishi, kielezi, kiashiria, kiunganishi na kiulizi. Udondoshaji huu ndio tumeuita aina za udondoshaji katika tasnifu hii na kuwa na udondoshaji wa silabi, nomino, kitenzi, kishazi na sentensi. Hizi ndizo aina zilizojadiliwa. Hata hivyo udondoshaji wa kimilikishi, kielezi, kiashiria na kiulizi umeonyeshwa pale ulipotokea katika matini.

## 5.1 Udondoshaji ulivyotokeza

Udondoshaji hutokea wakati kipashio katika matini kimedondoshwa katika sentensi fuatilizi na mahali pake kubaki pengo la kimuundo. Udondoshaji hutokea kwa kuondoa

urudufishaji. Hata hivyo tumeona katika matini zetu teule kuwa udondoshaji ni mtindo wa lugha ya mwandishi, na mara nyingi umetokea katika usemi halisi. Tuangalie jinsi umetokea katika matini hizo teule.

### 5.1.1 Udondoshaji wa Silabi

Katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* udondoshaji wa silabi unapatikana. Silabi zilizodondoshwa ama ni zile zinazotokea mwanzoni, katikati au mwishoni mwa neno. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (TUKI, 1990) inaeleza kwamba silabi ni kipashio cha utamkaji ambacho ni kikubwa kuliko fonimu na kidogo kuliko neno.

Gimson (1980: 55) anaeleza,

> "Silabi ni dhana ya kipashio cha juu kuliko fonimu au kipande cha sauti na tofauti na kipashio cha neno au mofimu." (Yafsiri Yetu)

Naye Jones (1979: 55) anasema,

> "Silabi ni sauti inayotawala katika usemi. Kinadharia silabi hujumuisha mfuatano wa sauti na kilele cha kutawala kwa sauti." (Tafsiri Yetu)

Mgullu (1999) anaeleza silabi kuwa ni kipashio kimojawapo ambacho hutumika kuelezea muundo wa lugha hasa katika kiwango cha fonolojia arudhi. Fudge katika Mgullu (1999: 72) anaeleza kuwa silabi ni kipashio cha kifonolojia ambacho kwa ukubwa kipo kati ya fonimu na neno. Aghalabu silabi huwa ni ndefu zaidi kuliko fonimu lakini ndogo kuliko neno kamili.

Mohammed (2001:11) anaeleza silabi kuwa ni kipashio cha utamkaji ambacho kawaida ni kikubwa kuliko sauti moja na ndogo kuliko neno. Nao Habwe na Karanja (2007:66-67) wanaeleza silabi kuwa ni sehemu ya neno. Sehemu hii huwa inatamkika na aghalabu

husikika kama sehemu tofauti na nyingine katika msingi wa neno. Wanaendelea kueleza kuwa silabi inaweza kuwa konsonanti, vokali pekee, konsonati moja au zaidi zikifuatwa na vokali. Ikiwa silabi inaishia kwa vokali/irabu huitwa "silabi wazi" au "huru" na inapoishia na konsonanti, huitwa "silabi funge".

Laver (1994:114) aneleza juu ya silabi wazi na funge na kuwa silabi kifonolojia hujengwa na elementi kiini na elementi kando (au iso kiini). Elementi kiini ni vokali na elementi kando ni konsonanti. Hata hivyo Laver alikuwa akirejelea lugha ya Kiingereza. Lugha za Kibantu, kama wasemavyo Habwe na Karanja (2007:54, 67) zina utaratibu mmoja wa silabi. Silabi zake huwa huru, na Kiingereza ina silabi funge. Massamba na wenzake (2008) wanaeleza kuwa silabi ni sehemu ya neno ambayo huweza kutamkwa kwa mara moja na kwa pamoja kama fungu moja la sauti.

Kwa hivyo, silabi ni kipashio cha sauti kinachotamkika katika neno ambacho ni kikubwa kuliko sauti moja na kidogo kuliko neno kinachoweza kuundwa na vokali pekee au konsonanti nazali au konsonati na vokali katika Kiswahili. Silabi zilizodondoshwa katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo*! ni silabi vokali na silabi konsonanti-vokali. Natuchunguze mifano ifuatayo:

> 146. Japo Jane, hakujaliwa na mtoto, sasa alikuwa na watoto! Ilibidi awalee watoto wa marehemu rafiki yake. Na pole pole jina lake likafa. Wakaazi wa Kisutu wakawa wanamwita Mama Kurwa. Ilikuwa kama (1 )kafa, kisha Mama Kurwa ( 2 )kafufuka tena.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 37)

Matini hii inadhihirisha udondoshaji wa silabi */a-/+/-me-/* na */a-/*. Silabi */a-/* na */-me-/* zilifaa ziwe katika kitenzi 'kafa' lakini lazima kibadilike kimofojolia na kuwa 'amekufa'.

Na silabi /*a*-/ imedondoshwa katika kitenzi 'kafufuka'. Sahihi ingekuwa '*a*kafufuka'. Silabi hii ni kiwakilishi cha nomino kiima Mama Kurwa.

> 147. ...Alichukuwa kitabu cha *Adili na Nduguze* kilichoandikwa na yule mwandishi maarufu, Shaaban Robert, akaanza ku( )soma katika mwanga hafifu wa koroboi.
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k. 9)

Katika matini hii, silabi /*ki*-/ imedondoshwa katika kitenzi 'kusoma'. Kwa minajili ya usahihi kimuundo, silabi hii ingeingizwa katika kitenzi hicho kwa kupachikwa katikati mwa silabi /*ku*-/ na /-*so*-/, hivyo kuwa 'ku*ki*soma'. Silabi hii ni kiwakilishi cha yambwa 'kitabu'.

> 148. Lomolomo alipepesuka, akataka kuanguka. Mamantilie alimdaka. "Niache we( ) mwanamke! Unanishikashika, unadhani mi( ) nimelewa!" Alikohoa *Ukho! Okhoo!*
> (*Watoto wa Mamantilie* u.k 11)

Hapa silabi /-*we*/ imedondoshwa katika kiwakilishi nafsi 'wewe'. Pia silabi /-*mi*/ imedondoshwa katika kiwakilishi nafsi 'mimi'. Udondoshaji wa silabi hapa ni mtindo hususan katika lugha ya maongezi. Wakati watu wanapozungumza kuna tabia ya kudondoa silabi za baadhi ya maneno. Matini hii ni maongezi kati ya Mzee Lomolomo na mkewe Mama Zita, na mwandishi ameweka mazungumzo haya katika usemi halisi. Hivyo kuonyesha udondoshaji wa silabi.

> 149. ...Macho yake yalimwangalia Zenabu akipakua sahani ya muhogo. Alimwekea mezani.
> "Kula wende ( ) kucheza."
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 15)

Silabi mbili zimedondoshwa, /*u*-/ na /-*ka*-/ katika kitenzi nomino 'kucheza'. Sahihi ingekuwa "ukacheze" lakini mwandishi hakutumia urefu wa kitenzi hiki bali alidondoa silabi hizo na kukiandika kwa ufupi akikiweka katika muundo wa kitenzi nomino.

150. ...Sasa tangu juzi ( )kazidiwa. Hatii kitu mdomoni ila kukutaja tu, Mama Zitaa, Mama Zita! Kaniitieni Mama Zitaa! Ee! Basi nd( )o nimefunga safari kukufuata hivyo."

(*Watoto wa Maman'tilie,* u.k 33-34)

Hapa udondoshaji umetokea mara mbili. Silabi /a-/ na /-me-/ zimedondoshwa katika kitenzi 'kazidiwa' na vokali /-i-/ na nusu vokali /-y-/ zimedondoshwa katika kibainishi 'ndo-'. Kikamilifu kitenzi 'kazidiwa' kingekuwa '*ame*zidiwa", na tunapoambisha silabi dondoshwa hizo, silabi /*ka*-/ hudondoshwa. Katika 'ndo' kuna vokali na nusu vokali zimedondoshwa, /*i*/ na /*y*/ na zinapoambishwa huunda neno 'nd*iy*o'.

151. Kwa wiki nzima Mama Kurwa alipigana na malaria. *Chloroquine* wapi! Kutapika, ( )toka jasho! ( )Tetemeka mwanamke!

(*Watoto wa Maman'tilie,* u.k 36)

Matini hii inaonyesha udondoshaji wa silabi /*a*-/ na /-*li*-/ katika vitenzi viwili 'toka' na 'Tetemeka'. 'toka' ingekuwa '*ali*toka' na 'Tetemeka' ingekuwa '*Ali*tetemeka'. Silabi hizi ni kiwakilishi nafsi cha kiima, *a*-, na kiambishi cha wakati uliopita -*li*-.

152. ...Mbwa wale walipotea machoni pake, wak( )enda zao.

(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 38)

Hapa vokali /-*a*-/ imedondoshwa katikati mwa kitenzi 'wakenda' na kitenzi hiki kinafaa kuwa "wak*a*enda".

153. "...Na nyinyi nd( )o mtafia jela, laanabuku!"0

(*Watoto wa Maman'tilie,* u.k 98)

154. ...Nilishangaa ni kwa nini watu wengine walisema Hawakumuona ye yote. Hata sauti hawaku( )sikia!...

(*Musaleo!* u.k 4)

Katika matini hizi mbili 153 na 154, vokali /-*i*-/ imedondoshwa katika kibainishi 'ndo' na kitenzi 'hawakusikia'. Katika 153 /-*i*-/ imebaki vokali tu lakini katika 153 ni silabi kwa

sababu ni sauti inayotamkika peke yake, na hapa ni kiambishi kiwakilishi cha nomino 'sauti' . Ukamilifu wa maneno haya ungekuwa 'nd*i*o' na 'hawaku*i*sikia'.

155. Haraka haraka Peter aliteka maji ya baridi sana ( )toka mtungini...

(*Watoto wa Maman'tilie,* u.k 61)

Hapa silabi /*ku-*/ imedondoshwa katika kitenzi 'toka'. Ukamili wake ni '*ku*toka'.

156. "Mugogo unaota wewe!"
"Nimeamka Bwa( )'Mbu!"

(*Musaleo!* u.k 6)

157. ..."*Ni kama hiki kitabu kitukufu, huwezi ku( )pinga yaliyoandikwa humo. Hiyo ni KAULI ya ukweli," walisema wengine.*

(*Musaleo!* u.k 27)

158. "Ipi?"
"Bei ya nguo...Shati hili nime( ) nunua kwao. Shilingi sitini..."

(*Musaleo!* u.k 64)

Katika matini hizi 156, 157, 158, kuna undondoshaji wa silabi mbalimbali. Katika matini 156 silabi /*-na*/ imedondoshwa katika kivumishi 'Bwa*na*', 157 silabi /*-ya-*/ imedondoshwa katika kitenzi 'kupinga' na 157 silabi /*-li-*/ imedondoshwa katika kitenzi 'nimenunua'. Kwa ukamilifu, kitenzi katika 157 kingekuwa 'ku*ya*pinga' na katika 158 kingekuwa 'nime*li*nunua'. Silabi /*-ya-*/ ni kiambishi kiwakilishi cha 'maneno' yanayorejelewa na silabi /*-li-*/ ni kiambishi kiwakilishi cha nomino 'shati'.

\

Udondoshaji wa silabi uliotokea katika matini zote mbili ni wa hiari. Kama wasemavyo Allerton (1975: 235) na Gunter (1963), nyakati zingine ni aina ya mtindo wa mwandishi. Kwa hivyo tunaona kwamba udondoshaji wa silabi katika matini hizi ni mtindo wa watunzi Emmanuel Mbogo na Kyalo W. Wamitila. Hapa udondoshaji huu haupotoshi mshikamano wa matini. Pia kama tulivyoeleza awali, udondoshaji hutumika sana katika

usemi hallisi katika matini. Kawaida katika usemi halisi wazungumzaji hudondosha silabi au maneno, na kwa vile mwandishi alitaka kuonyesha usemi huo halisi ilibidi adondoshe kama usemi ulivyo.

### 5.1.2 Udondoshaji wa Nomino

Udodondoshaji wa Nomino tumeugawanyika katika aina mbili;

i) wa Nomino inayojitokeza kama Kiima

ii) wa Nomino kama Yambwa.

Nomino hizi hutokea katika matini kama kiima au yambwa. Katika hali yoyote ya hizi, huweza kudondoshwa na kuacha pengo la kimuundo.

Udondoshaji wa nomino ni wakati nomino hiyo imeachwa nje ya sentensi na kuacha pengo la kimuundo, na ili kupata maana kamili, inabidi pengo hilo lijazwe kwa kudhania nomino hiyo kutoka kwingineko. Nomino hiyo lazima iwe imetangulia kutajwa katika matini. Udondoshaji wa nomino hujumuisha kupandisha daraja neno linalofanya kazi ya neno kisonde, hesabati, kisifa au kiainishaji kutoka kivumishi hadi daraja ya neno kuu. Nomino iliyodondosahwa, ili kujaza pengo lililopo la kimaana, huhitaji kuwe na asili au habari nyingine muhimu. Kawaida, asili ya habari hiyo ni KN iliyotangulia. KN ambayo ni dondoshi hudhaniwa kutoka KN iliyotangulia kutajwa katika matini na haijadondoshwa. Hii huleta mshikamano wa matini (Halliday na Hassan, 1976:148).

Udondoshaji wa KN hujumuisha nomino yenyewe au nomino na vifuasi vyake kama maneno kisonde mahususi yaliyo na uamilifu wa kibainishi, maneno kisonde baada ya neno kuu, visifa na vivumishi (Watajwa hapo juu: 163; Salkie, 1995: 57).

Burton-Roberts (1986) anasema kuwa udondoshaji wa kiima hutokea kwa kiwakilishi nafsi katika Kiingereza. Katika Kiswahili, udondoshaji huu haupatikani kwa sababu kiambishi nafsi ni sehemu ya kitenzi inayowakilisha kiima hicho, mfano "*Ni*limtembelea". Katika kitenzi hiki (pia ni sentensi sahili), *Ni-* ni kiambishi nafsi lakini katika Kiingereza ni neno kamili ( *I* ) na huweza kudondoshwa. Hata hivyo udondoshaji huu lazima uwe katika muktadha wa usemi. Katika utafiti huu tumegawanya udondoshaji wa nomino katika aina mbili; i) Nomino Kiima (NominoK) ii) Nomino Yambwa (NominoY). Baada ya maelezo haya tuangalie jinsi udondoshaji huu unavyojitokeza katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*:

#### 5.1.2.1 Udondoshaji wa Nomino Kiima

Udondoshaji wa NominoK umetokea katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* Katika matini hizi, nomino ambazo ni kiima zimedondoshwa katika baadhi ya sentensi ili kuondoa urudufishaji, na kuleta mshikamano. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) inaeleza kiima kama sehemu ya kwanza ya tungo ambayo huelezwa na kiarifu. Kiima ni kile kipashio ambacho hutenda kitendo katika sentensi. Mifano ifuatayo inadhihirisha udondoshaji huu.

> 159. Gari aina la *Landrover* lilifunga breki, likaserereka na kutoka nje ya barabara. Mbwa alilia bwe! Gari lilikuwa limeu-kwatua mkia wake. (   ) aliruka ng'ambo nyingine ya barabara ili kusalimisha maisha yake.
> (*Watoto wa Maman'tilie u.k 1*)

Hapa NominoK 'Mbwa' imedondoshwa katika sentensi fuatilizi ya tatu. Kwa hivyo ili kujua neno lililodondoshwa, lazima msomaji arejelee nyuma katika matini palipo nomino 'Mbwa' kujaza pengo hilo. Iwapo nomino 'Mbwa' ingerejelewa katika sentensi hiyo ya tatu, urudufishaji ungetokea na kuharibu mshikamano wa matini. Kwa hivyo udondoshaji

wa NominoK ulibidi. Udondoshaji huu umekwepa urudufishaji ambao ungetokea, ungeharibu mshikamano.

> 160. Mamantilie alimvuta ndani na Lomolomo akakaa kizingitini.
> Kisha, alitia komeo ya mlango akasema, " (  ) Twende ndani
> ukalale. (  ) Usianze kelele zako, kuwaamsha watoto."
> ( *Watoto wa Maman'tilie* u.k 11)

> 161. Zenabu alisema, "(   ) Hata kunawa hujanawa." Peter
> alitazama chini, dole lake gumba linachora mistari ardhini.
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 15)

Katika 160 NominoK, 'Lomolomo', imedondoshwa na ilibidi. Matini ingekuwa na muundo usioridhisha iwapo NominoK 'Lomolomo' ingetajwa mara tatu mfululizo. Kwa hivyo, ilibidi idondoshwe ili kuleta mshikamano wa kisarufi. Katika pengo ilipodondoshwa, tunarejelea nyuma kupata nomino 'Lomolomo' na kukamilisha maana. Katika 161 NominoK, 'Peter', imedondoshwa, na kulijaza pengo hili, inalazimu msomaji kurejelea mbele. Kwa hivyo udondoshaji hapa ni wa nyuma.

> 162. "Nimeyasikia mama."
> "Basi nyumba hii. Iangalie. *Wewe* si moto tena.
> (   ) Ni mwanamke, mtu mzima!"
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 34)

Hapa NominoK '*Wewe*' imedondoshwa. '*Wewe*' ni kiwakilishi cha nafsi na ndicho kiima. Kilitajwa katika sentensi tangulizi na kudondoshwa katika sentensi fuatilizi. Iwapo kingerudiwa tena, kingeleta urudufishaji na kuharibu mshikamano. Kwa hivyo, ilibidi kidondoshwe ili kuleta mshikamano katika matini.

> 163. Nilikuwa bado nikiyapitisha yale maneno
> kichwani niliposikia mfyatuko mkubwa. "Hiyo ni
> bunduki," nilijisemea.
> ... Miili miwili ilianguka *paap* vumbini! Niliachama.
> Nilivuta shingo kuangalia (   ) ilikotokea.
> (*Musaleo!* u.k 1)

Hapa 163 udondoshaji wa NominoK umetokea. Kiima hiki ni 'bunduki'. Kimeacha pengo katika matini. Ili kupata maana kamili, lazima tukirejelee nyuma kilikotangulia kutajwa na kuingizwa katika pengo kwa kudhani. Inapofanyika hivyo maana inakamilika na kudhihirisha mshikamano uliopo wa matini.

> 164. Ilikuwa Ijumaa jioni siku ambayo *Kingunge* ataikumbuka milele. Hamu aliyokuwa nayo kwa miaka sita iliyopita ilielekea kutimizika hatimaye.
> ... Kama mtumwa anayeelekezwa kwenye hatua zake zote, ( 1 ) alitii. ( 2 ) Alielekea kwenye chumba chake cha kuandikia.
> (*Musaleo!* u.k 1-2)

Katika matini hii 164 NominoK imedondoshwa, katika mapengo (1) na (2). NominoK hiyo ni *Kingunge.* Huyu ndiye mwandishi anayerejelewa katika matini. Kwa hivyo ili kuelewa vyema na kupata maana kamili, itambidi msomaji arudi nyuma katika matini kupata nomino hii ili kukamilisha maana. Hata ikiwa katika sentensi mbili za mwanzo, NominoK imewakilishwa na kiambishi nafsi *a-* na *A-* katika vitenzi 'tii' na 'elekea', lazima turejelee nyuma kwa nomino *Kingunge* ili kukamilisha maana na kupata ule mshikamano wa matini. Nomino hii ingeandikwa katika mapengo hayo, ingeleta urudufishaji na kuharibu mshikamano wa kisarufi katika matini.

> 165. Inasimuliwa kuwa watu walipata nguvu mpya baada ya kutoka kwenye Vita vya Fyuraa. (   ) Venyewe vilipiganwa huko mbali na wenyeji wengi walishawishiwa kujiunga na jeshi kwenda kupigana...
> (*Musaleo!* u.k 50)

> 166. "Na ndiyo matatizo yetu sisi, tunajisamehe kwa kuwalaumu wengine. Udhaifu wetu wa kuamba na kuambizana kuwa *zimwi* likujualo halikuli likakwisha..." Sauti nyingine: "Siku hizi (   ) halikuli tu bali linakufuata na kukufagilia kabisa; hufyuu!..."
> (*Musaleo!* u.k 70)

Katika matini hizi 165 na 166, NominoK 'Vita vya Fyuraa' na '*zimwi*' zimedondoshwa na kuacha mapengo katika muundo wa sentensi. Ili kujaza mapengo hayo ya udondoshaji, msomaji lazima arejelee nyuma kupata nomino hizo kukamilisha maana. Hivyo udondoshaji katika 165 ulikuwa wa lazima ili kuondoa urudufishaji na kuleta mshikamano. Na katika 166 udondoshaji ulikuwa wa hiari, hata hivyo ulichangia kuleta mshikamano katika matini.

### 5.1.2.2 Udondoshaji wa Nomino Yambwa

Udondoshaji wa NominoY ni ule wa Nomino yenye uamilifu wa yambwa katika sentensi. Kwa mujibu wa *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha* (1990) yambwa ni neno linaloashiria kitendwa au kitendewa katika sentensi. Yambwa ni nomino katika sentensi inayotendwa au kutendewa jambo fulani.

Habwe na Karanja (2007:163) wanaeleza kwamba yambwa ni elementi ambayo ni jina la yule anayetendwa au anayetendewa kitendo katika sentensi. Katika Kiswahili kuna yambwa tendwa na yambwa tendewa. Kwa ufupi yambwa ni kitendwa au kitendewa.

Katika utafiti huu hatukubainisha yambwa tendwa au yambwa tendewa, zote tumezichukulia kama yambwa kwa jumla. Udondoshaji wa yambwa umejitokeza katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*. Natuchunguze mifano ya aina ya udondoshaji huu:

167. Zenabu alimimina chai ya rangi kwenye kikombe cha
plastiki.
"Haya kunywa ( )!" Peter hakuichukua ile mara moja.
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 15)

168. Watoto wawili, mmoja mvulana na mwingine msichana,
waligeuka kumtazama yule aliyepiga chafya. Mara moja Peter
aligundua kuwa watoto wale walikuwa wanafanana sana.
...Peter aliwasogelea na kuwasalimu.
Msichana aliitikia, lakini mvulana alikaa kimya, kamkazia ( )
macho yaliyojaa chuki.
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 19)

Katika matini hizi udondoshaji wa yambwa ulitokea. Katika 167 yambwa ni 'chai' na 168 yambwa ni 'Peter'. Katika 167 udondoshaji ni wa hiari lakini 168 ni wa lazima. Nomino Peter (Yambwa) inaporudiwa kuandikwa katika pengo lililopo, urudufishaji unatokea na kuharibu mshikamano. Kwa hivyo udondoshaji ulistahili ili kukamilisha muundo wa matini hii unaokubalika na kuleta mshikamano:

169. Aliwasha koroboi, akafunga mlango. Alijitazama.
... Alivuta pumzi ndani ili kuyatazama mafua yasitoke nje.
Mkono wa kushoto koroboi, aliupeleka ( ) wa kulia dondani...
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 47)

Hapa udondoshaji wa yambwa umetokea. Yambwa iliyodondoshwa ni 'mkono'. Udondoshaji huu umeondoa urudufishaji na kuchangia mshikamano. Iwapo katika pengo, yambwa 'mkono' ingerudiwa tena, basi urudufishaji huu ungeharibu mshikamano wa matini.

170. ... *Hawa wahuni wanawafunza wanetu kuvuta bangi*,
niliyakumbuka maneno ya jirani yetu aliyekuwa
akifanya kazi serikalini...*Itabidi tujaribu kufanya jambo.
Wanafurika mijini hawa, hatuwezi kukaa tushangilie
uharibifu tu; tuchangamke anavyosema mzee!* niliyakumbuka ( )
mengine.
(*Musaleo!* u.k 1)

Katika matini hii, yambwa ni 'maneno' na imedondoshwa. Iwapo nomino 'maneno' ingerudiwa katika pengo hilo, sentensi hii ingekuwa na utata wa maana. Pengine ingeleta maana kuwa msomaji aliyakumbuka 'maneno' mengine nje ya hayo aliyosema jirani wa

msimulizi. Lakini alipodondosha yambwa, maana iliyobaki ni kuwa "aliyakumbuka maneno zaidi ya hayo". Udondoshaji huu umeondoa utata na umeleta mshikamano. Kwa hivyo, udondoshaji vile vile husaidia kuondoa utata katika matini:

> 171. Mtuo wa kusikiliza wa Zamda ulitokana na ( 1 ) moja.
> Alikuwa na hakika kuwa mumewe wa miaka inayokaribia kumi na tano ameingiwa na wazimu... Baada ya Kingunge kuridhika kuwa amefanikiwa kumweleza mkewe aliinuka na kwenda zake chumbani. Alishika kalamu yake...
> ... ( 2 ) Alikatizwa uandishi wake na Zamda aliyemgongea mlango. (*Musaleo!* u.k 12-13)

> 172. "Vipi Mzee unawaruhusu Wahindi hawa kutukaribia?"
> Naye ( 3 ) aliharamisha ununuzi huo kwa kutamka maneno fulani aliyoyaita **Ordinance**. Ununuzi wote wa ardhi kati ya watu tofauti haukuruhusiwa. Ilikuwa haramu!
> Wahindi walichukia ( 4 ).
> (*Musaleo!* u.k 37)

Katika 171 udondoshaji umetokea mara mbili. (1) yambwa 'neno' na (2) yambwa 'Kingunge' zimedondoshwa. Katika (1), kidondoshwa kinaweza kurejelewa kutokana na muktadha wa sentensi ilivyotamkwa na ufahamu wa Kiswahili. Gunter (1963:143) anaita udondoshaji huu udondoshi wa kimuktadha, na kueleza kuwa utegemezi wa muktadha hujumuisha muungano au mwambatano wa kisarufi kati ya sentensi dondoshi na muktadha wake. Hapa si sentensi iliyodondoshwa bali neno. Na kutokana na muktadha wa sentensi, kilichodondolewa ni yambwa 'neno' ambalo tunalirejelea kimuktadha kujaza pengo la kimuundo. Inapofanyika hivyo, tunapata maana iliyokamili na kuleta mshikamano. Pengo (2) yambwa 'Kingunge' imedondoshwa na tunairejelea nyuma katika matini kwani imetangulia kutajwa.

Katika 172 (4) yambwa '**Ordinance**' imedondoshwa na imeshatajwa awali katika matini. NominoY zote hizi zimewacha mapengo ya kimuundo ambayo kuyajaza inabidi msomaji arudi nyuma katika matini au atumie muktadha kama vile katika 171 (1). Na pengo (3) udondoshaji umetokea wa nomino 'Mzee' lakini si udondoshaji wa yambwa bali wa kiima na umeshajadiliwa.

### 4.1.3 Udondoshaji wa Kitenzi

Kitenzi ni sehemu muhimu ya sentensi. Ndiyo sehemu inayoeleza kinachotendeka katika sentensi. Hata hivyo katika udondoshaji, kitenzi kinaweza kudondoshwa na bado maana ikabakia ile ile. Maana hubakia ikiwa msomaji atarejelea nyuma kupata kitenzi hicho na kukijaza katika pengo la kimuundo. Kitenzi hiki kitarejelewa na kulijaza pengo kwa kudhania. Katika utafiti huu, tuligundua kuwa katika Kiswahili, kinyume na Kiingereza, udondoshaji katika vishazi viso-elekezi na vishazi viso-vitenzi hauwezikani. Hii ni kwa sababu viwakilishi nafsi katika Kiswahili ni viambishi vya ngeli katika vitenzi. Lazima viegemezwe na kitenzi na kuwa mofimu inayowakilisha nomino.

Udondoshaji wa kitenzi mara nyingi hutokea katika kauli halisi au katika majibizano. Natutalii mifano ifuatayo.

173. Baada ya ukimya, Peter alisema, "Mimi nakwenda."
"( 1 ) Wapi?"
"( 2 ) Safari fupi. Tutaonana."
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 18)

Matini hii inaonyesha udondoshaji wa kitenzi *-enda*. Kitenzi hiki kina sura mbili tofauti za kimuundo katika mapengo ya udondoshaji. Mzizi ni *–enda*, lakini kwa mujibu wa mfumo wa Kiswahili, mzizi huu umeambishwa viambishi mahususi ili kukubalika.

Katika pengo (1) kitakuwa "Una*enda*..." (katika nafsi ya pili umoja, ngeli ya *a-wa*) na pengo (2) kitakuwa "Na*enda*..." (nafsi ya kwanza umoja, ngeli ya *a-wa*). Kwa hivyo badala ya wazungumzaji kurudia kitenzi hicho katika mapengo (1) na (2), wamekidondosha. Udondoshaji huu haukuathiri maana au mshikamano kwa sababu tunarejelea nyuma kupata kitenzi hicho na kujaza mapengo hayo kukamilisha maana. Hivyo tunakidhania kitenzi '*-enda'* katika kuyajaza mapengo haya.

174. "Oh! Yule! Ni kaka yangu. Ni mkorofi sana wakati mwingine."
Walinyamaza kimya.
"Unakaa wapi?"
" ( 1 ) Manzese," Peter alijibu. "Na wewe ( 2 )?"
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 24-25)

Hapa udondoshaji wa kitenzi umetokea mara mbili pia. Katika mapengo haya (1) na (2), itamlazimu msomaji arejelee nyuma ya matini kupata vitenzi hivyo. Katika pengo (1) kitenzi '*Ninakaa*' kimedondoshwa na katika pengo (2) kitenzi + kiulizi vimedondoshwa, '*Unakaa* + *wapi*?'. Mzizi wa kitenzi ni *–kaa* lakini kwa mujibu wa mofolojia ya Kiswahili, kitenzi 1, kimeabishwa *Ni-* kusimamia nafsi ya kwanza umoja na katika kitenzi 2, kiambishi *U-* kimeambishwa katika mzizi kusimamia nafsi ya pili umoja, viambishi vyote hivi viko katika ngeli ya *a-wa*.

175. Watu walisongana! Walisukumana, kupigania mchele. Wengine walikuwa na vikapu, wengine ( ) magunia.
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 26)

176. "Mi siumwi mie, Peter."
"Basi na wewe lala. Si vizuri kukaa tu hivyo."
"Sawa ( )."
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 83)

Katika 175, kitenzi + kihusishi vimedondoshwa. Kitenzi chenyewe kimejengwa na kitenzi saidizi '*walikuwa*' + '*na*' (kihusishi milikishi). Katika 176 kitenzi

kilichodondoshwa ni '*nitalala*'. Vile vile hapa, ili kukamilisha maana, msomaji inambidi arejelee nyuma kupata vitenzi hivi na kuvijaza katika mapengo kwa kudhania.

> 177. "Hatukusikia sie. Labda wengine ( 1 ). Hayo tunapuuza.
> Jifunze kuyapuuza yasiyokuhusu; utajachomwa na ugali
> uliolala nje!"
> "Kwa hiyo hamkusikia?"
> "Hapana ( 2 )."
> "Kifaru hata wewe ( 3 )!"
> (*Musaleo!* u.k 6)

Kitenzi katika matini hii ni kimoja na kimedondoshwa mara tatu. Kitenzi chenyewe ni *–sikia*, lakini kwa kufumana na muundo wa Kiswahili kimeambishwa viambishi mahususi ili kukubalika. Pengo (1), kitenzi ni '*walisikia*'. Kiambishi *wa-* kimetangulia na kinasimamia wingi, nafsi ya tatu katika ngeli ya *a-wa*. Pengo la 2, kitenzi ni '*hatukusikia*'. Kitenzi hiki kina kiambishi kanushi '*ha-*', kiambishi cha nafsi ya kwanza wingi '*tu-*' na kiambishi '*ku-*' cha kimuundo ambapo lazima kitumike tunapokanusha (*ha+ tu+ ku+ sikia*). Hapa tunakidhania na kukipa miundo hii. Katika pengo la (3), kitenzi ni '*hukusikia*'. Hapa kiambishi '*hu-*' kimetumika kusimamia nafsi ya pili umoja, na '*ku-*' kimetumika kimuundo (*hu+ ku+ sikia*).

> 178. "Namjua sana!"
> "Je, unampenda?"
> "Una nini wewe? Sasa swali gani hilo?"
> "Jibu tu: Ndio au la."
> "Ndio ( )…! Alaaa!" (niliguna)
> "Basi yaache uliyonuia!"
> (*Musaleo!* u.k 22)

Katika matini hii kitenzi '*nampenda*' kimedondoshwa. Na kukamilisha pengo lililoachwa baada ya udondoshaji huo, lazima msomaji arejelee nyuma ambako kitenzi hicho

kimetokea na kukileta katika pengo hilo kwa kudhani. Inapotokea hivi, maana inakamilika na mshikamano kutokea.

> 179. Mabango makubwa na makaratasi makubwa yaliandika:
> Mzee anawaletea watu wote amani, kila mtu amtukuze.
> Yalisambazwa kila mahali.( 1 ) Shuleni. ( 2 ) Ofisini.
> ( 3 ) Hotelini. ( 4 ) Viwanjani. ( 5 ) Barabarani. ( 6 ) Vyooni.
> Popote ulipogeuka ulimuona yeye.
> (*Musaleo!* u.k 82)

Hapa kitenzi '*Yalisambazwa*' kimedondoshwa mara sita na kuondoa urudufishaji. Iwapo kitenzi hicho kingeandikwa katika mapengo yote sita, kungekuwa na urudufishaji usiofaa kimatini. Ili kukamilisha maana katika matini hii, itamlazimu msomaji kurejelea nyuma ya matini kupata kitenzi 'Yalisambazwa' na kukijaza katika mapengo kwa kudhani. Kwa hivyo udondoshaji hapa ulilazimu ili kuhifadhi mshikamano wa matini.

Katika matini hizi tuligundua udondoshaji wa kitenzi ambapo hakijatajwa kokote katika matini. Ili kukamilisha pengo hilo, hubidi msomaji akirejelee kutokana na muktadha na ufahamu wake wa muundo wa Kiswahili. Kuhusu udondoshaji huu, Thomas (1979:46) anaeleza hivi;

> "Ikiwa ufafanuzi wa pengo lililopo ni kwa kupitia ufahamu wetu wa lugha wala si kutoka kwa muktadha wa sentensi ilivyotumika, huo si udondoshaji bali *elision*". (Tafsiri Yetu)

Akaendelea kueleza kuwa ili kuelewa elementi iliyodondoshwa, msomaji hutumia ufahamu wa mfumo wa lugha iliyotumika wala harejelei muktadha au matini. Akatoa mfano wa Kiingereza;

"( ) *Got the tickets*?".

Hapa kilichodondoshwa ni "*Have you…*" na tumekirejelea kutokana na ufahamu wa lugha na kutegemea muktadha. Kwa kweli sentensi hii haikutamkwa katika ombwe tupu. Lazima ilitamkwa katika muktadha fulani. Kwa hivyo elementi dondoshwa itapatikana katika muktadha wa sentensi ilivyotumika na ufahamu wa lugha. Katika tasnifu hii tumechukulia huu kuwa ni udondoshaji wa kimuktadha ambapo neno halipo katika *matini* lakini linarejelewa kimuktadha. Inapofanyika hivi, tunakamilisha maana na kupata mshikamano wa matini. Udondoshaji wa aina hii tuliupata katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* tu. Natutalii udondoshaji wa vitenzi katika matini zifuatazo:

> 180. Mamantilie alikafungua kapochi kake, akatoa shilingi mia moja, "Hizi (1) za mafuta ya taa. Utumie pesa vizuri, sijui nitakaa huko siku ngapi. Unaelewa?"
> "Naelewa mama."
> Mamantilie na binti yake walitoka.
> "Mimi ( 2 ) tayari kaka."
> Mjomba alisimama. "Haya", aliwapa wapwa zake mkono wa kwa heri. "Tutaonana."
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 34-35)

Katika matini 180 vitenzi ungio '*ni*' na '*niko*' vimedondoshwa na havipo mahali popote katika matini na kuacha mapengo ya kimuundo (1) na (2). Ili kulijaza pengo lililopo, tunatumia ufahamu wa Kiswahili na muktadha. Kwa umilisi wa lugha hii, msomaji atavirejelea vitenzi hivi na kuvijaza katika mapengo (1) na (2), na kuleta dhana inayokusudiwa na mshikamano wa matini.

> 181. Kwa wiki nzima Mama Kurwa alipigana na malaria.
> ( ) *Chloroquine* wapi! Kutapika, toka jasho! Tetemeka mwanamke! Kichefuchefu, hamu ya chakula hakuna!
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 36)

Matini 181, kitenzi '*Alikula*' kimedondoshwa. Tunakirejelea na kukamilsha maana kimuktadha. Kwa mujibu wa mchakato na muundo wa Kiswahili dawa huliwa, hivyo

kitenzi kula ndicho hutumika katika ulaji wa dawa ikiwa ni vidonge. Maji au aina ya dawa iliyo maji maji hunywewa. Kutokana na mchakato huo wa Kiswahili pengo lililopo linaonyesha kitenzi *–kula* kimedondoshwa. Kufuatana na muundo wa Kiswahili, kitenzi hiki lazima kiegemezwe na kiambishi cha nafsi ngeli ya nomino kiima ambacho ni Mama Kurwa. Kiambishi sahihi ni *A-* na kuwekwa na kiambishi wakati uliopita *-li-*. Hivyo kitenzi kamili kilichodondoshwa kinakuwa hicho *Alikula.*

> 182. Aliwasha koroboi, akafunga mlango. Alijitazama. Goti
> la kushoto limekena, ngozi nje, damu zimesambaa. Alivuta
> pumzi ndani ili kuyakataza mafua yasitoke nje. Mkono wa
> kushoto ( ) koroboi, aliupeleka wa kulia ndani...
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 47)

Matini 182, kitenzi '*umesikia*' kimedondoshwa. Kinapatikana na kujaza pengo hilo kimuktadha. Tusomapo matini hii, tunafahamu kuwa kitenzi *-shika* ndicho kimedondoshwa. Sababu ni kuwa mkono wa mwanadamu hushika na umetajwa mwanzo wa sentensi ambayo kitenzi kimedondoshwa. Kawaida katika Kiswahili, nomino kiima lazima iwakilishwe na kiambishi nafsi cha kiima hicho. Hapa, nomino kiima ni Mkono na kiwakilishi chake ni *u-*, na kiambishi *–me-* ni cha wakati uliopo. Kwa hivyo kimuktadha ukijumuisha muundo wa Kiswahili ktinzi dondoshwa ni *umeshika.*

> 183. ...Zenabu aliingia chumbani kwake, akachukua akiba yake
> ya pesa. Huyoo! Alikimbia hadi Msufini. Hakuuliza, alifika,
> akafungua mlango wa taxi akakaa. "Upesi! Upesi dereva!"
> Dereva, kijana aliyekuwa kavaa dangrizi ya bluu, aliruka,
> akaingia ndani ya gari, "( 1 ) Wapi?"
> Zenabu alisema, "( 2 ) *Weekend Bar,* kata kushoto, Msikiti
> wa Ijumaa, kata kushoto, nyumba ya tatu."
> (*Watoto wa Maman'tilie* u.k 82-83)

Hatimaye katika matini 183, kitenzi '*Twende*' kimedondoshwa mara mbili, katika swali la dereva wa taxi kwa Zenabu na jibu la Zenabu. Vile vile vinapatikana kimuktadha

tukizingatia muundo wa Kiswahili. Msomaji au mnenaji Kiswahili atajua mapengo haya yanatokana na kudondoshwa kwa kitenzi *Twende*.

Vitenzi hivi katika matini 181, 182 na 183 havijatajwa popote katika matini lakini tunavirejelea kimuktadha na ufahamu wa lugha ya Kiswahili tunaposoma na kukamilisha maana. Kwa hivyo, huu pia ni udondoshaji unaochangia mshikamano katika matini kama asemavyo Allerton (1975:214);

> "Udondoshaji wa kimuktadha hudondoa kipashio ambacho kinaweza kurejelewa kutoka muktadha, ama kiisimu au kihali." (Tafsiri Tetu)

### 4.2.4 Udondoshaji wa Kishazi na Sentensi

Vishazi vilivyochunguzwa ni vishazi vikuu na vishazi tegemezi katika sentensi. Vishazi huru ambavyo pia ni sentensi sahili vimechunguzwa kama sentensi. Sentensi, kwa hivyo, imejumuisha sentensi sahili, changamano na ambatano katika tasnifu hii. Aidha udondoshaji wa mfululizo wa sentensi umechunguzwa chini ya sentensi vile vile. Udondoshaji wa kishazi ama kishazi kikuu au tegemezi umeonyeshwa pia.

Katika udondoshaji wa kishazi, sehemu kubwa ya kishazi huachwa nje ya matini (Salkie, 1995:59). Hii inamaanisha kuwa udondoshaji katika kishazi huwa wa sehemu tu, na ile sehemu nyingine hubakia katika matini. Kishazi hapa kinaweza kuwa sentensi kamili au tegemezi. Gunter (1963:143) anaeleza kuwa kuna aina mbili za udondoshaji wa sentensi;

a) Udondoshaji uliojiegemeza na uunganisho wa kisarufi miongoni mwa sentensi (matini) katika muktadha.

b) Udondoshaji ambao haujiegemezi kabisa na muktadha wa kiisimu.

Udondoshaji wa kimuktadha huegemea moja kwa moja sentensi iliyotangulia ili kuipanua sentensi dondoshwa. Utegemezi wa muktadha hujumuisha muungano au muambatano wa kisarufi kati ya sentensi dondoshwa na muktadha. Na udondoshaji ambao haujiegemezi na muktadha hujumuisha arafa fupi, mada kuu za magazeti, ishara, ilani na arifa zisizo rasmi. Udondoshaji uliopatikana katika matini zilizotumika katika tasnifu hii ni ule wa kisarufi katika muktadha.

Halliday (1985:300) anasema kuwa udondoshaji unaweza kuwa sehemu ya kishazi au kishazi chote. Katika udondoshaji wa kishazi, maneno yanayokosekana, hupatikana kutoka kwa vishazi (sentensi) vilivyotangulia, na athari yake ni kuleta mshikamano. Hii ina maana kuwa udondoshaji huchangia mshikamano wa matini. Tutalii udondoshaji huu katika mifano ifuatayo:

184. Mama alisema,"Msiwe mnacheza na kuchokoza mbwa, ala!"
"Hata mama ( )! Peter alisema, "Sisi tulikuwa tunapita tu,
Akaanza kutufukuza."
(*Watoto wa Maman'tile* u.k 6)

Hapa, Peter katika usemi wake amedondosha, "*hatukucheza na kuchokoza mbwa*". Hiki ni kishazi. Kwa hivyo udondoshaji wa kishazi umetokea. Kishazi hiki ni sentensi kamili.

185. Wiki ya pili sasa tangu Zita na Peter wafukuzwe shule.
Kila kukicha Mamantilie na Zita wanachukua sufuria,
maharagwe, unga na kuni hadi kiwanda cha Urafiki.
Hawarudi mpaka jioni, wamechoka, wananuka kutuzi la
moshi na vipesa vya kusukuma wiki. Lakini ( 1 ) ada ( 2 )?
( 3 ) Sare ( 4 )?
(*Watoto wa Maman'tile* u.k 14)

Katika matini hii vishazi '*pesa za*' (1 na 3) na '*ziko wapi?*' (2 na 4) vimedondoshwa na mapengo yake tunayajaza kwa kutumia muktadha wa sentensi dondoshwa katika matini.

Kishazi 'pesa za' ni sehemu ya kishazi au sentensi, hivyo kuwa tegemezi. Hakitoi maana kamili mpaka kitegemezwe na kile huru. Kishazi 'ziko wapi' ni kishazi ambacho ni huru, hivyo ni sentensi sahili. Kwa hivyo udondoshaji hapa ni ule wa kimuktadha.

186. "Hasemi kitu," Peter alijibu. "Ila mimi lazima nirudi shule."
"Na pesa!"
"Nina mipango yangu."
Musa alicheka, "Wewe ( )!"
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 17)

Hapa kishazi '...*Una mipango yako!*' kimedondoshwa. Kukamilisha maana na kupata mshikamano, lazima msomaji arejelee nyuma kishazi hicho kilikotajwa na kukitumia kulijaza pengo lililopo kwa kudhani. Kishazi hiki ni kishazi huru kwa hivyo ni sentensi sahili.

187. "Ee?"
Kimya.
"( 1 ) Mzigo wako?"
"Ndiyo (2)."
Zenabu alimkagua tena Peter akasema, "Ingia."
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 30)

Hapa 187, vishazi viwili vimedondoshwa, '*Huu ni*... 'na '*ni mzigo wangu*'. '*Huu ni...*' ni kishazi tegemezi, na '*ni mzigo wangu*' ni kishazi huru hivyo ni sentensi sahili. Pengo (1) tunalijaza kimuktadha na pengo (2) tunalijaza kwa kurejelea swali. Urejeleaji huu wa kipashio kutoka kwengineko katika matini ndio mshikamano. Kwa hivyo udondoshaji hapa una dhima ya kuleta mshikamano katika matini.

188. Ilikuwa saa 2.30 hivi za asubuhi. Nyumba haikuwa na mtu ila Peter... "Leo nitakwenda nijaribu ( )."
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 16)

Udondoshaji hapa ni wa sentensi moja inayopatikana katika u.k 9 wa matini. "...*Kesho nitakwenda Tabata nifanye upelelezi wangu.*" Kwa hivyo, ili kupata maana kamili, msomaji itambidi arejee katika u.k 9 wa matini na kupata sentensi hiyo, ailete katika pengo ( u.k 16) na kujaza pengo hilo kwa kudhani. Hata hivyo sentensi itabadili mpangilio wa maneno na kuwa, "Leo nitaenda nijaribu upelelezi wangu Tabata." Udondoshaji huu umeondoa urudufishaji wa kishazi tegemezi, 'upelelezi wangu Tabata'.

189. "Nini?"
"Mfyatuko mkubwa."
"( 1 ) Wa tairi?"
"Hapana, ( 2 ) risasi; nyuma karibu na mgunga!"
(*Musaleo!* u.k 6)

Vishazi vilivyodondolewa hapa ni '*Mfyatuko mkubwa...*' ( 1 ) na '*Mfyatuko mkubwa wa...*' ( 2 ). Vishazi hivi ni vishazi tegemezi na ni sehemu ya sentensi. Ni vishazi tegemezi kwa sababu havitoi maana kamili vikiwa pekee. Udondoshaji huu unaonyesha tabia ya lugha ya usemi halisi ambapo baadhi ya maneno hayatajwi katika majibu au maongezi ya wazungumzaji. Msikilizaji hurejea nyuma kuchukuwa neno au maneno yaliyodondoshwa na kujaza pengo lililopo ili kukamilisha maana. Hii huleta mshikamano katika matini kwa kuondoa urudiaji ma maneno yaliyotangulia katika sentensi fuatilizi.

190. "Unajuaje kuwa wamepotea? Inawezekana wamekwenda
mandhari tu. Mambo ya mapenzi huyajui wewe au kusema
wewe na mwenzio hamuendi mandhari."
"Siamini ( )!"
(*Musaleo!* u.k 43)

Katika matini hii kishazi tegemezi '...*kuwa wameenda mandhari!*' kimedondoshwa.

191. "Ndilo jina lake hilo hasa! Tena linasibu tu!"
"Umejuaje wewe ( )
(*Musaleo!* u.k 47)

Hapa vishazi kamili '*Ndilo jina lake hilo hasa!* na *Tena linasibu tu!*' vimedondoshwa na inabidi tuvirejelee kutoka nyuma kwenye sentensi tangulizi kukamilisha maana. Kwa hivyo hufaa kimuundo vishazi hivi visirejelewe katika sentensi fuatilizi kwani kufanya hivyo huleta urudufishaji unaoharibu muundo wa lugha na mshikamano katika matini.

> 192. "Je, uandishi wa riwaya huwa hivi kwa kawaida?'
> "La ( ). Nyingine ninazipa majina mimi, lakini hii imetwaa uwezo wa kujipa jina! Ni kisa kizuri cha Ukolongwe na Musaleo!"
> (*Musaleo!* u.k 11)

Hapa sentensi, "*Uandishi wa riwaya hauwi hivi kwa kawaida.*" imedondoshwa. Sentensi hii imetangulia kutajwa na tunairejelea nyuma kulijaza pengo lililopo. Hata hivyo urudufishaji wa sentensi hii dondoshwa, hauathiri mshikamano wa matini.

### 5.1.5 Udondoshaji wa Kiashiria, Kitenzi, Kimilikishi, Kiulizi na Kielezi

Kuna udondoshaji wa elementi mbalimbali za sentensi uliotokea katika matini mbili zilizochunguzwa. Elementi hizi ni kiashiria, kitenzi, kimilikishi, kiulizi na kielezi.

> 193. Kurwa aliuliza, "Nani ( 1 )?
> "( 2 )Baba," Peter alijibu. "Leo karudi mapema kidogo."
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 70)

Hapa kiashiria '*huyo*'$_1$ na '*Huyo*$_2$ + *ni*' (kitenzi ungio) vimedondoshwa. Tunavipata kwa kurejelea muktadha wa sentensi hizi katika matini hii 193. Viashiria hivi vinarejelea *Baba* na *ni* kina unganisha kiashiria *Huyo* na *Baba* na kuwa "*Huyo ni baba.*"

> 194. Walipomaliza kula, walipumzika, wakaongea kidogo, kisha wakagawana sehemu za kulala katika sebule ileile moja. Peter sehemu ( 1 ), Zita sehemu ( 2 ) na Kurwa naye sehemu yake.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 72)

Kimilikishi '*yake*' kimedondoshwa mara mbili (1) na (2), na kukirejelea inalazimu turejelee mbele katika matini hii kukipata kimilikishi hicho na kukijaza katika mapengo yaliyopo ili kupata maana kamili. Udondoshaji huu hapa ni muhimu kuondoa urudufishaji wa '*yake*' kwani kurudia rudia kimilikishi hicho kitafanya muundo wa lugha kusinya na mchakato wa Kiswahili na muundo wake hauwi hivyo.

195. "Inajiita Mzee!"
"Inajiita ( )?
(*Musaleo!*, u.k 10)

Hapa kiulizi '*nani*' kimedondoshwa, na kukirejelea inalazimu tuangalie muktadha wa sentensi iliyo na kipashio dondoshwa (nani) na ufahamu wa mchakato na muundo wa Kiswahili ili kujaza pengo lililopo na kukamilisha maana inayojitokeza.

196. "Bei ya nguo... Shati hili nimenunua kwao. Shilingi sitini..."
"( ) Sitini?"
(*Musaleo!*, u.k 64)

Kilichodondoshwa katika matini hii ni nomino "Shilingi" iliyo na uamilifu wa kielezi. Ni kielezi kwa sababu kinaeleza zaidi ya kitenzi 'nimenunua'. Kielezi hiki ni cha idadi, shilingi sitini.

197. *Na Ukolongwe naye alidhania kuwa watakuwa vi-**dukawallah** maisha yao yote. Lakini haikuwa* ( ).
(*Musaleo!* u.k. 37)

Hapa kionyeshi bainishi '*hivyo*' kimedondoshwa. Kiashiria hiki hakipo kabisa katika matini. Ili kukipata inabidi tutumie muktadha wa sentensi '*Na Ukolongwe naye alidhania kuwa watakuwa vi-dukawallah maisha yao yote*' na ufahamu mchakato na muundo wa Kiswahili na kujaza pengo lililoachwa kukamilisha maana. *hivyo* ni kiashiria katika 197.

### 5.1.6 Udondoshaji wa kiunganishi *na*

Katika matini kiunganishi *na* kinaweza kudondoshwa ikiwa vimefuatana kuunganisha vishazi kadha au nomino kadha. Hata hivyo, katika mshikamano, udondoshaji wa kiunganishi hiki hauchangii mshikamano huo. Hii ni kwa sababu kinachodondolewa ni kile kimetangulia kutajwa. Katika pengo hilo la udondoshaji, hubidi msomaji arejelee mbele ili kuunganisha maana iliyokusudiwa. Lakini udondoshaji uliojitokeza katika matini rejelewa ni ule wa kisarufi unaondoa urudufishaji. Viunganishi vilivyodondolewa ni vile tangulizi na kinachobaki ni kile fuatilizi:

> 198. Peter naye aliruka, akamzaba Doto makofi mawili mfululizo, lakini Doto alikuwa kazoea mapigano ya aina hii. Yeye na dada yake wamezaliwa vichochoroni, (1 ) wamekulia vichochoroni... Walikuwa chokora namba moja. Kupigana, (2 ) kulala na njaa, (3 ) kukamatwa na polisi, (4 ) kupigwa na baridi, (5 ) kuugua *na* kuponea chupuchupu, yote haya yalikuwa sehemu ya maisha yao katika jiji hili.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 22)

Katika matini hii tunaona udondoshaji wa kiunganishi *na* ambacho kilikuwa kiunganishe vishazi viwili vya mwanzo kama pengo (1) linavyoonyesha. Udondoshaji huu ni wa hiari. Iwapo kiunganishi *na* kingetumika, ungekuwa uunganishaji wa kuleta mshikamano wa dhana mbili katika vishazi hivyo. Vile vile kimedondoshwa na mshikamano bado upo. Kwa hivyo udondoshaji huu ni wa hiari. Katika mapengo (2-5) kuna udondoshaji wa *na* inayounganisha vitenzi. Ama kingetumika au kudondoshwa maana inabakia, na mshikamano vile vile unabakia. Urudufishaji wa *na* hauna madhara yoyote hapa. Kwa hivyo udondoshaji huu ni wa hiari pia.

## 5.2 Vikwazo katika Udondoshaji

Udondoshaji katika matini zilizochunguzwa kulitokea vikwazo katika matumizi yake kwa sababu ya muundo wa Kiswahili kuwa uambishaji wa kiambishi nafsi ni lazima. Tuchunguze vikwazo hivi:

199. Juma *a*likula chakula lakini *a*kaacha soda. Baadaye *a*kala matunda *a*liyoletewa na mamake.

Kiambishi *a-* hakiwezi kudondoshwa lakini katika Kiingereza, *a-* ikiwakilisha *he* inaweza kudondoshwa. Utafiti huu si linganishi, hata hivyo tumetumia mfano huu kufafanua hoja yetu. Kirejelea nafsi *a-* ni lazima katika matini hii kwenye vitenzi akaacha, akala na aliyoletewa ili kujenga mshikamano na kuleta usahihi wa sarufi.

Udondoshaji wa Kiima katika Kiswahili una utata kwa sababu kiambishi cha Kiima lazima kiweko katika kitenzi pindi Kiima kinapodondoshwa. Kwa hivyo kiambishi hicho kinakuwa Kiima. Hata hivyo Kiima Nomino lazima kiwe kimetangulia kutajwa katika matini:

200. Peter alimtupia macho msichana. ( 1 ) Alikuwa kava gauni lililopoteza rangi yake, chafu, ( 2 ) limechanika kifuani, ( 3 ) fupi, lililokataa kuyafunika magoti yake.
(*Watoto wa Maman'tilie* u.k 21)

Katika mfano huu, pengo (1) Kiima 'msichana' kimedondoshwa lakini kinawakilishwa na kiambishi *A-* katika kitenzi '*A*likuwa', na mapengo (2) na (3) Kiima 'gauni' kimedondoshwa lakini kimewakilishwa na kiambishi *li-* katika kitenzi '*li*mechanika'. Katika kivumishi 'fupi' hakuna kiwakilishi cha 'gauni' kwa sababu muundo wa Kiswahili hauruhusu kiambishi cha kiima 'gauni' katika kivumishi hiki. Kwa hivyo hapa hakuna udondoshaji pekee bali pia pana urejeleaji, yaani viambishi '*A-* na '*li-*' vinarejelea

Kiima Peter na gauni. Aidha ni uwakilishaji wa nomino unaoleta upatanisho wa kisarufi katika Kiswahili. Kwa hivyo tunapochunguza umbo la ndani kiima hakijadondoshwa, na katika umbo la nje ni ile nomino ndiyo imedondoshwa. Huu ni utata kwa sababu, kiima bado kipo kupitia kiwakilishi chake.

## 5.3 Hitimisho

Udondoshaji umejitokeza kwenye matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* kwa kiwango kikubwa. Umetumika kwa; i) kuleta mshikamano ii) kuondoa urudufishaji na iii) kama mtindo wa mwandishi. Udondoshaji umejitokeza zaidi katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* ambapo ule wa silabi umeongoza (mara 53), ukifuatwa na ule wa sentensi/kishazi (mara 25) na hamna udondoshaji wa Kiulizi, Kielezi na Kionyeshi (mara 0). Katika matini ya Musaleo! udondoshaji uliotokea zaidi ni ule wa Kitenzi (mara 22) ukifuatwa na ule wa NominoYambwa (mara 17) na hamna udondoshaji wa Kiashiria na Kimilikishi (mara 0).

Kwa jumla udondoshaji uliotawala katika matini zote mbili ni wa silabi, ambao umetokea mara hamsini na tisa (59) ukifuatwa na ule wa NominoK na NominoY mara hamsini na nane (58), ukifuatwa na wa Kishazi/Sentensi mara thalathini na sita (36), na ule wa Kitenzi uliojitokeza mara thalathini na tano (35). Udondoshaji wa kiulizi, kielezi na kionyeshi umetokea mara moja moja (1) katika matini zote mbili.

Kutokana na matokeo haya, tunaona kuwa kuna tofauti za utokeaji wa udondoshaji ilhali matini zote zimetumia Kiswahili. Hii ni sababu matini ya *Watoto wa Maman'tilie*

imetumia kauli halisi zaidi kuliko matini ya *Musaleo!* Kama tulivyoeleza hapo mwanzoni udondoshaji hutokea zaidi katika usemi halisi, na kwa vile ulitokea zaidi katika *Watoto wa Maman'tile* ndiyo kumekuwa na idadi hiyo kubwa zaidi ya udondoshaji. Aidha tumeona ingawaje udondoshaji hujenga mshikamano katika matini, pia tunakubaliana na Gunter (1963:150) kuwa udondoshaji huweza kuwa ni mtindo wa mwandishi. Matokeo ya matini hizi mbili yamedhihirisha hili, kuwa ni mtindo wa mwandishi.

Udondoshaji katika Kiswahili umedhihirisha vikwazo kadhaa. Katika baadhi ya vishazi hauwezekani kwa sababu ya muundo na mchakato wa Kiswahili wa uambishaji. Uambishaji ndio zaidi huleta usahihi wa sentensi na ni viambishi vya nafsi vitumike katika uundaji wa sentensi sahihi na yenye mshikamano.

# SURA YA SITA

## UUNGANISHAJI

### 6.0 Utangulizi

Sura hii imechunguza uunganishaji katika matini za *Watoto wa Mama N'tilie* na *Musaleo!*. Imeonyesha uunganishaji unavyoleta mshikamano katika matini. Aidha imechunguza na kuonyesha aina mbalimbali za uunganishaji na viuunganishi vilivyomo katika matini za *Watoto wa Mama N'tilie* na *Musaleo!*. Zaidi ya haya, imeonyesha ni aina gani ya uunganishaji na viunganishi vimetumika zaidi katika matini hizi mbili. Vikwazo vya uunganishaji kadha vilivyojitokeza katika matini hizi vimeangaziwa pia. Uunganishaji ulitokea katika matini zetu teule kama ifuatavyo:

| AINA YA UUNGANISHAJI | UTOKEAJI (100%) | | JUMLA YA IDADI % |
|---|---|---|---|
| | *Watoto wa Maman'tilie* | *Musaleo!* | |
| NYONGEZA | 23.17 | 37.75 | 60.92 |
| WAKATI | 5.86 | 13.74 | 19.60 |
| ELEZI | 5.86 | 10.95 | 16.81 |
| SABABISHI | 1.19 | 1.46 | 2.65 |

6.1 UTOKEAJI WA AINA YA UUNGANISHAJI KATIKA MATINI KWA ASILIMIA (100%)

Tukizingatia Jedwali 6.1, tunaona kuwa uunganishaji wa viunganishi nyongeza ndio uliotokea zaidi kwa asilimia sitini nukta tisa mbili (60.92%) ukifuatiwa na ule wa viunganishi wakati, asilimia kumi na tisa nukta sita sufuri (19.60%), viunganishi elezi, asilimia kumi na sita nukta nane moja (16.81%), na idadi ndogo zaidi ni viunganishi sababishi kwa asilimia mbili nukta sita tano (2.65%).

| AINA YA VIUNGANISHI | UTOKEAJI | | JUMLA YA UTOKEAJI |
|---|---|---|---|
| | *Watoto wa Maman'tilie* | *Musaleo!* | |
| NYONGEZA | 332 | 541 | 873 |
| WAKATI | 84 | 197 | 281 |
| ELEZI | 84 | 157 | 241 |
| SABABISHI | 16 | 21 | 37 |
| **JUMLA** | **516** | **916** | **1,432** |

6.2 MUHTASARI WA IDADI YA UTOKEAJI WA AINA YA VIUNGANISHI KATIKA MATINI ZA *Watoto wa Maman'tilie* NA *Musaleo*!

Katika Majedwali 6.1 na 6.2 tunaona kuwa aina ya viunganishi vinavyotumika zaidi ni viunganishi nyongeza. Idadi ya matumizi katika matini zote mbili ni mara mia nane na sabini na tatu (873) ambayo ni asilimia sitini na mbili nukta tatu moja (62.31%). Katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* idadi ni mara mia tatu na thalathini na mbili (332) ambayo ni asilimia ishirini na tatu nukta moja nane (23.18%) na katika matini ya *Musaleo!* idadi ni mara mia tano na arobaini na moja (541) ikiwa ni asilimia thalathini na

saba nukta saba nane (37.78%). Aina ya viunganishi inayofuata kwa idadi ya utokeaji ni viunganishi wakati vikiwa na idadi ya mara mia mbili na thamanini na moja (281) kwa jumla ikiwa ni asilimia kumi na tisa nukta sita mbili ( 19.62% ). Na katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* idadi yake ni mara thamanini na nne (84) ikiwa ni asilimia tano nukta nane saba (5.87%), na katika matini ya *Musaleo!* idadi ni mara mia moja tisini na saba (197) ikiwa ni asilimia kumi na tatu nukta saba sita (13.76%). Kisha aina inayofuata kwa idadi ni viunganishi elezi vilivyotokea mara mia mbili arobaini na moja (241) ikiwa ni asilimia kumi na saba nukta nane moja (16.81%) ambapo matini ya *Watoto wa Maman'tilie* ina idadi ya mara themanini na nne (84) ikiwa asilimia tano nukta nane saba (5.87% ), na matini ya *Musaleo!* ina idadi ya mara mia moja na hamsini na saba (157) ikiwa ni asilimia kumi na moja nukta sufuri ( 11.0%).

Aina iliyo na idadi ya chini kabisa ni viunganishi sababishi, idadi yake kwa jumla ni mara thelathini na saba (37) ikiwa ni asilimia mbili nukta tano sita (2.56%) ambapo matini ya *Watoto wa Maman'tilie* ina idadi ya kumi na sita (16) ikiwa ni asilimia moja nukta moja mbili (1.12%), na ile ya *Musaleo!* ina idadi ya mara ishirini na moja (21) ikiwa ni idadi ya asilimia moja nukta nne saba (1.47%).

| AINA | VIUNGANISHI | IDADI | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | | *Maman'tilie* | *Musaleo!* | |
| VIUNGANISHI NYONGEZA | Na | 298 | 502 | 800 |
| | Au/ama | 14 | 18 | 32 |
| | Pia | 8 | 5 | 13 |
| | Zaidi ya | 1 | 0 | 1 |
| | Wala | 6 | 5 | 11 |
| | Kando ya | 0 | 1 | 1 |
| | tena | 5 | 10 | 15 |
| VIUNGANISHI ELEZI | Lakini | 73 | 132 | 205 |
| | Ingawa/ingawaje | 0 | 18 | 18 |
| | Badala yake/bali | 8 | 10 | 18 |
| | Hata hivyo | 0 | 2 | 2 |
| | Vinginevyo | 0 | 0 | 0 |
| | Vyovyote | 0 | 0 | 0 |
| | Kwa minajili ya | 0 | 0 | 0 |
| | Japokuwa | 3 | 0 | 3 |
| VIUNGANISHI SABABISHI | Kwa sababu/ Kwa hivyo | 4 | 11 | 15 |
| | Hivyo | 3 | 5 | 8 |
| | Kutokana na | 9 | 0 | 9 |
| VIUNGANISHI WAKATI | Kisha | 34 | 60 | 94 |
| | Baada ya | 13 | 47 | 60 |
| | Baadaye | 9 | 23 | 32 |
| | Hatimaye | 14 | 44 | 58 |
| | Kabla (ya) | 5 | 13 | 18 |
| | Mara | 9 | 10 | 19 |
| | Awali | 0 | 0 | 0 |
| JUMLA | | **516** | **916** | **1432** |

## 6.3 UTOKEAJI WA VIUNGANISHI MAHUSUSI KATIKA MATINI ZA *Watoto wa Maman'tilie* NA *Musaleo!*

Jedwali 6.3, ni orodha ya viunganishi vyote vinavyoleta mshikamano katika matini. Tumeviweka viunganishi hivi kwa mujibu wa idadi ya utokeaji katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*. Katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie*, kiunganishi *Na* ndicho kimetumika zaidi, mara mia mbili na tisini na nane (298), kimefuatwa na kiunganishi *Lakini* kilichotumika mara sabini na tatu (73), na cha tatu ni kiunganishi *Kisha* kilichotumika mara thalathini na tatu (33). Viunganishi vilivyotumika kwa idadi ya chini zaidi katika matini hii ni *kabla (ya),* mara nne (4), *Kwa hivyo* mara tatu (3) na *Kutokana na, Kwa sababu*, *Ingawa* na *Hata hivyo* havikutumika kabisa.

Katika matini ya *Musaleo!*, kiunganishi *Na* kimetumika zaidi ya vyote, mara mia tano na mbili (502), kikifuatwa na kiunganishi *Lakini* kilichotumika mara mia moja na thalathini (130), na kiunganishi *Kisha* kilichotumika mara hamsini na nane (58). Viunganishi vilivyotumika kwa idadi ndogo zaidi ni *Kwa hivyo*, mara tatu (3) na *Hata hivyo*, mara mbili (2), *Wala* mara moja (1) na *Hivyo* hakikutumika kabisa.

Tunapochunguza matumizi haya, tunaona ya kuwa katika matini zote mbili kiunganishi *Na* ndicho kimetumika zaidi, kikifuatwa na *Lakini* na *Kisha.* Viunganishi vingine vimeonyesha idadi tofauti tofauti katika matini hizi. Aidha kuna viunganishi ambavyo vimetumika katika matini ya *Maman'tilie* lakini havikutumika katika matini ya *Musaleo!*, mfano, *Kutokana na*, *Kwa sababu*, na *Ingawa* havikutumika kabisa katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* ilhali katika matini ya *Musaleo!* kwa idadi ndogo; *Kutokana na* mara nne (4), *Kwa sababu* mara kumi na moja (11), *Ingawa* mara kumi na nane (18). Viunganishi *Wala*, na *Hivyo* havikutumika kabisa katika matini ya *Musaleo!* lakini

vimetumika katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie,* kiunganishi *Wala* kimetumika mara sita (6) na *Hivyo* kimetumika mara saba (7).

Kuna mkondo uliojitokeza unaonyesha viunganishi vinavyotumika zaidi katika Kiswahili na vile vinavyotumika kwa kiwango cha chini zaidi. Kwa jumla, ni kuwa matini ya *Musaleo!* imetumia viunganishi zaidi (mara 916) kuliko matini ya *Watoto wa Maman'tilie* (mara 516). Kulingana na uchunguzi huu, madai ya Salkie (1997:77) kuwa viunganishi vinavyotumika zaidi ni *kwa sababu* na *kwa hivyo* si kweli katika Kiswahili. Pengine ni hivyo katika lugha ya Kiingereza aliyoichunguza.

## 6.1 Uunganishaji na Aina zake Unavyotokeza katika Matini

Uunganishaji ni ile hali ya kuunganisha dhana au maana au elementi mbalimbali katika sentensi au matini kwa kutumia viunganishi. Viunganishi hivi huweza kuwa dhahiri na wakati mwingine vinaweza kutokuwa dhahiri katika sentensi zilizounganishwa. Uunganishaji husaidia wasomaji kufasili uhusiano kati ya vishazi (Hatch, 1992:225). Hivyo dhana katika vishazi, na vishazi vyenyewe pia huunganishwa kwa kutumia viunganishi mbalimbali. Kuna aina nne za uunganishaji kama tulivyoeleza katika 1.8.5 na Majedwali 6.1 na 6.3 Aina nne zote zilichunguzwa katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*. Hebu tuzichunguze uunganishaji ulivyojitokeza.

### 6.1.1 Uunganishaji Nyongeza

Huu ni uunganishaji unaoongeza habari juu ya nyingine na kuzifanya habari hizo kushikamana katika matini na kuleta mtiririko. Viunganishi *na, au/ama, zaidi ya, wala kando ya, tena* n.k. hutumika. Natuangalie jinsi vilivyotumika:

**6.1.1.1 Kiunganishi *Na***

*Na* ni kiunganishi kinachotumika zaidi katika kuleta mshikamano wa matini. Schiffrin (1985:128) anaeleza kuwa *Na* huunganisha matukio, vishazi, sababu na hushadidia wazo kwa mfano katika shairi. Vile vile hudokezea juu ya kipashio kinachofuata, huendeleza kitendo kwa kuonyesha msemaji ana mengine zaidi yakueleza na huunganisha maswali. Kwa jumla *Na* ina dhima mbili; kuunganisha vipashio vya mawazo katika matini na kuendeleza matendo ya msemaji. Dijk (1977:45) anasema *Na* pia huunganisha sentensi sahili na kuwa ambatano.

Halliday na Hassan (1976:244, 233) wanasema *Na* huunganisha mawazo au dhana mbalimbali na huunganisha sentensi kimuundo vile vile. Aidha huunganisha vipashio vya daraja moja, yaani sentensi na sentensi, nomino au virai nomino, vitenzi au virai vitenzi, vielezi au virai elezi, au virai husishi, pengine vishazi. Nao Quirk na Greenbaum (2000:257) wanasema *Na* hudhihirisha uhusiano kati ya maudhui ya vishazi. Hii ina maana kuwa maudhui huunganishwa na juu yake kuongezewa habari yale yaliyotangulia. Huonyesha tukio katika kishazi cha pili husababishwa na tukio la kishazi cha kwanza. *Na* inapotumika pamoja na *kisha* huonyesha mwendelezo katika matukio.

Katika tasnifu hii kilichozingatiwa ni uunganishaji wa dhana unaoleta mshikamano. Kwa hivyo unganishaji wa miundo hautazingatiwa bali utatajwa tu inapobidi kufafanua hoja zetu. Tuchunguze vile *na* inavyounganisha elementi mbalimbali kuleta mshikamano; kuunganisha vipashio vya mawazo, kuunganisha matendo au matukio na kuunganisha habari.

#### 6.1.1.1.1 Kuunganisha vipashio vya mawazo

*Na* huunganisha mawazo mbalimbali katika matini. Mawazo yanapounganishwa hushikamana na kuleta matinki. Wazo lililotangulia huunganishwa na lile linalofuata.Tuangalie mifano hii.

> 201. Magharibi jua lilionyesha rangi ya dhahabu nyekundu
> *na* Mamantilie alihisi baridi mwilini. Baridi ya huzuni ilimwingia
> moyoni, akifikiri juu ya elimu ya watoto wake.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 7)

Hapa kuna mawazo mawili yanayojitokeza; jua kuonyesha rangi ya dhahabu nyekundu kuashiria linatua na kumletea Mamantilie baridi. Kwa hivyo *na* imetumika kuunganisha dhana hizi mbili. Aidha tunapochunguza dhana hizi ni kuwa dhana ya 'Mamantilie kuhisi baridi' inatokana na 'kutua kwa jua'. Hivyo kuna uunganishaji wa mawazo unaoleta mshikamano.

> 202. WIMBO: *Mume wako sikumwita*
> *Kanisimamisha mwenyewe*
> *Kaiona dizaini na*
> *Hii shepu yenyewe.*
>
> *Mtaa wa Manzese*
> *Kuna mgome-mgome*
> *Na huo umbea wenu*
> *Shoga yangu mkome.*
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 16)

Katika mfano huu, tunapata dhana mbili zilizounganishwa. Kwanza ni 'mnenaji alisimamishwa na mume wa mwenyewe kutongozwa'. Watu wakamuona na kuanza kumsema. Aliposikia umbea huo, 'akawaomba wakome'. Dhana hizi zimeunganishwa kwa kutumia *na*. Dhana ya pili imedhania dhana ya kwanza. Hivyo tunapata mshikamano.

> 203. Upepo ulipiga kwa nguvu ajabu. Matawi ya mti yalikwaruza paa *na* kutoa sauti ya kukirihi masikio.
> (*Musaleo!*, u.k 1)

Hapa kuna dhana mbili pia, ile ya 'kukwaruzwa kwa paa' na ile ya 'kutoa sauti'. Hivyo dhana za 'kukwaruzwa kwa paa' na 'kutoa sauti' zimeunganishwa kwa kutumia kiunganishi *na*. Dhana ya pili inatokana na ya kwanza, hivyo kuongeza habari zaidi juu ya dhana iliyotangulia.

> 204. ...Inasemekana aliishi kule juu milimani alikokuwa akijitumbuiza na magoma yake makubwa ajabu. Uzeeni alijiona mkiwa *na* kuamua kuzaa watoto aliowaamuru nao wazaane.
> (*Musaleo!*, u.k. 5)

Katika 204, dhana ni mbili; 'ukiwa' na 'kuzaa'. Dhana hizi zimeunganishwa na kiunganishi *na*. Kwa sababu ya ukiwa wa uzeeni, mhusika aliamua kuzaa watoto. Hivyo dhana fuatilizi imetokana na dhana tangulizi. Uzee ukijumlishwa, na ukiwa ndio uliomfanya kuamua kuzaa.

Katika mifano hapo juu, dhana/mawazo yameunganishwa na *na,* na kuleta mshikamano. Dhana fuatilizi imetokana na dhana tangulizi, na hazikuachwa hivi bali kuunganishwa na kushikamana kidhana. Hivyo dhana hizi kuwa na mshikamano.

#### 6.1.1.1.2 Kuunganisha matendo au matukio

*Na* huunganisha matendo mbalimbali katika matini na kudhihirisha nyongeza ya habari. Nyongeza hii hufafanua habari zaidi ama kuonyesha matendo zaidi yaliyotendeka. Mifano ifuatayo inathibitisha hoja hii:

> 205. ...Lakini hayo hayakuwasumbua watoto wakati huu. Walijawa na furaha ya kurudi nyumbani. Walichina, wakakimbizana, wakacheka *na* kupigana vidali. (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 1)

Hapa kiunganishi *na* kimeunganisha vitendo vilivyotendwa mfululizo na watoto hao. Kiliunganisha vitendo walichina, wakakimbizana, wakacheka na kupigana vidali. Vitendo hivi vilifanywa kwa wakati mmoja mfululizo. Kwa hivyo na imetumika kuunganisha vitendo vyote na haikutumika hadi mwisho wa kitendo ili kuondoa urudufishaji. *na* kutumika kabla ya kitendo cha mwisho, kumeongeza habari ya watoto walivyofanya na kushikanisha kitendo cha mwisho na hivyo vilivyotangulia. Kushikanisha huku kumeleta mtiririko wa masimulizi na mshikamano katika matini hii.

206. ...Gari liliinuka nyuma *na* kumwaga mchele uliochanganyika na vumbi.

(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 25-26)

Katika 206, *na* imeunganisha vitendo vya 'kuinuka' na 'kumwaga'. Hivyo kuongezea habari zaidi ya yaliyofanyika. Kitendo cha pili kimetokana na kitendo cha kwanza. Dhana tangulizi 'kuinuka nyuma kwa gari' imedhaniwa na dhana fuatilizi 'kumwaga'. Kawaida lori linapoinuka nyuma, humwaga kilichomo.

207. ...Niliinuka nilikokuwa *na* kuelekea dirishani, nikajinyoosha *na* kuyaelekeza macho kule mbele.

(*Musaleo!*, u.k 1)

208. Nilijikohoza *na* kusogea mbele. Nilipinda *na* kutokezea huko mbele. Sikumuona mtu.

(*Musaleo!*, u.k 6)

Katika 207, *na* imeunganisha vitendo 'inuka' + 'kuelekea'; 'kujinyoosha' + 'kuyaelekeza'. Hii inaonyesha vile msimulizi alivyofanya kitendo kimoja kikifuatwa na kingine katika utaratibu unaoleta maana. Uunganishaji huu umeleta mshikamano. Katika 208, *na* imeunganisha vitendo 'kujikohoza' + 'kusogea mbele'; 'pinda' + 'kutokezea'. Uunganishi huu ni nyongeza ya habari katika matini, habari moja ikiongezwa juu ya

nyingine. Baada ya kujikohoza, msimulizi aliendа mbele. Kitendo cha kwanza kimeunganishwa na cha pili kwa kutumia *na*. Kisha kitendo pinda kikaunganishwa na kitendo kutokezea. Vitendo hivi viliunganishwa na kuleta mtiririko, hivyo kujenga mshikamano katika matini hii.

#### 6.1.1.1.3 Kuunganisha habari

*Na* vile vile hutumika kuunganisha habari mbalimbali zilizopo katika matini. Inapounganisha habari hizo pia huwa inaongeza habari mpya kwa ile habari asilia. Kufanya hivi ni kuongezea na kushikanisha habari hizo na kuleta mshikamano wa hali hizo:

> 209. Katika uchochoro, karibu na kituo cha Msufini, alitokezea mbwa…Watoto walitembea katika vikundi vidogovidogo vilivyopungua kwa vidali na kwa heri ya kuonana. Sasa walikaribia sokoni. *Na* ghafla yule mbwa mweusi alisimama, akaunguruma.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 1-2)

*Na* imeunganisha habari zinazosimuliwa; habari juu ya watoto na juu ya mbwa. Sentensi fuatilizi ya '*Na* ghafla yule mbwa mweusi…' inadhania ile ya kwanza kabisa katika 184. Pia inaongezea habari zaidi juu ya alichofanya yule mbwa alipowaona wale watoto.

> 210. …Alikuwa jamaa aliyetimkwa na nywele *na* aliyevalia suruali ya kaki na fulana iliyoishia shingoni. Viatu vilikuwa vya makubadhi. Hii ilikuwa mara ya kwanza kukutana naye uso kwa uso *na* kusema kweli sikumtarajia awe hivi.
>
> (*Musaleo!*, u.k 10)

Vile vile katika 210, *na* imeunganisha habari juu ya mtu anayetajwa na anayesimulia. Habari hizi zimeshikanishwa vyema na kuleta mshikamano huku habari kadhaa kuongezwa juu ya mtu mtajwa alivyovaa na kukutana na msimulizi wa taarifa hii. Habari

nyongeza iliyoongezwa juu ya msimulizi ni 'kule kutomtarajia aliyemuona kuwa hali hiyo'. Habari hii imeongezwa kwa kutumia *na*.

Kwa hivyo *na* huunganisha mawazo, vitendo, matukio na habari katika matini. Mambo haya huunganishwa ili habari iwe na mtiririko, mantiki na mshikamano. Habari moja huongezewa habari zaidi juu, na wakati huo huo zikidhaniana. Habari fuatilizi ikidhania ile tangulizi na kuendeleza habari zaidi. Hii inadhihirisha kuwa *na* ni kiunganishi muhimu sana katika matini ili kuleta mshikamano wa dhana tofauti tofauti.

#### 6.1.1.2 Kiunganishi *Au*

*Au* ni kiunganishi kimojwapo kinachoongezea habari zaidi katika matini. Huunganisha zaidi ya vishazi viwili. Vishazi hivi huwa na mawazo mawili, mojawapo ndilo linatakikana litimizwe (Quirk na Greenbaum, 2000:256-7). Maana ya msingi ya *au* ni 'chaguo'. Hutoa nafasi ya kuchagua chaguzi fulani. Hujikita zaidi katika maswali, maombi, ruhusa na utabiri. *Au* inapotumika katika taarifa huchukua mantiki ya fasili-badala, yaani hutoa fasili mbalimbali. Pia *au* huonyesha msisitizo (Halliday na Hassan, 1976:246-7). Hivyo *au* huonyesha nyongeza ya mawazo au habari fulani katika matini au usemi.

*Au* pia hutumika kama kitambulisho cha chaguo katika matini au usemi. Humpa mhusika chaguo la kukubali dhana moja au nyingine au zote mbili (Schiffrin, 1987:177). Dhana hizi huwa katika muktadha fulani. Hivyo *au* hushikanisha dhana katika matini na kuleta mshikamano. Katika Kiswahili kisawe cha neno *au* ni *ama*. Ni maneno yanayoonyesha

chaguo. Mifano ifuatayo inaonyesha *au/ama* inavyotumika katika Kiswahili kama kiunganishi nyongeza na kuleta mshikamano.

> 211. Wakati huo Kisutu ilikuwa sehemu ya watu wa hali ya chini sana katikati ya jiji. Vibanda vyake vya ukuta wa mbavu za mbwa viliezekwa madebe ya kutu yaliyochakaa. Madebe $au_1$ mabati haya yalishikizwa kwa misumari $au_2$ kukandamizwa kwa mawe $au_3$ magogo ya miti ili yasipeperushwe kwa upepo.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 36)

Matini hii ina kiunganishi *au* kinachotokea mara tatu. $Au_1$ inaunganisha nomino mbili; madebe + mabati. Inatuonyesha kuwa madebe pia huitwa mabati. *Au* hii haileti mshikamano, imetumika kama kiunganishi kisarufi. $Au_2$ na $au_3$ zinaelezea chaguo. Zinatueleza kuwa katika baadhi ya vibanda, mabati yalishikanishwa kwa misumari na miongoni mwa baadhi, mawe yalitumika kukandamiza mabati hayo na katika vibanda vingine, magogo ya miti yalitumika. Hivyo kuna uunganishi wa chaguo hizo kama habari nyongeza. Habari iliyoongezwa kwa ile ya kwanza ya 'mabati kushikanishwa' ni 'kukandamizwa kwa mawe' na 'magongo ya miti'. Matumizi ya $au_1$ na $au_3$ yameleta mshikamano katika matini.

> 212. Kurwa alikuwa mwenye furaha. Mamantilie mara moja aligundua mtoto yule alikuwa mwenye nguvu na bidii ya kazi. Mara kwa mara ungemsikia Kurwa akisema, "Mama wacha hivyo vyombo, nitaviosha mimi," *au* "Mama nipe nguo zako nikufulie." *Au* "Vipi mama? Una homa?'
> ( *Watoto wa Maman'tilie*, u.k.76)

*Au* katika matini hii imetoa chaguo za vitendo vya Kurwa angetaka afanye. Alitaka kumsaidia mama yake katika mambo mbalimbali. Hivyo, vitendo hivi vikaunganishwa kwa kutumia *au* kama chaguo. Habari nyongeza hapa imetolewa mbali na lile chaguo la kwanza 'kuosha vyombo'.

> 213. ...Watumishi wengine walionekana wakisukuma matroli ya machela ya wagonjwa waliozidiwa, wakipelekwa thieta wakapasuliwe, *ama* mochware, wakapumzike jumla.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 89)

*Ama* katika matini hii imetumika kama *au*. Hivyo imetueleza sehemu mbili chaguzi, 'waliobebwa katika matroli wakipelekwa thieta' na wengine 'wakipelekwa mochware' kutegemea hali ya wagonjwa hawa. Hali aliyo nayo mgonjwa ndiyo humchagulia pa kupelekwa, theta au mochware. Chaguo hizi zimeunganishwa, na lile chaguo la pili, mochware ni habari nyongeza ya wanakopelekwa wagonjwa waliofariki. *Ama* vile vile hutumika kuonyesha chaguo mbadala. Inapotumika hivi, huwa kiunganishi cha kisarufi tu kisicholeta mshikamano.

> 214. *Landrover* ama karandinga ilisogezwa na wale 'majambazi sugu' watatu wakatumbukizwa ndani.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 98)

*Ama* hapa imetumika kama chaguo la neno mbadala lenye maana sawa na neno tangulizi. Kwa hivyo halichangii mshikamano wa matini bali linatoa chaguzi *Landrover* na karandinga.

> 215. *Uwezekano uliokuwako ni kuwa msingi muhimu wa kuwako kwangu utaanza kudadisiwa. Isitoshe, watu wataishia kuniona mwenzao mno kiasi cha kunichezea au kunijenga kiota kama alivyosema mshairi wangu wa zamani.*
> (*Musaleo!*, u.k 91)

Katika 215 au imetumika kuonyesha chaguo. Watu wanaotajwa katika matini watachagua moja kati ya 'kumchezea' na 'kumjenga' msemaji. Hivyo kuna nyongeza ya habari katika lile chaguo la pili. Chaguo hizi zimeunganishwa kwa kutumia *au* na kuleta mshikamano wa habari katika matini.

> 216. ...Uvumi unatawala mahali ambako taarifa hazitolewi hivi hivi. Magazeti nayo yalifuata mkondo huo. Yaelekea hayana mengi ya kusema *au* yameamua kusema kwa kubania mengine kama jamii yenyewe ilivyo.
>
> (*Musaleo!*, u.k 101)

Tunapochunguza matini hii, *au* imetumika kueleza chaguo zinazofanywa na magazeti kuongezea habari zaidi ya yale yanayofanyika. Magazeti yanaeleza machache tu kwa sababu hakuna ya kueleza, ama yapo mengi ya kueleza lakini yameamua kutoa habari chache. Hivyo habari zaidi juu ya magazeti yanavyotoa taarifa zimetolewa. Hii ni nyongeza ya habari. Habari hizi zimeunganishwa kwa kutumia *au.*

#### 6.1.1.3 Kiunganishi *Pia/Tena*

Kiunganishi *pia* hutambulisha habari ngeni au kuashiria kuwa matini ifuatayo itaelezea yale yaliyotangulia kwa kutumia njia tofauti (Salkie, 1997:77). Nao Quirk na Greenbaum (2000:289) wanaeleza kuwa *pia* huonyesha kutilia mkazo jambo linalotajwa au tendo linalofanyika. Katika Kiswahili kisawe cha *pia* ni *tena* kutegemea muktadha wa matumizi. Kwa hivyo, katika tasnifu hii kiunganishi *tena,* kimetumika kuwa na maana ya *pia*, na ilipotokea hivyo kimejadiliwa kama kiunganishi nyongeza sawa na *pia*. Aidha kinaweza kutumika kama '*na*'.Tuchunguze mifano ifuatayo.

> 217. ...Peter alijaribu kuendelea na hadithi yake lakini wapi? Alikifunga kitabu, akaamua kujilaza... Akabaki kuwaza. Aliwaza nini? Aliwaza juu ya kufukuzwa shule, juu ya ada na pesa za sare. *Pia,* Peter aliwaza jinsi atakavyoifanya biashara ya mama yake iwe kubwa, ilete faida.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 9)

Hapa 217, *pia* inaongeza na kuunganisha habari. Mbali na Peter kuwaza juu ya shule, aliwaza na biashara ya mama yake. Hivyo *pia* imeunganisha mawazo. Vile vile

imeongeza wazo jipya kwa wazo la kwanza. Wazo jipya ni 'atakavyoifanya biashara ya mama yake iwe kubwa, ilete faida'.

> 218. ...Sasa nilikuwa na furaha sio tu kwa kutambua kuna mtu aliyekuwa na mawazo sawa nami bali *pia* kwa sababu ya aliyoyafanya baadaye.
> (*Musaleo!*, u.k 10)

Vile vile katika mfano huu, *pia* imetumika kuongezea habari juu ya ile iliyotangulia ya 'sababu ya kuwa na furaha' na sababu nyingine ya 'aliyoyafanya baadaye' na 'kumfurahisha msimulizi'. Kama tulivyotangulia kusema, *tena* inaweza kutumika kama *pia*. Kimsingi huwa na maana ya 'mara ya pili'. Lakini katika baadhi ya miktadha, huwa na maana ya '*pia*'.

> 219. ...Hapana! Si hivi: kulikuwa na kitu, kulikuwa na mengi, *tena* machungu.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 73)

Katika mfano huu, *tena* imetumika kama kiunganishi nyongeza. Imeongezea habari zaidi juu ya mambo yaliyotendeka awali. Habari hii zaidi ni kuwa mambo hayo yalikuwa machungu. Kuongezea habari pia kumeleta uunganishi wa habari tangulizi na ile fuatilizi.

> 220. ...Hiki ni kisiwa cha amani. Unasikia bwana, kisiwa; *tena* cha amani katika bahari yenye machafuko ya kila aina!
> (*Musaleo!*, u.k 3)

Hapa, *tena* imetumika kama kiunganishi nyongeza. Kinaongeza habari kuhusu 'kisiwa cha amani' kilichotajwa. Kando na kuwa kisiwa cha amani, pia kina sifa ya kuwa hicho pekee ndicho chenye amani miongoni mwa vingi ambavyo vina machafuko ya kila aina. Hivyo, habari hii imeongezwa kwa kutumia *tena*. Licha ya kuongeza habari, imetumika kusisitiza amani iliyopo katika kisiwa hicho pekee kinyume na visiwa vingine vilivyosheheni machafuko mengi.

Kama nilivyotangulia kusema (**6.1.1.3**), muktadha unaweza kufanya *tena* kuwa na maana nyingine mbali na ile yake ya msingi. Katika mfano ufuatao, muktadha umeifanya *tena* kuwa na maana ya '*na*' (kiunganishi). Imeunganisha dhana mbili, 'kuandika' na sifa ya uzuri. Tuchunguze mfano huu:

> 221. "Siandiki? Naandika sana. *Tena* mara hii riwaya ya kisawasawa itakayojisoma yenyewe...
>
> (*Musaleo!*, u.k 10)

Hapa *Tena* imetumika kama *na*. Kwa hivyo *tena* inaweza kubadilishwa na kiunganishi *na* na maana na uamilifu ukabaki vile vile. Matumizi ya *tena* hapa ni ya kuongezea habari mpya juu ya ile ya awali na kuzishikanisha habari hizo kuwa moja. Habari katika sentensi ya pili inafafanua na kuongezea habari nyingine.

**6.1.1.4 Kiunganishi *Wala***

*Wala* ni kikanushi katika uunganishi nyongeza. Huonyesha dhana ya '*la*'. Huonyesha kukataa katika sehemu zote za vishazi vilivyounganishwa kwa kutumia *wala* (Halliday na Hassan, 1976:245). Viunganishi nyongeza huonyesha wazi kwamba sehemu ya sentensi ni nyongeza kwa yale yaliyotangulia kutajwa au kuelezwa na kudhaniwa. Matumizi ya *wala* huhitaji kwamba sentensi zinazounganishwa ziwe katika hali ya kukanusha au ziwe sentensi kanushi (Quirk na Greenbaum, 2000:289). Tuchunguze mifano hii:

> 222. Zita alisema, "Mwalimu Mkuu amesema wote ambao hawana nguo za shule *wala* hawajalipa ada asiwaone shuleni tena."
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 6)

> 223. Ilikuwa Mei Mosi siku ya sherehe ya Sikukuu ya Wafanyakazi, huku wanaiita kwa kifupi Leba Dei. Anima hakuenda kazini *wala* hakuandamana na wafanyikazi wenyewe kwenda kusikiliza hotuba... Hakuweza wala asingeweza.
>
> (*Musaleo!*, u.k 78)

Katika mifano hii 222 na 223, *wala* imeunganisha sentensi mbili ambazo zote ni kanushi. Habari zote zinazojitokeza zimekanushwa. Hivyo imeunganisha na kuongeza habari zilizokanushwa. Vionyeshi vya ukanushi ni '*ha-*' na '*si-*' katika vitenzi 'hawajalipa'(222), 'hakuweza' (223) na 'asiwaone'(222), 'asingeweza' (223). Sharti linalojitokeza hapa ni kuwa *wala* inapotumika kuunganisha vishazi au sentensi lazima vitenzi hivi katika vishazi hivyo kuwa kanushi au kitenzi katika kishazi/sentensi fuatilizi lazima kiwe kitenzi-nomino.

Viunganishi vingine vilivyoorodheshwa mwanzoni mwa sura hii, kama viunganishi nyongeza, havikupatikana katika matini zilizochunguzwa, mfano *zidi ya hayo, fauka ya hayo, kwa kuongezea, kwa maneno mengine.*

### 6.1.2 Uunganishaji Elezi

Uunganishaji huu hutokea wakayi viunganishi vifuatavyo vimetumika kuunganisha mawazo au dhana au maaana katika matini; *lakini, ingawaje, ingawa, bado, hata hivyo, badala yake, vinginevyo, kwa vyovyote, kwa minajili ya.* Sasa tuangalie baadhi ya viunganishi hivi jinsi vinavyotumika katika matini teule kwani si vyote vilivyotumika. Sasa tuangalie baadhi ya viunganishi hivi jinsi vinavyotumika katika matini za Kiswahili.

#### *6.1.2.1 Kiunganishi* Lakini

Kwa mujibu wa Keith na Miller (1991:148-9) *lakini* ni kiunganishi cha mshikamano kinachounganisha sentensi mbili zilizo katika daraja moja, na sentensi hizi zinajitegemea kisarufi. Vile vile wanadai kuwa sentensi hizi unganishi zinaongozwa na sheria za kimantiki wala si sheria za kisarufi. Maelezo haya yanatudhihirishia kuwa uunganishi unaojitokeza ni mara mbili, wa kimuundo na wa kimaana/mawazo. Kwa vile tasnifu hii

inashughulikia mshikamano, uunganishi utakaozingatiwa ni ule wa maana unaoleta mshikamano katika matini.

*Lakini* ni kiunganishi kinachoweza kutokea mwanzoni mwa sentensi na huwa kinaunganisha maana au habari kutoka sentensi tangulizi na ile fuatilizi. Huunganisha tu vishazi viwili na haiwezi kutumika pamoja na kiunganishi kingine, mfano **lakini kwa hivyo*, **lakini na*. Hudhihirisha mlinganuo katika matumizi yake (Quirk na Greenbaum, 2000:256,259). Schriffin (1987:153) anadai kwamba *lakini* haiwezi kuunganisha vipashio viwili isipokuwa pawe pana uhusiano wa mlinganuo katika dhana au muktadha mtagusano. Uhusiano huu hupatikana katika muktadha wa kisemantiki wa dhana dhaniwa. Kwa hivyo *lakini* ni kiunganishi kinachounganisha sentensi na maana, kikielezea zaidi maana hizi kwa njia ya mlinganuo na kuleta mshikamano katika matini. Tuchunguze mifano hii.

> 224. Peter hakuitikia. Alikuwa bado kashangazwa na mabadiliko ya Musa, Musa yule wa miaka 10 au 12 tu! *Lakini* tazama. Aliongea na kufanya mambo kama mtu mzima.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 18)

Hapa pana mlinganuo ulioletwa na kiunganishi *lakini*. Kinalinganua umri wa Peter na mambo ayafanyayo. Mambo haya hayapaswi kufanywa na mtu wa umri wa Peter, yanastahili mtu mwenye umri mkubwa. Umri wa Peter uko kinyume na matendo yake. Kwa hivyo, kwa ajili ya kuunganisha dhana hizi mbili, *lakini* imetumika. Imelinganua na kuongezea habari kwa umri wa Peter.

> 225. …Walipofika sehemu hii walianzisha vibiashara vidogo. Wakawa wanaitwa ***dukawallah*** tu. Na Ukolongwe naye alidhania kuwa watakuwa ***vi-dukawallah*** maisha yao yote. *Lakini* haikuwa. Biashara zao zilikua sasa na hata wengine kuthubutu kutaka

kununua ardhi...

(*Musaleo!* u.k 37)

Katika 225, *lakini* imeunganisha dhana mbili; biashara ndogo na kuwa zitabakia milele + kule kupanuka kwa biashara hizo. Dhana ya pili inaenda kinyume na dhana ya kwanza (alivyodhani Ukolongwe). Ukolongwe alidhani biashara hizo hazingepanuka lakini zikapanuka sana. Hiki ni kinyume cha dhana ya Ukolongwe. Kiunganishi *lakini* huonyesha kinyume cha matarajio. Vile inavyotarajiwa kutokea sivyo bali kinyume chake. Matini 224 na 225 zinadhihirisha hili.

226. Aliniangalia kwa muda. Lazima alitambua kukanganyika nilikokuwa nako. Aliendelea, "Hata inajikosoa yenyewe!" Kwa kweli sikumwelewa *lakini* sikutaka kuonekana mbumbumbu kwa hivyo nilitikisa kichwa mara kadhaa kama mbunge wa kwetu ambaye sasa alikuwa waziri. Hana ufahamu mpana wa mambo *lakini* wataalam wanapoanza kuongea huwa wa kwanza kuitikia kwa kichwa kama mjusi kafiri asiachwe nyuma katika welewa wa maelekeo ya matukio.

(*Musaleo!* u.k 11)

Katika 226 kinyume cha maana kinajitokeza. Kwanza msikilizaji hakuelewa na hakutaka kuonyesha kuwa hakuelewa, akaendelea kujifanya ameelewa. Pili, waziri hana ufahamu wa mambo na anajionyesha anao ufahamu huo. Kwa hivyo uunganishaji wa dhana mbili hizi umetokea ukidhihirisha kinyume cha matarajio. Aidha kuleta mshikamano katika matini.

227. ...Baba yao, mzee Lomolomo, alikuwa hajawalipia ada wala kuwanunulia sare. *Lakini* hayo hayakuwasumbua watoto wakati huu.

(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 1)

*Lakini* katika matini hii, imeunganisha dhana mbili zilizo kinyume. Sentensi ya kwanza inatoa dhana ya kutofanyika kwa jambo ambalo ni kulipa ada. Kwa kawaida watoto hawa wangeingiwa na wasiwasi kwa sababu ya jambo hili kwani wangefukuzwa shuleni.

Sentensi ya pili inatueleza watoto hao hawakujali hilo. Hiki ni kinyume. Kwa hivyo dhana mbili zimeunganishwa kwa kutumia *lakini* na kuleta mshikamano. Huu ni uunganishi elezi.

**6.1.2.2 Viunganishi *Ingawa/Ingawaje/ Japo/ Japokuwa***

*Ingawa* na *ingawaje* ina maana ile ile moja. Ni kiunganishi elezi. Huonyesha ukubalifu baada ya mlinganuo (Mohammed, 2001:237). Huunganisha vishazi viwili. Kiunganishi hiki kinapotumika huzaa tungo tegemezi. Hudhihirisha kinyume cha matarajio (Halliday na Hassan, 1976:252; Quirk na Greenbaum, 2000:252,254). Kinaweza kutumika kwa kuanza sentensi au kuwa katikati ya sentensi.

*Japo* na *Japokuwa* ni viunganishi vyenye maana moja. Viunganishi yote vinne katika Kiswahili vina dhana ile ile moja na vinafanya kazi sawa ya kulinganua. Kwa hivyo tumevijadili pamoja kwa sababu ya maana zao na uamilifu wao. Tuchunguze viunganishi hivi katika matini ya *Musaleo!* Katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* viunganishi *Ingawa / Ingawaje* havikutumika.

228. Nilipofika lile lango nilisimama na kuangalia upande wa ndani. Sikuweza kumwona mtu yeyote *ingawa* nilihisi kuwa walikuwako watu.

(*Musaleo!* u.k 46)

229. Kingunge alipouvuta mlango wa nyumba alishangaa. Alikuwako Kitungule na Anima; nyuso zao zilikuwa zinameremeta ishara ya jasho lililokaukiana. *Ingawa* ilikuwa mara ya kwanza kumwona hakuhitaji kuelezwa alikuwa nani.

(*Musaleo!* u.k 56)

Katika 228, kiunganishi *ingawa* kiko katikati ya sentensi. Kinaonyesha uunganishi wa dhana mbili ambapo kuna kinyume cha matarajio. Msimulizi alidhani atawapata watu

ndani ya nyumba lakini hawakuwaona. Hapa kuna kinyume cha matarajio yake. Na 229, *Ingawa* imeanza katika sentensi fuatilizi. Inaunganisha dhana mbili; aliona mtu kwa mara ya kwanza + alijua ni nani. Hapa vile vile (228), pana kinyume cha matarajio, yaani kumwona mtu kwa mara ya kwanza na hata bila ya kujulishwa ni nani, alimjua ni nani, ama alijua jina na sifa zake. Kawaida ya maisha, mtu hawezi kumjua mwingine bila ya kujulishwa. Lakini Kingunge alimjua mtu ni nani bila kujulishwa. Kwa hivyo kiunganishi *ingawa* kimeunganisha dhana hizo mbili na kuleta mantiki na mshikamano katika matini.

Kiunganishi *Japo* na *Japokuwa* hulinganua habari. Huonyesha kinyume cha matarajio. Sehemu mbili za sentensi au dhana mbili zinazounganishwa hukinzana kimaana. Sehemu moja huonyesha kinyume cha matarajio.

> 230. *Japokuwa* ilikuwa saa nne tu asubuhi, *lakini* tayari jaa lilikuwa limejaa watafuta riziki.
> (*Watoto wa Maman'tilie,* u.k. 49)

Katika matini hii, kiunganishi *Japokuwa* kimeunganisha dhana mbili ambazo zinakinzana. Dhana ya 'kuwa saa nne tu' ni kwamba ni asubuhi bado na hatutarajii watu wawe pale jaani. Lakini kinyume ni kuwa 'kumejaa watu tayari wakitafuta riziki'. Tunapochunguza zaidi tunagundua kuwa katika matini hii, kiunganishi *lakini* kimetumika pamoja na *Japokuwa*. Katika Kiswahili tukio hili ni sahihi na linakubalika kisarufi. Katika u.k 61 tukio hili linapatikana.

> 231. Harakaharaka Peter alileta maji ya baridi sana toka mtungini. Aliyasafisha madonda ya Kurwa. *Japo* ulikuwa uchungu mkumbwa, *lakini* Kurwa hakulia, hakufurukuta. Aliuma meno, akakaa kimya.
> (*Watoto wa Maman'tilie,* u.k. 61)

Hapa vile vile kunaonyesha ukinzani wa dhana au mawazo, na *Japo* na *lakini* vimetumika kwa pamoja. Bado sarufi hapa ni sahihi.

### 6.1.2.3 Viunganishi *Badala ya…/Bali*

Katika Kiswahili maneno *badala ya/yake* na *bali* yana maana au dhana moja. Huunganisha dhana mbili zilizo chaguo na hubidi kuteuwa moja kati ya hizo. Pia huonyesha mlinganuo (Quirk na Greenbaum, 2000:292). Tuchunguze matini hizi:

> 232. …Zenabu alimmiminia chai ya rangi kwenye kikombe cha plastiki. "Haya kunywa!" Peter hakuichukua chai ile mara. Badala yake alikausha mikono yake kwenye kaptura.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 15)
>
> 233. "Mnaona jahazi lile?" alisema profesa akituelekeza majini. Badala ya kuangalia majini nilijikuta nikimgeukia yeye.
> (*Musaleo!* u.k 95)

Katika 232 na 233 viunganishi *badala yake* na *badala ya* vimetokea mwanzoni mwa sentensi. Pia vinaweza kuwa katikati ya sentensi. Hapa vimeunganisha dhana mbili ambazo ni chaguo na linganuo. Vile vile vinaonyesha kufanya jambo tofauti na dhana tangulizi. Katika matini hizi wahusika wamechagua chaguo moja na kutenda kinyume cha muktadha wa dhana tangulizi. Katika 232, Peter alitarajiwa anywe chai hiyo mara anapopewa lakini hakufanya hivyo. Alikausha mikono yake. Na katika 233, msimulizi hakuangalia majini alivyotarajiwa, ila aligeuka na kumwangalia profesa (mtoaji amri). Kwa hivyo wahusika walichagua kitendo kingine kinyume na matarajio ya muktadha wa dhana. Viunganishi hivi vimeunganisha vitendo au dhana mbili na kuleta mantiki na mshikamano pia. (Dondoo liko katika *italiki* kama lilivyo katika matini asili.)

> 234. …*Inadaiwa kuwa kuna jamaa mmoja wa Ukolongwe aliyesema kwa sauti ya juu. "Kwa njia hii tutapunguza uzembe na uovu wa jamaa wa huku kwa sababu watakuwa na kazi ya kufanya badala ya kujizungukia majiani tu."*

(*Musaleo!* u.k 28)

Katika matini 234, *badala ya* iko katikati ya sentensi ikiunganisha dhana mbili; kuwa na kazi ya kufanya + kujizuungukia ovyo. Dhana hizi zimejitokeza kama chaguo na zimeunganishwa. Hivyo wahusika watachagua dhana moja. Uunganishaji huu umeleta mantiki na mshikamano katika matini hii:

> 235. Asubuhi, siku iliyofuata Zita alibaki nyumbani. Peter aliondoka akaelekea jaa la Tabata. Hakufuata barabara, *bali* alichukua njia ya mkato.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 49)

Katika 235 kiunganishi *bali* kimetumika kuunganisha dhana-chaguo mbili; kufuata barabara + njia ya mkato. Peter aliamua kufuata ile njia ya mkato, hakutumia barabara. Viunganishi hivi vyote vilivyotumika katika 207-210 ni elezi ambavyo Salkie (1995) ameviita pinzani, na vimeunganisha dhana mbili na kuleta mshikamano katika matini.

**6.1.2.4 Kiunganishi *Hata hivyo***

Halliday na Hassan (1976:252) wanadai kuwa kiunganishi *hata hivyo* kina mlinganuo fulani ndani mwake na huonyesha msisitizo. Huunganisha dhana mbili na kusisitiza:

> 236. Kwa bahati mbaya sikuijua maana ya jina la Ukolongwe kabla ya kuondoka. Kipindi chote nilipokuwa nimehama sikujiwa na shauku ya kutaka kujua maana ya jina hilo. Nilijua *hata hivyo* kuwa jina lenyewe lazima lilikuwa na maana.
>
> (*Musaleo!* u.k 14)

Katika matini hii dhana mbili zimeunganishwa; kutojali kujua maana ya 'jina Ukolongwe + kujua maana ya jina hilo'. Msimulizi hakujali kutafuta maana ya jina Ukolongwe lakini akilini mwake alijua bayana lina maana. Kisha kuna msisitizo kwamba jina hilo lina maana. Hapa tunaona mlinganuo ambapo msimulizi hakujali na vile vile kusisitiza kuwa jina hilo lina maana. Uunganishi huu unaonyesha mlinganuo, msisitizo na mshikamano.

Kutokana na haya imedhihirika kwamba viunganishi elezi huunganisha dhana, huonyesha mlinganuo na husisitiza dhana katika matini. Na katika kufanya hivyo vinaleta mshikamano katika matini. Katika matini zilizotumika, *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* kuna baadhi ya viunganishi elezi havikutumiwa kabisa, navyo ni *bado, vinginevyo, kwa vyovyote, kwa minajili ya.*

### 6.1.3 Uunganishaji Sababishi

Uunganishaji huu huonyesha sababu ya jambo kutokea kutokana na kitendo fulani. Kuna viunganishi mbalimbali vinavyotumika katika uunganishi huu, navyo ni *kwa sababu, kwa kuwa, kwa hivyo, hivyo, kutokana na*. Viunganishi hivi vilitokeza katika matini kama ifuatavyo:

#### 6.1.3.1 Viunganishi *Kwa sababu/Kwa kuwa*

Viunganishi *Kwa sababu* na *Kwa kuwa* vina maana moja katika Kiswahili. Kwa hivyo, vimechanganuliwa pamoja katika tasnifu hii. *Kwa sababu* ni kiunganishi ambacho hueleza sababu (Schriffin, 1987:195). Yaani matokeo au dhana katika kipashio tangulizi kilisababishwa na dhana katika kipashio fuatilizi. Kiunganishi *Kwa sababu* ni kitambulisho cha kipashio tegemezi cha usemi. Huonekana kuingiza dhana katika sentensi zilizo tegemezi katika matini (Kama hapo juu:196). Kiunganishi hiki huonyesha sababu ya jambo kutokea:

> 237. Peter alijaribu kuinua gunia lake, alishindwa. Sio *kwa sababu* gunia lile lilikuwa zito, la! Bali masikio na moyo wake vilisumbuliwa na kile kilio cha mtoto aliyekuwa hatua ishirini mbele yake.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 51)

Hapa, *kwa sababu* imeunganisha dhana mbili na wakati huo huo kuonyesha sababu. Peter alishindwa kubeba gunia lake na sababu imetolewa, nayo ni 'kilio cha mtoto'. Kando na kutuonyesha sababu ya Peter kubeba gunia lake, habari nyongeza imetolewa juu ya Peter na mzigo wake. Habari hii ina mantiki na ni kubalifu. Hivyo mshikamano umepatikana katika matini hii.

> 238. Huko nje, mzee Lomolomo alianguka chini pale mlangoni… Alikuwa kachanwa na lile bati la mlangoni… *Kwa kuwa* Mamantilie alichelewa kufungua mlango, Lomolomo aliuanzisha tena wimbo wake.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 10)

Katika 238 *Kwa kuwa* imeanza katika sentensi ya pili na kueleza sababu ya mzee Lomolomo kuimba tena. Imeshikanisha dhana mbili; kuchelewa kufungua mlango + kuimba tena. Tumeona kuwa sababu ya Lomolomo kuimba wimbo wake tena, ni Mamantilie kuchelewa kufungua mlango. Hivyo kiunganishi *kwa kuwa* ni sawa na *kwa sababu* na kimeonyesha sababu ya dhana fuatilizi. Hivyo kimeunganisha dhana mbili na kuleta mshikamano katika matini.

> 239. …Usingizi ulikatizwa na mlio wa simu nyumbani. Nilishangaa sana *kwa sababu* simu yenyewe iliharibika miezi miwili iliyopita.
>
> (*Musaleo!* u.k 8)

Katika matini hii, *kwa sababu* imetokea katika kishazi fuatilizi. Kimeunganisha dhana mbili; kushangaa + simu kulia, ilhali iliharibika kitambo. Vile vile kimetuonyesha sababu ya kushangaa kwa msimulizi. Uamilifu wa kiunganishi hiki ni kushikanisha hizo dhana mbili na kimeleta mshikamano.

### 6.1.3.2 Kiunganishi *Kwa hivyo*

*Kwa hivyo* ni mojawapo ya viunganishi sababishi. Kama adaivyo Salkie (1995:77) *kwa hivyo* ni kiunganishi kitumikacho zaidi katika usemi. Schriffin (1987:201) anaeleza kuwa *kwa hivyo* ina maana ya kisemantiki inayijitokeza katika sentensi. Yaani kiunganishi hiki huleta maana tu katika kiwango cha sentensi. Hutoa maana ya matokeo. Kitendo hufanyika, na *kwa hivyo* hutumika kuonyesha matokeo ya kitendo hicho. Mifano ifuatayo inadhihirisha haya.

> 240. ...Uozo wa takataka ulileta harufu, ukazalisha wadudu na funza. Majani yasiyofyekwa yalikuwa maskani ya vijoka na majoka. Maji yaliyosimama yalikuwa zahanati nzuri kwa mbu, wakataga mayai yao, kwa mamia, na *kwa hivyo*, ugonjwa wa malaria ulikuwa tishio kwa afya, maisha na uhai wa wakazi wa Kisutu.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 36)

Katika matini hii 240, uchafu na maji yaliyosimama katika mtaa wa Kisutu, matokeo yake ni ugonjwa wa malaria unaouwa watu, mfano mama yake Kurwa ( *Watoto wa Maman'tilie*, u.k 37). Hapa tumeonyeshwa matokeo ya uchafu na kusimama kwa maji. Dhana hizi zimeunganishwa na *kwa hivyo*. Kiunganishi hiki kimeambatanishwa na kiunganishi *na* ambacho ni kiunganishi nyongeza, tukawa na, *na* + *kwa hivyo*. Mwambatano huu umeleta maana iliyo na mantiki na kuleta mshikamano katika matini hii:

> 241. ...Kwa kweli sikumwelewa *lakini* sikutaka kuonekana mbumbumbu *kwa hivyo* nilitikisa kichwa mara kadhaa kama mbunge wa kwetu ambaye sasa ni waziri.
> (*Musaleo!* u.k 11)

Mfano huu unaonyesha kiunganishi *kwa hivyo* kimetumika kuonyesha matokeo. Kimeunganisha dhana tatu; kutoelewa + kuonekana mbumbumbu + kutikisa kichwa (kuelewa) ingawaje dhana mbili za kwanza zina kiunganishi *lakini*. Ili kupata mantiki

katika matini hii ni lazima dhana zote tatu ziunganishwe. Msemaji hakuelewa aliyoelezwa na hakutaka ajulikane kama hakuelewa. Matokeo yake ni kutikisa kichwa kuonyesha ameelewa na kuficha tatizo hilo. Uunganishi huu umeleta mshikamano katika matini hii. Katika utafiti huu ilionekana kuwa kiunganishi *kwa hivyo* kimejitokeza katika kishazi fuatilizi tu.

### 6.1.3.3 Kiunganishi *Hivyo*

Schriffin (1987:201) anasema kiunganishi *hivyo* hutoa maana ya matokeo. Hutumika kuongeza habari kutokana na habari inayofahamika. Dhana ya kwanza katika sentensi tangulizi (au kisabiki) ilisababisha dhana inayojitokeza katika sentensi fuatilizi. Tukichunguza matumizi ya kiunganishi *hivyo* ni kwamba kinaweza kuondolewa na kusimamiwa na kiunganishi *kwa hivyo* na maana ikabaki ile ile na uamilifu ni ule ule. Hii inaonyesha kuwa viunganishi hivi vinaweza kutumika kama vibadala. Kisemantiki ni maneno mawili yenye maana moja lakini yenye maumbo tofauti. Katika utafiti huu tuligundua kuwa kiunganishi *hivyo* katika matini, kilitokea zaidi katika sentensi fuatilizi na mwanzoni mwa sentensi (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 10, 40, 56, 76, 82). Kilitokea katikati mwa sentensi mara moja (1) tu, u.k 10. Katika matini ya *Musaleo!* hakikutumika kabisa.

Tuchanganue mifano hii:

> 242. ...Fulana yake iliyoandikwa kifuani: DALLARS ilikuwa fupi, ikikataa kukutana na kiuno. *Hivyo*, kitovu chake, kama jicho moja chongo, saa zote kilikaa wazi.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 40)

Katika mfano huu *Hivyo* imeunganisha dhana mbili na kuelezea matokeo; fulana fupi + kitovu kukaa wazi. Dhana ya kwanza katika kisabiki ilisababisha dhana ya pili katika kishazi fuatilizi.

> 243. Huko nje, Mzee Lomolomo....Alikuwa kachanwa na lile bati la mlango. Haukuwa mpira, *hivyo* aliumia.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 10)

Hapa kiunganishi *hivyo* kimetokea katikati mwa sentensi moja lakini kimeunganisha vishazi viwili; Haukuwa mpira + aliumia. Kinaeleza sababu ya kuumia. Kimeunganisha dhana mbili, ya kwanza ni matokeo na ya pili ni sababu.

Vile vile tukichunguza zaidi kiunganishi *kwa hivyo* kinaweza kutumika badala ya *hivyo* na maana ikabaki ile ile na uamilifu huo huo. Kiunganishi *hivyo* kimeunganisha hizo dhana mbili na kuleta mshikamano katika matini.

### 6.1.3.4 Kiunganishi *Kutokana na*

Kiunganishi *kutokana na* kinaonyesha sababu na matokeo kinapounganisha dhana katika matini. Huunganisha dhana mbili ambapo moja inasababisha nyingine. Tuangalie mifano hii:

> 244. ...Nasikia kijijini, nchi na barani watu wanasema aliaga dunia *kutokana na*$_1$ mzigo wa maumivu. Wengine wanadai kifo chake *kilitokana na*$_2$ juhudi za kuuchukua ubavu aliowanyang'anya wanaume.
>
> (*Musaleo!* u.k 2)

Katika matini hii 244 kiunganishi *kutokana na* kimetumika mara mbili kuonyesha sababu, na wakati huo huo kuunganisha dhana mbili; kufa + maumivu/kuchukua ubavu. Kifo chake kimeelezwa na kishazi tangulizi na kishazi fuatilizi kinaeleza sababu za kifo hicho. Sababu ya kwanza ni 'maumivu mengi' na sababu ya pili ni 'kuchukua ubavu'. Kiunganishi *kutokana na* kimeunganisha 'kifo' na 'sababu za kutokea'. Kwa hivyo, kiunganishi hiki kinaonyesha sababu na matokeo katika dhana zilizounganishwa na

kuleta mshikamano. Kiunganishi hiki kimetokea katikati ya kishazi tangulizi na fuatilizi katika uunganishaji wake. (Dondoo hili liko katika italiki katika matini asili).

> 245. *Mambo yalininyookea. Kutokana na uhusiano uliokuwako kati yangu na watu wengine nchini, hali yangu ilianza kubadilika asteaste.*
>
> (*Musaleo!* u.k 12)

Mfano huu unaonyesha sababu na matokeo kwa wakati mmoja. Kiunganishi *kutokana na* kimetoa maana hizo mbili na kimetokea mwanzoni mwa sentensi fuatilizi. Kimeunganisha dhana mbili; mambo kumnyookea + uhusiano mzuri. Kimeonyesha sababu ya mambo kumnyookea msimulizi. Na matokeo ni 'mabadiliko ya hali yake'. Kiunganishi *kutokana na* kinaweza kutokea mwanzoni au katikati mwa sentensi. Vyovyote vile kitakavyotokea, uamilifu haubadiliki, ni kiunganishi sababishi kinacholeta mshikamano katika matini. Katika *Watoto wa Maman'tilie* hakikutumika.

### 6.1.4 Uunganishaji Wakati

Uunganishaji huu huonyesha wakati unavyounganishwa katika matini. Huonyesha wakati fulani jambo lilitokea, kisha baadaye jambo linguine kufuata. Kwa hivyo kinachounganishwa ni nyakati za vitendo au mambo kutokea. Tuangalie jinsi uunganishaji huu ulivyotumika katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*

#### 6.1.4.1 Kiunganishi *Kisha*

Kiunganishi *kisha* huonyesha wakati mfululizo kati ya mazungumzo tangulizi na yale fuatilizi. Kiunganishi hiki huweza kutumika na *ikiwa*, yaani *ikiwa...kisha*. Na inapotokea hivi hugeuka kuwa sharti (Schriffin, 1987:246).

Kiunganishi hiki huunganisha matukio mawili kiwakati katika usemi. Matukio haya hupangwa kwa mujibu wa wakati yalipotokea. Katika matini, wakati hujitokeza iwapo msemaji anasimulia matukio kwa mpango maalumu na kwa mujibu wa wakati (kama hapo juu:262). Hili hufanyika kwa kutumia kiunganishi *kisha*. Tuchunguze mifano ifuatayo.

> 246. Mamantilie alimvuta ndani na Lomolomo akakaa kizingitini. *Kisha* alitilia komeo ya mlango akasema, "Twende ndani ukalale..."
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 11)

Katika 246 vitendo viwili vimetokea, kimoja baada ya kingine, kumvuta ndani Lomolomo + kutia komeo ya mlango. Vitendo hivi vimeunganishwa na kiunganishi *kisha*. Kitendo 'kuvuta ndani' kilitangulia na kufuatiliwa na 'kutia koleo ya mlango'. Hivyo kiunganishi *kisha* kimeunganisha vitendo hivi kiwakati, na kimetokea mwanzoni mwa sentensi tangulizi.

> 247. Aliipiga mafunda kadha soda iliyokuwa imebaki chupani *kisha* akamnyoshea mwenye kioski ambaye alikuwa kayatuliza macho yake kwa jamaa aliyekuwa akisogea kutoka huko mbele.
> (*Musaleo!* u.k 16)

Katika matini hii *kisha* vile vile imeunganisha vitendo viwili vilivyofuatana kimoja baada ya kingine; kunywa + kumnyoshea chupa. Uunganishaji huu umeleta mshikamano katika matini. Hapa kiunganishi *kisha* kimetokea katikati mwa sentensi ambatano. Pia kiunganishi *kisha* kinaweza kuunganishwa na kiunganishi kingine na kuwa na uamilifu ule ule. Tuchunguze mifano hii.

> 248. Zita alichukua jiko, akajaza makaa; *kisha tena* akachukua mafuta ya taa kwenye chupa...
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 7)

> 249. Waliendelea kuongea *kisha baada ya* muda wakaondoka wote. Walishika njia kuelekea *Western Style Cosmetics and Salon.*

(*Musaleo!* u.k 42)

Katika 248 *kisha* imetumika pamoja na *tena*. Kwa mujibu wa muktadha wa matumizi haya kiunganishi *tena* kimetumika kwa kusisitiza vitendo vilivyotumika kiwakati. Pia inaonyesha nyongeza 'juu ya'. Hivi vyote ni viunganishi, kimoja cha wakati na kingine ni cha nyongeza kwa mujibu wa muktadha. Na katika 249 *kisha* imefuatiliwa na *baada ya*. Viunganishi vyote hivi viwili ni vya wakati (Halliday na Hassan, 1976). Hapa linalojitokeza ni kwamba baada ya kitendo cha kwanza kuna muda wahusika fulani waliendelea kuongea ndipo wakaondoka pamoja. Hivyo ni wakati unaosisitizwa. Watajwa hapo juu (u.k. 261) wanaeleza kwamba kiunganishi kinaweza kuongezewa kiunganishi kingine kuonyesha wakati kama vile *kisha* + *baadaye*, *kisha* + *mara moja*, *kisha* + *baada ya*. Kwa hivyo, kiunganishi *kisha* kinaweza kutumika pamoja na kiunganishi wakati kingine. Utafiti huu umeonyesha kuwa kiunganishi *kisha* lazima kitangulie viunganishi hivyo vingine.

> 250. ...Nje ya duka la Rhemtula gogo kubwa la mti liliungua taratibu, likatoa cheche ndogondogo. Cheche hizi ziliruka mita moja hivi hewani, *kisha tena* zikageuka majivu na kuzimika.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 42)

Katika 250 viunganishi viwili vimetumika. Kiunganishi *kisha* kikifuatwa na kiunganishi *tena*. *Tena* ni kiunganishi kwa sababu kiunganishi *kisha* kinaweza kutolewa na *tena* ikawa na uamilifu wa kiunganishi. Kwa hivyo *tena* kimetumika kusisitiza dhana ya 'kugeuka majivu'. Viunganishi hivi vimeleta mshikamano na hakuna urudufishaji ila msisitizo.

### 6.1.4.2 Kiunganishi *Baada ya*

Kiunganishi *baada ya* vile vile kinaunganisha vitendo viwili na kuonyesha wakati. Kinaonyesha kitendo kimoja kikitokea na kikifuatwa na kingine. Kitendo awali huwa kimetimia na kile kingine hufuata. Tuchunguze mifano hii.

> 251. Peter alichagua kibao kimoja kizuri. Alichukua kopo la rangi aliloliokota dampo akakaa pembezoni mwa Kurwa. "Ngoja... jina gani?" Aliwaza hivi: Rojo Hotel? Mmm! Hapana! Sheraton Hotel? Kilimanjaro Hotel? Eemm! Ndiyo! Ngoja...
> ...*Baada ya* muda Peter alitafuta nyuzi za katani, akatengeneza brashi nzuri na kuinamia kibao.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 65-66)

Katika matini hii *baada ya* inaunganisha vitendo vinne alivyofanya Peter kiwakati, kitendo kimoja kikifuatwa na kingine. Alichukua kibao na kopo la rangi kwanza. Halafu akafikiria jina lifaalo. Alipoamua, ndipo Peter akatengeneza brashi na kuandika. Kwa hivyo kuna; kuchukua kibao + kufikiri + kutengeneza brashi + kuandika. Kitendo cha 'kuandika' (kuinamia brashi) kilikuja mwisho kabisa kikitanguliwa na hivyo vingine. Vitendo hivi vilifuatana kiwakati, kimoja baada ya kingine na kuleta mshikamano wenye mantiki. Kiunganishi kimetokea mwanzoni mwa sentensi.

> 252. ...Yule mhudumu alirudi wakati huo na kusimama upande wa nyuma mwa Anima. Kitungule ambaye alitaka kumpurukusha asiangalie picha zile *kwa kuwa nchi hii huwezi kumwamini kila mtu* alishika meza na kuitikisa kidogo. "Aisee, meza hii inalegalega!"
> Sasa ilimbidi mhudumu huyu aitue shehena aliyokuwa nayo juu ya meza jirani na kujaribu kuangalia meza. Wote walitazamana. *Baada ya* muda alichukua sinia aliyotumia kubebea vinywaji na kuweka mezani.
>
> (*Musaleo!* u.k. 85)

Matini 252, pana dhihiri mfuatilizo wa vitendo vilivyoshikanishwa na kiunganishi *baada ya;* Mhudumu alitua shehena + akaangalia meza + akachukua sinia. Vitendo hivi

vilifuatana kiwakati, kila kimoja kilipotimia, kingine kilifuata na kuleta mshikamano. Kiunganishi hiki kimetokea mwanzoni mwa sentensi.

Kiunganishi *baada ya* huweza pia kutanguliwa na kiunganishi *kisha* (tazama 196 hapo juu) au *na.* Aidha kuna matumizi ya kitendo fuatilizi kutangulia katika matini, kisha kitendo tangulizi kufuatiliza kimantiki.

> 253. …Hapakuwa na mabadiliko yoyote. Kufuli waliloishia kutia *baada ya* kulikata lile jingine lilikuwa bado pale.
> (*Musaleo!* u.k. 84-85)

Hapa pana vitendo viwili; kutia kufuli + kukata kufuli. Hivyo kimantiki kitendo tangulizi kingekuwa 'kukata kufuli' kikifuatwa na 'kutia kufuli', lakini msimulizi alibadili nafasi za vitendo hivi. Hata hivyo, mshikamano wa wakati upo ila tu ameanza na kitendo kilichokuwa matokeo. Hapa dhana inarejelea mbele.

> 254. …Walipewa dawa ya kuendesha *na baada ya* muda, kama kuku, walitaga 'mayai ya dhahabu'.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 95)

Hapa pana uunganishaji wa sentensi kwa kutumia *na;* Walipewa dawa ya kuendesha + kama kuku walitaga 'mayai ya dhahabu'. Uunganishaji wa wakati umeletwa na matumizi ya *baada ya* muda. Neno <u>muda</u> limetumika kushadidia ule wakati. Uunganishi huu umeleta mshikamano wa nyongeza ya habari na mfuatilizo wa vitendo kiwakati. Kiunganishi *baada ya* kimetokea katikati mwa sentensi.

Kwa hivyo, tumeona kwamba kiunganishi *baada ya* kinaweza kutanguliwa na *na.* Pia kinaweza kikafuatwa na neno 'muda' ili kushadidia wakati. Aidha kinaweza kufuatwa na

nomino, mfano *baada ya* + safari (255). Inaweza pia kufuatwa na kitenzi, mfano *baada ya* + kuipokea (256).

> 255. ...*Jina najiita na utaniita Musaleo! Usiniulize. Labda utajua mwishowe au nitakueleza baada ya safari ndefu kwenye makaratasi haya...*
>
> (Musaleo! u.k 2)

> 256. ...*Mwishowe alipoachiwa uhuru wa kubwakura ile nyama alikuwa karibu kukata tamaa. Baada ya kuipokea tu alimwendea yule mzee. Akiunyonganyonga ule mkia...*
>
> (*Musaleo!* u.k 20)

### 6.1.4.3 Kiunganishi *Baadaye*

*Baadaye* ni kiunganishi kinachoonyesha wakati unaofuata baada ya kitendo fulani. *Baadaye* huunganisha nyakati mbili ambazo hufuatana baada ya kitendo kimoja (kitendo awali) kukamilika. Tuchunguze mifano hii:

> 257. Peter macho yake yalielekea barabarani lakini hakuona magari yaliyokuwa yanapita. Ubongo wake ulikuwa umevurugika... Hakulia, alinyamaza kimya kitambo.
>
> *Baadaye*, alimmwagia Kurwa maswali, "Ilikuwaje? Alikuwaje? Alikufaje? Lini?..."
>
> (*Watoto wa Maman'tilie,* u.k 53)

Katika 257 tunaona mfuatilizo wa wakati juu ya vitendo vilivyotendeka. Vitendo vya 'kufikiri' na 'kunyamaza' vilitangulia. Vilipomalizika, kitendo cha 'kuuliza maswali' kikafuata. Kwa hivyo, vitendo hivi viliunganishwa kiwakati na kiunganishi *baadaye* na kuleta mshikamano katika matini. Aidha, kiunganishi hiki kimetokea mwanzoni mwa sentensi lakini katikati mwa dhana; Kunyamaza kimya kitambo (*baadaye*) kuuliza maswali.

> 258. ...Mwanamke mmoja aliniangalia kisha akasema, "Ndiyo mtu ukiwa na kiu hata kuwasalimu watu huwezi?' Niliona haya kwa kutotanguliza na salamu. *Baadaye* walinichotea maji na kunipa

kwenye kifaa kilichofanana na fuvu la binadamu.
(*Musaleo!* u.k 59)

Katika matini hii kuna mfuatilizo wa matokeo, tukio moja likitangulia na kufuatwa na lingine, kule kuomba maji, kuuliza swali na kupewa maji. Matukio haya yalikuja moja baada ya lingine. Hivyo kushikanisha matukio hayo kiwakati. Kiunganishi *baadaye* hapa kimetokea mwanzoni mwa sentensi lakini katikati ya dhana hizo tatu. Kuomba maji + kuuliza maswali (*baadaye*) kupewa maji. Uunganishi huu umeleta mshikamano katika matini hii.

259. ...Sikumwelewa. Nilipoachana naye *baadaye* alikuwa akilalamika kuhusu maumivu ya kifuani.
(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 77)

Kiunganishi *baadaye* kinaonyesha mfutilizo wa wakati. Msimulizi alikuwa na mhusika (Mamanchi) wakiongea na baada ya muda mazungumzo yaliisha na wakaachana lakini alikuwa akilalamikia maumivu ya kifua. Yaani kitendo cha mazungumzo kilipomalizika, msemaji aliondoka na kuachana na Mamachi. Vitendo hivi viliunganishwa na *baadaye*. Hivi kiunganishi *baadaye* kinaunganisha 'kukaa na muhusika (Mamanchi)' + 'kuachana'. Kwa hivyo, kimeunganisha dhana mbili zilizofuatana kiwakati na kuleta mshikamano. Aidha kiunganishi *baadaye* kinaweza kuunganishwa na wakati mahususi. Wakati huu lazima utangulie kiunganishi hicho:

260. ...Nilipotewa na fahamu njiani. Ziliponirudia masaa manne *baadaye* yule daktari alikuwa amenisimamia.
(*Musaleo!* u.k 74)

Katika mfano huu wakati mahususi umetajwa wa kitendo kingine kutokea, 'masaa manne'. Hivyo tuna, masaa manne + *baadaye*. Uliotokea hapa ni uunganishaji wa nyuma. Kitenzi 'Ziliponirudia' ndicho kinaunganishwa na wakati. Ama sentensi hii ingekuwa, 'Masaa manane *baadaye* zilinirudia...'. Jambo la muhimu ni kuwa dhana mbili

zimeunganishwa na kiunganishi *baadaye*, nazo ni 'kupotewa na fahamu' (*baadaye*) 'kurudiwa na fahamu'. Zilivyounganishwa zimeleta mshikamano katika matini hii kwa sababu pamoja na usanii wa mwandishi katika sentensi yake, kuna mantiki ya yanayosimuliwa. Mtindo huu unatumika katika matini za Kiswahili:

Siku chache + *baadaye* (*Musaleo!* u.k 3)

Saa mbili + *baadaye* (*Musaleo!* u.k 8)

Dakika tano + *baadaye* (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 44)

### 6.1.4.4 Kiunganishi *Hatimaye*

Kiunganishi *hatimaye* kinaonyesha wakati wa mwisho kabisa. Yaani baada ya vitendo fulani kutangulia, kuna kitendo kilichotendeka mwisho kabisa kumalizia vitendo hivyo au matukio hayo. Hivyo kuna msururu wa vitendo na kile cha mwisho kabisa kinaunganishwa na vile vingine kwa kutumia kiunganishi *hatimaye*. Katika Kiswahili kiunganishi *hatimaye* kina kisawe chake, nacho ni *mwishowe*. Kiunganishi *mwishowe* pia kimetumika katika matini tulizozirejelea katika utafiti huu. Tuchunguze mifano hii.

261. Kurwa alipakuwa sahani mbili za wali. Juu akajaza mboga za maboga, akawapa. "Kuleni." Alikuwa kachuma majani hayo ya boga lililokuwa limejiotea pale nje, juu ya kichuguu cha takataka, majivu na nyasi. Kaka zake walikula haraka na kwa hamu, bila kuzungumza.

*Hatimaye*, Kurwa aliuliza, "Mipango yote mmekamilisha?"
*(Watoto wa Maman'tilie,* u.k. 40*)*

Hapa kiunganishi *hatimaye* kimeunganisha vitendo vyote katika matini hii na kutuonyesha kile kilichotendeka mwisho kabisa; aliupakuwa + akajaza mboga + akawapa + walikula haraka (*hatimaye*) akauliza. Vitendo hivi vimeunganishwa na *hatimaye* na kuleta mshikamano katika matini. Uunganishi huu ni wa kiwakati, yaani jinsi vitendo vilivyofanyika na kufuatana kwa mujibu wa wakati.

Katika 261 kiunganishi *hatimaye* kimetokea mwanzoni mwa sentensi lakini kimuktadha kiko katikati ya dhana. Lakini kinaweza kutokea vile vile mwishoni mwa sentensi na uamilifu ukabaki ule ule. Mfano;

> 262. ...Aliusahau mguu wake na kurudia swali lake, "Sema Kurwa! Madonda haya makubwa hivi; gotini na usoni. Sema ilikuwaje?" Shauri ya riziki Peter," Kurwa alijibu *hatimaye*.
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 53)

Mfano huu unatuonyesha kuwa baada ya maswali aliyoulizwa, Kurwa aliyajibu mwisho kabisa. Kwa hivyo, kuna mfuatano wa vitendo kwa mujibu wa jinsi vilivyotokea kiwakati. Kiunganishi *hatimaye* kimetumika kuunganisha vitendo hivi vyote kwa kurejelea nyuma. Huu ni uunganishi nyuma na mshikamano upo katika matini kwani dhana zilizounganishwa zinaleta mantiki. Kiunganishi *hatimaye* pia kinaweza kutanguliwa na viunganishi *lakini* na *na* katika matini. Tuchunguze mifano hii:

> 263. ...Alichukuwa muda mrefu *lakini hatimaye* alinikabidhi muswada mrefu...
> (*Musaleo!* u.k 15)

Katika mfano huu, *lakini* imeonyesha ule mlinganuo uliopo, na *hatimaye* imeunganisha vitendo hivyo viwili kiwakati, kimoja kikifuata kingine na kuleta mshikamano unaokubalika; kuchukua muda mrefu + kukabidhi muswada. Katika matini mbili zilizotumika, uunganishi huu wa *lakini* + *hatimaye* ulijitokeza mara tano (5) katika *Musaleo!* u.k 15, 25, 79, 85, 93. Na katika *Watoto wa Maman'tilie* haukutokeza kabisa.

> 264. ... Waliweza kufuatilia yote yaliyofanyika hapo mbele yao. Ngoma za kila aina, watoto wakikariri mashairi, misafara ya madaktari na maguo yao meupe na *stethiskopu* chungu mbovu, kufyatuliwa kwa mizinga na majeshi *na hatimaye* hotuba zilizoishia kwa watu kusema *Mkombozi wetu! Mkombozi wetu! Mkombozi wetu!*
> (*Musaleo!* u.k 80)

Katika mfano huu *na* imetangulia *hatimaye* na kuunganisha vishazi viwili huku ikiongezea habari zaidi. Nayo *hatimaye*, imeunganisha wakati. Yaani mambo yaliyofanyika yakiunganishwa kwa mujibu wa yalivyotokea kiwakati, moja likifuata lingine. Uunganishi huu wa *na* + *hatimaye* umetokea mara moja (1) tu katika matini ya *Musaleo!* u.k 80, na haupo katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie*. Kwa jumla, matumizi ya kiunganishi *hatimaye* katika matini zote mbili ni mara hamsini na tatu (53) na matumizi zaidi ni yale ya kiunganishi hiki kutokea mwanzoni mwa kishazi au sentensi, mara arobaini na nane (48). Na mara tano (5) ni matumizi ya *lakini* + *hatimaye*, na mara moja (1) ni ya *na* + *hatimaye*.

Kama tulivyotangulia kusema neno *hatimaye* lina kisawe chake ambacho ni *mwishowe*. Tuchunguze kisawe hiki kilivyotumika katika kuunganisha wakati.

> 265. ... *Watu walijiandaa kuyasikiliza maneno yake. Walitulia wakimsikiliza. Wakamngojea. Wakasubiri; kimya! Mwishowe aliposema alichekesha...*
>
> (*Musaleo!* u.k 90)

*Mwishowe* hapa ina uamilifu wa kuunganisha matukio kiwakati. Inaonyesha tukio lililokuwa la mwisho kabisa ni 'kutoa matamshi yaliyochekesha' hadhira yake. Matukio mengine ni 'walijiandaa' + 'walitulia kumsikiliza' + 'wakangoja' (*mwishowe*) 'alisema'. Uunganishi huu umeleta mshikamano kwani kuna mfuatilizo wa matukio wenye mantiki na kukubalika.

### 6.1.4.5 Kiunganishi *Kabla (ya)*

*Kabla* ni kiunganishi cha wakati na huweza kutumika peke yake au pamoja na *ya* unganifu na kuwa, *kabla ya*. Matumizi yote haya yana uamilifu sawa wa kuunganisha wakati. Tuchunguze mifano hii.

266. ...Na sasa alikuwa anataka amwone Kurwa yeye mwenyewe *kabla* hajaondoka kwenda kazini, kilabuni.
(*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 68)

267. ...Alishakula yamini kuwa lazima amalize kuiandika hadithi yake *kabla ya* shule kufungwa kwa ajili ya mapumziko ya muhula wa tatu.
(*Musaleo!* u.k 43)

Katika 266, *kabla* imetumika peke yake na katika 267, imetumika pamoja na *ya*. Hapa nyakati zimeunganishwa. Katika 266, Zenabu alitaka kufanya kitendo cha 'kuona' kabla hajafanya kitendo cha 'kuondoka'. Kwa hivyo *kabla* ikaunganisha vitendo hivi na kuleta mshikamano. Katika 267, dhana ni ile ile. Kiunganishi *kabla ya* kinaonyesha kitendo kimoja kikifanyika kabla ya kingine; amalize kuiandika (*kabla ya*) shule kufungwa. Viunganishi hivi vyote vimetokea katikati mwa sentensi na kuunganisha dhana zilizopo. Vile vile katika matini hii vitendo viwili vimeunganishwa na kuleta mshikamano.

Kwa jumla, kiunganishi *kabla* kimetumika mara nne (4) katika matini zote mbili zilizorejelewa; katika *Musaleo!* mara tatu (3) u.k 1, 55, 96, na katika *Watoto wa Maman'tilie*, mara moja (1) tu, u.k 68. Na kiunganishi *kabla ya* kimetumika mara tisa (9) kwa jumla katika matini zote; katika *Musaleo!* mara nane (8), u.k 26, 43, 45, 53, 57, 58, 75, 79, na katika *Watoto wa Maman'tilie* mara moja (1) tu, u.k 87. Linalojitokeza katika matumizi yote haya ni kwamba *kabla* inapotumika, kitenzi kinachofuata huwa katika hali ya kukanusha. Na *kabla ya* inapotumika, kitenzi kinachofuata huwa ni kitenzi-nomino au nomino. Hivyo inakuwa i) *kabla* + kitenzi kanushi

ii) *kabla ya* + kitenzi-nomino/nomino

### 6.1.4.6 Kiunganishi *Mara*

Kiunganishi *mara* kinaonyesha kitendo fuatilizi kimetokea baada ya kile tangulizi bila kupishana muda. Yaani kitendo tangulizi kinapoisha tu hivi, kitendo fuatilizi kinafanyika bila kupitisha muda wowote. Dhana inayopatikana katika uunganishi wa kutumia kiunganishi *mara* ni ile haraka ya kutokea. Tuchunguze mifano hii.

> 268. Zita alipaza sauti, "Nikuletee chakula baba?"
> "Ee! Niletee mwanangu, tia nyama nyingi! Na mchuzi!"
> *Mara* alianza kuimba tena, uleule wimbo wake wa "Siwezi kuua mtu..."
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 71)

Kiunganishi *Mara* katika mfano huu 268 kinaonyesha ile haraka ya kitendo fuatilizi kilivyofanyika. Hapakuwa na mapumziko yoyote. Kiunganishi *mara* vile vile kinaweza kutumika pamoja na *lakini, na*; *lakini* + *mara*, *na* + *mara*. Tuchunguze matumizi haya.

> 269. ...Bado alikuwa hakuelewa tabia ya mbwa yule. Alidhani haikuwa tabia ya kawaida. *Lakini mara* yule mbwa aliingia kichochoroni, akapotea machoni.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 17)

Kiunganishi *lakini* hapa, kinaonyesha mlinganuo wa 'kutopata fursa ya kumwangalia yule mbwa hadi kumwelewa tabia yake'. *mara* inaonyesha uunganishi wa wakati wa jinsi vitendo vilitokea, yaani kitendo cha 'mbwa kuingia kichochoroni' na 'kupotea' machoni mwa mhusika kilitokea haraka sana. Hivyo tunapata uunganishi elezi wenye mlinganuo ambao umetumika pamoja na ule wa wakati na kuleta mshikamano kwenye matini. *na* + *mara* imetumika katika *Watoto wa Maman'tilie*.

> 270. Aliporudi pale sebuleni alisema, "Dada Zita." Zita alimtazama, hakumjibu. Uzuri wa Zita, Peter aliwaza ni kuwa hakai na hasira kwa muda mrefu. Hasira zake hutumbuka pwaachaa! Na kumbambua ngozi yule aliyemkifu, *na mara*, baada ya muda mfupi huyeyuka...
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 64)

Hapa *na* + *mara* vimetumika kwa pamoja na vile vile kuonyesha ule utokeaji wa haraka vitendo vikifuatana. Hivyo kuunganisha vitendo viwili vinavyofuatana na kuleta mshikamano katika matini.

*Mara* vile vile huunganisha wakati katika matini. Huunganisha wakati wa mbele na wakati wa sasa. Mfano mtu alifanya jambo mbeleni na sasa analifanya tena lakini kivingine. Hapo mwandishi ataunganisha matendo na nyakati hizi mbili. (Dondoo liko katika italiki kwenye matini halisi.)

> 271. *$Mara_1$ ya pili aliporudi mshauri wangu alikuwa na kisa kingine cha ajabu. Hakuanza visa vya pepo au mvua (msimu huu wa masika ulielekea kuwa mrefu kuliko kawaida) iliyokuwa ikianguka. $Mara_2$ hii alisema alikuwa na kisa cha maajabu ya kilimwengu.*
>
> (*Musaleo!,* u.k. 89)

Katika matini hii kiunganishi *Mara* kimetumika mara mbili. Katika hali hizi zote ni kwamba kuna wakati uliotangulia alipokuwa na kisa na wakati wa sasa ana kisa kinginge cha ajabu. Kwa hivyo, wakati uliotangulia unaunganishwa na wakati wa sasa uliopo katika masimulizi haya. Hivyo kimeleta mshikamano wa matukio mawili yaliyotokea katika nyakati tofauti.

Katika matini zilizorejelewa katika utafiti huu, kiunganishi *mara* kimetumika mara tisa (9) katika *Watoto wa Maman'tilie*. Na katika *Musaleo*! kiunganishi hiki kimetumika mara kumi (10). Matumizi yake yamedhihirisha unganishaji wa matokeo kwa utokezi wao na kuunganisha nyakati mbili, ule uliotangulia na wa wakati uliopo. Hivyo kutokana na uchunguzi wa matini hizi mbili, inadhihirika kuwa kiunganishi *mara* hutumika kwa uchache kama kiunganishi cha kuleta mshikamano katika matini za Kiswahili

### 6.2 Vikwazo katika Uunganishaji

Uunganishaji hutumika kuunganisha vitendo na dhana katika matini ili kuleta mshikamano. Kwa kufanya hivyo, viunganishi hutumika. Hata hivyo vikwazo kadha vilijitokeza katika Kiswahili tunapotumia viunganishi hivi. Navyo ni kama ifuatavyo.

#### 6.2.1 Kiunganishi *Na*

Kiunganishi hiki ni kiunganishi nyongeza. Huongezea habari zaidi katika matini na wakati huo huo kuunganisha habari hizo. Hata hivyo jambo hili hutokea kutegemea muktadha. Katika miktadha mingine *na,* katika Kiswahili, huwa kihusishi wala si kiunganishi cha mshikamano. Kwa hivyo si kila wakati *na* inapotokea katika matini ni kiunganishi. Jambo hili linadhihirishwa na mifano ifuatayo.

> 272. Watoto walisambaa $na_1$ kuelekea nyumbani. Zita Lomolomo, darasa la sita, $na_2$ Peter Lomolomo, darasa la tano, walikimwa $na_3$ tangazo la mwalimu Chikoya.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 1)

Katika mfano huu $na_1$ ni kiunganishi cha mshikamano lakini $na_2$ si kiunganishi cha mshikamano bali kiunganishi cha nomino mbili, Zita na Peter. $na_3$ ni kihusishi. Kwa hivyo' *na* inakuwa kiunganishi cha mshikamano katika muktadha wa kilivyotumika katika matini au usemi. *Na* vile vile hutangulia tu viunganishi vingine na hakitanguliwi na kiunganishi kingine katika matini. Kinaweza kutokea mwanzoni mwa sentensi kinapounganisha dhana, aidha katikati kinapounganisha sentensi mbili na dhana zilizomo katika sentensi hizo.

### 6.2.2 Kiunganishi *Tena*

Katika Kiswahili *tena* ina maana mbili kwa mujibu wa muktadha. Maana ya kwanza ni 'kurudia' au 'kufanya kwa mara nyingine', na maana ya pili ni 'na' au 'pamoja na' (Mohammed, 2000:248). Tuchunguze mifano hii.

> 273. Peter alikuwa kasawajika, mchafu zaidi kuliko asubuhi alipompa chai kwa muhogo wa kuchemsha. *Tena* macho yake yalitua juu ya lile gunia la mchele...
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 29)

> 274. Mamantilie alipeleka ...Alitema mate *tena*$_1$, phuuu! Na kuingia ndani. Kisha *tena*$_2$ alitoka na ndoo ya maji, kipande cha sabuni...
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k 5)

Katika 273 *Tena* ni kiunganishi nyongeza kinacholeta mshikamano. Kinaongeza habari zaidi katika matini. Kwa hivyo, ni kiunganishi cha mshikamano. Na katika 274, *tena*$_1$ na *tena*$_2$ si viunganishi, ni vielezi na havichangii mshikamano wa matini. Kwa hivyo, si kila *tena* inapotumika ni kiunganishi cha mshikamano.

### 6.2.3 Kiunganishi *Hivyo*

*Hivyo* inaweza kuwa kiunganishi cha mshikamano ikiwa inaunganisha dhana mbili na kuleta matokeo ya usababishi. Na kutegemea muktadha, *hivyo* huweza kuwa kibadala:

> 275. Kitungule alikwenda uwanja wa Mafanikio kuhudhuria sherehe zilizokuwako. Hii ilikuwa mara yake ya kwanza kufanya *hivyo*.
>
> (*Musaleo!* u.k 79)

> 276. Musa alicheka, akasema, "Wacha uishe! We unaogopa kufa? "Sio *hivyo*." Aliendelea kuramba ile ndimu huku kakunja uso.
>
> (*Watoto wa Maman'tilie*, u.k. 95)

Katika matini hizi mbili 275 na 276, kiunganishi *hivyo* kimejitokeza kama kibadala na si kiunganishi. Katika 275 ni kibadala cha 'Kingunge kuhudhuria sherehe katika uwanja wa Mafanikio'. Na katika 276 ni kibadala cha 'kuogopa kufa'. Matumizi yake katika mifano hii ni kuwa si kiunganishi sababishi bali ni kibadala. Kwa hivyo, si kila wakati *hivyo* inapotumika ni kiunganishi. Hii inatudhihirishia kuwa muktadha ni muhimu katika matumizi ya *hivyo* katika matini.

### 6.2.4 Kiunganishi *Baadaye*

Kutegemea matumizi, kiunganshi *baadaye* kinaweza kukosa uamilifu wa mshikamano na kuwa *kielezi* tu. Mfano;

> 277. Nilimwita chemba mwenzangu mmoja, Ngwena, na kumweleza ayaandike majina yao yote *na* kumkabidhi *baadaye*.
> (*Musaleo!* u.k 15)

Hapa kiunganishi *baadaye* hakiunganishi wakati wala matukio au vitendo. *Baadaye* kimetumika kama kielezi cha wakati. Uamilifu wa kiunganishi umechukuliwa na *na*. Lakini iwapo *baadaye* ingefuatana na *na* katika kishazi kimoja na kuwa, *na baadaye,* kingekuwa na uamilifu wa kiunganshi cha wakati na kuchangia mshikamano katika matini. Kwa hivyo, tunapochanganua viunganishi vya mshikamano, lazima tahadhari ichukuliwe na kuzingatia muktadha wa matumizi. Aidha kudhania kuzingatiwe.

### 6.2.5 Kiunganishi *Hatimaye*

Kikwazo kingine kilichojitokeza ni kuwa iwapo kiunganishi *hatimaye* kitatumika pamoja na viunganishi *lakini, kisha* na *na*, lazima viunganishi hivi vitangulie *hatimaye*. Isipofanyika hivyo sarufi huwa imepotoka na haikubaliki katika Kiswahili. Kwa mfano,

i) **hatimaye lakini*...

ii) **hatimaye kisha…*

iii) **hatimaye na..*

Kwa hivyo mshikamano una vikwazo na masharti yake ambayo yanajitokeza katika Kiswahili. Mwandishi hawezi kuandika tu apendavyo, lazima maandishi yake yatatawaliwa na vikwazo hivi. Vikwazo hivi vinaletwa na muundo wa Kiswahili chenyewe.

## 6.3 Hitimisho

Baada ya kutalii uunganishaji, katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* kiutokeaji, tumeona kuwa katika Kiswahili viunganishi vinatumika kwa idadi tofauti tofauti. Kiunganishi kilichotumika zaidi katika matini zote ni *Na*, mara mia nane (800) ambayo ni asili mia hamsini na tano nukta nane mbili (55.82%), kikifuatiwa na kiunganishi *Lakini* kikitokea mara mia mbili na tano (205) ambayo ni asili mia kumi na nne nukta tatu moja (14.31%) na kiunganishi *Kisha* kilichotokea mara tisini na nne (94) ambayo ni asili mia sita nukta tano sita (6.56%). Vipo viunganishi ambavyo havikutumika kabisa, navyo ni; *Awali*, *Vinginevyo*, *Vyovyote* na *Kwa minajili ya*.

Kwa hivyo waandishi Emmanuel Mbogo na Kyalo Wamitila katika matini hizi zao zimeonyesha wote wakitumia *Na* zaidi ikifuatiwa na *Lakini* na *Kisha*. Vile vile wote hawakutumia viunganishi kadhaa katika matini zao kama ilivyoonyeshwa hapo juu. Maoni yetu ni kuwa huu ni mchakato na muundo katika maandishi ya Kiswahili ambapo baadhi ya viunganishi hutumika zaidi kuliko vingingine hata kama waandishi wa Kiswahili wanatoka nchi mbalimbali na mazingira tofauti. Kwani waandishi hawa matumizi yao ya viunganishi kando na idadi kubwa ya *Na, Lakini* na *Kisha* kwa wote,

yanatofautiana. Mfano, Mbogo ametumia kiunganishi *Japokuwa* mara tatu (3) tu, Wamitila hakukitumia kamwe, Mbogo ametumia kiunganishi *Baada ya* mara kumi na tatu (13), Wamitila amekitumia mara arobaini na saba (47) na Mbogo ametumia kiunganishi *Hatimaye* mara kumi na nne (14), Wamitiai amekitumia mara arobaini na nne (44). Mbogo ametumia kiunganishi *Kutokana na* mara tisa (9) na Wamitila hakukitumia (0) wakati kiunganishi *Ingawa,* Mbogo hakukitumia (0) na Wamitila amekitumia mara tano (5).

Hata hivyo imedhihiri kuwa uunganishaji ni kijenzi muhimu katika kuunganisha dhana na mawazo katika Kiswahili ili kuleta mshikamano wa kisarufi, vile vile kama muundo na mtindo wa lugha hii. Mwandishi yeyote hawezi kuepuka matumizi ya viunganishi kwa kuleta mshikamano katika matini yake ambao unachangia kudhibiti sarufi na usahihi wa Kiswahili.

# SURA YA SABA

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.0 Utangulizi

Sura hii ni hitimisho la utafiti huu. Imeeleza yaliyojadiliwa kwa muhtasari katika kila sura. Imeonyesha jinsi malengo na nadharia tete za utafiti zilivyothibitishwa. Imefafanua yale tuligundua katika utafit ihuu na vikwazo vinavyojitokeza katika matini za Kiswahili tunapojenga mshikamano wa kisarufi. Aidha umeonyesha msimamo wangu juu ya Nadharia ya Mshikamano (Halliday na Hassan) tunapoitumia kwa kuongoza utafiti na matatizo yaliyomo tunapochunguza mshikamano katika matini za Kiswahili.

## 7.1 Hitimisho

Lengo la utafiti huu lilikuwa kuchunguza mshikamano wa kisarufi katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* Matini hizi ni riwaya. Ulichunguza jinsi mshikamano hutokea katika matini husika.

Mshikamano ni kipengele muhimu sana katika matini na lugha kwa jumla ili kuleta maana. Aidha huchangia katika kuunda sentensi zinazokubalika katika lugha yoyote ile, Kiswahili ikiwa mojawapo. Kuna mshikamano wa kisarufi na wa kileksia. Mshikamano wa kisarufi uliotafitiwa katika utafiti huu huletwa na vijenzi kadha kama urejeleaji, udondoshaji, ubadilishaji na uunganishaji. Kila kijenzi kina nafasi sawa ya uamilifu wa kuchangia mshikamano wa kisarufi katika matini. Kwa hivyo, vyote ni muhimu. Matini yoyote, iwe andishi au usemi, haikosi viunganishi hivi ndani yake ili kuleta mshikamano wa kisarufi. Kila kijenzi kimechunguzwa katika sura mbalimbali.

Sura ya kwanza imefafanua swala la utafiti, nadharia ya kuongoza utafiti, upeo wa utafiti, umuhimu wa utafiti, mapitio ya maandishi ya mshikamano , njia za ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

Sura ya pili imejadili urejeleaji katika matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!* Urejeleaji umedhihirika kuwa ni muhimu sana katika Kiswahili na hujitokeza katika kila sentensi. Urejeleaji huondoa urudufishaji unaoharibu sarufi ya lugha na mshikamano wa kisarufi. Kuna urejeleaji nje na ndani, kisha mrejeosabiki na mrejeombele. Kuna aina mbalimbali za urejeleaji zilizojadiliwa. Katika urejeleaji huu kuna vikwazo vilivyojitokeza katika Kiswahili ambapo urejeleaji hautumiki kiholela. Miongoni mwa vikwazo hivi ni kuwa wakati mwingine urejeleaji hupotosha maana, na ili kukwepa jambo hili, urudufishaji lazima utumike.

Sura ya tatu imeshughulikia ubadilishaji. Ubadilishaji ni kijenzi cha mshikamano ambacho vile vile kinaondoa urudufishaji na kujenga mshikamano wa kisarufi katika matini. Ubadilishaji umejitokeza katika daraja mbalimbali za sentensi kama vile Kirai Nomino, Kirai Kitenzi na sentensi au msururu wa sentensi. Ubadilishaji kwenye matini za *Watoto wa Maman'tilie* na *Musaleo!*, imebainika una utofauti wa utokeaji. *Matini ya Musaleo!* ina ubadilishaji zaidi (62.5% ) kuliko ile ya *Watoto wa Maman'tilie* (37.5% ). Tunasema utofauti huu umetokea kwa sababu ya mitindo ya wandishi hao. Matumizi yao ya lugha imesababisha kutokea kwa utofauti huu. Ubadilishaji haukuonyesha vikwazo vyovyote katika Kiswahili.

Sura ya nne imejadili udondoshaji na jinsi ulivyojitokeza katika matini za Kiswahili na kujenga mshikamano wa kisarufi. Udondoshaji umetumika zaidi katika matini ya *Watoto wa Maman'tilie* (57.1%) kuliko matini ya *Musaleo!* (42.9%). Imedhihirika vile vile udondoshaji unatokea katika daraja mbalimbali za sentensi. Unatokea katika daraja za neno, kirai, kishazi na sentensi. Nao pia una vikwazo vyake katika matumizi kwenye matini za Kiswahili. Vikwazo hivi ni kwamba udondoshaji katika vishazi viso-elekezi na vishazi viso-vitenzi hauwezikani katika Kiswahili. Aidha udondoshaji wa Kiima (KN) katika Kiswahili unakanganya kwa sababu daima kiwakilishi cha kiima lazima kiwepo katika kitenzi. Kwa hivyo umbo la ndani la sentensi huonyesha kuwa kiima kipo. Kwa hivyo dhana ya udondoshaji katika Kiswahili ina mushkeli.

Fauka ya hayo, idadi ya utokeaji imetofautiana katika matini hizo mbili zilizorejelewa katika uchunguzi, *Watoto wa Mama n'tilie* ni asilimia hamsini na saba nukta moja (57.1%) na katika *Musaleo!* ni asilimia arobaini na mbili nukta tisa (42.9%). Kwa hivyo matini ya *Watoto wa Maman'tilie* imetumia udondoshaji zaidi kuliko matini ya *Musaleo!*. Tunadai kuwa jambo hili ni kwa sababu ya mitindo ya wandishi hawa Emmanuel Mbogo na Kyalo Wamitila. Tumefikia uamuzi huu kwa sababu matini ya *Musaleo!* ni ndefu kuliko ya *Watoto wa Maman'tilie* kwa kurasa nne (4). *Musaleo!* ina kurasa mia moja na mbili (102) na ya *Watoto wa Maman'tilie* ina kurasa tisini na nane (98). Kwa hivyo kimantiki ni kuwa ile ya *Musaleo!* ingekuwa na utumiaji zaidi kwa sababu ya urefu wake. Lakini si hivyo. Basi udondoshaji hutofautiana kati ya wandishi kwa sababu ni mtindo. Uamuzi wetu unashadidiwa na Traugott na Pratt (1980:29) kuwa mtindo ni tabia ya

mwandishi katika uteuzi wake wa miundo fulani zaidi kuliko mingine ipatikanayo katika lugha.

Sura ya tano ilichunguza uunganishaji na jinsi unavyochangia mshikamano katika matini za Kiswahili. Umejitokeza kama kipengele muhimu cha lugha na mshikamano katika lugha. Hakuna lugha isiyo na uunganishaji. Uunganishaji hutokea katika katagoria za leksia, sentensi na dhana. Ule wa katagoria za leksia hauchangii mshikamano wa matini, bali uunganishi wa vishazi na sentensi. Nao hufanya kazi mbili, kuunganisha sentensi na pili kuunganisha dhana katika sentensi hizo.

Utafiti huu uligundua mambo kadhaa ya mshikamano wa kisarufi katika Kiswahili. Kuna aina mbalimbali za uunganishaji, na kati ya hizi, aina ya uunganishi nyongeza ndiyo inayotumika zaidi na aina ya uunganishi sababishi ndiyo hutumika kwa uchache zaidi. Pia kiunganishi *Na, Lakini* na *Kisha* hutumika zaidi katika Kiswahili, na vinavyotumika kwa uchache zaidi ni *Kabla, Kwa hivyo, Ingawa, Wala* na *Hivyo*. Jambo hili tunadai si mtindo wa waandishi ila ni mchakato na mfumo wa lugha ya Kiswahili. Ingekuwa mtindo, hakungekuwa na mwelekeo (trend) mmoja wa matumizi ya viunganishi katika matini zote mbili ambapo waandishi wa matini zilizochunguzwa ni watu tofauti kutoka nchi tofauti za Afrika Mashariki, Kenya (Wamitila) na Tanzania (Mbogo).

Vile vile viunganishi *Na, Tena, Hivyo* na *Baadaye* katika Kiswahili huwa na uamilifu zaidi ya moja. Kiunganishi *Na*, kinaweza kuwa kihusishi. *Tena* na *Baadaye* vikawa vielezi, na *Hivyo* kikawa kibadala au kirejelea kando ya kuwa kiunganishi sababishi.

Haya hutokea kwa sababu ya muktadha. Kwa hivyo si kila kiunganishi cha katagoria leksia ni kiunganishi katika mshikamano. Na yapo maneno ambayo si viunganishi kwa mujibu wa katagoria leksia lakini katika mshikamano wa matini huwa viunganishi kwa mfano *baadaye, mara, kabla (ya), baada ya* n.k.

Kiunganishi *Wala* hutumika na vitenzi kanushi na kimoja wapo ya hivi, kiwe kitenzi-nomino, hasa kile kinatokea baada ya *Wala. Kwa hivyo* hutokea katika kishazi fuatilizi tu katika matini. *Baada ya* hufuatwa na kitenzi-nomino au nomino tu. *Baadaye* kikiunganishwa na wakati mahususi, lazima wakati huo uje kabla ya kiunganishi hiki.

Mshikamano unapotokea katika matini huja na upekee wa matumizi ya lugha. Hii imeonyesha kuwa vijenzi vya mshikamano hutokea sehemu mahususi kwa mujibu wa mfumo wa lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu umegundua ya kwamba vijenzi vya mshikamano wa kisarufi katika Kiswahili ni muhimu sana katika kuleta mshikamano wa matini. Vijenzi hivi huondoa urudufishaji ambao huharibu mshikamano wa matini na sarufi ya Kiswahili na hushikanisha dhana na sentensi au sehemu za sentensi ili kuleta maana.

Kwa jumla katika Kiswahili, urejeleaji na uunganishaji hutumika zaidi. Udondoshaji na ubadilishaji hautumiki kwa kiwango kikubwa lakini ni muhimu katika mshikamano wa kisarufi ili kujenga miundo ya sentensi yenye maana kimatiki na kisarufi. Vijenzi hivi tumegundua vinaenda sambamba na sarufi ya lugha. Ingawaje lugha ya fasihi

inadaiwa kuwa na upekee lakini mshikamano lazima uzingatiwe ili miundo ya sentensi ilete maana inayokubalika.

Ufundi wa mwandishi wa matumizi ya lugha hutegemea sarufi ya lugha. Mwandishi hawezi kuandika kiholela kwa madai kuwa kuna upekee wa lugha ya fasihi. Lazima upekee huu ujikite katika sarufi ya lugha anayoitumia katika kazi yake na ahakikishe inaleta mshikamano. Bila mshikamano kazi yake haitaeleweka kwa wasomaji. Kama wadaivyo Traugott na Pratt (1980:20-21) isimu huchangia sana katika kuelewa matini.

Mshikamano pia, husaidia kusuluhisha matatizo ya ufasili kwa kuelezea kwa nini miundo kadha ya sentensi inakubalika na mingine haikubaliki. Hii ndiyo maana kuna mshikamano wa kisarufi katika lugha. Vijenzi vya mshikamano vina sheria zake katika Kiswahili na havitumiki kiholela. Vijenzi hivi vinapotumika kama Kiswahili kinavyoelekeza kimuundo, sarufi ya Kiswahili imedumishwa. Kwa hivyo, shikamano ni muhimu sana katika lugha hususan, ile sanifu na huchangia ujumi katika kazi za waandishi.

Imebainika kwamba, vijenzi vya mshikamano wa kisarufi vimetumika katika virai, vishazi na sentensi. Vijenzi hivi hutumika katika sehemu mahususi za sentensi na vinginevyo huharibu sarufi na mshikamano. Kwa hivyo waandishi lazima wazingatie mchakato na muundo wa Kiswahili katika matini zao. Hivi ndivyo vikwazo katika matumizi ya Kiswahili katika uandishi wa matini. Mwandishi hawezi kuandika Kiswahili kama aonavyo yeye au apendavyo bali hudhibitiwa na lugha yenyewe.

Vile vile utafiti umegundua ya kuwa Nadharia ya Mshikamano ya Halliday na Hassan (1976) kama ilivyo haisibu yote katika mshikamano wa Kiswahili. Kuna vipengele au maoni yao hayakubaliki katika Kiswahili. Hii ni kwa sababu, wao walishughulikia lugha ya Kiingereza ambayo ni tofauti na muundo wa Kiswahili. Kwa hivyo kuna haja ya kuirekebisha tunapoirejelea katika Kiswahili, kwa mfano urejeleaji katika Kiswahili hutukea hata katika sentensi moja. Aidha katika ubadilishaji neno *so* kiwakilishi chake ni *hivyo* katika Kiswahili ambapo kwa mujibu wa muktadha kibadala hiki huwa kirejelea.

Utafiti umeonyesha jinsi vijenzi vya mshikamano hutumika katika matini kuleta mshikamano unaohitajika ili kueleweka na kuhifadhi usarufi wa Kiswahili. Vikwazo vinavyojitokeza vimeovyeshwa na kudhihirisha kuwa kuna sheria katika matumizi yake kuleta usahihi wa Kiswahili.

Kwa hivyo, utafiti ulifikia malengo yake na kuthibitisha nadharia tete zilizozingatiwa katika uchanganuzi wa mshikamano. Ulidhihirisha kuwa vijenzi vya mshikamano havitumiki kiholela katika Kiswahili. Vinatumika kwa mujibu wa sheria za kisarufi ya Kiswahili. Vikitumika kinyume na sheria hizi, mshikamano hukosekana na kupotosha maana na sarufi pia. Hutumika katika daraja mbalimbali za sentensi, ikiwamo kirai, kishazi na sentensi. Virejelea na vibadala hutumika katika daraja ya neno, liwe nomino au kitenzi. Na vijenzi vinapotumika kwa kuzingatia sheria ya muundo wa Kiswahili, mshikamano hutokea katika matini na sarufi sahihi kudumishwa.

### 7.2 Mapendekezo

Kutokana na tuliyoyagundua katika utafiti huu tunapendekeza yafuatayo. Kwanza, matini zilizotumika si ndefu mno na ni mbili tu. Kwa hivyo ninapendekeza yafuatayo:

i) Pengine utafiti ufanywe kwa kutumia matini zaidi ya mbili kuthibitisha au kupinga hoja zetu.

ii) Tunapendekeza utafiti wa mshikamano ufanywe kwa kutumia matini (riwaya) nyingine za waandishi Wamitila na Mbogo kuchunguza kama matokeo yake yatadhihirisha matumizi ya vijenzi kama yalivyojitokeza katika utafiti huu. Hili litafanya uamuzi utolewe kama matumizi ya vijenzi vya mshikamano huwa mtindo wa mwandishi au la.

iii) Aidha utafiti ufanywe kuchunguza mshikamano katika matini nyingine za waandishi mbalimbali. Matokeo yatasaidia kufahamu ikiwa matumizi ya vijenzi vya mshikmano ni mfumo wa lugha ya Kiswahili au la, au kuna sababu nyingine zinazoleta utofauti huo. Vile vile tafiti zaidi zitaweza kudhihirisha zaidi utofauti wa matumizi ya vijenzi hivi vya mshikamano wa kisarufi miongoni mwa waandishi mbalimbali. Tafiti hizi zitaweza kushadidia au kukataa madai yetu ya mitindo ya wandishi.

iv) Pia utafiti ufanywe kwa kutumia matini (riwaya) za Kiswahili zilizotafsiriwa kuchunguza iwapo matokeo yake yatakuwa kama ya utafiti huu au yatakuwa tofauti.

v) Utafiti vile vile ufanywe kwa kutumia matini za waandishi ambao Kiswahili ni lugha ya kwanza kwao (kwa sababu ya umilisi) ili kujaribu kuchunguza utumiaji wa vijenzi vya mshikamano wa kisarufi katika matini hizo. Matini zilizotumika katika utafiti wetu si za wandishi ambao ni wazawa wa Kiswahili. Kama adaivyo Chomsky (1962) kuwa wazawa

wa lugha wana umilisi zaidi kuliko aliyejifunza lugha, huenda kukatokea matokeo tofauti na utafiti wetu.

vi) Kwa hivyo tunapendekeza mshikamano katika Kiswahili ufundishwe katika somo la lugha kwa wanafunzi wa shule za msingi, za upili na vyuo vikuu ili kukuza matumizi sahihi na bora ya Kiswahili katika usemi na isha. Mshikamano ni muhimu sana katika lugha hususan, ile sanifu. Huchangia ujumi katika kazi za waandishi (Traugott na Pratt, 1980:30).

**7.3 Mchango wa Utafiti**

Ni matumaini yetu, utafiti huu utachangia kujaza pengo katika isimu ya Kiswahili, hususan jinsi ya kupata mshikamano wa kisarufi katika matini. Utafiti huu utachangia katika ufafanuzi wa mshikamano wa kisarufi katika matini. Utasaidia wanafunzi na waandishi wanapoandika insha au kazi za fasihi kutumia Kiswahili sahihi na bora ili kuchangia ujumi wa kazi zao. Wanafunzi watafaidika kwa kufahamu njia bora za kuunganisha sentensi na mawazo ili kuwa na mtiririko ukubalikao katika insha za Kiswahili.

Utafiti huu utachochea watafiti wengine kuchunguza na kuthibitisha madai yetu, pengine kwa kutumia matini nyingine za Kiswahili. Pia watafiti wachunguze mshikamano katika lugha ya maongezi na mshikamano wa kileksia katika kuleta mshikamano katika matini za Kiswahili. Wanapofanya hivyo, watachangia kipengele hiki, na dhana ya mshikamano kwa jumla iwe imejadiliwa kikamilifu.

## MAREJELEO

### VITABU

Ashton, E. O. (1944) *Swahili Grammar*, England: Longman

Baker, C.L. (1978) *Introduction to Generative-Transformational Syntax*, New Jersey: Prentince-Hall Inc

Beaugrande, R. na Wolfgang, D. (1981) *Introduction to Text Linguistics*, New York: Longman

Brown, G. na Yule, G. (1983) *Discourse Analysis*, Cambridge: Cambridge University Press

Brown, K. na Jim, M. (1991) 2nd Ed *Syntax: A Linguistic Introduction to Sentence Structure*, London: Harper Collins Academic Publishers

Burton- Roberts, N. (1986) *Analysing Sentence: An Introduction to English Syntax*, England: Longman

Chimera, R. (2000) *KISWAHILI: Past, Present and Future Horizons*, Nairobi: Nairobi University Press

Chomsky, N. (1962) *Syntactic Structures*, Hague: Mouton and Co. Publishers

Courlthard, M. (1977) *An Introduction to Discourse Analysis*, Essex: Longman

Crystal, D. (1997) *The Cambridge Encyclopedia of Language*, Cambridge: Cambridge University Press

Culicover, P. W. (1976) *Syntax* New York: Academic Press Inc.

Dijk, T. A. V. (1977) *TEXT AND CONTENT:Explorations in the Semantics and Pragmatics of Discourse*, London: New York

Finch, G. (2000) *Linquistic Terms and Concepts*, London: Macmillan

Gimson, A.C. (1980) *An Introduction to the Pronounciation of English*, London: E.L.B.S and Edward Arnold Publishers Ltd.

Greenbaum, S. na wenzake (1972) *A Grammar of Contemporary English*, London: Longman

Habwe, J. na Peter, K. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi: Phoenix Publishers

Haegeman, L. (1995) *Introduction to Government and Binding Theory*, Malden, U.S.A: Blachwell Publishing

Halliday, M.A.K. (1985) *An Introduction to Functional Grammar*, London: Edward Arnold.

Halliday M. A. K. na Hassan R. (1976) *Cohesion in English*, New York: Longman

Hatch, E. (1992) *Discourse and Language Education*, Cambridge: Cambridge University Press

Hubbard, H. (2000) "Discourse: Language in context" ktk Kembo Sure na Webb Vic (wah) *The African Voices*, Cape Town: Oxford University Press

Huddleston, R. (1988) *English Grammar: An Outline*, Cambridge: Cambridge University Press

Jones, D. (1979) *An Outline of English Phonetics*, New Delhi: Kalyan Publishers

Kapinga, M. C. (1983) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: TUKI

Kihore, Y. M. na wenzake (2008) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA)*, Sekondari na Vyuo, Dar es Salaam: T.U.K.I

Kothari, C. R. (1990) *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi: Wishwa Prakashan

Laver, J. (1994) *Principles of Phonetics*, Cambridge: Cambridge University Press

Leech, G. na Svartvik, J. (1975) *A Communicative Grammar of English*, London: Longman

Matthews, P.H. (1981) *Syntax*, Cambridge: Cambridge University Press

Mbaabu, I. (1985) *Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi: Kenya Publishing and Book Marketing Co. Ltd

Mbogo, E. (2002) *Watoto wa Maman'tile*, Dar es Salaam: Heko Publishers

Mdee, J. S. (1986) *Kiswahili: Muundo na Matumizi Yake*, Nairobi: Intercontinental Publishers, Ltd

Mgullu, R. S. (1999) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*, Nairobi: Longhorn Puplishers

Mohamed, A. M. (2001) *Modern Swahili Grammar*, Nairobi: East African Educational Publishers

Mugenda, O. M. na Mugenda, A. G. (1999) *Research Methods: Quantitantive and Qualitative Approaches*, Nairobi: ACTS Press

O'Grady, W. na wenzake (1996) *Contemporary Linguistics: An Introduction*, Harlow Essex: Longman

Oliver, P. (2004) *Writing Your Thesis*, New Delhi: Vistaar Publication

Orodho, J. A. 2nd ed (2005) *Techniques of Writing Research Proposals and Reports*, Nairobi: Kanezja HP Enterprise

Quirk, R. na Greenbaum, S. (2000) *A University Grammar of English*, Delhi: Pearson Education Ltd

Safir, K. (2004) *The Syntax of Anaphora,* New York: Oxford University Press

Salkie, R. (1995) *Text and Discourse Analysis*, London: Routledge

Toolan, M. (1998) *Language in Literature*, London: Arnold

Traugott, E.C. na Pratt, M. L. (1980) *Linguistics for Students of Literature*, New York: Harcourt Brace Jovanovich, Inc.

TUKI (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: TUKI

_____ (1990) *Kamusi ya Isimu na Lugha*, Dar es Salaam: TUKI

____ (2000) *English- Swahili Dictionary*, Dar es Salaam: TUKI

Waihiga, G. (1999) *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*, Nairobi: Longhorn Publishers

Wamitila, K. W. (2004) *Musaleo!*, Nairobi: Vide- Muwa Publishers Ltd

Yule, G. (1996) *The Study of Language*, Cambridge: Cambridge University Press

**MAJARIDA**

Allerton, R. (1975) "Deletion and Proform Reduction" ktk *Journal of Linguistics 11*, uk 213-237

_____________ (1978) "The Notion of 'Givenness' and its Relations to Presupposition and to Theme" ktk *Lingua 44*, uk. 133-168

Carrell, P. L. (1992) "Cohesion Is Not Coherence" ktk *TESOL QUARTERLY Vol. 16, No. 4*, uk. 479-488

Delisle, D. (1973) "Discourse and Backward Pronominalization: Preliminary version" Stanford University , U.S.A

Gunter, R. (1963) "Elliptical Sentences in American English" ktk *Lingua 12*, Amsterdam: North- Holland Publishing Co. uk. 137- 150

Olateju, M. A. (2006) "Cohesion in ESL Classroom Written Texts" *Nodic Journal of African Studies* 15 (3): uk 314- 331

Hankames, J. na Sag, I, (1976) "Deep and Surface Anaphora" ktk *Linguistic Inquiry Vol. 7, No. 3*, uk. 391-426

Thomas, A.L. (1979) "Ellipsis: The Interplay of Sentence Structure and Context" ktk *Lingua 47*, uk.43-68

**TASNIFU**

Barongo, S, O. (1996) "Dhima ya Ushikamano katika Utendaji kwenye Insha za Kiswahili za Wanafunzi wa Kidato cha Nne, Wilayani Kisii, Kenya", Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret Tasnifu ya M.Phil (Haijachapishwa)

Contini-Morava, E. (1985) "Text Cohesion and the Sign: Connectedness between Events in Swahili Narratives", Virginia: University of Virginia (Unpublished PhD dissertation)

Mohamed, M. A. (1986) "A Comperative Study of Swahili and English Discourse" Colombus: Columbia University (Unpublished PhD dissertation)

Munyua, J.G. (1992) "Uwakilishaji wa Nomino Katika Kiswahili" Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret: Tasnifu ya M.Phil (Haijachapishwa)

Omondi, T. (1993) "A Discriptive Study of Cohesion Based on the Written Work of Form Four Students" M.Phil Thesis, Moi University (Haijachapishwa)